# FASIRI YA BIBLIA ISIYOGHARAMIWA

## UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA!

## *NAMNA VYOTE VILIVYOANZA: MWANZO 1-11*

Na Dr. Bob Utley,
Profesa mstaafu wa kanuni za ufasiri
(utafasili wa Biblia)

*STUDY GUIDE COMMENTARY SERIES*
*OLD TESTAMENT, VOL.01AOT*

Copyright © 2013 Bible Lessons International. Haki zote zimehifaziwa. Nukuu au usambazaji wowote wa sehemu ya maandishi haya lazima utolewe pasipo malipo yoyote. Nukuu au usambazaji huo lazima pongezi zimwendee mwandaaji Dr. Bob Utley na ikijumuisha nukuu toka www.freebiblecommentary.org
Msingi wa Mandiko ya Kibiblia yaliyotumika katika fasihi hii yametoka katika toleo la: New American Standard Bible (lililoboreshwa, 1995) Copyright ©1960, 1962, 1963, 1968, 1971, 1972, 1973, 1975, 1977, 1995 by The Lockman Foundation, P. O. Box2279, La Habra, CA 90632-2279

# ORODHA YA YALIYOMO

Maelezo sahihi ya zana za kiufundi zilizotumika katika fasili hii ........ i

Maelezo sahihi ya muundo wa maneno ya Kiebrania yanayogonganisha fasili ya maandiko ........ iii

Vifupisho Vilivyotumika Katika Fasihi Hii ........ viii

Neno Toka kwa Mwandishi: Ni kwa namna gani fasiri hii inaweza kukusaidia! ........ ix

Mwongozo Mzuri wa Usomaji wa Biblia: Utafiti Binafsi kwa Ukweli Uliothibitika ........ xi

Fasiri:

Maelezo ya ufunguzi juu ya usomaji wa kitabu cha mwanzo ........ 1

Utangulizi wa Kitabu cha Mwanzo ........ 3

Mwanzo 1:1-2:3 ........ 11

Mwanzo 2:4-25 ........ 37

Mwanzo 3:1-24 ........ 47

Mwanzo 4:1-26 ........ 65

Mwanzo 5 ........ 73

Mwanzo 6:1-22 ........ 77

Mwanzo 7 ........ 90

Mwanzo 8:1-22 ........ 94

Mwanzo 9:1-29 ........ 98

Mwanzo 10:1-32 ........ 107

Mwanzo 11:1-32 ........ 115

Kiambatisho:

Maelezo ya Kimaandiko ........ 119

# VIELELEZO VYA MADA MAALUM


Umri na uumbaji wa dunia, Mwanzo 1, Maelezo ya ufunguzi ........ 15

*Yom,* Mwa. 1:5 ........ 22

Mali asili, Tambuzi za Kimuktadha kwa Mwa. 1:24-2:3 ........ 28

Kuabudu, Mwa. 2:3 ........ 33

Majina ya Uungu, Mwa. 2:4 ........ 38

Maendeleo ya Thiolojia ya Agano Jipya juu ya anguko, Mwanzo 3 Utangulizi ........ 49

Nyoka, Mwa. 3:1 ........ 50

Uovu Binafsi, Mwa. 3:1 ........ 52

Kwa nini Mungu aliwavisha Adamu na Hawa ngozi za wanyama, Mwa. 3:21 ........ 59

*'OLAM* (Milele), Mwa. 3:22 ........ 60

Makerubi, Mwa. 3:24 ........ 62

Akamjua, Mwa.4:1 ........ 66

"Wana wa Mungu" katika Mwanzo 6, Mwa.6:4 ........ 78

Maneno yaliyotumika kwa mashujaa wenye nguvu au makundi ya watu, Mwa. 6:4 ........ 81

Haki, Mwa. 6:9 ........ 83

Agano, Mwa. 6:18 ........ 88

Mvinyo na kinywaji kikali, Mwa. 9:21 ........ 101

Ubaguzi wa kimbari, Mwa. 9:25 ........ 103

# MAELEZO MAFUPI YA VYANZO VYA KIUFUNDI VILIVYOTUMIKA KWENYE KIFUNGU"UNAWEZA KUIELEWA BIBLIA" KATIKA AGANO LA KALE KWENYE MFURULIZO WA FASIHI

I. Maneno/misamiati

Kuna maneno memngi mazuri mbali mbali yanayopatikana katika Kiebrania cha kale.

A. *Hebrew and English Lexicon of the Old Testament* by Francis Brown, S. R. Driver, na Charles A. Briggs. Yanaegemea juu ya misamiati ya Kijerumani ya William Gesenius. **Yanajulikana kwa vifupisho vya BDB.**

B. *The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na Ludwig Koehler na Walter Baumgartner, yaliyotafasiliwa na, M. E. J. Richardson. **Yanajulikana kwa vifupisho vya KB.**

C. *A Concise Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament* na William L. Holladay na inaegemea juu ya maneno ya Kijerumani (#A).

D. Idadi tano mpya za usomaji wa neno la kithiolojia lililoandikwa *The New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis*, kilichohaririwa na Willem A. Van Gemeren. **Yanajulikana kwa vifuapisho vya NIDOTTE.**

Ambapo kuna aina ya maneno muhimu, nimeonyesha tafasiri mbali mbali za Kiingereza (NASB, NKJV, NRSV, TEV, NJB) toka kwenye tafasiri za "neno-kwa-neno" na "mlinganyo wa nguvu" (kama vile Gordon Fee & Douglas Stuart, *How to Read the Bible For All Its Worth*, kur. 28-44).

II. Visarufi

Utambulisho wa kisarufi mara nyingi huzingatia juu ya John Joseph Owens' *Analytical Key to the Old Testament* katika juzuu nne. Hili limehakikiwa na Benjamin Davidson's *Analytical Hebrew and Chaldee Lexicon of the Old Testament.* Vitu vingine vya kusaidia kwa ajili ya visarufi na sintaksi ambazo zinatumika sana katika vipengere vya juzuu za agano la kale za mtiririko wa "kuelewa Biblia" ni "ule msaada wa mfuatano wa watafasiri" toka kwa United Bible Societies. Yameandikwa "kitabu kidogo cha mkononi ________."

III. Kimaandiko

Mimi nimejikita kwenye uvuvio wa konsonanti za maneno ya Kiebrania(sio katika hoja za voweli za Kimasoreti na maoni.kama ilivyo katika maandiko yote yaliyonukuliwa kwa mkono,kwenye maandiko ya kale, kuna baadhi ya sura zenye maswali. Hili huwa hivyo mara nyingi kwa sababu ifuatayo:

A. *hapax legomenon* (maneno yaliyotumika mara moja tu katika Agano la Kale la Kiebrania)

B. Maneno ya kinahau (maneno na vifungu ambavyo maana yake iliyo wazi imekwisha potea)

C. Kutojulikana kihistoria (kukosekana kwa habari kuhusu ulimwengu wa kale)

D. Wingi wa elimu-maana ya Kisemitiki wa misamiati finyu ya Kiebrania

E. Matatizo yanayohusianishwa na uandishi wa maaandishi ya Kiebrania ya kale ya waandishi wa mwanzo kwa kutumia mkono.

F. Waandishi wa Kiebrania waliosomea huko Misri waliojisikia kuwa huru kuyahariri maandiko waliyoyanakili kwa ajili ya kuyafanya kuwa kamili na ya kueleweka wakati wa siku zao (NIDOTTE kur. 52-54). Kuna vyanzo mbali mbali vya maneno na maandiko ya Kiebrania nje ya tamaduni ya kimaandiko ya Kimasoreti.

1. Torati ya Kisamaria
2. Magombo ya Bahari ya Chumvi
3. Baadhi ya sarafu, herufi na vigae vya vyungu vilivypatikana baadaye (vipande vya vigae vya vyungu vilivyotumika kuandikiapo maandiko), lakini kwa maeneo mengine, hakuna uhusiano wa

kimachapisho katika Agano la Kale kama yale yaliyoko katika machapisho ya Agano Jipya la Kiyunani. kwa ajili ya ufasaha wa makala mazuri juu ya uendelevu wa kimaandiko ya andiko la Kimasoreti (miaka ya 900 B.K) angalia “Uendelevu wa andiko la Agano la Kale” na Bruce K. Waltke katika toleo la NIDOTTE, juzuu. 1, kur. 51-67. Andiko la Kiebrania lililotumika ni *Biblia Hebraica Stuttgartensia* toka German Bible Society, 1997, ambayo inaegemea juu ya Leningrad Codex ( 1009 B.K). Mara chache, matoleo ya kale (maandiko ya kale ya Kiyunani, Kiarama Targums, Syriac Peshitta, na Latin Vulgate) yanazungumzika kama Kiebrania ni kigumu au kinatatiza kwa wazi.

## MAELEZO SAHIHI YA MUUNDO WA KIVITENZI VYA KIEBRANIA AMBAVYO VINAGONGANA NA FASILI YA MAANDIKO

I. Maendeleo mafupi ya kihistoria ya Kiebrania

Waebrania ni sehemu ya kifamilia ya lugha ya Shemu kusini mwa Asia. Jina (lililotolewa na wasomi wa sasa) limetokana na Mwana wa Nuhu, Shemu (kama vile Mwa. 5:32; 6:10). Kizazi cha Shemu kimeorodheshwa katika Mwa. 10:21-31 kama Waarabu, Washamu, Waarameni, na Waashuru.

Kiukweli, baaadhi ya lugha za Kisemiti zinatumia na mataifa yaliyoorodheshwa katika ukoo wa Hamu (kama vile Mwa. 10:6-14), Wakaanani, Wafoeniki, na Waethiopia.

Waebrania ni sehemu ya kikundi cha kaskazini Magharibi mwa lugha hizi za Kisemiti. Wasomi wa leo wana mifano ya kikundi cha lugha ya kale toka :

A. Waamori (*Mari Tablets* tokea karne ya 18 K.K. huko Akadi
B. Wakaanani (*Ras Shamra Tablets* tokea karne ya 15 Ugariti
C. Wakaanani (*Amarna Letters* tokea karne ya 14 wakaanani wa huko Akadi)
D. Wafoeniki (Waebrania walitumia alfabeti za Wafoeniki)
E. Wamoabu (Mawe ya mfalme Mesha, 840 K.K)
F. Waaramaiki (lugha rasmi ya Himaya ya Uajemi iliyotumika katika Mwa. 31:47; Yer. 10:11; Dan. 2:4b-6; 7:28; Ezr. 4:8-6:18; 7:12-26 na iliongewa na Wayahudi katika karne ya kwanza huko Palestina

Lugha ya Kiebrania iliitwa “lugha ya Kaanani.” Mara ya kwanza iliitwa “Kiebrania” katika utangulizi Mhubiri (Hekima ya Yoshua Bin Sira) kuhusu 180 K.K. na baadhi ya maeneo mengine ya awali, kama vile *Anchor Bible Dictionary*, vol. 4, uku. 205 na kuendelea).sana sana yanakaribiana kufanana na Wamoabu na kabila lililotumika huko Ugariti. Mifano ya ya Waebrania wa kale wanaopatikana nje ya Biblia ni

1. Kalenda ya Gaza, 925 K.K. (andiko la kijana wa shule)
2. Andiko /ujumbe wa Siloam, 705 K.K (maandiko yaliyopatikana katika njia za chini)
3. Vigae vya waebrania, 770 K.K (kodi inanakiriwa kwenye vigae vya chungu)
4. Herufi zilizoandikwa kwenye vigae, 587 K.K (mawasiliano kwenye vita)
5. Mihuri na sarafu za watu wa Makabi
6. Baadhi ya maandiko yaliyopatikana katika magombo ya Bahari ya Chumvi
7. Maandiko mbali mbali (kama vile “lugha[Kiebrania], “ ABD 4:203 nakuendelea)

Kama ilivyo lugha zingine za Kisemiti, inaainishwa na maneno yaliyoundwa na konsonanti tatu (mizizi mitatu ya kikonsonanti). Ni lugha thabiti isiyopindika. Mizizi mitatu ya konsonanti inabeba msingi wa maana ya neno, wakati kiambishi awali, kiambishi tamati, au maneno ya nyongeza yanaonyesha utendaji wa kisarufi (voweli zinaongezeka baadae, kama vile Sue Green, *Linguistic Analysis of Biblicla Hebrew*, uk 46-49).

Misamiati ya Kiebrania inaonyesha tofauti kati ya lugha ya mjazo na ushairi. Maana ya neno imehusianishwa na asili ya ngano/hadithi (sio usanifu wa lugha). Mchezo wa neno na mchezo wa sauti ni vitu vya kawaida (*paronomasia*)

II. Dhana ya utabiri

A. VITENZI

Neno la kawaida linalotarajiwa ni KITENZI, KIWAKILISHI, KIIMA (likiwa na vivumishi vyake), KISHAMIRISHO (kikiwa na vivumishi chake). KITENZI cha msingi kisicho pungua ni *Qal,* chenye muundo wa UMOJA, JINSI YA KIKE, na TIMILIFU. Ni namna misamiati ya Kiebrania na Kiaramaiki inavyopangwa. VITENZI vinanyumbulishwa majina kuonyesha

1. Namba-umoja, wingi, umiliki wa vitu viwili
2. Jinsi-jinsi ya kiume na jinsi ya kike (isio na jinsi)
3. Dhamira-elekezi, tegemezi, shurutishi (kwa kulinganisha lugha za Magharibi ya leo, uhusiano wa kitendo kuelekea ukweli halisi)
4. Njeo-(dhana)
   a. WAKATI TIMILIFU, inayomaanisha kutimiliza, kwa maana ya kuanza, kuendelea, na kuhitimisha kitendo. Mara zote muundo huu ulitumika kwa ajili ya kitendo kilichopita,

tukio linatokea. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema "muundo mzima ulioelezewa kwa wakati timilifu pia umezingatiwa kuwa wenye uhakika. Wakati usiotimilifu unaweza kuonyesha hali ya kuwezekana au shauku au yenye kutarajiwa, lakini wakati timilifu unaliona hili kama lenye uhakiki, halisi na kweli" (uk. 36). S. R. Driver, *A Treatise on the Use of the Tenses in Hebrew*, inaielezea kama: wakati timilifu unaofanya kazi kuonyesha vitendo vyenye kutimilizwa ambavyo hakika vinasimama wakati ujao, lakini vinachukulia kama vyenye kujitegemea juu ya kusudi lisilobadilika la nia thabiti ambalo laweza kuongewa kama kitu halisi kilichochukua nafasi: kwa hiyo suluhisho, ahadi,au tamko, hasa lile la ki-Ungu mara nyingi linatamkwa katika njeo ya wakati timilifu"(uk. 17 mf., utimilifu wa kinabii). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anauelezea muundo wa kimaneno kwa namna hii:

"….inaiangalia hali kutokea nje, kwa ukamili wake. Kwa namna hiyo kinaelezea ukweli mrahisi, ingawa kinawezakuwa ni kitendo au hali (ukijumuisha hali ya kuwa au fikra). Kinapotumika katika vitendo, mara nyingi inakitazama kitendo kama kilicho kamili toka kwenye hoja ya mzungumzaji mwenye ustadi au msimuliaji (ikiwa ni kamili au sio kamili kwa maana ya uhalisia au ukweli na sio hoja). Utimilifu unaweza kuhusika katika kitendo /hali ya wakati uliopita, uliopo ao ujao. Kama ilivyoelezewa hapo juu, muda, ambao unashawishi namna gani mtu anaweza kutafasiri utimilifu kwenda kwenye njeo ya lugha iliyobobea kama Kiingereza, lazima ipimwe toka kwenye muktadha"(uk.86)

b. WAKATI USIOTIMILIFU, unaoelezea kitendo kilichoko katika mchakato (kisichotimilifu, chenye kujirudia, chenye kuendelea, au chenye udharura), mara nyingi huenenda kuelekea lengo. Mara nyingi muundo huu ulitumika kwa kitendo cha wakati uliopo na ujao. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anasema "NYAKATI ZOTE ZISIZOTIMILIFU zinawakilisha hali yakutokukamilika. Zinaweza kuwa ni zenye kujirudia au kuendelea au za dharura. Kwa maneno mengine, au kwa sehemu Fulani inaanza au kiasi Fulani inahakikiwa. Kwa namna zozote katika baadhi ya maana haijamalizika, yaani., haijakamilika" (uk. 55). Robert B. Chisholm, Jr. *From Exegesis to Exposition*, anasema "ni vigumu kupunguza kiini cha kutokutimia kwenda dhana moja, kwa vile inajumuisha vyote dhima na dhamira. Muda mwingine wakati usiotimilifu hutumika kwa namna ya kuarifu na kutengeneza maelezo pingamizi. Wakati mwingine inakitazama kitendo zaidi kitegemezi, kama kinadharia, dharura, chenye kuwezekana na nakadharika" (uk. 89)

c. Neno lililoongezewa *waw,* linalounganisha KITENZI kwenye kitendo cha KITENZI kilichopita

d. Dhana SHURUTISHI, inayosimamia juu ya uhiari wa mnenaji na kitendo muhimu cha wasikilizaji

e. Katika Uyahudi ya kale muktadha mpana uliweza kuamua mwelekeo wa muda wa uandishi uliokusudiwa.

B. Miundo mikuu saba iliyobadilishwa na maana zake. Kiuhalisia miundo hii inatenda pamoja na nyenzake katika muktadha na haipaswi kutengwa

1. *Qal* (*Kal*), ni muundo wa kawaida na wa msingi katika miundo yote. Unadokeza kitendo rahisi au hali ya nafsi. Hakuna kisababishi au ulazima uliotumika.
2. *Niphal*, ni muundo wa pili ulio wa kawaida sana. Mara nyingi huwa katika hali ya KUTENDWA, lakini muundo huu pia hutenda kama wenye kubadilishana na kujirejea. Pia hauna kisababishi au ulazima uliotumika.
3. *Piel*, muundo huu ni muundo tendaji na huelezea kuhusu kukifanya kitendo kuwa katika hali ya nafsi. Maana ya msingi ya shina la neno *Qal* inajitokeza au kuendelea kwenye hali ya nafsi.
4. *Pual*, ni neno mfanano TENDWA wa neno *Piel*. Mara nyingi huelezewa kwa KIAMBATA
5. *Hithpael*, ambalo ni shina la kujirejea au kubadilishana. Linaelezea usisitiaji wa kitendo au hali ya kudumu ya kitendo kulinganisha na shina la neno *Piel* . Muundo adimu TENDWA unaitwa *Hothpael*.

6. *Hiphil*, ni muundo tendaji wa usababishaji shina tofauti na neno *Piel*. Unawezakuwa na dhana ya ruksa, lakini mara nyingi unarejelea kwenye sababu ya tukio. Ernst Jenni, Mjerumani Muebrania , mwana sarufi, anaamini kuwa neno *Piel* linadokeza kitu Fulani kuja kwa hali ya nafsi, wakati *Hiphil* inaonyesha jinsi inavyotokea.
7. *Hophal,* ni neno mlingano TENDWA kulinganisha na neno *Hiphil*. Haya mashina ya mwisho mawili ndiyo madogo yaliyotumika kati ya yale mashina saba.

Wingi wa habari hii unapatikana toka *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, by Bruce K. Waltke na M. O'Connor, kur. 343-452

Chati ya kundi na kisababishi chake. Namna moja katika uelewa wa muundo wa KITENZI cha Kiebrania ni kukiangalia chenyewe katika kipengere cha mahusiano ya IRABU. Baadhi ya mashina ya maneno yanatofautiana na mashina ya maneno mengine (yaani *Qal - Niphal; Piel - Hiphil)* . Chati iliyoonyeshwa hapa chini inajaribu kuangazia kwenye utendaji wa msingi wa mashina ya KITENZI na visababishi vyake.

| **IRABU au KIIMA** | **HAKUNA KUNDI LINALOFUATA** | **KUNDI TENDAJI LINALOFUATA** | **KUNDI TENDEWA LINALOFUATA** |
|---|---|---|---|
| TENDAJI | *Qal* | *Hiphil* | *Piel* |
| YA KATI TENDWA | *Niphal* | *Hophal* | *Pual* |
| KUJIREJEA/KUTENDEANA | *Niphal* | *Hiphil* | *Hithpael* |

Chati hii imechukuliwa toka katika majadiliano mazuri ya muundo wa kivitenzi katika uelewa wa utafiti wa lugha ya Akkadia (kama vile Bruce K. Waltke, M. O'Conner, *An Introduction to Biblical Hebrew Syntax*, uk. .354-359)

R. H. Kennett, *A Short Account of the Hebrew Tenses*, ametoa onyo lenye kufikirika kuwa muhimu. "mara nyingi nimeweza kuanzisha katika mafundisho, kuwa kiongozi cha wanafunzi kilicho kigumu katika vitenzi vya Kiebrania ni kupata maana iliyoelezewa katika fikra za Waebrania wenyewe; kuwa ndiyo kusema, kuna tabia ya kutoa kwa mwelekeo wa kufanana kwa kila njeo za Kiebrania kama namba fulani ya muundo wa Kilatini au Kiingereza ambapo njeo hiyo mahsusi kwa kawaida yaweza kutafasiriwa. Matokeo ni kushindwa kutofautisha wingi wa hivi vivuri venye maana, ambavyo vinatoa uhai aina hiyo na nguvu kwenye lugha ya Agano la Kale. Ugumu katika matumizi ya vitenzi vya Kiebrania uko tu katika hoja ya mtizamo, kwa hiyo moja kwa moja yanatofautiana na ya kwetu, kutokana na kile Waebrania wanaangalia kitendo; muda wa mambo, ambao pamoja nasi ni upendeleo wa kwanza, kama neno lenyewe, "njeo" linavyoonyesha, kwao kuwa ni chaguo la pili. Kwa hiyo, ni muhimu kuwa mwanafunzi kwa uwazi aweze kuchukua, sio kwa wingi miundo ya Kilatini au Kiingereza ambayo inaweza kutumika kutafasiri kila njeo za Kiebrania, bali kiasi Fulani dhana ya kila kitendo, kama kilivyowasilishwa katika fikra za Waebrania. Jina la 'njeo" kama lilivyotumika katika vitenzi vya Kiebrania vinapotosha. Kile kinachoitwa 'njeo' za Kiebrania hakielezei muda lakini kwa kidogo hali ya kitendo. Hakika hakikuwekwa kwa ajili ya kuleta mkanganyiko ambao ungaliweza kutokea kupitia matumizi ya neno 'kauli' kwa namna zote mbili ya nomino na vitenzi, 'kauli' zingalikuwa nzuri zaidi kwenye usanifu kuliko 'njeo.' Mara nyingi ni lazima kitu kiwekwe akilini kuwa haiwezekani kutafasiri kitenzi cha Kiebrania kwenda kwenye Kiingereza bila kutumia udhibiti ambao haupo kabisa katika Kiebrania. Waebrania wa mwanzo kamwe hawakufikiria kitendo chaweza kuwa katika wakati uliopita, uliopo na ujao, lakini walifikilia tu kwenye *utimilifu* yaani., kitendo kilichokwisha tendeka, au *kisicho timilifu,* yaani., kama katika njia ya kusonga mbele. Tunaposema kuwa njeo Fulani ya Kiebrania wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao katika Kiingereza, hatumaanishi kuwa mawazo ya Kiebrania ya hicho kama wakati timilifu, wakati timilifu ainishi, au wakati ujao, lakini tu kuwa lazima itafasiliwe katika Kiingereza.

Wakati wa kitendo Waebrania hawakujaribu kuelezea kwa namna yeyote ya muundo wa kuongea kwa maneno (utangulizi na uk.1). kwa angalizo la pili, , Sue Groom, *Linguistic Analysis of Biblical Hebrew*, anatukumbusha sisi, "hakuna namna ya kuweza kujua ikiwa muundo wa wasomi wa sasa wa elimu-maana na uhusiano wa maana katika lugha zilizokufa au kupotea ni taswira ya fikra zao, au lugha zao mama, au maeneo hayo yalikuwepo katika Waebrania wenye hadhi" (uk. 28).

C. Dhamira (ambazo ni mifanano ilichukuliwa toka kwenye lugha za kimagharibi ya sasa)
   1. Imetokea, inaendelea kutokea (NI KAULI ELEKEZI), mara nyingi inatumia njeo WAKATI TIMILIFU au WAKATI UNAOENDELEA ( KAULI ZOTE ENDELEVU ziko katika KAULI ELEKEZI).
   2. Itatokea, ingalia tokea (KAULI TEGEMEZI)
      a. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU ya wazi
         1) Zenye KUFUNGAMANA (likiongezewa herufi h), nafsi ya kwanza KAULI ISIOTIMILIFU ambayo mara nyingi huelezea kutakia heri, hitaji, au kutia moyo (yaani., matendo ya hiari ya mzungumzaji)
         2) ASILI NA UFAFANUZI ZAIDI WA NENO (badiliko la ndani), mtu wa tatu KAULI ISIOTIMILIFU (inawezakuwa mtu wa pili katika sentensi kanushi) ambayo mara nyingi inaelezea ombi, ruhusa, maonyo, au ushauri
      b. Hutumia njeo ya WAKATI TIMILIFU ikiwa na *lu* au *lule.* Miundo hii inafanana na sentensi YENYE MASHARTI DARAJA LA PILI katika lugha ya Koine ya huko Uyunani. Maelezo yasiyo sahihi (Kishazi chenye kuelezea tamko ndani ya sentensi yenye masharti) yenye kuleta hitimisho lisilo sahihi (Kishazi kikuu ndani ya sentensi yenye masharti).
      c. Hutumia njeo ya WAKATI USIOTIMILIFU na muktadha wa *lu,* vile vile maelekezo wa wakati ujao, kuangalia matumizi ya KAULI TEGEMEZI. Baadhi ya mifano inapatikana kwa J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament ni* Mwa.13:16; Kumb. 1:12; I Fal. 13:8; Zab. 24:3; Isa. 1:18 (kama vile kur. 76-77).

D. *Waw* – Kinyume chake/yenye matokeo yaliyofuatana/rejeshi. Huu muonekano wa kipekee wa isimu zenye kushughulikia kupanga maneno ya kisarufi ya Kiebrania imeleta mkanganyiko mkubwa kwa miaka mingi. Imetumika kwa namna nyingi mara nyingi ikizingatia juu ya uwasilishaji. Sababu ya mkanganiyiko ni wale wasomi wa mwanzo walikuwa watu wa Ulaya na wakajaribu kutafsiri katika ulelewa wa lugha zao za asili. Na hili lililopoonekana kuwa gumu wakaanza kulaumu lugha ya Kiebrania kuwa ni ya zamani, lugha ya kikale. Lugha za Ulaya ni NJEO (za muda) zinazoegemea kwenye VITENZI. Baadhi ya namna na madokezo ya visarufi yaliainishwa na herufi WAW ambayo iliongezwa kwenye shina la KITENZI TIMILIFU au KITENZI ISIOTIMILIFU. Hii inabadilisha namna ya kitendo kilivyo tazamwa.
   1. Katika simulizi za kihistoria VITENZI vinaunganishwa pamoja katika mfuatano vikiwa na mwongozo wa kawaida
   2. Kiambishi awali cha *waw* kinaonyesha uhusiano maalum kikiwa na KITENZI kilichopita.
   3. Muktadha mpana mara nyingi ni kiini cha uelewa wa mfuatano wa KITENZI. VITENZI vya Kisemiti haviwezi kutathimini utengano. J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament*, anaeleza utofauti wa Waebrania katika matumizi ya neno *waw* kabla ya KAULI TIMILIFU na KAULI ISIOTIMILIFU (kur. 52-53). Kama wazo la msingi la KAULI TIMILIFU ni muda uliopita, kuongezeka kwa neno *waw* mara zote linatenda kwa dhana ya wakati ujao. Hili pia ni kweli kwa KAULI ISIOTIMILIFU ambayo wazo lake la msingi ni la wakati uliopo au wakati ujao; kuongezeka kwa neno *waw* lililowekwa katika wakati uliopita. Hili ni badiliko la muda lisilo la kawaida ambalo linaelezea kungezeka kwa neno *waw,* sio kwenye badiliko la maana yake ya msingi ya njeo yenyewe. KAULI TIMILIFU ya neno *waw* inatenda kazi vizuri kwenye unabii, wakati KAULI ISIOTIMILIFU ya neno *waw* inatenda vizuri kwenye simulizi (kur. 54,68). Watts anaendeleza ufafanuzi wake, " kwa ajili ya kuonyesha tofauti iliyopo ya msingi kati ya neno *waw* kiunganishi na neno *waw* linalojirudia, utafasiri ufuatao unatolewa:
      1) Neno *waw* ambalo ni kiunganishi hutokea mara nyingi kuonyesha ufanano.

2) Neno *waw* kwa mfululizo linatokea mara zote kuonyesha mwendelezo. Ni muundo pekee wa neno *waw* unaotumika ukiwa na mfululizo wa kauli isiotimilifu. Uhusiano kati ya kauli zisizotimilifu zilizounganishwa nayo yaweza kuwa ni mfuatano wa muda, matokeo ya kimantiki, sababu za kimantiki, au tofauti za kimantiki. Kwa namna yeyote ile kunamfuatano"(uk.103)

E. KITENZIJINA-Kuna aina mbili ya vitenzijina
   1. KITENZI JINA CHA MOJA KWA MOJA, chenye "nguvu, kinachojitegemea, kinachoshambulia maelezo yaliyotumika kwa ajili ya matokeo ya kuvutia…..kama kiima, mara nyingi hakina kitenzi kilichoandikwa, kitenzi 'kuwa" kikiwa kinaeleweka, hakika, neno linabaki kusimama lenyewe wazi,"(J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Hebrew Old Testament,*" uk. 92).
   2. KITENZI JINA KINACHOJENGA, ambacho "kinahusiana kisarufi kwenye sentensi na vihusishi, viwakilishi milikishi, na uhusiano uliojengeka" (uk.91). J. Weingreen, *A Practical Grammar for Classical Hebrew*, anaelezea hali ya muundo:

      "ikiwa maneno mawili (au zaidi) yanaunganikana kwa karibu ambapo kwa pamoja yanatengeneza wazo moja ambatani, neno lenye kujitegemea (au maneno) yanasemekana kuwa katika hali ya muundo." (uk. 44).

F. VIWAKILISHI VYA KUULIZA
   1. Mara zote huonekana kwanza kwenye sentensi.
   2. Umuhimu wa kufasiri
      a. *ha*- haitarajia mwitikio
      b. *halo'*- mwandishi anategemea jibu la "ndiyo"

   KAULI HASI
   1. Mara nyingi hujitokeza kabla ya maneno yenyewe yanayo kanushwa.
   2. Neno mojawapo kanushi ni *lo'.*
   3. Neno *al* lina kidokezo dharura na hutumika likiwa na asili na ufafanuzi zaidi wa neno.
   4. Neno *lebhilti*, linamaanisha "ili kwamba……sio" linatumika likiwa na VITENZI JINA.
   5. Neno *'en* linatumika likiwa KAULI ENDELEVU.

G. SENTENSI ZENYE MASHARTI
   1. Kuna aina nne ya sentensi zenye masharti ambazo kimsingi zinafanana katika lugha ya Koine ya huko Ugiriki.
      a. Kitu fulani kinaonekana kuwa kikitokea au mawazo kama yalivyotimilizwa (DARAJA LA KWANZA katika Kiyunani)
      b. Kitu Fulani kinyume na ukweli ambacho utimilisho wake hauwezekani (DARAJA LA PILI)
      c. Kitu fulani ambacho kinawezekana au hata kuonekana kutokea(DARAJA LA TATU)
      d. Kitu fulani ambacho ni yumkini kutokea, kwa hiyo utimilisho ni agharabu(DARAJA LA NNE)
   2. ALAMA ZA VISARUFI
      a. Vinafikiliwa kuwa kweli au hali iliyopo inatumia KAULI TIMILIFU ELEKEZI au KAULI ENDELEVU na mara zote kishazi kidogo kinatambulishwa kwa
         1) *'im*
         2) *Ki*
         3) *hin* au *hinneh*
      b. muundu ulio kinyume na ukweli mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU kikiwa na utangulizi wa KIAMBATA *lu* au *lule*
      c. zaidi muundo wenye uyumkini mara zote hutumia KITENZI KISICHOTIMILIFU au KITENZI ENDELEVU katika kishazi kidogo, mara zote *'im* au *ki* vinatumika kama kauli ya mwanzo ENDELEVU
      d. Yumkini muundo mdogo hutumia KAULI TEGEMEZI ISIYOTIMILIFU katika kishazi kidogo na mara zote *'im ni* utambulisho wa KAULI ENDELEVU.

# VIFUPISHO VILIVYOTUMIKA KATIKA FASIRI HII

| | |
|---|---|
| AB | Anchor Bible Commentaries, ed. William Foxwell Albright and David Noel Freedman |
| ABD | Anchor Bible Dictionary (6 vols.), ed. David Noel Freedman |
| AKOT | Analytical Key to the Old Testament by John Joseph Owens |
| ANET | Ancient Near Eastern Texts, James B. Pritchard |
| BDB A | Hebrew and English Lexicon of the Old Testament by F. Brown, S. R. Driver and C. A. Briggs |
| IDB | The Interpreter's Dictionary of the Bible (4 vols.), ed. George A. Buttrick |
| ISBE | International Standard Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. James Orr |
| JB | Jerusalem Bible |
| JPSOA | The Holy Scriptures According to the Masoretic Text: A New Translation (The Jewish Publication Society of America) |
| KB | The Hebrew and Aramaic Lexicon of the Old Testament by Ludwig Koehler and Walter Baumgartner |
| LAM | The Holy Bible From Ancient Eastern Manuscripts (the Peshitta) by George M. Lamsa |
| LXX | Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970 |
| MOF | A New Translation of the Bible by James Moffatt |
| MT | Masoretic Hebrew Text |
| NAB | New American Bible Text |
| NASB | New American Standard Bible |
| NEB | New English Bible |
| NET | NET Bible: New English Translation, Second Beta Edition |
| NRSV | New Revised Standard Bible |
| NIDOTTE | New International Dictionary of Old Testament Theology and Exegesis (5 vols.), ed. Willem A. VanGemeren |
| NIV | New International Version |
| NJB | New Jerusalem Bible |
| OTPG | Old Testament Passing Guide by Todd S. Beall, William A. Banks and Colin Smith |
| REB | Revised English Bible |
| RSV | Revised Standard Version |
| SEPT | The Septuagint (Greek-English) by Zondervan, 1 970 |
| TEV | Today's English Version from United Bible Societies |
| YLT | Young's Literal Translation of the Holy Bible by Robert Young |
| ZPBE | Zondervan Pictorial Bible Encyclopedia (5 vols.), ed. Merrill C. Tenney |

# NENO TOKA KWA MWANDISHI
# NI KWA NAMNA GANI FASIHI HII ITAKUSAIDIA?

Kutafasiri Biblia ni uwiano wa wastani na wa kiroho ambao unajaribu kumwelewa mwandishi wa kale aliyevuviwa kuandika ili kuwezesha ujumbe wa Mungu uweze kueleweka na kutumiwa katika zama hizi.

Mchakato wa kiroho ni muhimu sana lakini mugumu sana kuelezea. Unahusisha kujitoa na kuwa wazi kwa Mungu. Lazima pawepo na njaa (1) kwa ajili yake (2) ya kumjua yeye na (3) kumtumkia yeye. Mchakato huu unahusisha maombi, ukiri na kuwa tayari kubadili mfumo wa kuishi. Roho Mtakatifu ni wa muhimu sana katika mchakato wa utafasiri, lakini kwa nini wakristo waaminifu, wanaompenda Mungu wanaielewa Biblia tofauti kabisa na kuitafasiri visivyo.

Mchakato wa uwiano huu ni rahisi kuuelezea. Lazima tuwe na msimamo na haki kwa maandiko badala ya kuathiriwa na hali ya upendeleo binafsi au wa ki-madhehebu. Sote tumefungamanishwa ki-historia. Hakuna yeyote mtafasiri miongoni mwetu awezae kubisha. Fahiri hii inatoa kwa uangalifu uwiano ulio sahihi wenye kanuni tatu za tafasiri zilizoundwa kusaidia kudhibiti hali zetu za upendeleo.

## KANUNI YA KWANZA

Kanuni ya kwanza ni kuona muundo wa kihistoria ambao kwayo Biblia iliandikwa na tukio zima la kihistoria katika uandishi wake. Mwandishi wa mwanzo alikuwa na kusudi, ujumbe wa kuwakilisha. Andiko haliwezi kumaanisha kitu kwetu ambacho hakikumaanishwa na ile asili, na mwandishi aliyevuviwa wa zama hizo. Kusudi lake na wala sio mahitaji yetu ki-historia, ki-musisimko, ki-tamaduni na mapokeo ya ki-madhehebu yetu ni—ufunguo.

Matumizi ni mbia mkubwa wa tafasiri, lakini tafasiri sahihi lazima ipate kipaumbele kwa matumizi. Lazima isisitizwe kwamba, kila andiko la Biblia lina tafasiri moja tu, na si vinginevyo. Maana hii ndiyo mwandishi wa mwanzo wa Biblia alivyokusudia akiongozwa na roho kuiwasilisha katika enzi zake. Maana hii moja yaweza kuwa na matumizi anwai, katika tamaduni na mazingira tofauti. Matumizi haya lazima yaambatane na ukweli halisi wa mwandishi wa awali. Kwa sababu hii, mwongozo wa fasiri hii imetayalishwa kwa namna ya kutoa utangulizi kwa kila kitabu cha Biblia.

## KANUNI YA PILI

Kanuni ya pili ni kuibainisha fasihi moja. Kila kitabu cha Biblia ni hati ya kumbukumbu iliyounganishwa. Wafasiri hawana haki ya kutenganisha hoja moja ya ukweli kwa nyingine. Kwa hiyo hatuna budi kujaribu kuelewa kusudi la kitabu kizima cha Biblia kabla ya kutafasiri fasihi ya kitabu kimoja kimoja. Sehemu moja—sura, aya, au mistari haiwezi kumaanisha ambacho kitabu kizima hakimaanishi. Tafsiri sharti iwiane na mtizamo mzima kuelekea mtimzamo wa sehemu ya vifungu vya Biblia. Kwa hiyo mwongozo huu wa fasiri ya mafunzo haya umelenga kuwasaidia wanafunzi kuchambua muundo wa kila andiko ki-aya. Mgawanyo wa ibara na sura havikuvuviwa bali ni kutusaidia tu ili kubaini mawazo.

Kutafasiri katika ngazi ya aya na sio sentesi, ibara,kifungu au ngazi ya neno ndio ufunguo katika kufuata maana ya mwandishi aliyokusudia. Aya zimejengwa kwenye mada iliyounganishwa pamoja, mara nyingi huitwa sentesi yenye dhamira au mada. Kila neno, kifungu, ibara na sentesi katika aya kwa kiasi fulani vinahusiana na dhamira iliyo pamoja. Aidha haya huweka ukomo, inapanua , kuieleza na/ au kuihoji. Maelekezo sahihi (ufunguo) kwa tafsiri sahihi ni kufuata wazo la mwandishi wa awali aya kwa aya kufuatana na fasihi binafsi ambayo inatengeneza Biblia nzima..Tafsiri hizi zimechaguliwa kwa sababu zinatumia nadharia mbalimbali za tafsiri.

1. Andiko la Kiyunani la United Bible Society ni rekebisho la chapisho la Nne la (UBS[4]). Andiko hili liliandikwa ki-aya na wasomi wa maandiko ya kisasa.

2. Toleo la New King James Version (NKJV) ni utafsiri wa fasihi wa neno kwa neno uliosimamia kwenye mapokeo ya machapisho ya Kiyunani yaliyojulikana kama “Upokeaji wa Maandishi”. Mgawanyo wa aya zake ni mrefu kuliko tafasiri zinginezo. Urefu wa aya hizi unamwezesha wasomi kuona mada zilizo pamoja.
3. Toleo la New Revised English Version(NRSV) ni tafsiri ya neno kwa neno lililoboreshwa. Inatengeneza pointi ya kati baina ya matoleo mawili ya kisasa yanayofuata. Mgawanyo wa aya zake ni wa msaada mkubwa katika kubainisha masomo.
4. Toleo Today’s English Version(TEV) ni utafsiri sawia wenye nguvu uliyochapishwa na muungano wa vyama vya Biblia. Unajaribu kutafasiri Biblia kwa njia ya kumwezesha msomaji au mnenaji wa kiingereza cha kisasa kuelewa maana iliyomo katika andiko la Kigiriki. Mara nyingi, hasa hasa katika injili, inagawanya aya kufuatana na mnenaji hata kuliko somo lenyewe, sawa na NIV. Kwa kusudi la mtafasiri, hili halina msaada. Inapendeza kuona kuwa vitabu vya UBS[4] na TEV vimechapishwa na mtu yule yule lakini aya zake zinatofautiana.
5. The Jerusalem Bible(JB) ni tafsiri sawia yenye mlinganyo wa nguvu iliyosimamia kwenye tafasiri ya Katoriki ya Ufaransa. Ni nzuri mno katika kufanya ulinganifu wa aya kutoka katika mtizamo wa ki-Ulaya.
6. Chapisho la andiko ni uboreshaji wa mwaka 1995 wa toleo la Biblia New American Standard Bible (NASB) ambalo ni tafasili ya neno kwa neno. Pia maoni ya mstari kwa mstari yanafuata aya hizi.

## KANUNI YA TATU

Kanuni ya tatu ni kusoma Biblia tofauti tofauti ili kupata uwezekano mpana wa maana (somo la maana ya maneno) kwamba maneno ya Kibiblia au vifungu yanaweza kuwa nayo. Daima, neno au fungu la maneno katika Kiyunani yanaweza kueleweka kwa njia mbalimbali. Tafsiri hizi tofauti husaidia kubaini na kuelezea utofauti uliopo katika maandiko ya awali ya Kiyunani. Lakini haya hayaathiri mafundisho, bali husaidia katika kujaribu kurejelea maandiko asili yaliyoandikwa na mwandishi wa kwanza aliyevuviwa.

Fasiri hii humpa mwanafunzi njia ya haraka ya kuchunguza fasiri zake. Hii haina maana kuwa ni ya kumalizia, bali ni ya utoaji taarifa na udadisi kimawazo. Mara nyingi tafsiri nyingine hutusaidia tusiwe ving’ang’anizi na wafinyu wa mawazo na mapokeo ya kimadhehebu. Watafasili wanapaswa kuwa na upana mkubwa wa kuelewa tafsiri tofauti tofauti na kuweza kubaini ni kwa ugumu upi maandiko ya kale yanaweza kuwa. Inashangaza kuona ni kwa kiasi kidogo kilioje cha makubaliano yaliopo kati ya Wakristo ambao wanadai kuamini biblia kama chanzo chao pekee cha ukweli. Kanuni hizi zimenisaidia kushinda hali yangu ya kufungwa kihistoria na kunifanya nipambane na maandiko ya zama hizo. Ni matumaini yangu kuwa kanuni hizi zitakuwa za Baraka kwako.

Bob Utley
June 27, 1 996
Haki Miliki © 2013 Bible Lessons International

# MWONGOZO KWA USOMAJI MZURI WA BIBLIA:

# UTAFITI BINAFSI KWA UKWELI ULIOTHIBITIKA

Kinachofuata ni maelezo mafupi ya Dr. Bob Utley mwana falsafa wa kanuni za ufasili na njia alizotumia katika fasihi yake.

Tunaweza kuufahamu ukweli? Unapatikana wapi? Tunaweza kuuthibitisha kimantiki? Kweli, kuna mamlaka ya kimsingi? Kuna imani kamili inayoweza kulinda maisha yetu, na ulimwengu wetu tuliomo? Kuna maana yeyote katika maisha? Kwa nini tuko hapa? Tunakwenda wapi? Maswali haya yanauliza kwa watu wote wenye tafakuri zenye uwiano—wameyatawala maarifa ya binadamu tangu mwanzoni mwa nyakati (Mhu. 1:13-18; 3:9-11). Naweza kukumbuka utafiti wangu binafsi kwa ajili ya ungamanisho la maisha yangu. Nimekuwa mwamini katika Kristo kwenye umri mdogo, awali kabisa nikizingatia juu ya ushahidi wa watu wengine muhimu kwenye familia yangu. Nilivyokuwa kufikia utu uzima, maswali juu yangu na ulimwengu ninamoishi ulivyokuwa.Tamaduni za kawaida na dini hazikuleta maana yeyote kwenye uzoefu niliousoma au kukutana nao. Ulikuwa ni muda wa kuchanganyikiwa, kutafuta, kutamani, na mara nyingi fikra zisizokuwa na tumaini katika uso wa ulimwengu mgumu, usiojali nilimoishi.

Wengi walidai kuwa na majibu kwa maswali haya ya msingi, lakini baada ya utafiti na kufikiri nikapata majibu yao yamelenga juu ya (1) falsafa binafsi, (2) hadithi za kubuniwa za kale, (3) uzoefu binafsi, au (4) Saikolojia zilizojichomoza. Nilihitaji digrii fulani ya uthibitisho, baadhi ya vielelezo, kiasi cha busara ambamo ningelenga mtazamo wangu wa kidunia, kiini cha uzima wangu, sababu yangu ya kuishi.

Niliyapata haya katika usomaji wangu wa biblia. Nilianza kutafuta ushahidi wa udhamini niliopata katika (1) utegemezi wa historia ya biblia kama ulivyothibitishwa na elimu kale, (2) usahihi wa Nabii za Agano la Kale, (3) umoja wa jumbe za Biblia zaidi ya miaka 1600 ya kutolewa kwake na (4) shuhuda binafsi za watu ambao maisha yao yalibadilika moja kwa moja baada ya kusoma biblia. Ukristo, kama mfumo wa imani na kuamini uliounganishwa, una uweo wa kukabiliana na maswali magumu ya maisha ya mwanadamu. Siyo haya tu yanaweza kutoa muundo kazi, lakini mwelekeo unaotokana na uzoefu wa imani za kibiblia uliniletea furaha zenye hisia na ustahimili.

Nilijiridhisha ya kuwa nimepata kiini cha uzima wa maisha yangu—Kristo, kama ninavyoelewa kupitia maandiko.Ulikuwa ni uzoefu mgumu, msukumo wenye kuweka huru. Ingawa, naweza kukumbuka mshituko na maumivu yalipoanza kunifahamisha juu ya tafasiri ngapi tofauti ya kitabu hiki zimetetewa, wakati mwingine hata ndani ya makanisa hayo ya aina moja. Nikithibitisha mwongozo wa Ki-Mungu na uaminifu wa biblia haukuwa mwisho, lakini ni mwanzo pekee. Ni kwa vipi naweza kuthibitisha au kukataa tafsiri zinazotofautiana na kugongana za kurasa nyingi ngumu ndani ya maandiko kwa wale waliokuwa wakidai mamlaka yake na uaminifu?

Kazi hii imekuwa lengo la maisha yangu na hija ya imani. Nilifahamu ya kuwa imani katika Kristo imeniletea furaha na amani kubwa. Mawazo yangu yametamani baadhi ya imani kamili katikati ya nadharia ya utamaduni wangu na mfumo wa imani gonganishi wa dini na majivuno ya kimadhehebu. Katika utafiti wangu wa mitazamo halali kwenye utafsiri wa fasihi ya kale, nilishangaa kuvumbua historia yangu, ya kitamaduni, ya kimadhehebu na uzoefu wa kipendeleo. Kwa kawaida kabisa, mara nyingi, nimesoma Biblia ili kuimarisha mtizamo wangu. Nimeutumia kama chanzo cha mfumo wa imani kuvamia imani nyingine wakati nikijihakikishia usalama wangu na utoshelevu. Ni kwa namna gani utambuzi wa maumivu haya yalikuwa kwangu!

Ingawa siwezi kuwa kipingamizi moja kwa moja, naweza kuwa msomaji mzuri wa biblia. Naweza kuweka ukomo wa upendeleo kwa kutambua na kukubali uwepo wao. Sijawaweka huru,lakini nimeukabiri udhaifu wangu. Mtafsiri mara nyingi ndio adui mbaya wa usomaji mzuri wa biblia! Ngoja nitaje baadhi ya dhanio nilizoleta kwenye usomaji wa biblia ili, msomaji, aweze kuzichunguza pamoja nami:

# I. DHANIO


1. Ninaamini biblia ni uvuvio wa ki-pekee wa ufunuo binafsi wa Mungu mmoja na aliye wa kweli. Kwa hiyo, ni lazima itafsiriwe katika mwanga wa kusudi la Ki-Ungu la mwandishi wa mwanzo (yaani Roho) kupitia mwandishi wa kibinadamu katika muundo wa historia uliokusudiwa.
   - Wapokeaji wa mwanzo
   - Ujumbe ulioandikwa
   - Kusudi la mwandishi wa mwanzo
2. Ninaamini biblia iliandikwa kwa ajili ya mtu wa kawaida—kwa watu wote! Mungu alilazimika mwenyewe kuongea kwetu waziwazi kupitia historia na tamaduni zilizomo. Mungu hakuuficha ukweli, anatutaka sisi kuelewa! Kwa hiyo, inalazimika kutafsiriwa katika (uwazi) katika siku hizo, na siku hizi tulizomo. Biblia haitakiwi kumaanisha kwetu yale ambayo hayakumaanisha kwa wale wa mwanzo walioisoma au kuisikia. Inaeleweka kwa wastani wa mawazo ya kibinadamu na kutumia aina ya njeo mbadala za kawaida za mawasiliano ya ki-binadamu.
3. Ninaamini Biblia inakusudi na ujumbe uliowekwa pamoja. Haina mkanganyiko ndani yake, ingawa inajumuisha (njia ngumu na zinazokinzana). Hivyo basi, mtafsiri mzuri wa biblia ni biblia yenyewe.
4. Ninaamini kwa kila kurasa (pasipo kujumuisha unabii) ina maana moja iliyosimama kwenye kusudi la mwanzo la mwaandishi aliyevuviwa. Ingawa hatuwezi kutia shaka kutambua kusudi la mwandishi wa mwanzo, viashirio vingi daima vimeelekeza katika uelekeo wake;
   a. Aina ya fasihi tanzu uliochaguliwa kuelezea ujumbe
   b. Mtindo wa kihistoria na/au muda maalumu ulioshawishi maandiko kuandikwa
   c. Muundo wa fasihi wa kitabu husika pamoja na kila fasihi moja
   d. Muundo wa maandishi (elezewa kwa fasaha) wa fasihi moja kama zinavyo husiana na ujumbe
   e. Umbo la kisarufi husika lililowekwa kuwasilisha ujumbe
   f. Maana zilizochaguliwa kuwakilisha ujumbe

Mafunzo ya kila eneo hili liwe chanzo cha mafunzo yetu katika aya. Kabla sijaelezea njia zangu za usomaji mzuri wa biblia, hebu nielezee angalau njia zisizosahihi zinazotumiwa siku hizi zilizopelekea kuwepo kwa tafsiri tofauti nyingi na hivyo basi zinatakiwa kuepukika.


# II. Mbinu zisizofaa

1. Kutojali mazingira ya fasihi ya vitabu vya Biblia na kutumia kila sentesi, ibara, au maneno binafsi kama maelezo ya kweli yasiyohusiana na kusudi la mwandishi wa mwanzo au mtindo mpana. Hii mara nyingi huitwa “uhakiki wa andiko”
2. Kutoujali muundo wa ki-hisoria wa vitabu kwa kubadilisha muundo wa ki-historia unaodhaniwa kuwa ni mdogo au usiosaidika kutoka kwenye andiko lenyewe.
3. Kutojali muundo wa kihistoria wa vitabu na kusoma kama gazeti la mtaani lililoandikwa asili kwa wakristo binafsi wa kisasa.
4. Kuupa muundo wa kihistoria wa vitabu kwa kuliistiari andiko ndani ya ujumbe wa falsafa/theolojia isioendana na wasikiaji wa kwanza na kusudi la mwandishi wa mwanzo.
5. Kutojali muundo wa mwanzo kwa kubadilisha mtindo wa theolojia ya mtu, mafundisho yanayopendeka, au mambo ya kisasa yasiyoendana na kusudi la mwandishi wa mwanzo na ujumbe uliotolewa. Tabia hii mara nyingi hufuata usomaji wa mwanzo wa biblia kama kigezo cha kuanzisha mamlaka ya mnenaji. Hii mara nyingi hurejewa kama “mwitikio wa msomaji” (utafsiri wa-andiko-lililomaanisha-kwangu). Kwa wastani, vitu vitatu vinavyoendana vinaweza kupatikana katika mawasiliano ya binadamu yalioandikwa.

| Kusudi la Mwandishi | | Andiko lililoandikwa | | Wapokeaji wa |
|---|---|---|---|---|




Siku za nyuma, mbinu tofauti za usomaji zimenitazamisha juu ya moja kati ya vitu vitatu. Lakini kweli tunatamka kwa dhati uhuisho wa Biblia wa kipekee na mchora uliofanyiwa mabadiliko unaofaa zaidi:




Kwa kweli vitu hivi nyote vitatu lazima vijumulishwe katika mchakato wa ufasiri. Kwa kusudi la uthibitisho, ufasiri wangu unalenga juu ya moja kati ya vitu viwili: mwandishi wa mwanzo na maandiko. Ninayamkinika kujibu matusi mabaya niliyoyachunguza (1) shutumu au kutakasa maandiko na (2) tafasili ya "mwitikio wa msomaji" (unamaanishwa nini kwangu).Matusi yanaweza kutokea katika kila hatua. Ni lazima kila mara tuchunguze mienendo yetu, upendeleo wetu, mbinu na matumizi. Lakini ni kwa jinsi gani tunaweza kuyachunguza kama hapatakuwepo na mipaka ya ufasihi, ukomo au kigezo? Hapa ni pale kusudi la mwandishi na muundo wa maandiko yaliponipa baadhi ya vigezo kuzuia maeneo ya fasiri zilizo halali. Katika kuangazia hizi mbinu za usomaji zisizofaa, zipi ni baadhi ya mitazamo mizuri ya usomaji mzuri wa biblia ambao unatoa digri ya uthibitisho na misimamo?

## III. Mitazamo inayofaa katika usomaji mzuri wa Biblia

Katika hatua hii sijadili mbinu pekee za ufasiri wa namna mahususi lakini kwa pamoja kanuni halali kwa aina yote ya maandiko ya kibiblia. Kitabu kizuri kwa namna ya mitazamo mahususi ni *How To Read The Bible For All Its Worth*, ya Gordon Fee na Douglas Stuart, kilichochapishwa na Zondervan.

Utaratibu wangu mwanzoni ulinitizamisha juu ya msomaji aliyemruhusu Roho Mtakatifu kuangaza biblia kupitia kwa miduara minne ya usomaji binafsi. Hii inamfanya Roho, andiko na msomaji wawe kiwango cha mwanzo, na siyo cha juu. Vile vile hii inamlinda msomaji kutokuwa na mwanya wa kushawishiwa na mtoa maoni. Nimesikia ikisemwa: "Biblia inaangazia zaidi katika fasihi". Hii haimaanishi kukashifu maoni juu ya msaada wa usomaji lakini ni ombi kwa muda unaofaa kwa matumizi yao. Tunalazimika kuusaidia ufasiri wetu kutoka katika andiko lenyewe. Maeneo matatu yanatoa angalau ukomo wa uthibitisho:

1. muundo wa kihistoria
2. mazingira ya fasihi
3. muundo wa kisarufi (vipashio)
4. matumizi ya maneno ya kisasa
5. milango muhimu iliyo sambamba
6. namna tanzu ya uwasilishaji

   Tunahitajika kuweza kutoa sababu na mantiki zilizo nyuma ya ufasii wetu. Biblia ndiyo chanzo pekee cha imani yetu na mazoezi. Kwa huzuni, mara nyingi wakristo hawakubali juu ya kile kinachofundishwa au kukiri. Ni kushindwa kudai uhuisho juu ya Biblia na kupelekea waamini washindwe kukubali juu ya kile kinachofundishwa na kutakiwa! Miduara mine ya usomaji imeundwa kutupatia utambuzi wa ufasili ufuatao:

### 1. Mzunguko wa kwanza wa usomaji

a. Soma kitabu katika mkao mmoja. Soma tena katika fasili tofauti , kwa matumaini kutoka katika fasili tofauti za nadharia

    1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
    2) Mlinganyo wenye nguvu (TEV, JB)
    3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
  b. Angalia kiini cha kusudi la uandishi mzima. Tambua dhamira yake.
  c. Tenga (ikiwezekana) fasihi moja, sura, ibara au sentesi inayoelezea waziwazi Kiini cha kusudi au dhamira
  d. Tambua fasihi tanzu yenye nguvu
    1) Agano la kale
      a) Simulizi za waebrania
      b) Mashairi ya waebrania (fasihi za hekima, zaburi)
      c) Unabii wa ki-Ebrania (lugha ya mjazo, shairi)
      d) Alama za siri za ki-sheria
    2) Agano jipya
      a) Simulizi (Injili, matendo)
      b) Hadithi za mafumbo (Injili)
      c) Barua/nyaraka
      d) Fasihi za mafunuo

## 2. Mzunguko wa pili wa usomaji

a. Soma kitabu kizima tena, ukitafuta kufahamu mada muhimu au masomo.
b. Elezea kwa muhtasari wa mada muhimu na elezea kwa kifupi yaliomo kwa maelezo rahisi
c. Angalia kusudi la maelezo yako na eleza kwa mapana kwa msaada wa usomaji.

## 3. Mzunguko wa tatu wa usomaji.

a. Soma tena kitabu kizima, ukitafuta kutambua muundo wa ki-historia na Matukio lengwa kwa ajili ya uandishi kutoka katika kitabu cha Biblia yenyewe.
b. Taja vipengele vya ki-historia ambavyo vinatajwa katika kitabu cha Biblia.
  1) Mwandishi
  2) Tarehe
  3) Wapokeaji
  4) Kusudu mahsusi la uandishi
  5) Mwelekeo muundo wa kitamaduni unaorandana na kusudi la mwandishi
  6) Marejeo toka kwenye matukio na watu wa kihistoria/ kale
c. Panua maelezo yako kwa kiwango cha aya kutoka katika sehemu ya kitabu cha biblia unayotafasiri. Mara nyingi tambua na kuelezea fasihi. Inaweza kuwa na vifungu na aya nyingi. Hii inakuwezesha wewe kufuata wazo na muundo wa maandiko ya mwandishi wa mwanzo.
d. Angalia muundo wako wa kihistoria kwa kutumia msaada wa usomaji

## 4. Mzunguko wa nne wa usomaji

a. Soma tena bayana fasihi moja katika tafasiri nyinginezo nyingi
  1) Neno kwa neno (NKJV, NASB, NRSV)
  2) Mwenendo linganifu (TEV, JB)
  3) Ufafanuzi (Living Bible, Amplified Bible)
b. Angalia fahisi au muundo wa kisarufi
  1) Misemo ya kujirudia Waefeso.1:6, 12, 14
  2) Muundo wa kisarufi unaojirudia Warumi 8:31
  3) Mbinyo wa mawazo (dhana zinazoafikiana)
c. Taja vipengele vifuatavyo:-
  1) Istilahi muhimu
  2) Istahili zisizo za kawaida
  3) Muundo muhimu wa kisarufi
  4) Maneno magumu, ibara, na sentesi
d. Angalia njia muhimu zilizosambamba

1) Angalia njia za wazi za ufundishaji kwenye somo lako kwa kutumia
    a) Vitabu vya thiolojia
    b) Biblia za marejeo
    c) Itifaki
2) Angalia maneno mawili yanayokinzana katika somo lako. Kweli nyingi za ki-Biblia zinatolewa katika rahaja mbili zinazofanana. Migongano mingi ya ki-madhehebu hutokea kutokana na uthibitisho nusu wa maandiko ya Biblia. Biblia zote zimevuviwa. Ni lazima tutafute ujumbe mzima ili kutoa mlinganyo wa ki-maandiko katika tafasiri zetu.
3) Angalia milinganisho ndani ya kitabu, kile kile, mwandishi Yule Yule, au namna ileile, Biblia ina mfasiri wake mzuri kwa sababu ina mwandishi mmoja ambaye ni Roho Mtakatifu.

e. Tumia misaada ya kusoma kuangalia uchunguzi wako wa muundo wa kihistoria na tukio.
    1) Soma biblia
    2) Ensaikolopidia za biblia, vitabu vya mkononi na kamusi
    3) Tangulizi za biblia
    4) Fasihi za biblia (katika hatua hii kwenye usomaji wako ruhusu jamii ya waamini, waliopita na waliopo, kusaidia na kusahihisha usomaji wako binafsi)

## IV. Matumizi ya utafasiri wa Biblia.

Katika hatua hii tunageukia matumizi, umechukua muda kuelewa andiko katika muundo wake, sasa lazima utumie katika maisha yako, utamaduni wako, na elezea mamlaka ya Ki-biblia kama "uelewa ule mwandishi wa ki-biblia wa mwanzo alivyosema katika zama zake na kutumia ukweli huo katika zama hizi". Matumizi lazima yafuate utafasiri wa kusudi la mwandishi wa mwanzo katika muda na mantiki.

Hatuwezi kutumia njia ya Biblia katika zama zetu mpaka pale tutakapo fahamu kile alichokuwa akikisema katika zama hizo. Njia ya Biblia isimaanishe kile asicho kimaanisha!
Maelezo yako kwa kirefu, kwa kiwango cha aya (mzunguko wa usomaji≠3) yatakuwa mwongozo wako. Matumizi lazima yafanyike katika kiwango cha aya, na sio kiwango cha neno, maneno yana maana pekee katika mazingira, ibara zina maana pekee katika mazingira na sentensi zina maana pekee katika mazingira. Mtu pekee aliyevuviwa ambaye amejumuishwa katika mchakato wa utafsiri ni mwandishi wa mwanzo. Kipekee unafuata utangulizi wake kwa mwanga wa Roho Mtakatifu. Lakini nuru sio uvuvio. Kusema "asema Bwana"lazima, tufungamane na kusudi la mwandishi wa mwanzo. Matumizi lazima yaendane bayana na kusudi lote la uandishi mzima, maandishi bayana, na muendelezo wa kiwango cha aya.

Usiruhusu mambo ya zama hizi yatafasiri Biblia, iruhusu Biblia ijiongee yenyewe. Hii itatuhitaji kuvuta kanuni kutoka kwenye andiko. Hii itakubalika kama andiko litaiwezesha kanuni. Bahati mbaya wakati mwingi kanuni zetu ni "zetu" na si kanuni za ki-maandiko.

Katika kutumia Bibilia, ni muhimu kukumbuka kuwa (isipokuwa katika unabii) maana moja na moja pekee itakubalika kwa andiko la Kibiblia pekee. Maana hiyo iendane na kusudi la mwandishi wa mwanzo kama alivyo eleza tatizo au hitaji katika zama zake. Mengi ya matumizi yanayowezekana yanaweza kutolewa kutoka katika maana hii moja. Matumizi yatategemea mahitaji ya wapokeaji lakini ni lazima yaendane na maana ya mwandishi wa mwanzo.

## V. Sura ya utafasiri wa kiroho.

Zaidi ya hapo nimejadili mantiki na mchakato wa ki-maandiko uliojumuishwa kwenye utafasiri na matumizi. Sasa ngoja nijadili kwa kinaga ubaga mwelekeo wa kiroho wa utafasiri. Mfuatano ufuatao umekuwa wa msaada sana kwangu.

1. Omba kwa ajili ya msaada wa Roho (kama vile 1Kor. 1:26-2:16)

2. Omba kwa ajili ya msaada binafsi na kusafishwa kutoka katika dhambi inayojulikana (kama vile 1 Yohana 1:9)
3. Omba kwa ajili ya hamu kubwa ya kumjua Mungu (kama vile Zab. 19:7-14, 42:1, 119:1)
4. Tumia utambuzi wowote mpya mara moja katika maisha yako.
5. Baki mnyenyekevu na anayefundishika.

Ni vigumu kuweka mlinganyo kati ya mchakato wa kimantiki na uongozi wa kiroho wa Roho Mtakatifu. Dondoo zifuatazo zimesaidia kulinganisha hizi mbili:

1. Kutoka kwa mwandishi James W.Sire, *scripture twisting*,kr. 17-18
   "Nuru huja kwenye mawazo ya watu wa Mungu na sio tabaka la watu wa kiroho. Hakuna daraja la ualimu katika ukristo wa kibiblia. Hakuna kuongoza, hapana mtu awaye yote ambaye tafsiri zote nzuri zitoke kwake. Na hivyo, wakati roho mtakatifu anatoa karama maalumu ya hekima, maarifa na utambuzi wa kiroho huwa pamoja. Hakutoa hizi kwa wakristo waliokirimiwa kuwa wao ndo pekee watafsiri wenye mamlaka ya Neno lake. Ni juu ya kila watu wake kujifunza, kuamua na kutambua kwa kufanya marejeo kwenye Biblia ambayo inasimama kama yenye mamlaka hata kwa wale ambao Mungu amewapa uwezo pekee. Kwa kufupisha, wazo mnalofanya kupitia kitabu kizima ni kuwa Biblia ni ufunuo wa kweli wa Mungu kwa watu wote, ya kuwa ni mamlaka yetu ya mwisho katika mambo yote ambayo inayaongelea, kuwa sio fumbo lote lakini inaweza kueleweka vya kutosha na watu wa kawaida kwa kila tamaduni."
2. Juu ya Kierkegaard, inayopatikana toka kwa Benard Ramm, *Protestant Biblical Interpretation (tafsiri ya biblia ya ki-protestanti*) Uk.75:
   Kutokana na Kierkegaard, kisarufi, misamiati na usomaji wa kihistoria wa Biblia ulikuwa ni muhimu lakini utangulizi wa usomaji wa kweli wa Biblia na kusoma Biblia kama neno la Mungu mmoja lazima alisome kwa moyo wake wote mdomoni mwake, kutoka ncha ya kidole, na shauku ya matarajio katika mazungumzo na Mungu. Usomaji wa Biblia pasipo tafakari, kutojali au kielimu, au weledi sio usomaji wa Biblia kama neno la Mungu, kama mmojawapo asomavyo barua ya mapenzi isemavyo, tena mmoja asoma kama neno la Mungu.
3. H.H Rawley katika *The Relevance of the Bible*, Uk.19:
   Hakuna uelewa mdogo wa kisomi wa Biblia, ingawa yote, inaweza kumiliki hazina yote. Haidharau uelewa huo, kwa kuwa ni muhimu kwa uelewa wote. Lakini ni lazima iongeze uelewa wa kiroho wa hazina ya kiroho ya kitabu hiki kwa ujumla. Kwa huo uelewa wa kiroho kitu fulani ambacho ni zaidi ya hadhari ya kiroho ni muhimu. Mambo ya kiroho ni utambuzi wa kiroho, na wanafunzi wa Biblia wanahitaji fikra za upokeaji wa kiroho. Ile hamu ya kumtafuta Mungu ambayo inaweza kumsababisha ajitoe kwake. Ni kama kupita zaidi ya usomaji wa kisayansi kuingia kwenye urithi wa utajiri wa hiki kitabu kikubwa kuliko vyote.

## VI. Njia hizi za Fasiri

*Study Guide Commentary (Mwongozo wa usomaji) wa* fasihi umeundwa kusaidia njia zako za utafsiri katika njia zifuatazo:

1. Maelezo fasaha ya kihistoria yanayotambulisha kila kitabu baada ya kufanya "mduara wa usomaji #3" angalia taarifa hizi.
2. Utambuzi wa ki-mazingira unapatikana katika kila kurasa. Hii itakusaidia kuona jinsi gani maandishi/fasihi imeundwa.
3. Katika kila mwanzo wa kifungu au fasihi kubwa inaunganisha mgawawanyo wa aya na maelezo ya kichwa cha makala yanatolewa kutoka katika tafsiri za kisasa.
   a. United Bible Society Greek Text.Toleo la nne lililobadilishwa (UBC)
   b. The New American Standard Bible 1995 ya kisasa (NASB)
   c. The New King James Version (NKJV)
   d. The New Revised Standard Version (NRSV)
   e. Today's English Version (TEV)
   f. The Jerusalem Bible (JB)

Aya zilizogawanywa hazikuvuviwa. Lazima ziyakinishwe kutoka katika mazingira fulani. Kwa kulinganisha tafsiri nyingi za kisasa kutoka tafsiri nyingi za ki-nadharia na mitizamo ya kitheolojia, tunaweza kuchanganua muundo

unaokusudiwa wa mawazo ya mwandishi wa mwanzo, kwani kila aya ina ukweli mmoja mkubwa. Huu uliitwa "mada ya sentensi" au wazo la kati la andiko, hilo wazo lililounganishwa ni ufunguo kwa tafsiri nzuri ya kihistoria na kisarufi. Mmojawapo asitafsiri, kuhubiri au kufundisha chini ya aya, vilevile ukumbuke ya kuwa kila aya inahusiana na aya zingine. Hii ndo maana kiwango cha aya kinachoelezea kitabu kizima ni muhimu. Ni lazima tuweze kufuata mtiririko wa kimantiki wa somo lililotolewa na mwandishi wa mwanzo aliyevuviwa.

4. Muhtasari wa Bob unafuata mtazamo wa kifungu kwa kifungu kwa utafsiri wake. Hii inatulazimisha kufuata mawazo ya mwandishi wa mwanzo. Muhtasari unatoa habari kutoka sehemu nyingi.
    a. Mazingira ya fasihi
    b. Utambuzi wa kihistoria na tamaduni
    c. Habari za kisarufi
    d. Usomaji wa neno
    e. Njia muhimu zilizo sambamba
5. Mahali fulani katika fasihi, andiko lililochapishwa toka toleo jipya la Marekani (1995 mpaka sasa hivi) litaongezewa na tafsiri za matoleo mbalimbali ya kisasa.
    a. New King James Version (NKJV) ambayo unafuata mswaada wa "Upokeaji wa Maandiko halisi".
    b. The New Revised Standard Version (NRSV) ambayo ni rudio la neno-kwa-neno Kutoka katika Umoja makanisa asili ya Revised Standard Version
    c. The Today's English Version (TEV) ambayo ni tafsiri ya mlinganyo wa nguvu Kutoka American Bible Society.
    d. The Jerusalem Bible (JB) ambayo ni tafsiri ya Kiingereza inayotegemea kutoka tafsiri ya Mlinganyo wa nguvu wa Katoriki ya Ufaransa.
6. Kwa wale wote ambao hawasomi ki-giriki, ukilinganisha na tafsiri za kiingereza inaweza kusaidia kutambua matatizo katika andiko:
    a. Tofauti za mswada
    b. Maana ya maneno mbadala
    c. Muundo na maandiko magumu ya kisarufi Ingawa tafsiri za kiingereza haziwezi kuleta suluhu kwenye matatizo hayo yanayalenga kama sehemu ya ndani na usomaji kamili.
    d. Karibia kila kifungu, maswali muhimu ya majadiliano yanatolewa ambayo yanajaribu kulenga maswala muhimu ya utafsiri wa kifungu hicho

# MAELEZO YA UFUNGUZI JUU YA USOMAJI WA MWANZO 1-11

A. Ni namna gani Mwanzo 1-11 inahusiana na sayansi ya sasa ya kimagharibi?
   1. Moja kwa moja vinapingana
   2. Makubaliano ya moja kwa moja
   3. Hoja za ufanano

   Sayansi ni njia ya utafiti. Ni tabia ya kisasa lakini kila mara inabadilika kwa uelewa wa maarifa mapya. Mungu kama muumbaji na Mungu kama mwokozi anashikiliwa na "vitabu viwili," asilia (mafunuo ya kiasili, kama vile Zab. 19:1-6) na maandiko (mafunuo maalum, kama vile Zab. 19:7-11). Mungu aliyaandika yote! Hawakukubaliana nayo!

B. Ni kwa namna gani Mwanzo 1-11 inahusiana na historia ya sasa?
   1. Uwasilishaji wa fasihi ya Kimashariki na Kimagharibi ni tofauti. Sio kweli au uongo, sio sawa au kosa, lakini ni tofauti. Mwanzo 1-11 ni historia ya mwanzo. Ni ya muhimu kithiolojia, lakini kwa kiasi Fulani imefichwa (habari sahihi ya fasihi). Imefichwa katika uwasilishaji wa fasihi, imefichwa katika tamthilia za kihistoria, imefichwa kama ni mwisho wa historia (yaani ufunuo)
   2. Ukristo, kama ilivyo dini ya Kiyahudi, ni dini iliyojikita kihistoria. Inasimama au kuanguka juu ya matukio ya kihistoria. Hata hivyo, baadhi ya matukio (yaani., Mwanzo 1-11) yako zaidi ya uwezo wetu wa kuyakabili, kwa hiyo yanawasilishwa kwa namna ambayo mwanadamu anaweza kuielewa (yaani fadhili). Hii haiko kwa namna yeyote kukana uaminifu wao, bali ni kusisitiza kusudio lao la kithiolojia. Biblia inachagua kutazama sio tu kwenye uumbaji, bali kwenye kuumba tena(ukombozi)
   3. Mwanzo imewekwa ndani ya muda wa marejeo "kihistoria." Tunaweza kuweka kumbukumbu za viunganishi vya wazi kwenye mwanzo wa historia ya kiulimwengu kwa sura ya 12 (yaani vibao vya kuandikia Nuzi na Mari). Ingawa, sura 1-3 ni zaidi ya uthibitisho wa kihistoria na kutambua namna ya uwasilishaji.

C. Ni kwa namna gani Mwanzo 1-11 inahusiana na fasihi?
   1. Kuna ufanano mwingi wa sura ya 1-2, 3 na 6-9 kutoka vyanzo vya huko Mesopotamia. Mara nyingi misamiati, maelezo, na habari zinafanana. Hata hivyo, watu wenye imani ya Mungu mmoja ndani ya Biblia na utu wa mwanadamu ni wa kipekee.
   2. Kuna angalau hatari mbili katika kuikabili Biblia kama fasihi.
      a. Kama fasihi ni ya kubuniwa, moja kwa moja isio historia
      b. Kama fasihi ni halisi, hakuna lugha jumuishi, hakuna uwasilishaji wa kimashariki, hakuna matukio ya kitamthilia.

      Mungu amejidhihilisha mwenyewe kwa wakati maalum na tamaduni akitumia lugha ya binadamu (yaani, sitiari, ufanano, na ukanushaji). Ni kweli na amini, lakini haichoshi.
   3. Uumbaji ni ukweli wa mafunuo endelevu. Mwanzo 1-2 ndio msingi, lakini Zaburi na Agano Jipya ni vya muhimu kwa mtazamo ulio mzuri. Kila kimoja kati ya vyanzo vitatu kinaongeza kwenye uelewa wa kithiolojia wa namna na kusudi la uumbaji .

D. Kwa namna gani tunaitafasiri Mwanzo 1-11?
   1. Namna gani ilianza na namna gani itaisha hilo limefichika (Mwanzo 1-11 na Ufunuo, yaani tunaona giza kupitia kwenye glasi)
   2. Tuna kweli yote ya kutusababisha kujongea mbele za Mungu na kuielewa Biblia. lakini, hatuna kweli za kuchosha , halisi, na zilizo kamili. Tuna uchaguzi wa kithiolojia na matukio yaliyo fasiriwa.
   3. Lazima tuiangalie Mwanzo 1-11 kupitia
      a. Uwasilishaji wa fasihi
      b. Misisitizo ya kithiolojia
      c. Matukio ya kihistoria
      d. Sayansi ya Magharibi ya sasa/ tamaduni/upendeleo
   4. Wanadamu walioanguka wote wanasimamia kwenye Biblia (yaani mafunuo ya Mungu) na wanahukumia kwayo. Ni zaidi ya uwezo wetu wa ufahamu, lakini yatupasa kukabiliana nayo ili kwamba tuweze kuitikia vizuri kwayo. Waamini wanaitafasiri tofauti (baadhi hairidhishi), lakini sote tunawajibika kwenye ukweli wanaouelewa. Inamdhihirisha Mungu; inadhihirisha uasi wa

mwanadamu; inathihirisha ukombozi wa ki-Ungu. Umilele wetu unahusiana na kweli hizi, sio maswali yanayohusi uumbaji wa namna gani na lini na matukio ya Mwanzo 1-11. Ndiyo msingi wa nani na kwa nini, ambayo ni ya muhimu.

Mungu tunaomba rehema yako (na amekwisha toa)!

# UTANGULIZI WA KITABU CHA MWANZO

I. JINA LA KITABU
   A. Katika Kiebrania(yaani andiko la Kimesoreti) ni neno la kwanza la kitabu, *bereshith*, "hapo mwanzo" au "kwa namna ya kuanza."
   B. Toka kwenye Biblia ya Kiyunani (yaani., tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiyunani), ni neno *Genesis,* lenye kumaanisha "mwanzo" au " asili," lililochukuliwa toka Mwa.2:4a. hiki chaweza kuwa ndiyo "kifungu chenye maelezo" cha jibu la mwandishi au wasifu wa mwandishi kuunganisha pamoja wasifu mbali mbali wa kithiolojia kama kikabari cha mwandishi wa Kibabeli alivyofanya. Jibu hili linaelezea kazi ya kifungu kama hitimisho, na sio utangulizi.

II. KUTAKATIFUZA
   A. Hiki ni kitabu cha mwanzo cha kipengele cha kwanza cha kanuni za kanisa la Kiebrania kiitwacho "sheria za Musa" au "mafundisho" au "sheria."
   B. Kipengele kwenye mafundisho ya kale ya Kiyunani kinajulikana kama "torati" (yaani., vitabu viatabu vya mwanzo).
   C. Wakati mwingine kinaitwa "Vitabu vitano vya Musa" katika Kiingereza.
   D. Kuanzia Mwanzo hadi Kumbukumbu la Torati ni habari mwendelezo ya (au iliyohaririwa na) Musa kuhusu uumbaji kupitia maisha ya Musa.

III. UWASILISHAJI-Kitabu cha Mwanzo kimsingi ni cha kithiolojia, simulizi za kihistoria lakini pia inajumuisha aina nyingine ya uwasilishaji wa fasihi:
   A. Tamthilia za kihistoria-mfano: 1:1-3
   B. Ushairi-mfano: 2:23; 4:2; 8:22
   C. Unabii-mfano: 3:15; 49:1na kuendelea(pia ni ya kiushairi)

IV. UANDISHI
   A. Biblia yenyewe haitaji jina la mwandishi (kama ilivyo kweli kwa vitabu vingi vya Agano la Kale). Kitabu cha Mwanzo hakina kipengele cha "Mimi"kama ilivyo kwa Ezra, Nehemia, au kipengele cha "sisi"kama Matendo ya Mitume. Hatimaye mwandishi ni Mungu!
   B. Tamaduni za Kiyahudi:
      1. Waandishi wa kale wa Kiyahudi wanasema Musa ndiye aliyekiandika:
         a. *Ecclesiasticus* na Ben Sirah, 24:23, kilichoandikwa yapata mwaka 185 K.K
         b. *Baba Bathra* 14b, sehemu ya sheria za Kiyahudi
         c. Filo wa Iskanderia, huko Misri, mwanafalsafa wa Kiyahudi, aliyeishi yapata mwaka 20 K.K hadi 42 B.K
      2. Huu ulikuwa ni ufunuo kwa Musa
         a. Musa anasemekana kuwaandikia watu:
            1) Kutoka 17:14
            2) Kutoka 24:4,7
            3) Kutoka 34:27,28
            4) Hesabu 33:2
            5) Kumbukumbu 31:9,22,24-26
         b. Mungu ameongea na watu kupitia Musa
            1) Kumbukumbu 5:4-5,22
            2) Kumbukumbu 6:1
            3) Kumbukumbu 10:1
         c. Musa ameongea na maneno ya sheria ya Mungu kwa watu:
            1) Kumbukumbu 1:1,3
            2) Kumbukumbu 5:1
            3) Kumbukumbu 27:1
            4) Kumbukumbu 29:2
            5) Kumbukumbu 31:1,30
            6) Kumbukumbu 32:44

7) Kumbukumbu 33:1

3. Waandishi wa Agano la Kale wanaliona kuwa ni la Musa
   a. Yoshua 8:31
   b. 2 Wafalme 14:6
   c. Ezra 6:18
   d. Nehemia 8:1; 13:1-2
   e. 2 Nyakati 25:4; 34:12;35:12
   f. Daniel 9:11
   g. Malaki 4:4

C. Tamaduni za Kikristo

1. Yesu anaziainisha nukuu toka sheria za Mungu kwenda kwa Musa
   a. Mathayo 8:4; 19:8
   b. Marko 1:44; 7:10; 10:5; 12:26
   c. Luka 5:14; 16:31; 20:37; 24:27,44
   d. Yohana 5:46-47; 7:19,23
2. Waandishi wengine wa Agano Jipya wanaainisha sheria ya Mungu kwenda kwa Musa:
   a. Luka 2:22
   b. Matendo 3:22; 13:39; 15:1, 15-21; 26:22; 28:23
   c. Warumi 10:5,19
   d. 1 Wakorintho 9:9
   e. 2 Wakorintho 3:15
   f. Waebrania 10:28
   g. Ufunuo 15:3
3. Wazee wa kanisa wa mwanzo walikubaliana na uandishi wa Musa. Hata hivyo, Ireneaus, Clement wa Iskanderia, Origen na Tertullian wote walikuwa na maswali kuhusu uhusiano wa Musa na muundo wa sasa wa sheria za kanisa wa kitabu cha Mwanzo (kama vile D.2. kwenye ukurasa wa 5)

D. Utaalamu wa sasa

1. Pamekuwepo na baadhi ya ongezeko la wazi la kiuhariri kwenye sheria ya Mungu( inavyoonekana, kuyafanya yale ya kale kuweza kueleweka zaidi kwa viongozi wa sasa, ambao ulibainishwa na waandishi wa ki-Misri)
   a. Mwanzo 12:6; 13:7; 14:14; 21:34; 32:32; 36:31; 47:11
   b. Kutoka 11:3; 16:36
   c. Hesabu 12:3; 13:22; 15:22-23; 21:14-15; 32:33na kuendelea
   d. Kumb. 3:14; 34:6
   e. Waandishi wa kale walikuwa ni watu wasomi walifundishwa sana. Mbinu zao, ingawa zilikuwa tofauti toka nchi na nchi.
      1) Huko Mesopotamia, walikuwa waangarifu kutobadilisha chochote, na hata waliweza kukagua kazi yao kwa ajili ya uhakiki zaidi. Hapa pana tanbihi ya kiuandishi wa kale wa Sumeria: “kazi ilikwisha kukamilishwa toka mwanzo hadi mwisho, imekwisha kunukuliwa, imepitiwa upya, imelinganishwa na kuthibitishwa alama kwa alama” toka yapata mwaka 1400 B k.k
      2) Huko Misri kwa uhuru kabisa wanayapitia upya maandiko ya kale wanayatengeneza upya kwa ajili ya viongozi wa sasa. Waandishi kwenye maeneo ya makumbusho ya kale (yaani., magombo ya bahari ya chumvi) walifuatisha mtizamo huu.
2. Wasomi wa karne ya 19 waliweka nadharia kuwa sheria ya Mungu muunganiko wa nyaraka toka vyanzo vingi kwa kipindi cha muda mrefu (Graff-Wellhausen). Nadharia hii ilisimamia juu ya:
   a. Majina tofauti ya Mungu
   b. Jozi za kufanana zinaoonekana katika andiko
   c. Habari za muundo wa fasihi
3. Vyanzo vinavyodhaniwa na tarehe:
   a. Chanzo cha herufi J (kilichotumika kwa YHWH huko Israel ya kusini)-mwaka 950 K.K

b. Chanzo cha herufi E (kilichotumika kwa jina *Elohim* huko Israeli ya Kaskazini)-mwaka 850 K.K
c. Muunganiko wa herufi JE- mwaka 750 k.k
d. Chanzo cha herufu D ("kitabu cha sheria," 2 Fal. 22:8, iliyogunduliwa kwenye mageuzi ya Yosia pindi wakilirekebisha hekalu ndipo penye kudhaniwa kitabu cha Kumbu kumbu la Torati, kilichoandikwa na kuhani asiyejulikana kwenye kipindi cha Yosia ili kuunga mkono mageuzi haya) - mwaka 621 K.K
e. Chanzo cha herufi P (uandishi wa kikuhani wa Agano la Kale, hasa ibada na taratibu) - 400 K.K
f. Pamekuwepo dhahiri ongezeko la kiuhariri kwenye sheria za Mungu. Wayahudi wanadai kuwa alikuwa
   1) Kuhani Mkuu (au mmoja wa wanafamilia) wakati wa uandishi
   2) Nabii Yeremia
   3) Mwandishi Ezra-Esdras IV anasema aliandika tena kwa sababu yale ya mwanzo yaliharibiwa kwenye anguko la Yerusalemu katika mwaka 586 K.K
g. Hata hivyo, nadharia ya J. E.D.P inasema zaidi kuhusu nadharia zetu za fasihi ya sasa na aina kuliko ushahidi toka kwa R. K. Harrison, *Introduction to the Old Testament,* kur. 495-541 na *Tyndale's Commentaries,* "Walawi" kur. 15-25).
h. Uainishaji wa fasihi ya Kiebrania
   1) Jozi ya kufanana, kama ilivyo Mwanzo 1 na 2, zinafahamika katika Kiebrania. Mara nyingi maelezo ya jumla yanatolewa, yakifuatiwa na habari maalum (amri kumi za Mungu na mfumo wa utakatifu). Hii imewezakuwa ni njia ya kusema ukweli.
   2) Walimu wa dini ya Kiyahudi wa kale walisema majina mawili ya kawaida ya Mungu yana umuhimu wa kithiolojia:
      a) YHWH - Jina la agano la Uungu kama linahusianishwa na Israel kama mkombozi na mwokozi (kama vile Zab. 19:7-14; 103)
      b) *Elohim* - Mungu kama muumbaji, Mpaji, na mwezeshaji wa maisha yetu hapa duniani (kama vile Zab. 19:1-6; 104).
      c) Maandishi mengine ya kale karibia na Mashariki ya Karibu wanatumia majina mbalimbali kuielezea miungu yao (kama vile *Encyclopedia of Bible Difficulties* by Gleason L. Archer, uk. 68).
   3) Ni fasihi isiyo ya kibiblia huko Mashariki ya Karibu kwa namna mbali mbali ya mitindo na misamiati kutokea katika kazi ya pamoja ya fasihi (kama vile *Introduction to the Old Testament*, R. K. Harrison, kur. 522-526).

E. Ushahidi toka kwa fasihi ya kale huko Mashariki ya Karibu unadokeza kuwa Musa alitumia nyaraka za kikabari zilizoandikwa au mtindo wa Mesopotamia (wa wazee wa kaya) wa mapokeo simulizi kuandika kitabu cha Mwanzo. Hili halina namna ya udokezaji wa kupunguza uvuvio bali ni jaribio la kutaka kuelezea tabia ya kifasihi ya kitabu cha Mwanzo (kama vile P. J. Wiseman's *New Discoveries in Babylonia about Genesis)*. Ukianzia Mwanzo 37, Mmisri aliyeonekana kusababisha mitindo, miundo, na misamiati anaonekana kumtaja Musa kuwa alitumia utengenezaji wa fasihi au mapokeo ya kusimuliwa toka nyakati za Waisraeli kwa wote Wamisri na watu wa Mesopotamia. Elimu rasmi ya Musa ilikuwa ni ya Kimisri! Uanzishwaji wa fasihi yenyewe ya Torati haujulikani. Ninaamini kuwa Musa ni mkusanyaji na mwandishi wa sehemu kubwa ya Torati, ingawa inawezakuwa aliwatumia waandishi na/au mapokeo ya kusimuliwa(wazee wa kaya) au kuandikwa. Maandiko yake yalirekebishwa baadaye na waadishi. Wanahistoria na wale waliokuwa waaminifu wa hivi vitabu vichache vya mwanzo wa Agano la Kale wamekwisha kuelezewa na wanaakiolojia wa sasa.

F. Kuna nadharia inayoibuka kuwa palikuwepo na waandishi (sehemu mbali mbali za Israel) wakifanyia kazi sehemu tofauti tofauti za Torati kwa wakati mmoja chini ya maongozi ya Samwel (kama vile I Sam. 10:25). Hii nadharia kwanza kabisa ilipangwa na E. Robertson's *The Old Testament Problem*.

V. TAREHE

A. Kitabu cha mwanzo kinaenea toka uumbaji wa ulimwengu mpaka kwenye familia ya Ibrahimu. Ni rahisi kuweka tarehe za maisha ya Ibrahim toka katika fasihi ya kiulimwengu ya kipindi hicho. Kadirio la tarehe lingalikuwa miaka 2000 K.K, karne ya pili K.K. msingi wa hili ni

1. Baba kutenda kama kuhani wa familia (kama Ayubu)
2. Maisha yalikuwa ya kuhamahama yakifuata makundi ya ng'ombe, mbuzi na kondoo
3. Kuhamahama watu wa Kisemiti wakati wa kipindi hiki

B. Matukio ya mwanzo ya kitabu cha Mwanzo 1-11 ni matukioa ya kweli ya kihistoria (yumkini ni tamthiria za kihistoria) lakini yasiyo wekewa kumbukumbu za tarehe kwa maarifa yanayopatikana sasa.
   1. Mimi mwenyewe nimekuja kukubaliana na umri wa dunia yapata miaka mabilioni (yaani., miaka 14.6 bilion kwa ajili ya ulimwengu na miaka bilioni 4.6 kwa ajili ya dunia, kama vile Hugh Ross' *The Genesis Question* and *Creation and Time*).
   2. Hata hivyo, bado naamini katika uumbaji maalum wa Adamu na Hawa ni wa kipindi kirefu. Inavyoonekana kwangu ni kuwa kitabu cha Mwanzo kinawekwa kwa namna ya muundo kazi wa "kihistoria," lakini dhana ya kihistoria haitambuliki sawasawa pale mwanzoni (yaani Mwa.1-3). Wana wa Adamu na Hawa walianza ustaraabu wa Mesopotamia (yaani., sura ya 4). Ikiwa muundo huu utazingatiwa hivyo Adamu na Hawa watakuwa wa kisasa (*homo sapien*) na sio yule wa kale asiyesitaarabika (*homo erectus*). Kama hili ni kweli basi pamekuwepo na mabadiliko ya maendeleo toka kwenye mafuvu ya kale (kama vile *Tyndale O T Commentaries*, "Mwanzo" cha Kidner and *Who Was Adam?* na Fazale Rana na Hugh Ross) pamoja na uumbaji maalum wa Mungu baada ya ule mwisho uliofanywa kwa wakati. Mie sijafurahi moja kwa moja na hili, bali ni kile kizuri ninachoweza kukifanya kwa uelewa wangu wa sasa wa Biblia na sayansi.

C. Lazima ikumbukwe ukiwa unasoma kitabu cha Mwanzo kuwa matukio ya kihistoria yamewekwa katika kumbukumbu na Musa ambaye aliwaongoza watu wa Mungu toka Misri kati ya (1) mwaka 1445 K.K, ikiangaliwa kwenye 1 Fal. 6:1; au (2) mwaka 1290 K.K, toka kwenye ushahidi wa wana elimukale. Kwa hiyo, huenda kwa simulizi za kimapokeo, vyanzo vingine visivyojulikana, au ufunuo wa moja kwa moja wa ki-Ungu, musa akayaandika "namna yote yalivyoanza" akitazamisha juu ya "nani" na "kwa nini," na sio "lini" na "wapi"

D. Nimeandika hii fasihi (Mwanzo 1-11) mwaka 2001. Nilijitahidi kwa kiasi kikubwa kuleta uhusiano kati ya Mwanzo 1 na tamaduni zangu za sasa za kimagharibi. Kitabu kipya kilichoandikwa na John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*, IVP (2009) kimenisaidia mimi kuona ni kwa namna gani nilikuwa na ushawishi kwa muundo wangu nilioishi. Ninaaamini kuwa kanuni nzuri za ufasiri zilianza na kusudio la mwandishi lakini ni wazi kwangu kuwa nadharia yangu ya kanuni za ufasiri zilikuwa nzuri kuliko utendaji. Kitabu hiki kilichoandikwa na Walton ni kielelezo chenye kubadili fikra kuhusu Mwanzo 1 kama kinavyohusiana na utendaji wa mwanzo, na sio vile vitu vya mwanzo vya ulimwengu. Ni kifungua macho cha kweli. kimenishawishi mimi njia mpya kuliona andiko hili muhimu ambalo linatafuta njia nyingine mbadala wa mjadala juu ya sayansi dhidi ya imani, dunia ya kale dhidi ya dunia ya sasa, mabadiliko dhidi ya uumbaji wa aina ya viumbe. Nakipendekeza kitabu hiki kwako!

VI. VYANZO VYA UTHIBITISHO WA MUUNDO WA KITHIOLOJIA

A. Vitabu vingine vya Kibiblia
   1. Uumbaji- Zaburi 8; 19; 33; 50; 104; 148 na Agano Jipya (kama vile Yohana 1:3; I Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2)
   2. Kipindi cha Ibrahimu - Ayubu

B. Vyanzo vya akiolojia/elimukale
   1. Fasihi ya mwanzo iliyotambulika yenye ufanano na muundo wa kitamaduni wa Mwanzo 1-11 ni vikabari vya vigae vya vyungu vya Mji wa Ebla toka Kaskazini mwa Shamu yapata miaka ya 2500 K.K., yaliyoandikwa kwa lugha ya Akkadia.
   2. Uumbaji
      a. Habari za karibu sana za Mesopotamia zinazojishughulisha na uumbaji, *Enuma Elish*, zilianzia toaka (1) NIV Study Bible, yapata mwaka 1900-1700 K.K. au (2) John H. Walton's *Ancient Israelite Literature in Its Cultural Context*, uk. 21, yapata mwaka 1000 K.K. Yalipatikana katika maktaba ya shurbanipal huko Nineva na nakala zingine zilipatikana sehemu mbali mbali. Kuna

vikabari saba vya viagae vya vyungu vilivyoandikwa kwa lugha ya Akkadia ambavyo vinaelezea uumbaji uliofanywa na Marduk.

(1) miungu, *Apsu* (maji baridi—jinsi ya kiume) na *Tiamat* (maji ya chumvi—jinsi ya kike) walikuwa na watoto wakaidi, wenye kelele. Miungu hawa wawili walijaribu kuinyamazisha miungu wadogo.

(2) (2) moja ya watoto *Ea na Damkina*, *Marduk* (mungu mkuu wa mji unaoinuka wa Babeli), akamshinda *Tiamat*. Akaumba dunia na mbingu toka kwenye mwili wake.

(3) (3) *Ea* akaumba mtu toka kwa mungu mwingine aliyeshindwa, *Kingu*, ambaye alikuwa mwenza wa kiume wa *Tiamat* baada ya kifo cha *Apsu*. Ubinadamu ulikuja toka kwenye damu ya *Kingu's*.

(4) (4) *Marduk* alifanywa kuwa mkuu wa hekalu la miungu ya Babeli.

b. "muhuri wa uumbaji" ni kikabari cha kigae cha chungu ambacho ni picha ya mwanaume uliye uchi na mwanamke akiwa pembeni ya mti wa matunda ukiwa na nyoka aliyezungushiwa kwenye shina na kuelekea kwenye bega la mwanamke kama vile akimsemesha. Profesa asiyependa mabadiliko wa mambo ya kale katika chuo cha Wheaton, Alfred J. Hoerth, alisema kuwa mnyama sasa unatafasiliwa kama alama ya ukahaba. Huu ni mfano mzuri wa jinsi wapinga ukweli toka huko nyuma wanatafasiliwa kivingine na watu binafsi na kupitia nyakati. Kipande hiki cha ushuhuda ni lazima kitathiminiwe upya.

3. Uumbaji na mafuriko- *The Atrahasis Epic* unaweka kumbu kumbu ya uasi wa miungu wadogo kwa sababu ya kujitaabisha na kazi ya uumbaji wa wanadamu saba na wenza wao (toka kwenye udongo, damu na mate) ili kutenda kazi za hawa miungu wadogo. Binadamu waliangamizwa kwa sababu ya: (1) kuongezeka kwa idadi ya watu na (2) kelele. Wanadamu walipunguzwa ki-idadi na mapigo, njaa kali zilizotokea mara mbili na mwisho mafuriko, yaliyopangwa na *Enlil*. *Atrahasis* alitengeneza boti na kuwaingiaza wanyama ndani yake ili kuwaokoa kutokana na maji. Matukio haya makubwa yanaonekana katika utaratibu ule ule ulioko Mwanzo 1-8. Muunganiko huu wa kikabari ulianza yapata muda ule ule wa *Enuma Elish* na *Gilgamesh Epic*, yapata mwaka 1900-1700 K.K. yote yalikuwa katika lugha ya Akkadia.

4. Mafuriko kipindi cha Nuhu

a. Kigae cha chungu cha Sumeria toka Nippur, aitwae *Eridu wa Mwqanzo*, toka yapata mwaka wa 1600 K.K., inatuambiat *Ziusudra* na kuja kwa mafuriko.

(1) *Enka*, mungu wa maji, akamwonya *Ziusudra* kuhusu kuja kwa mafuriko.

(2) *Ziusudra*, kuhani mfalme, akaamini huu ufunuo na kutengeneza boti kubwa ya mraba na kuweka ndani yake kila aina ya nafaka.

(3) Mafuriko yalidumu siku saba.

(4) *Ziusudra* alifungua dirisha kwenye boti na kuawaachia ndege aina mbali mbali ili wakaone kama ardhi imekauka.

(5) Pia alitoa dhabihu ya dume la ng'ombe na kondoo alipotoka ndani ya boti

b. Habari ambatani za mafuriko ya Babeli toka kwenye vigae vya vyungu vya Sumeria, vijulikanavyo kama *Gilgamesh Epic* mwanzoni kabisa vikianza toka mwaka 2500-2400 K.K., ingawa muundo ambatani ulioandikwa katika kikabari cha lugha ya Akkadia, ni cha baadaye (mwaka 1900-1700 K.K.). kinaongelea kuhusu waliopona kwenye mafuriko, *Utnapishtim*, ambaye alimwambia *Gilgamesh*, mfalme wa *Uruk,* namna alivyopona kwenye yale mafuriko na kupewa maisha ya milele.

(1) *Ea*, mungu wa maji, akaonya juu ya kuja kwa mafuriko na kumwambia *Utnapishtim* (mtu wa Babel mwenye muundo wa *Ziusudra*) kuitengeneza boti.

(2) *Utnapishtim* na familia yake, kukiwa na miti ya uponyaji iliyochaguliwa, iliyookoka kwenye mafuriko.

(3) Mafuriko yalidumu muda wa siku saba.

(4) Boti ilikuja kutua huko Kaskazini mwa Uajemi, kwenye Mlima Nisir.

(5) Akawatuma ndege watatu tofauti kuona kama ardhi imekauka.

5. Fasihi ya Mesopotamia ambayo inaelezea mafuriko yaliyotokea huko nyuma yote yalitoka katika chanzo kimoja. Mara zote majina hutofautiana, lakini sehemu ni moja. Mfano ni kuwa *Zivusudra, Atrahasis* na *Utnapishtim* wote wanawakilisha mfalme yule yule.
6. Ufanano wa kihistoria kwenye matukio ya awali ya kitabu cha Mwanzo yanaweza kuelezewa katika uwazi wa kutawanyika kabla kwa maarifa ya mwanadamu (Mwanzo 1-11) na maarifa ya Mungu. Hizi kumbukumbu za kweli za vitovu vya kihistoria zimekwisha kuelezewa na kusimuliwa ndani ya habari za mafuriko yaliyoenea sehemu zote za ulimwengu. Kile kile pia kinaweza kusemwa sio tu uumbaji (Mwa. 1,2) na mafuriko (Mwa. 6-9) bali pia kuhusu muunganiko wa mwanadamu na malaika (Mwanzo 6)
7. Siku ya wazee wa kaya (shaba ya kati)
   a. Vigae vya huko Mari – kikabari cha sheria (tamaduni za waamoni) na maandiko binafsi katika lugha ya Akkadia yapata mwaka 1700 K.K.
   b. Vigae vya huko Nuzi – kikabri cha nyaraka za familia fulani (tamaduni za Horite au Hurrian) zilizoandikwa katika lugha ya Akkadia yapata maili 100 Kusini Mashariki mwa Nineva mwaka 1500-1300 K.K. waliratibu taratibu za familia na biashara. Kwa mifano maalum zaidi, angalia Yohana 9 H. Walton's *Ancient Israelite Literature in its Cultural Context*, kur. 52-58
   c. Vigae vya huko Alalak – maandiko ya kikabari toka Kaskazini mwa Shamu yapata miaka 2000 K.K.
   d. Baadhi ya majina yaliyopatikana katika kitabu cha Mwanzo na kuandikwa kama sehemu ya majina katika vigae vya huko Mari: Serugi, Pelegi, Tera, na Nahori. Majina mengine ya kibiblia yalikuwa ya kuzoeleka: Abraham, Isaka, Yakobo, Labani, na Yusufu. Hii inaonyesha kwamba majina haya ya kibilia yaliendana na muda na mahali.
8. "utafiti shirikishi wa kihistoria umeonyesha kuwa, pamoja na Wahiti, Waebrania wa kalae walikuwa sahihi, waratibu waliokusudia na kuhusika na historia ya Mashariki ya Karibu." R. K Harrison, *Biblical Criticism*, uk. 5.
9. Wana akiolojia wamethibitisha kuwa yenye kufaa kwenye upatikanaji wa Biblia. hata hivyo, neno la tahadhari ni la muhimu. Wana akiolojia sio mwongozo wa moja kwa moja wa kuamini kwa sababu ya
   a. Mbinu duni kwenye uchimbaji wa mwanzo
   b. Tafasiri mbali mbali, zenye upendeleo za walio kinyume na kweli ya yale yaliyogunduliwa
   c. Kutokukubaliana- juu ya mpangilio wa matukio ya kale huko Mashariki ya karibu (ingawa moja imeishaanzishwa toka kwenye mfumo wa ngazi za mduara na vyungu).

C. Habari za uumbaji wa ki-Misri zinaweza patikana katika John H. Walton's, *Ancient Israelite Literature in Its Cultural Context* (Grand Rapids, MI: Zondervan, 1990) kur. 23-24, 32-34.
   1. katika fasihi za ki-Misri, uumbaji ulianza na maji yasiokuwa na umbo maalum, yasiokuwa pamoja.uumbaji ulionekana kama kuendeleza umbo nje ya maji yasiokuwa pamoja
   2. katika fasihi za ki-Misri huko Memphis, kusini mwa Misri, uumbaji ulitokea kwa kutamka neno la Ptah.
   3. Kila mji mkubwa wa Misri ulikuwa na mila tofauti zikisisitiza miungu yao yenye kuwasaidia.

D. Kitabu kipya kilichoandikwa na John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*, IVP, 2009, kinaonyesha uhusiano kati ya imani ya kale ya Mashariki ya Karibu (ANE) kuhusu uungu na ulimwengu katika mwanga mpya. Anadai kuwa (nami nakubaliana) haijalishi nani anamnakili nani bali maridhiano ya tamaduni ya pamoja ya Mahariki ya Karibu yote ya kale kuhusu umoja wa "asilia" na "uwezo wa kiasili." Tamaduni zote zilitumia mtazamo jumuishi wa pamoja wa kitamaduni. Israeli ilikuwa na imani ya Mungu mmoja pekee lakini pia walitumia mtazamo wa kitamaduni.

VII. SEHEMU YA FASIHI (MUKTADHA)

A. Maelezo yanazingatia juu ya matumizi ya Musa ya kifungu "vizazi vya" (*toledoth*)
   1. Asili ya mbingu na nchi, 1:1-2:3
   2. Asili ya mwanadamu, 2:4-4:26
   3. Kizazi cha Adamu, 5:1-6:8

4. Kizazi cha Nuhu, 6:9-9:17
5. Kizazi cha wana wa Nuhu, 10:1-11:9
6. Kizazi cha Shemu, 11:10-26
7. Kizazi cha Tera (Ibrahimu), 11:27-25:11
8. Kizazi cha Ishmaeli, 25:12-18
9. Kizazi cha Isaka, 25:19-35:29
10. Kizazi cha Esau, 36:1-8
11. Kizazi cha wana wa Esau, 36:9-43
12. Kizazi cha Yakobo, 37:1-50:26 (#1-11 ina mazingira ya fasihi ya Mesopotamia lakini #12 una vionjo vya fasihi ya Misri.)

B. Maelezo ya kithiolojia
  1. Uumbaji kea ajili ya ubinadamu na binadamu, 1-2
  2. Mwanadamu na anguko la uumbaji, 3
  3. Matokeo ya anguko, 4-11
     a. Uovu ukamwathiri Kaini na familia yake
     b. Uovu ukamwathiri Seth na familia yake
     c. Uovu ukamwathiri kila mmoja
     d. Mafuriko makubwa
     e. Uovu bado ungalipo katika familia ya Nuhu
     f. Mwanadamu yuko bado katika uasi, mnara wa Babeli
     g. Kutoweka kwa Mungu
  4. Mtu mmoja kwa ajili ya binadamu wote (3:15), 12-50 (Rum. 5:12-21)
     a. Ibrahimu (12:1-3), 11:27-23:20
     b. Isaka, 24:1-26:35
     c. YaKobo, 27:1-36:4
        (1) Yuda (ukoo wa Masihi)
        (2) Yusufu (umiliki mara mbili wa nchi), 37:1-50:26

VIII. KWELI KUU

A. Ilianza kwa namna gani
  1. Ilianza na Mungu (Mwanzo 1-2). Mtazamo wa kiulimwengu juu ya Biblia sio imani ya miungu wengibali ni imani ya Mungu mmoja. Haiangazii juu ya "namna gani" bali "nani" alihusika na uumbaji. Ni kwa kifupi, lakini ni uwasilishaji wa nguvu. Thiolojia ya Biblia ilikuwa ya kipekee katika siku zake ingawa baadhi ya maneno, maelezo ya shughuli nzima, na mada zake zinapatikana katika fasihi zingine za Mesopotamia.
  2. Mungu alihitaji ushirika. Uumbaji ni hatua tu kwa ajili ya Mungu kuwa na ushirika na Mwanadamu. Hii ni "sayari inayogusika" (kama vile C.S.Lewis).
  3. Hapana uwezekano kwa kuelewa sehemu ya Biblia iliyobaki pasipo Mwanzo 1,2-4 na 11-12
  4. Wanadamu ni lazima waitikie kwenye imani kwa kile wanachokijua kuhusu mapenzi ya Mungu (mwa.15:6 na Rum. 4)

B. Kwa nini ulimwengu umekuwa wa kiovu na usio wa haki? Ulikuwa "mzuri" (1:31), lakini Adamu na Hawa wakatenda dhambi (kama vile Mwanzo 3, Rum. 3:9-18,23; 5:17-21). Matokeo ya kutisha yako wazi:
  1. Kaini akamuua Abeli (kifungu cha 4)
  2. Malipizi ya Lameck (4:23)
  3. Mapatano yasiyo ya kisheria (6:1-4)
  4. Uovu wa mwanadamu (6:5,11-12;8:21)
  5. Ulevi wa Nuhu (9)
  6. Mnara wa Babeli (11)
  7. Imani ya miungu wengi wa Ur (11)

C. Ni namna gani Mungu anakwenda kulitengeneza?

1. Masiha atakuja kwa ajili ya wanadamu wote (3:15)
2. Mungu anamwita mtu kuwaita wote (Mwa. 12:1-3, Kut. 19:5-6, kama vile Rum. 5:12-21)
3. Mungu anawiwa kutenda na mwanadamu aliyeanguka (Adam, Hawa, Kaini, Nuhu, Ibrahimu, Wayahudi na watu wa mataifa) na kwa neema yake hutoa
   a. Ahadi
   b. Maagano (yenye masharti na yasiyo na masharti)
   c. Dhabihu
   d. Ibada

## MZUNGUKO WA KWANZA WA USOMAJI **(Kutoka "A Guide To Good Reading" (Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")**

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika ufahamu tuliopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu chote cha Biblia kwa mara moja. Eleza dhamira kuu ya kitabu kizima kwa maneno yako mwenyewe (mzunguko wa usomaji #1)

1. Dhamira kuu ya kitabu kizima
2. Aina ya fasihi (aina ya fasihi aliyotumia katika kuwasilisha ujumbe wake).

## MZUNGUKO WA PILI WA USOMAJI **(Kutoka "Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia" (Mwongozo wa Usomaji Mzuri wa Biblia")**

Huu ni mwongozo kujisomea wa fasiri wenye maana kuwa unawajibika kwa tafsiri zako za Biblia mwenyewe. Kila mmoja wetu lazima atembee katika ufahamu tuliopewa. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hupaswi kumuachia kazi hii mfasiri.

Soma kitabu kizima cha Biblia kwa mara ya pili kwa mara moja. Weka kwa muhtasari masomo makuu (mzunguko wa Usomaji #2) na elezea somo kwa sentensi moja.

1. Somo la kipengele cha kwanza cha fasihi
2. Somo la kipengele ya pili cha fasihi
3. Somo la kipengele cha tatu cha fasihi
4. Somo la kipengele cha nne cha fasihi

# MWANZO 1:1-2:3

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Uumbaji | Historia ya uumbaji | Hadithi ya uumbaji | Hadithi ya uumbaji | Uumbaji wa ulimwengu |
| (1:1-2:3) | (1:2-2:7) | (1:1-2:4a) | (1:1-2:4a) | |
| 1:1-5 | 1:1-5 | 1:1-5 | 1:1-5 | 1:1-2 |
| | | | | 1:3-5 |
| 1:6-8 | 1:6-8 | 1:6-8 | 1:6-8 | 1:6-8 |
| 1:9-13 | 1:9-13 | 1:9-13 | 1:9-13 | 1:9-10 |
| | | | | 1:11-13 |
| 1:14-19 | 1:14-19 | 1:14-19 | 1:14-19 | 1:14-19 |
| 1:20-23 | 1:20-23 | 1:20-23 | 1:20-23 | 1:20-23 |
| 1:24-25 | 1:24-25 | 1:24-25 | 1:24-25 | 1:24-25 |
| 1:26-31 | 1:26-28 | 1:26-31 | 1:26-2:4a | 1:28-31 |
| | (27) | | | 1:28-31 |
| Uumbaji wa Mwanadamu | 1:29-31 | | | |
| 2:1-3 | 1:1-3 | 1:1-3 | | 2:1-3 |
| | 2:4-7 | 2:4a | | 2:4a |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (<u>angalia ukurasa wa vii)</u>

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. <u>Aya ya kwanza</u>

* Ingawa hazijavuviwa, migawanyo ya aya ndiyo ufunguo wa kuelewa na kufuatilia kusudio la asili la mwandishi. Kila tafsiri ya kisasa imegawanya na kufanya muhtasari wa aya. Kila aya ina mada kuu, kweli au wazo. Kila toleo limebeba hiyo mada kwa namna yake ya pekee. Unaposoma maandiko ya mwandishi jiulize ni tafsiri ipi inawiana na uelewa wako wa somo na mgawanyo wa mistari.

Katika kila sura lazima tusome Biblia kwanza na kujaribu kutambua somo (aya), kisha tulinganishe na matoleo ya kisasa. Ni pale tunapoelewa kusudi la asili la mwandishi kwa kufuata mantiki yake na jinsi alivyojieleza tunaielewa

kwa Biblia kiukweli. Ni mwandishi wa asili tu aliyevuviwa —wasomaji hawana haki ya kurekebisha ujumbe. Wasomaji wa biblia wana wajibu wa kutumia ukweli uliovuviwa kwenye siku na maisha yao.

**Kumbuka kwamba maneno yote ya kiufundi na vifupisho vinaelezwa kwa ukamilifu katika viambatisho Moja, Tatu na Nne.**

2. Aya ya pili

3. Aya tatu

4. N.k

## MAELEZO YA UFUNGUZI

A. Kujifunza Mwanzo 1-11 ni vigumu kwasababu:
   1. Tunaathiriwa na desturi zetu wenyewe na mafunzo ya kimadhehebu
   2. leo kwa shinikizo kadhaa kwa kutambua na kutojitambua kunathiri mitazamo yetu ya mwanzo"
      a. hifadhi za vitu vya mabaki ya kale ya kisasa (Usambamba wa Mesopotamia)
      b. sayansi ya kisasa (nadharia za kisasa)
      c. historia ya ukalimani
         (1) dini ya Kiyahudi
         (2) kanisa la kwanza
   3. Kipengele hiki cha kwanza cha kuanzia cha Biblia kinawasilishwa kama historia lakini vitu kadhaa vinashangaza mfasiri
      a. Usambamba wa Mesopotamia
      b. mbinu za kwanza za kifasihi za mashariki (hadithi mbili za kidhahiri za uumbaji)
      c. matukio yasiyo ya kawaida
         (1) Mwanamke kuumbwa kutokana na "mbavu"
         (2) Nyoka anayezungumza
         (3) Merikebu ikiwa na wanyama wawili wawili ikisafiri kwa mwaka mzima
         (4) kuchanganywa kwa malaika na wanadamu
         (5) maisha marefu ya watu
      d. mchezo wa maneno kadhaa juu ya majina ya wahusika wakuu (kama vile K. 3)
   4. Wakristo wanahitaji kukumbushwa namna ya kufasiri upya Agano Jipya Mwanzo. 1 na 2 katika ufahamu wa Kristo. Yeye ni wakala wa Baba katika uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; I Kor. 8:6; Ebr. 1:2), ya vyote katika ulimwengu unaoonekana na usioonekana (kama vile Kol. 1:16). Funuo hizi mpya zinaonesha uhitaji wa umakini wa uhalisia katika Mwanzo. 1-3. Utatu unajumuishwa katika uumbaji.
      1. Mungu Baba katika Mwanzo 1:1
      2. Mungu Roho katika Mwanzo 1:2
      3. Mungu Mwana katika Agano Jipya kwa namna ya ufunuo unaoendelea
         Hii inaelezea WINGI katika Mwanzo 1:26; 5:1,3; 9:6

B. Mwanzo 1-11 si nyaraka ya kisayansi, lakini katika namna fulani sayansi ya kisasa ina weka usambamba katika uwasilishaji wake (mpangilio wa uumbaji na viwango vya kijiolojia). Haiko kinyume na sayansi lakini ilikuwepo kabla ya sayansi.
   inawasilisha ukweli:
   1. kutoka katika mtazamo wa kidunia (mwanadamu shahidi katika sayari hii)
   2. kutoka katika mtazamo wa kimatukio (yaani mifumo mitano ya ufahamu: namna mambo yanavyoonekana kwa mwanadamu mtazamaji) Inafanya kazi kama mfunuaji wa kweli kwa desturi nyingi kwa miaka mingi. Inawasilisha kweli kwa desturi za kisasa lakini bila maelezo halisia ya matukio.14

C. Iinashangaz sana kiukweli wa uzuri ikifunua na ikichorwa kisanaa.
   1. kugawanywa

2. vitu kukua
3. kutoka katika machafuko kuingia katika sayari ya kushikika iliyojaa uhai

D. Funguo za uelewa zinapatikana katika
1. aina zake za fasihi
2. uhusiano wake wa siku zake zenyewe (angalia John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*)
3. muundo wake
4. hali yake ya imani kwa Mungu mmoja
5. makusudi yake ya kithiolojia

Ufasiri wake lazima uwiane:
1. ufasiri wa mistari ya kibiblia
2. uelewa wa kimfumo wa maandiko yote
3. ubayana wa aina ya fasiri

Inafunua asili ya vitu vya mwilini ("na ilikuwa nzuri," kama vile. 1:31) na uharibifu wa vitu hivi (kama vile sura ya 3). Katika namna nyingi tukio la Kristo ni uumbaji mpya na Yesu ni Adamu mpya (kama vile Rum. 5:12-21). Uzao mpya unaweza ukawa kilele cha urejesho wa Bustani ya Edeni na ukaribu wake wa ushirika pamoja na Mungu (linganisha na Mwanzo 1-2 pamoja na Ufunuo. 21-22).

E. Kweli kuu ya sura hii sio kwa jinsi gani au lini lakini nani na kwa nini!

F. Mwanzo inaaksi maarifa ya kweli na sio maarifa yachoshayo. Inatolewa kwetu katika miundo ya kimawazo ya kale (ya Ki-Mesopotamia) lakini ni kweli ya kithiolojia ya kutegemewa. Inahusiana na siku yake lakini ni ya upekee kabisa. Inazungumzia kutoelezeka na bado inazungumza ukweli. Kimsingi ni mtazamo (nani na kwanini), sio taswira ya ulimwengu (kwa namna gani na lini).

G. Bila Mwanzo 1-3 Biblia haiwezi kuelezeka. Tazama namna gani ambayo kwa haraka hadithi inahama kutoka (1) dhambi kuelekea ukombozi (2) ubinadamu kwenda kwa Israeli. Uumbaji unatengeneza sehemu muhimu lakini sehemu ipitayo ya simulizi ya uchaguzi wa Mungu wa Israeli kwa kusudi la ukombozi wa kiulimwengu (kama vile Mwanzo. 3:15; 12:3; 22:18; Kutoka. 19:5-6 na Yohana 3:16; Mdo. 3:25; Gal. 3:8; I Tim. 2:4; II Pet. 3:9).

H. Jibu lako kwa swali, "Nini makusudio ya uvuvio na ufunuo?" Itaathiri namna unavyoitazama Mwanzo 1. Ikiwa unaona kusudi kama kuwekewa kweli kuhusu uumbaji, utaona kama njia moja (yaani kweli inayopendekezwa). Ikiwa unaiona kama kuelezea ukweli wa jumla kuhusu Mungu, ubinadamu na dhambi, hivyo yawezekana utaliona hivyo kithiolojia (yaani ya kielelezo). Ikiwa hata hivyo unaona kusudi la msingi kama kuanzishwa kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu, yawezekana nyingine (yaani yenye kuwepo).

I. Kipengele hiki cha Mwanzo ni hakika kithiolojia. Kama mapigo ya kitabu cha Kutoka yalivyoonesha nguvu ya YHWH juu ya asili ya miungu ya anga ya Misri, Mwanzo 1,2 inaweza kuonesha nguvu ya YHWH juu ya miungu ya Mesopotamia. Somo kubwa ni Mungu. Mungu pekee alifanya hivyo kwa makusudi yake

J. Nashangaa sana juu ya ujinga wangu mwenyewe nilionao! Nashangazwa na hali zangu mwenyewe za kihistoria, kidesturi na kidhehebu! Jinsi Mungu tunayemwabudu alivyo mkubwa na mwenye nguvu! Mungu huyu aliyetufikia ni mzuri kiasi gani (hata katika uasi wetu)! Biblia ni uwiano wa upendo na nguvu; neema na haki! Kadiri tunavyojua ndivyo tunavyoendelea kujua kwamba hatujui!

K. Hivi hapa ni baadhi ya mijongeo ya baadhi ya vitabu vya kusaidia:
1. Mwanzo 1-2 ikifasiriwa sambamba na mistari ya sayansi ya kisasa:
   a. Bernard Ramm's *The Christian View of Science and Scripture* ( kizuri kisayansi na kithiolojia)
   b. Hugh Ross' *Creation and Time* and *The Genesis Question* (Kizuri kisayansi lakini dhaifu kithiolojia)
   c. Harry Peo and Jimmy Davis' *Science and Faith: An Evangelical Dialog* (kina msaada mkubwa)
   d. Darrel R. Falk, *Coming to Peace with Science: Bridging the Worlds Between Faith and Biology* (mjongeo wa kiinjili kwa mabadiliko ya kiimani kwamba Mungu yupo na ni muumba na Mtawala wa dunia)
   e. Francis S. Collins, *The Language of God*
   f. Fazale Rana na Hugh Ross, *Who Was Adam?*
2. Mwanzo 1-2 ikifasiriwa sambamba na mistari ya kale yenye mfanano wa Mashariki ya Karibu
   a. R. K. Harrison's *Introduction to the Old Testament* and *Old Testament Times*

b. John H. Walton's *Ancient Israelite Literature in Its Cultural Context*
c. K. A. Kitchen's *Ancient Orient and Old Testament*
d. Edwin M. Yamauchi's *The Stones and the Scriptures*

3. Mwanzo 1-2 inafasiriwa sambamba na mistari ya thiolojia kutoka LaSor, Hubbard na Bush's *Old Testament Survey*
   a. "Vifaa vya kifasihi pia vinapatikana katika majina yanayotumika. Mwitikio wa majina pamoja na kazi ya mtu au jukumu linapindisha katika mazingira kadhaa. Adamu inamaanisha "mwanadamu" na Hawa "(yeye atoaye) uhai." Hakika kipindi mwandishi wa hadithi anatoa majina ya wahusika wakuu, kitu fulani kinawasilishwa kuhusu kiasi cha udhahiri unaokusudiwa! Vivyo hivyo Kaini inamaanisha "muhunzi (wa vyuma)"; Henoko anaunganishwa pamoja na "kuwekwa wakfu, kutakaswa" (4:17; 5:18); Jubal pamoja na pembe na baragumu (4:21); wakati Kaini alihukumiwa kuwa *n~d*, a "mtangaji," akienda katika ardhi ya *Nod*, jina ambalo kwa uwazi linatokana na mzizi huo huo wa Kiebrania, hivyo ardhi ya kutangatanga! Hii inapendekeza kuwa mwandishi anaandika kama msanii, mtoa hadithi ambaye anatumia mbinu ya kifasihi na ustadi. Mtu yapaswa ajishughulishe na kutofautisha kile anachokikusudia kukifundisha kutoka katika fasihi ikimaanisha mwajiri" ukur. 72.
   b. muhusisho wa kithiolojia wa mwanzo 1-11:

      "*Implication for Gen. 1-11*. Utambuzi wa mbinu ya kifasihi na muundo na kutambua usuli wa kifasihi wa sura za 1-11 hakujumuishi changamoto kwa ukweli, ile "hali ya tukio," la kweli inayoonyeshwa. Mtu hatakiwi kuchukulia habari hii kuwa hadithi ya kusadikika tu ama mzaha; hatahivyo sio "historia" katika namna ya kisasa ya ushuhuda, kutoa taarifa kwa kile kilichoonwa. Hatahivyo inaelezea kweli ya kithiolojia kuhusu matukio, yanayoelezewa kwa sehemu kubwa kiishara na kitaswira kwa namna ya aina ya fasihi. Hii haina maana kwamba Mwanzo 1-11 inatoa uongo wa kihistoria. Hitimisho hilo lingefuatia pale tu ikiwa maana yake ingejumuisha kuwa na maelezo ya kile kilichoonwaushahidi wa wazi tayari unaonesha na kufunua kwamba hayo hayakuwa makusudio. Kwa upande mwingine, mtazamo kwamba kweli inayofundishwa katika sura hizi hazina msingi wa kilichoonwa una makosa sana. Wanakiri kweli kuu: uumbwaji wa vitu vyote na Mungu muingiliano wa kimaalumu wa kiungu katika kuzaliwa kwa mwanadamu wa kike na wa kiume wa kwanza; umoja wa wanadamu; kuamuliwa kwa uzuri wa ulimwengu ulioumbwa, ukijumuisha uanadamu; uingiaji wa dhambi kupitia kutotii kwa jozi za kwanza; kushamiri kwa dhambi na kushushwa hadhi baada ya anguko. Kweli hizi zote ni kweli za hakika, na uwepo wake wa hakika unamaanisha uhalisia wa kweli. Weka kwa namna nyingine, waandishi wa kibiblia wanatumia desturi za kifasihi kufunua matukio ya ukipekee ya mwanzo ambayo hayana muda uliowekwa kama sharti, kuwekwa masharti ya kibinadamu, uzoefu wa aina 16 uliojikita katika analojia za kihistoria na hivyo zinaweza kuelezewa tu kwa ishara. Tatizo hilohilo linainuka mwisho wa muda: mwandishi wa kibiblia hapo, katika kitabu cha Ufunuo, unachukua taswira za siri na kuhusisha stadi za kisanaa za kifasihi za nyakati za mwisho" ukurasa wa 74.

   c. Ikiwa ni kweli kwamba lugha moja ilizungumzwa katika Mwanzo 1-10 (kama vile Samuel Noah Kramer, *The Babel of Tongues: A Sumerian Version*, "Journal of the American Oriental Society, 88:108-11), hivyo inahitajika kuwekwa vizuri kwamba haikuwa ni Kiebrania. Hivyo maneno yote na utumizi wa sanaa ya maneno ya kiebrania yanatoka siku za Musa au desturi za masimulizi ya midomo ya kiume. Hii inathibitisha asili ya fasihi ya Mwanzo 1-11.

4. Ningependa nitoe maoni binafsi. Napenda na natambua wale wanao tambua Biblia. Nashukuru kwa ajili ya watu ambao huchukua ujumbe kama uvuvio, ujumbe wa mamlaka kutoka kwa Mungu mmoja wa Kweli. Sisi sote ambao tunajifunza maandiko tunajaribu kumwabudu na kumtukuza Mungu kwa akili zetu (kama vile Mt. 22:37). Ile ukweli kwamba sisi kama mtu mmoja mmoja mwamini tunajongea na kuiangalia Biblia tofauti tofauti si kwamba kipengele cha kutoamini au uasi lakini ni tendo na kujitoa kikweli kweli na jaribio la kuelewa ili kuijumuisha kweli ya Mungu katika maisha yetu. Kadiri

ninavyosoma Mwanzo 1-11 na kwa namna hiyo zaidi kitabu cha Ufunuo, nafahamu kuwa ni kweli lakini kifasihi na sio uhalisia. Msingi katika ufasiri wa Biblia si suala la kutumia vipimo vyangu vya kifalsafa au vya utafsiri wa maandiko juu ya kifungu cha habari lakini kuruhusu kusudio la uvivio wa asili wa waandishi ujielezee wenyewe. Kuchukua kifungu cha habari cha fasihi na kutaka kiwe halisi wakati andiko lenyewe linatoa dokezo za asili yake ya kimafumbo na kiishara inaweka upendeleo/ubaguzi wangu juu ya ujumbe wa kiungu. Aina ya fasihi ni msingi wa uelewa wa kithiolojia wa "namna gani mambo yote yalianza" na "namna gani yote yataisha." Natambua ukweli na kujizatiti kwa wale wote kwa sababu yoyote, siku zote kwa aina ya utu au mafunzo ya kisomi wanafasiri Biblia kisasa, kiuhalisia, vipengele vya kimagharibi wakati kiukweli ni vitabu vya mashariki ya kale. Ninasema yote haya kusema kwamba nashukuru kwa Mungu kwa wale wanaoijongea Mwanzo 1-11 kwa makisio kwamba binafsi sishirikishi, kwakuwa najua watasaidia, kutia moyo na kuwafikia watu wa aina hiyo hiyo na mtazamo wa upendo, imani na kufanyia kazi Kitabu cha Mungu kwenye maisha yao!

Hata hivyo sikubaliani kwamba Mwanzo 1-11 au kitabu cha Ufunuo kinatakiwa kijongewe kiuhalisia, Hata kama ni *Creation Research Society* (yaani dunia changa) au Hugh Ross's *Reasons to Believe* (yaani dunia nzee/kuukuu). Kwangu mimi sehemu hii ya Biblia inasisitiza "nani" na "kwa nini" na sio "kwa namna gani" na "lini" ya uumbaji. Nakubali ukweli wa sayansi ya kisasa katika kujifunza vipengele vya uumbaji wa kimwili. Nakataa "nadharia ya uasili" (yaani maisha yote ni bahati na ukuaji wa michakato ya asili), lakini kiukweli naona mchakato kama halali na kipengele cha kuelezeka cha ulimwengu wetu na dunia yote. Nafikiri Mungu aliongoza na kutumia michakato. Lakini michakato ya asili haielezei anuwai na ugumu wa maisha wa sasa na uliopita. Ili kuweza kuelewa ukweli wa sasa nataka vyote mifano ya kinadharia ya sayansi ya kisasa na mifano ya kithiolojia ya Mwanzo 1-11. Mwanzo1-11 ni ulazima wa kithiolojia kwa uelewa sehemu inayobaki ya Biblia lakini ni uwasilishaji wa kifasihi, wa uwazi , wa kisanaa, wa kimashariki na sio uhalisia wa kisasa na uwasilishaji wa kimagharibi. Sehemu za Biblia hakika ni masimulizi ya kihistoria. Kuna sehemu ya ufasiri wa maandiko ya kiuhalisia: kulikuwa na wito wa Ibrahimu, na kutoka, kuzaa kwa bikra, Kalvari, ufufuo; kutakuwa na kuja kwa Mara ya Pili. Swali ni moja ya aina ya fasihi sio ukweli au kusudio la kimaandiko, upendeleo binafsi katika fasiri. Wacha wanadamu wote wawe waongo na Mungu awe mkweli (kama vile Rum. 3:4)!!!

## MADA MAALUM: UMRI NA UUMBAJI WA DUNIA(toka Mwanzo 1-11)

*I.* Sehemu hii ya kujifunza ina upendeleo kwasababu ya makisio kwamba yanatakiwa yafanywe hata kutafta namna ya kufikiri kwa usahihi kuhusu somo hili. Makisio lazima yawe na shabaha ya kutathminika kwa kutofautiana kwa maoni yanayoelezewa na wanaanga, wanajiolojia na sayansi zinazofanana na hizo ukilinganisha na uelewa wa kithiolojia na fasiri. See John H. Walton, *Genesis One As Ancient Cosmology.*

II. Katika sayansi madhanio yake ya dhahiri ni:

A. kwamba kiwango cha ubadilishaji (yaani kimwili, kikemikali na kibaiyolojia) kunakowekwa kumbukumbu na kupimwa duniani leo hakubadiliki huko nyuma (nadharia ya kuendana saresare, "ya sasa ni msingi kwa ya kale")

B. Kuwekwa tarehe ya upimaji wa mionzi (kunakoitwa tarehe kamili), ambayo ndiyo msingi wa kufuatana kwa kuwekewa tarehe kwa matukio ya dunia na anga lote kuwawekea msingi wa kitanda kiovu cha makisio kadhaa:

1. yaani utengenezaji wa asili wa miamba (yaani uhusiano wa chembe chembe mama na mwana za kiatomiki zisizo imara)
2. maisha yasiyo kamili ya elementi hizi
3. joto pia linaathiri viwango vya kiasilimia vya mwamba mama na vizaliwa katika sampuli (yaani muda wa utengenezwaji na/au vyumba vya ujiuji wa kivolkeno)
4. Chanzo cha asili na muda wa uumbaji wa elementi za utoaji wa mionzi hakijulikani. Nadharia za kisasa zinzsema kwamba namna ambavyo elementi ni nzito zinatengenezwa na mkutano wa nyuklia za joto katika sekunde na kizazi cha tatu cha nyota na kuenea kwa njia ya kulipuka kwa nyota.

C. kwamba ya sita ilikisiwa kufuata kanuni za jiolojia (ziitwazo tarehe zinazohusiana) zinazoathiri elimu juu ya mabaki ya wanyama na mimea:
    1. sheria ya nafasi ya juu ya Dhambi na mfuatano usiosumbuliwa wa miamba ya mashapo, safu ya sakafuni (chini) juu na safu ya kati chini yake ni kuu kuu (ya zamani)
    2. Kanuni ya asili ya mlalo-safu ya miamba ya mwando ilirundikwa karibia na uwanda wa mlalo
    3. Kanuni ya uhusiano wa mkato-wakati miamba ikikatwa au kusawazishwa na mpasuko, lazima ziwe zenye umri kubwa zaidi ya mpasuko
    4. kanuni ya ujumuisho wa miamba S mikubwa iliyopakana yenyewe kwa yenyewe, moja siku zote utakuwa na vipande vya kubebana moja chini katika safu ya juu ambayo inathibitisha makisio ya #1
    5. kanuni ya uwiano wa mimba S ya maumbo sawa lakini kutoka katika maeneo tofauti tofauti lazima yalinganishwe na kufananishwa, wakati hili haliwezi kufanyika hivyo mabaki ya wanyama na mimea yanatumika kuonesha tarehe zinazofanana za uumbaji.
    6. kanuni ya mabaki S ya viumbe haikutangulia moja baada ya nyingine katika namna inayoeleweka na mfuatano wa uashiria:
        a. utawanyikaji mpana wa mabaki ya viumbe
        b. kuwepo kwa ukomo wa muda mfupi wa muda wa kijiolojia

III. maoni kadhaa ya wanasayansi
  A. Wanasayansi wengi wanatambua kwamba sayansi ya kweli ni mbinu ya kitafiti ambayo inatafuta kupatanisha kweli zinazojulikana na makosa katika nadharia zinazojabika. Baadhi ya vitu kwa asili yake vyenyewe havijaribiki.
  B. Baadhi ya maoni kutoka kwa wanasayansi kuhusu makisio ya kisayansi katika eneo hili
    1. "Mafundisho (yaani nadhania ya U-yunifomu) haitakiwi kuchukuliwa kiuhalisia. Kusema kwamba michakato ya kijiolojia wakati wa nyuma haikuwa kama ile inayotokea leo sio kupendekeza kwamba zilikuwa siku zote na umuhimu za kimahusiano na kufanya kazi vizuri kabisa kwa kiwango kilekile" (Tarbuck na Lutgens, *Earth Science,* 6th ed. Ukrasa wa 262).
    2. "Ni muhimu kutambua kwamba tarehe ya ukwel; wa upimaji wa mionzi inaweza kupatikana tu ikiwa madini yataendelea katika mfumo uliofungwa wakati wa kipindi cha uundwaji wake; hiii ni kwamba tarehe sahihi haiwezekani mpaka kulikuwa hakuna kuongezeka ama kupungua kwa mwamba aisotopu mama au mtoto" (*Earth Science,* 6th ed. Ukurasa wa 276).
    3. "Tunachelea kusisitiza kwamba uyunifomu huu ni madhanio kwamba tunatengeneza asili, hivyo ni fundisho kuliko sheria ya kuthibitishwa kimantiki" (Dott na Balten, *Evolution of the Earth*, 4th ed. Ukurasa wa 44).
    4. "Kuendelea kuoza bila kukoma kunaweka tabia ya kiwango cha kuoza kutoa mionzi na kutawala uhusiano kati ya taarifa za ki-isotopu na mrejeo wa nyakati za radio isotopu. Kwa matokeo, usahihi wa baadhi ya mbinu bora za uwekaji wa tarehe kama vile mbinu ya 40Ar/39Ar, inaweza kuwa utaratibu wa ukubwa au mbaya zaidi kuliko usahihi wake ("Progress and challenges in geochronology" cha Renne, Ludwig na Karner katika *Science Progress* [2000], 83 [1], 107).
    5. "Watu bila mafunzo ya kisayansi hawawezi kuelewa kwamba mbinu yoyote ya upimaji wa mionzi ya uwekaji wa tarehe inaweza tu kuaminiwa kwa sampuli pamoja na umri karibu na nusu umri wa elementi inayoulizwa (Hugh Ross, *Reasons to Believe* newsletter).

IV. Makisio sio ya upekee wa jamii ya kisayansi lakini kwa uwazi pia yanatukia katika jamii ya kidini
  A. Wanadamu wanaletwa karibu kna kanuni ya uletaji umoja au mfano kupatanisha maana zao za uzoefu na kutoa uthabiti wa kihisia. Katika sayansi kanuni hii ya uunganishaji pamoja imekuwa "mabadiliko"
    1. Theodosius Dobzhansky, "Mtu aliyebadilika," *Science*, 155, 409-415, "Mabadiliko ni mchakato ambao umezalisha maisha kutoka pasipo kuwa na maisha, ambayo imeleta

mwanadamu kutoka katika wanyama na ambalo linaweza kuendelea kufanya vitu vya kushangaza katika siku za usoni."

2. Brian J. Alters na Sandra M. Alters, *Defining Evolution*, ukurasa wa 104, "mabadiliko ni msingi wa muktadha wa sayansi za kibaiyolojia....mabadiliko ni muundo unaoelezeka, nadharia inayounganisha. Ni sharti kusoma biolojia kama nadharia ya ki-atomiki ilivyo lazima kujifunza kemia."

B. Kwa wakristo wengi wenye kushikilia msimamo nadharia ya uunganishaji (yaani ufasiri) imefanyika ufasiri halisi wa Mwanzo 1-3. Hii ni kweli kwa wanahalisia wa dunia changa (*Creation Research Society* inaweka tarehe ya dunia kama miaka 10,000) na wanahalisia wa nchi kuu kuu (*Reasons to Believe* wanaweka tarehe ya dunia katika ufahamu wa jiolojia ya kisasa miaka bilioni 4.6). Tafsiri ya mtu ya maadiko inakuwa kioo ambacho kupitia kwacho vitu vingine vyote vinaonekana na kutathminiwa. Mtu hawezi kupasua makisio yanajikita juu ya maoni ya mtu, kwa kuwa maarifa ya kibinadamu katika ya viwango fulani ni kufikirika na kukisia kabla. Hatahivyo, tathmini ya madhanio ya mtu ni muhimu kwa ajili ya tathmini sahihi ya kauli za "kweli" yao.

C. Ukristo wa kimsingi ni kujaribu kujivika wenyewe hoja za "kisayansi" pale ambapo jambo jambo kuu ni tafsiri za kimbinu. Hii ni kumaanisha kwamba "sayansi ya mabadiliko ya sasa" sio ya kufikirika kabla au kwamba hitimisho lake halichongwi na mtazamo wa kiulimwengu wa kabla. Lazima tuwe makini na kuwa na ufafanuzi wa vyote. Hapo panaonekana kuwa na ushahidi wa pande mbili. Lazima nijiulize mwenyewe kwa mtazamo gani kwamba navutiwa nao kiasili, kihisia au kielimu (yaani makisio ya kujirishisha wenyewe)?

V. Hitimisho binafsi

A. Kwakuwa mimi ni mwana thiolojia na sio mwanasayansi, ilikuwa muhimu kwangu kusoma na kufananisha kadiri nilivyoweza kutoka katika sayansi za mfanano mmoja. Kibinafsi sisumbuliwi na "mabadiliko" lakini na "asilia" (maana moja iliyofanywa maarufu na Carl Sagan ni, "Ulimwengu ni vile ulivyokuwa na vile utakavyokuwa"). Natambua kwamba huu ni ubaguzi na upendeleo lakini nadharia yangu ya kuweka pamoja ni uasilia wa kupita kawaida na uumbaji maalumu lakini sikatai au kujiskia kutishwa na nadharia ya mabadiliko. Mtazamo wangu wa msingi ni kwamba kuna Mungu ambaye alianzisha na anaongoza mchakato kwa ajili ya kusudi! Kwangu mimi "uumbaji wenye akili" inakuwa nadharia ya kimantiki (kama vile M. J. Behe, *Darwin's Black Box* na William A. Demski, ed. *Mere Creation: Science, Faith and Intelligent Design*). Ni "kutawanyika" kwa mabadiliko "kutokuwepo kwa wakili" wa asili ambao unanisababishia maumivu binafsi na kuchanganyikiwa. Mchakato ni sehemu ya maisha. Lazima niwe na hakika kwamba sishikilii kile ambacho kinaleta faraja bila tathmini. Nimejaribu kubainisha makisio yangu:

1. Mwanzo 1-3 (na kwa namna hiyo zaidi kitabu cha Ufunuo), hakikusudiwa na mwandishi wake wa asili aliyevuviwa kuchukuliwa kibayana. "Namna yote yalivyoanza" na "kwa namna gani vyote vitakavyoisha" imefumbwa (na lazima iwe kwa mwanadamu aliyeanguka) kwa namna ya uwasilishaji.
2. Mabadiliko yako wazi katika viwango fulani ("mabadiliko mlalo," "mabadiliko madogo madogo," mabadiliko ya ndani ya viumbe) lakini sio sababu kiunganishi pekee. Kuna fumbo na jambo la kushangaza hapa! Binafsi najisikia vizuri na Biblia (yaani ufunuo maalumu) unaoniamba "nani" na "kwa nini" na asili (yaani ufunuo wa asili), ambayo ni utafiti wa sayansi ya kisasa unaoniambia "namna gani" na "lini" ikijikita kwenye mifano, vielelezo na nadharia.
3. Hata kilele cha uhalisia wa "mabadiliko ya kiimani juu ya Mungu kama mtawala wa dunia" hauwezi kusababisha mimi kukataa makisio yangu yoyote ya imani. Angalia Darrel R. Falk, *Coming to Peace with Science: Bridging the World's Between Faith and Biology* na Francis S. Collins,*The Language of God*. Ninayo madhanio ya imani (kama wewe ulivyo nayo)! Mtazamo wangu wa kiulimwengu wa Kibiblia jii ya Ukristo.Taswira yangu ya kiulimwengu inakua na kubadili uelewa wangu.

B. Umri “halisi” wa dunia sio jambo kubwa katika thiolojia yangu isipokuwa:

1. Dhana inayoonekana ya “Big Bang (kutokea ghafla)” kwa mpangilio wa kiulimwengu wa maada ambayo inaelezea mwanzo wa ulimwengu unaonekana kuweka ukomo wa uwezekano wa muda usio na kikomo kwa maendeleo ya kimabadiliko (yaani uasili).
2. Kuanza na kuhitimishwa katika kumbukumbu za mabaki ya viumbe “uingizaji wa ulinganifu” ambayo inaelezea kwamba nafasi ya mabadiliko inatokea katika kuchepusha (yawezekana matendo ya uumbaji ya Mungu yanayoendelea) na sio muhimu mabadiliko ya kihatua baada ya muda.
3. Dunia ya kuu kuu na uumbaji maalum wa ubinadamu ni kielelezo kinachopendekezwa, nachagua kushikilia mpaka nielewe zaidi kutoka katika kujifunza Biblia, elimu ya viumbe wa kale. Utaratibu wa haya unaonesha ubaguzi (lakini sisi sote huwa tunao)!
4. Sayansi sio adui kwangu, wala mwokozi! Inafurahisha sana kuishi katika hiki kizazi cha kuongeza maarifa! Inafariji sana kama mwamini kuwa na maarifa ya utafsiri wa neno la Mungu! Muingiliano wa imani na mantiki au Biblia na Sayansi na sifa ni uwezekano mzuri sana! Kitabu kipya kimenitia moyo katika uchunguzi huu- John H. Walton, *The Lost World of Genesis One: Ancient Cosmology and the Origins Debate.*

VI. Makisio ya sasa kama kwa kizazi cha dunia

A. Kuweka tarehe kwa miamba ya mwezini na vimondo kwa utumiaji wa mionzi imekuwa endelevu kwa miaka Bilioni 4.6. Zinajumuisha elementi ileile kama sayari za mfumo wa nyota hivyo kuhitimisha ni kwamba jua letu, vimondo na asteroidi vilifanyika wakati huu. Miamba ya zamani zaidi imetambuliwa kwa kutumia mionzi miaka Bilioni 3.8.

B. Tarehe ya kuumbwa kiungu kwa jozi ya kwanza ya binadamu (Homo sapiens) ni jambo gumu sana lakini ni utofauti wa nyuzi makumi elfu yawezekana 40,000. Angalia Fazale Rana na Hugh Ross, *Who was Adam?.* Muda unakuwa ni jambo tu kwa wale sisi tulioumbwa katika mfululizo wa mpangilio wa muda fulani. Mungu haathiriwi na upitaji wa muda. Naamini dunia na mazingira yake yaliumbwa kwa muda kwa ajili ya kusudi maalumu ya utoaji wa “sehemu” kwa Mungu kufanya ushirika na uumbwaji wake wa juu walioumbwa na yeye katika sura na mfano. Chanzo pekee kwa imani hizi ni Biblia iliyovuviwa. Nashikilia na kuruhusu sayansi ya kisasa kuongeza uelewa wa vipengele vya shughuli za Mungu za uumbaji!

VII. Vitabu vilivyonisaidia kuielewa Mwanzo 1-11 ni:

A. Derek Kidner, <u>Genesis</u>, Tyndale OT Commentaries, vol. 1

B. Hugh Ross' books

C. John H. Walton's books

D. Phillip E. Johnson's books

E. R. K. Harrison's books

F. Bernard Ramm's books

Wandishi hawa wamekuwa ni maombi yaliyojibiwa kwenye fikra zangu za kitafiti. Nimeipata amani ya namna hiyo machoni pao na ufafanuzi wa maandiko. Kama ingalipasa kumchagua mwandishi mmoja kati ya hawa, nisingalifanya. Kama ni asili au ,maendeleo ya kiulimwengu au Mwanzo ndiyo inakufurahisha wewe, basi nakuomba uwasome ndugu hawa!

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1:1-5**
**[1]Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. [2] Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa vilindi vya maji; Roho ya Mungu ikatulia juu ya uso wa maji. [3] Mungu akasema, Iwe nuru; ikawa nuru. [4] Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema; Mungu akatenga nuru na giza. [5] Mungu akaiita nuru Mchana, na giza akaliita Usiku. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku moja.**

**1:1 "hapo mwanzo"** *Bereshith* (BDB 912) ni kichwa cha kiebrania cha kitabu. Tunapata *Mwanzo* kutoka katika fasiri ya agano la Kale ya Kiyunani. Huu ni mwanzo wa historia lakini sio shughuli za Mungu (kama vile Mt. 25:34; Yohana 17:5,25; Efe 1:4; Tito 1:2; II Tim. 1:9; I Pet. 1:19-20; Ufu. 13:8). R. K. Harrison anasema inatakiwa ifasiriwe "kwa namna ya mwanzo" (*Introduction to the Old Testament*, ukurasa wa 542 dokezo 3). John H. Walton, *The Lost World of Genesis One* inasema inatakiwa itambulishwe kipindi cha muda (ukurasa wa 45).

◙ **"Mungu"** *Elohim* (BDB 43) Ni muundo wa WINGI wa jina la jumla kwa Mungu wa Mashariki ya Karibu ya kale, *El* (BDB 42). Tunapokuwa tuna maanisha Mungu wa Israeli, kitenzi siku zote (isipokuwa 6) UMOJA. Walimu wa kiyahudi wanasema kwamba inazungumzia Mungu kama muumbaji, mtoaji na anayetustahimilisha maisha yote katika sayari ya dunia (kama vile Zaburi. 19:1- 6; 104). Tazama namna ambavyo mara kwa mara neno hili linatumika katika sura ya 1.

Naamini kwamba huu mstari ni tungo inayojitegemea: Ibn Ezra anasema kwamba ni tungo tegemezi ikiwa na msisitizo juu ya mstari wa 2 wakati Rashi anasema kwamba mstari wa 2 ni maelezo ya ziada na msisitizo ni mstari wa 3. Watoaji wa maoni wa leo wanasema kwamba mstari wa 1 ni tungo tegemezi yenye kuweza kusaidia maoni yao ya anguko la awali lililotangulia (nadharia ya ombwe). Tazama kwamba hakuna maelezo ya asili ya Mungu. Inafanya kuelezea kwamba Mungu aliumba maada na hakuweka mtindo wa maada iliyopo (nadharia ya uumbwaji wa ulimwengu ya Kiyunani). Katika *Enuma Elish*, (Hadithi ya uumbaji ya Kibabeli), kama Wayunani walivyofikiri, Roho (ambaye ni mwema) na maada (ambayo ni ovu) vina umilele wa pamoja unaoendana. Biblia haijadili au kufunua asili ya Mungu (kama vile Zaburi 90:2). Hakika hapa pana maajabu. Mwanadamu hawezi akaelewa ukamilifu wote wa Mungu!

Mjadala huu wa tungo ni muhimu kithiolojia. Jamii ya Kiyahudi ya machapisho ya Kimarekani 21 imefasiri Mwanzo 1:1 ni tungo iliyojifunga katika muda, "Mungu alipoanza kuziumba mbingu na nchi. Nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu. . ." Fasiri hii inaweza kuhitimisha kwamba Mungu na maada vina tokea katika umilele wa pamoja kama elimu ya uumbaji wa ulimwengu ya Wayunani (kama vile "Uumbaji na elimu juu ya uumbaji wa ulimwengu" katika *Encyclopedia Judaica*, vol. 5, ukurasa wa 1059). Hadithi ya Wa-Sumeri ya uumbaji, *Enuma Elish*, inaanza na "hapo mwanzo. . ." Angalia Mada Maalum: Majinaya Kiungu katika 2:4. will

◙ **"aliumba"** *Bara* (kama vile 1:1,21,27; 2:3,4) Ni KITENZI cha kiebrania (BDB 135, KB 153, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) kinachotumika bila kuhusisha shughili za uumbaji za Mungu. Maana yake ya msingi ni kutengeneza kwa kukata. Mungu aliona vyema kuwa kila kitu lakini yeye mwenyewe. Zaburi 33:6,9; Ebr. 11:3 na II Pet. 3:5 uumbaji wa sasa (elimu juu ya uumbaji wa ulimwengu) kwa neno la kuzungumzwa na Mungu (*fiat*) kutoka katika kutokuwa na kitu (*ex nihilo*), Ingawa maji hayasemwi kuwa yaliumbwa (kama vile Mwanzo 1:2). Falsafa za Kiyunani na Ki-mesopotamia (walimu wa uongo) zinasisitiza u-wili wa milele kati ya "roho" na "maada." Chochote ambacho *bara* inamaanisha inapelekea shughuli za Mungu na kusudi!

Biblia inaelezea kwamba uumbaji una sehemu inayoanzia. Sayansi ya karne ya ishirini na moja ingeweza kutengeneza tabia ya "big bang (nadharia ya utokeaji wa dunia kwa ghafla)." Nadharia ya asili sasa haiwezi kuelezea kurudi nyuma kusiko na kikomo kwa muda wa nyuma. Hatahivyo inawezekana kwamba Mwanzo 1

inamaanisha kuwa mwanzo wa kufanya kazi kwa dunia, sio kuanza kwa maada zinazoshikika (John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*).

◙ **"mbingu"** Neno "mbingu" (BDB 1029) inaweza ikatumika katika namna kadhaa: (1) inamaanisha anga hewa la dunia kama ilivyo katika mstari wa 8 na 20; (2) inaweza kumaanisha ulimwengu mzima (yaani uwepo wa vitu vyote vinavyoshikika ); au (3) inaweza kumaanisha uumbaji wa vitu vyote vinavyoonekana (vitu vinavyoshikika) na visivyoonekana (malaika, mbingu kama enzi ya Mungu). Ikiwa mbadala wa tatu ni kweli hivyo usambamba unatakiwa uwe wa Kol. 1:16. Ikiwa sio, itakuwa Mwanzo inaweka shabaha tu katika uumbaji wa sayari hii. Biblia inaweka msisitizo katika mtazamo wa kitovu (yaani uumbaji unaonekana kama mtazamaji wa sayari hii angeitazama). Baadhi wangeeleza kwamba Mwanzo 1 inalenga uumbaji wa ulimwengu (yaani jua, mwezi, nyota na mfumo wote wa vieleavyo angani, wakati Mwanzo 2-3 inaweka shabaha katika sayari hii na uumbaji wa mwanadamu. Hii hakika inawezekana kwasababu Sura za 2-4 inatengeneza kipengele cha kifasihi. Katika zote (yaani Mwanzo 1 na 2-4) uumbaji ni wa kitovu (yaani shabaha ya kidunia).

◙**"Dunia"** Neno (BDB 75) Inaweza kumaanisha ardhi halisia, nchi na sayari nzima. Mwanzo 1 inachukuliwa kuwa kitovu (kama vile Mstari wa 15). Hii inashabihiana kna kusudi la kithiolojia la sura na sio sayansi. Kumbuka kwamba Biblia iliandikwa katika lugha ya kuelezea kwa ajili ya makusudi ya kithiolojia. Haipingi sayansi isipokuwa ipo kabla ya Sayansi.

**1:2 "dunia ikawa"** KITENZI hiki (BDB 224, KB 243, *Qal* KAULI TIMILIFU) inaweza tu kwa nadra kufasiriwa "ikafanyika." Kisarufi na kimuktadha "ikawa" inapendelewa. Usiruhusu makisio ya awali ya kithiolojia ya kuanguka mara mbili (yaani Millenia itolewayo iliyotangulia hapo awali) (nadharia ya ombwe) inaathiri ufasiri wa andiko.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ukiwa na utupu"** |
| **NKJV** | **"bila umbo, na tupu"** |
| **NRSV, NJB** | **"bila umbo na tupu"** |
| **TEV** | **"bila umbo na ukiwa"** |
| **NIV** | **"bila umbo na tupu"** |
| **REV** | **"taka kwa sehemu kubwa"** |
| **SEPT** | **"isiyoonekana na isiyonakishiwa"** |
| **JPSOA** | **"isiyopewa umbo na tupu"** |

Maneno haya mawili yanapatikana katika BDB 1062, KB 1688-1690 and BDB 96, KB 111. Je hii inamaanisha maji tu? Dunia inabadilisha muundo (yaani kutembea kwa visahani dunia) kwa mwendelezo (yaani bara moja la asili liitwalo Pangea lilifanyika mabara kadhaa). Swali tena ni umri wa dunia. Maneno haya yanatokea kwa pamoja katika Yer. 4:23. Yanatumika katika hadithi za uumbaji za ki- Sumeri na Kibabeli lakini katika namna ya kimithiolojia. Hii hali ya uumbaji inaonesha kwamba Mungu alitumia mchakato unaoendelea kwenye dunia isiyokaliwa na watu (kama vile Isaya 45:18). Haya maneno mawili yanafunua sio mwanzo wa maada lakini hali ya mfumo wa utaratibu usikuzwa na usiofanya kazi (John H. Walton, *The Lost World of Genesis One* ukurasa wa 49). Haijawa tayari kwa ajili ya binadamu!

◙**"giza"** Neno hili (BDB 365) Haiwakilishi uovu lakini kwa asili machafuko. Mungu anatoa jina kwa giza katika mstari wa 5. Kama anavyofanya kwa nuru. Maneno haya mawili japo yanatumika mara kwa mara katika Biblia kuahiria ukweli wa Biblia, hapa yanawasilisha hali ya mwili ya asili.

◙ **"vilindi"** Neno la Kiebrania *tehom* (BDB 1062 #3, KB 1690-91). Inayofanana na hiyo lakini tofauti, mzizi wa ki-semitiki inapewa sifa ya kibinadamu *Tiamat* katika uumbaji wa ki-Sumerian na hadithi za kimiujiza za kibabeli kama majitu yenye kuleta machafuko na mama wa miungu, mke wa Apsu. Alijaribu kuuwa miungu yote midogo ambayo ilijitokeza kutoka kwake. Marduk alimuua. Nje ya mwili wake Marduk alitengeneza mbingu na nchi katika

kitabu cha Mwanzo wa ki-Babeli inayoitwa *Enuma Elish*. Waebrania waliamini kwamba maji yalikuwa elementi ya mwanzo ya uumbaji (kama vile Zaburi. 24:1; 104:6; II Pet. 3:5). Haijawahi kusemwa kuwa iliwahi kuumbwa. Hatahivyo neno la Kiebrania ni la kiume na sio la kike, na halihusiani kiasili yake na Tiamat. Kuna vifungu katika Agano la Kale ambalo linamfunuaYHWH katika mgogoro na machafuko ya maji yaliyobinafsishwa (kama vile Zaburi 74:13-14; 89:9-10; 104:6-7; Isaya 51:9-10). Hatahivyo hivi siku zote ni vifungu vya habari vya kishairi, kisitiari. Maji ni kipengele muhimu cha uumbaji (kama vile 1:2b,6-7).

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV, TEV, NIV** | **"Roho wa Mungu"** |
| **NRSV, JPSOA** | **"upepo kutoka kwa Mungu"** |
| **NJB** | **"upepo wa kiungu"** |
| **REB** | **"roho wa Mungu"** |
| **SEPT** | **"pumzi ya Mungu"** |

Neno la Kiebrania *ruach* (BDB 924) na neno la Kiyunani *pneuma* (kama vile Yohana 3:5,8) inaweza kumaanisha "roho," "pumzi" au "upepo" (kama vile Yohana 3:5,8). Roho mara nyingi inahusiana na uuumbaji (kama vile Mwanzo 1:2; Ayubu 26:13; Zaburi. 104:29-30; 147:14-18). Agano la Kale haliweki wazi kimaana kuhusu mahusiano kati ya Mungu na Roho. Katika Ayubu 28:26-28; Zaburi 104:24 na Mithali 3:19; 8:22-23 Mungu alitumia hekima (nomino ya kike) kuumba vitu vyote. Katika Agano Jipya Yesu anasemekana kuwa wakala wa Mungu katika uumbaji (kama vile Yohana 1:1-3; I Kor. 8:6; Kol. 1:15-17; Ebr. 1:2-3). Kama ilivyo katika ukombozi, ndivyo ilivyo pia katika uumbaji, nafsi zote tatu za kichwa cha Mungu zilihusika. Mwanzo 1 yenyewe haiweki mkazo katika sababu ya pili.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, TEV** | **"..kitembea"** |
| **NKJV, NIV** | **"tanda juu ya"** |
| **NRSV** | **"ikipita kwa kufagia"** |
| **NJB** | **"..kuburuza juu ya"** |

Neno hili (BDB 934, KB 1219, *Piel* KAULI ENDELEVU) lilikuza kisawe cha "kuanguliwa" au "kukaa juu ya kwa hali ya utayari tayari" (kama vile toleo la JB). Hili ni neno la mama ndege (kama vile Kutoka 19:4; Kumb. 32:11; Isa. 31:5; 40:31; Hos. 3; 11:4). Haiusiani na elimu juu ya uumbwaji wa ulimwengu wa ki-Foinike ambayo inaelezea kwamba dunia ilikuja kutoka katika yai, lakini sitiari ya kike kwa kule kujali kwa Mungu kama mzazi, kama ilivyo ukuaji wa uumbaji wake katika hatua hii ya Mwanzo ya Uumbaji wake!

**1:3"Mungu akasema"** Hii ni dhana ya kithiolojia ya uumbaji kwa neno la kusemwa, kwa kutumia neno la Kilatini *fiat* (kama vile 9,14,20,24,29; Zaburi 33:6; 148:5; II Kor. 4:6; Ebr. 11:3). Hii imekuwa mara kwa mara ikielezewa kama"kutoka katika hali ya kutokuwepo na kitu maada ikatokea ikitumia," kwa amri ya Mungu, tukitumia tungo ya Kilatini *ex nihilo* (kama vile II Macc. 7:28). Hatahivyo inawezekana kwamba Mwanzo 1 haihusiani na uumbaji wa asili wa maada lakini mpangilio wa maada iliyopo (kama vile John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*, ukurasa wa 54 na kuendelea). Hii nguvu ya neno linalozungumzwa linaweza pia :

1. baraka za kiaskofu
2. neno la ukombozi la binafsi la Mungu, Isa. 55:6-13, hasa mstari wa 11
3. Yesu kama neno katika Yohana 1:1 na
4. Yesu kama anayerudi na upanga ukatao kuwili katika kinywa chake (kama vile II The. 2:8; Ebr. 4:12; Ufu. 1:6; 2:12,16; 19:15,21). Hii ni njia ya kinahau ya uumbaji kwa mapenzi ya Mungu kupitia mawazo na neno. Kile ambacho Mungu hukitaka, ukipata!

◙ **"Na iwe"** Hizi ni KAULI AMRISHI (kama vile mistari 3, 6[mara mbili], 9[mara mbili katika maana, sio mfumo], 11, 14, 20 [mara mbili katika maana na sio muundo], 22, 24, 26[katika maana na sio muundo]).

**1:4 "Mungu akaona kuwa nuru ni njema"** (Mistari 4,10,12,18,21,25,31) Uumbaji wote ulikuwa mzuri (kama vile 1:31). Maovu hayakuwa sehemu ya uumbaji wa asili wa Mungu lakini upotovu wa wema. "vizuri" Hapa yawezekana "inashabihiana na kusudi lake" (kama vile Isa. 41:7) au "kiundani bila makosa" (BDB 373).

◙ **"Mungu akatenganisha"** KITENZI hiki (BDB 95, KB 110, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU) ni tabia ya namna gani Mungu anaendeleza na kukuza Uumbaji wake. Anagawanya (KJV) na kuanza vitu vipya (kama vile mistari ya 4,6,7,14,18).

◙ **"Nuru"** Kumbuka kwamba hakuna nuru bado. Kuwa makini usibebe imani ya kidini juu ya mfuatano wa muda (yaani masaa 24 kwa dunia kuzunguka jambo ambalo halijawa endelevu katika historia yote ya dunia). Nuru (BDB 21) ni ishara ya kibiblia ya uzima, usafi, na kweli (kama vile Ayubu 33:30; Zaburi. 56:13; 112:4; Isa. 58:8,10; 59:9; 60:1-3; Yohana 1:5-9; II Kor. 4:6). Katika Ufu. 22:5 kuna nuru bila ya jua. Pia tazama kwamba giza linaumbwa (kama vile Isa. 45:7) na kupewa jina na Mungu (kama vile Mstari wa 5) ambalo linaonesha Uweza wake wa kuendesha mambo (kama vile Zaburi 74:16; 104:20-23; 139:12). John H. Walton, *The Lost World of Genesis One* (ukurasa wa 55 na kuendelea), imejikita katika mistari ya 4 and 5, inaelezea kwamba hii ina maanisha "kipindi cha nuru," na sio asili ya jua.

**1:5 "Mungu akaita"** (mistari ya 8,10) Huku kuita majina kunaonesha uweza wa Mungu wa umiliki na kuendesha na kushughulikia uumbaji.

◙ **"kukawa jioni kukawa asubuhi"** Mpangilio huu unaweza kuaksi uwepo wa giza kabla ya uumbaji wa nuru. Walimu wa kiyahudi waliifasiri hii kama siku ya kipengele cha muda wa kuanza jioni. Kukawa na giza na tena kukawa na nuru. Hii inaaksi siku za Yesu pia ambapo siku mpya ilianza mawio, wakati wa jioni.

◙ **"siku"** Neno la Kiebrania *yom* (BDB 398) linaweza kuamaanisha kipindi cha muda (kama vile 2:4; 5:2; Ruth 1:1; Zaburi. 50:15; 90:4; Muhubiri 7:14; Isa. 4:2; 11:2; Zek. 4:10) lakini siku zote ikimaanisha masaa 24-ya siku (yaani Kutoka 20:9- m10)

## MADA MAALUM: SIKU (*YOM* BDB 398, KB 399)

Nadharia za maana ya *yom* (siku) ikichukuliwa na kufanyiwa kazi na Dr. John Harris' (Mnadhimu wa School of Christian Studies na Profesa wa Agano la Kale katika chuo cha East Texas Baptist ) OT Survey I Notebook:

1. Nadharia ya kipindi cha masaa 24 ya uhalisia
   Hii ni nadharia inayoleta mkabiliano wa moja kwa moja (kama vile Kutoka 20:9-11). Maswali yanayotokana na mbinu hii:
   a. ilikuwaje kukawa na nuru siku ya kwanza ambapo jua lilikuwa bado halijaumbwa mpaka siku ya nne?
   b. Ni kwa namna gani wanyama wote (hasa wale watokao sehemu zingine za ulimwengu) waliweza kupewa majina wote ndani ya siku moja? (kama vile Mwanzo. 2:19-20)?
2. Nadharia ya Umri-wa siku
   Nadharia hii ianajaribu kupatanisha sayansi na maandiko (hasa jiolojia) pamoja na maandiko. Nadharia hii inasema kwamba "siku" zilikuwa "nyakati/umri wa kijiolojia" kwa urefu. Urefu wake si sawasawa na unakisia tabaka mbalimbali zinazoelezewa katika mfumo unaofanana kijiolojia.Wanasayansi wanafanya kukubaliana na ukuaji wa jumla wa Mwanzo 1: mvuke na aga la maji lilitangulia kutenganishwa kwa ardhi na maji kabla ya kutokea kwa uhai/maisha. Maisha ya mimea ya kondeni yalikuja kabla ya maisha ya wanyama na binadamu aliwakilisha mfumo wa kisasa na ulio mgumu zaidi. Maswali yanayoibuka kutoka katika mbinu hii:
   a. Ni kwa namna gani mimea iliweza kuishi kwa "miaka" bila kuwepo kwa jua?
   b. Mchavusho uliwezaje kufanyika katika mimea ikiwa wadudu na ndege walikuwa bado

hawajaumbwa mpaka “miaka mingi” laterbaadaye?

3. Nadharia ya mbadilishano wa Nyakati-Siku

   Siku kusema ukweli ni kipindi cha saa 24, lakini kila siku ikitenganishwa na miaka/zama ambazo kila kilichoumbwa kilikua. Maswali yanayoibuka kutoka katika mbinu hii.

   a. Matatizo hayohayo yanaibuka katika nadharia ya Siku-Nyakati.
   b. Je andiko linaonesha “siku” kutumika kote kote kama saa 24 na kama nyakati?

4. Nadharia ya uumbaji endelevu-machafuko

   Nadharia hii inaenda namna hii: Kati ya Mwanzo. 1:1 na 1:2, kulikuwa na kipindi ambapo nyakati za kijiolojia zilitokea; wakati wa kipindi hiki, viumbe vya kabla ya historia katika utaratibu vilipendekezwa na mabaki ya viumbe hai yakaumbwa; karibia miaka 200,000 iliyopita, baa kubwa la kimiujiza lilitukia na kuaribu maisha katika sayari hii na kufanya wanyama wengi baadaye siku za Mwanzo 1 ikatukia. Nyakati hizi zinamaanisha kuumbwa upya, kuliko uumbaji wa asili.

5. Nadhari ya Edeni pekee

   Simulizi za uumbaji inamaanisha uumbaji tu na vipengele vya kimwili vya Bustani ya Edeni.

6. Nadharia ya Ombwe

   Kulingana na Mwanzo 1:1, Mungu aliumba ulimwengu mkamilifu. Kulingana na Mwanzo 1:2, Lusifa (Shetani) alikuwa amewekwa zamu ya kusimamia ulimwengu wote na akaasi. Hivyo Mungu alihukumu Lusifa na ulimwengu kwa uharibifu wa kushangaza. Kwa miaka mingi mamilioni, ulimwengu uliachwa peke yake na nyakati za Biblia zilipita. Kulingana na Mwanzo 1:3-2:3, katika 4004 B.C.E., siku sita za kawaida za masaa 24 za uumbwaji upya zilitokea. Askofu Ussher (1654 b.k) alitumia vizazi vya Mwanzo 5 na 11 kupiga hesabu na tarehe ya uumbaji wa mwanadamu ca. 4004 B.C.E. Hata hivyo, vizazi haviwakilishi utaratibu kamili wa mfuatano.

7. Nadharia ya Wiki takatifu

   Mwandishi wa kitabu cha Mwanzo alitumia dhana ya siku na wiki kama mbinu ya kifasihi ili kuweka sawa ujumbe wake wa kiungu wa shughuli za ki-Mungu katika uumbaji. Muundo wa namna hiyo unaelezea uzuri na mlingano wa kazi ya uumbaji na ubunifu wa Mungu.

8. Uanzishwaji rasmi wa Hekalu la Ki-ulimwengu

   Katika maoni ya hivi karibuni ya John H. Walton, *The Lost World of Genesis One*, IVP. 2009, ambayo yanaona siku sita kama “elimu ya viumbe hai inayofanya kazi, na sio ya kawaida ya kushikika. Wanamuelezea na kumfunua Mungu kwa mfululizo au kuweka rasmi ulimwengu ufanyao kazi kwa ajili ya wema wa mwanadamu. Hii inashabihiana na elimu juu ya ulimwengu ya kale. Kwa mfano siku za kwanza tatu zingemwalikisha Mungu anayetoa “majira (yaani muda),” “hali ya hewa (yaani kwa mazao)” na chakula. Tungo inayojirudia “ni vyema” ingeweza kumaanisha hali ya ufanyaji kazi.

   Siku ya saba ingemuelezea Mungu akiingia katika “hekalu la kiulimwengu” linalofanya kazi asilimia mia moja na lisiloishiwa na mtu kama mmiliki halali mwenyewe, mwendeshaji na mwongozaji. Mwanzo 1 haina kitu kinachohusiana na uumbaji wa vitu vinavyoonekana vya uumbaji wa maada lakini kwa kuweka utaratibu wa maada hiyo kwa ajili ya nafasi ifanyayo kazi kwa ajili ya Mungu na mwanadamu kuwa na ushirika.

   Hizi “Siku/nyakati” zinafanyika chombo cha kifasihi cha kuzungumzia makubaliano ya jumla ya ANE(Ancient Near Easten) ya kwamba:

   1. Hakuna utofautisho kati ya “asili” na “kilicho zaidi ya asili”
   2. Uungu unahusishwa katika kila kipengele cha maisha. Upekee wa Israeli haukuwa katika mtazamo wake wa kidunia wa kiujumla lakini katika vifuatavyo
      a. hali yake ya kuamini Mungu mmoja
      b. Uumbaji ulikuwa umelengwa kwa ajili ya wanadamu na sio kwa ajili ya miungu
      c. hakuna mgogoro kati ya miungu au miungu na ubinadamu katika taarifa ya Israeli.

Hakuazima uumbaji wake kutoka kwa wengine lakini walishirikisha mtazamo wao wa kiulimwengu. Neno “siku”mara nyingi hurejelea mduara wa masaa 24 ya mzunguko wa dunia (yaani., Kut. 20:9-10), lakini yaweza kurejelea kipindi cha muda usiojulikana (kama vile Mwa. 2:4; 5:2; Ruth 1:1; Zab. 50:15; 90:4; Wimb. 7:14; Isa. 4:2; 11:2; Zak. 4:10).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1:6-8**

**6 Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji. 7 Mungu akalifanya anga, akayatenga yale maji yaliyo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo. 8 Mungu akaliita lile anga Mbingu. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya pili.**

**1:6** Mstari huu una *Qal* KAULI AMRISHI (“na iwe...”) Kutoka katika kitenzi “kuwa” (BDB 224, KB 243). Tungo hii hii ina mistari ya 14 na 22.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NET, JPSOA** | **“anga”** |
| **NKJV** | **“nguzo”** |
| **NRSV, TEV** | **“kuba”** |
| **NJB** | **“kuba”** |

Neno hili (BDB 956, KB 1290) linaweza kumaanisha “kuponda na nyundo” au “kunyoosha” kama katika Isa. 42:5. Hii inaweza kumaanisha anga la hewa la dunia (kama vile 1:20) ikichukuliwa kisitiari kama kuba la hewa au tufe lililogeuzwa juu ya uso wa dunia (kama vile Isa. 40:22).

◙ **“maji”** Maji baridi na maji ya chumvi ni elementi muhimu katika masimulizi ya ziada ya uumbaji wa kibiblia lakini katika Biblia yanaongozwa na Mungu. Hakuna utofauti katika Mwanzo 1 uliotenganisha maji yasio ya chumvi na yale yenye chumvi. Maji katika hewa la anga yanagawanywa kutoka katika maji ya dunia. Uchambuzi wa Mwanzo 1 unaonesha kwamba Mungu alitenganisha vitu kadhaa kama mchakato kwenye nchi isiyokaliwa (nuru kutoka katika giza, maji ya juu kutoka katika maji ya chini, maji ya chini kutoka katika ardhi kavu, muda wa jua kutoka katika muda wa mwezi).

◙**“akatenganisha maji”** Mungu anajishughulisha na machafuko ya maji (BDB 95, KB 110, *Hiphil* KAULI ENDELEVU). Anaweka mipaka (kama vile Ayubu 38:8-11; Zaburi 33:6-7; Isa. 40:12).

**1:7 “na ikawa hivyo”** Chochote ambacho Mungu alikitaka kitokee kilitokea (kama vile 1:9,11,15,24,30).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 1:9-13**

**9 Mungu akasema, Maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja, ili pakavu paonekane; ikawa hivyo. 10 Mungu akapaita pale pakavu Nchi; na makusanyiko ya maji akayaita Bahari; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. 11 Mungu akasema, Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi; ikawa hivyo. 12 Nchi ikatoa majani, mche utoao mbegu kwa jinsi yake, na mti uzaao matunda, ambao mbegu zake zimo ndani yake, kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. 13 Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tatu.**

**1:9-10** VITENZI viwili vya kwanza (BDB 876, KB 1082 na BDB 906, KB 1157) vyote ni *Niphal* VISHURUTISHI vilivyotumika kama KAULI AMRISHI. Je hii inamaanisha bara moja (yaani Pangaea)? Dunia inabadilisha muundo (yaani mabamba gandunia) kwa kuendelea. Swali tena ni umri wa dunia. Tazama kwamba Mungu anashughulikia majanga ya asili. Hakuna miungu ya asili!

**1:9 "na iwepo nchi kavu"** Hii ni sawa na elimu ya kimisri ya asili ya mlima mtakatifu. Mfano mwingine wa kushirikisha huku kwa mtazamo wa kiulimwengu wa kawaida kipindi chote cha ANE (Mashariki ya Karibu ya kale) ingekuwa wanadamu kuumbwa kutokana na mfinyanzi. Hii ni kawaida kwa masimulizi ya uumbaji ya Mesopotamia, Misri na Israeli.

**1:11-12** Hii haikusudiwi kuwa maelezo ya kiufundi kwa asili ya maisha yote. Inaonekana kumaanisha aina tatu za mimea: majani, nafaka na matunda. Wanyama watakula ya kwanza; wanadamu watakula cha pili na cha tatu. Mungu anaandaa dunia hatua kwa ahatua kwa hatua kama jukwaa au ulingo ambapo ushirika na kustahimili uumbaji wake wa juu, wa kibinadamu.
Kumekuwa na nadharia kadhaa za kisayansi za kisasa kama mpangilio wa ukuaji wa maisha ya mimea. Baadhi ya wanasayansi wangeelezea utaratibu huu. Lakini lazima kuwa makini kwasababu ya mabadiliko ya kinadharia. Wakristo hawaamini katika Biblia kwasababu sayansi na elimu ya mabaki ya kale inathibitisha maada. Tunaiamini kwasababu ya amani tuliyopata katika Kristo na kauli za uvuvio za Biblia yenyewe.

**1:11 "Na nchi ichepue"** Hii ni *Hiphel* KAULI AMRISHI ya kitenzi "ichepue" (BDB 205, KB 233).

◙ **"kila moja kwa aina yake"** Uumbaji imewekwa katika muundo (kama vile mistari ya. 12,21,24,25; 6:20; 7:14) hivyo mara baada ya kuumbwa, mimea, wanyama na wanadamu inaweza kuzalisha na kuchukuliana na vyema. Mungu aliumba maisha ili tuyazoee. Katika kiwango hiki, mabadiliko kutofautishiana hali kwa hakika kunatokea kwa muda (mabadiliko – mdogomdogo au mabadiliko mlalo).
Kuna mwelekeo unaokua katika thiolojia kuelekea dhana ya uumbaji endelevu ambao unamaanisha kwamba Mungu anaweza kuwa aliumba mwanadamu (1) katika hatua au (2) Adam na Hawa waliumbwa katika hatua za baadaye wakiwa kamili kabisa (kama vile maandiko ya Bernard Ramm na Hugh Ross). Kwa mlinganisho kwa Mashariki Karibu ya kale ambapo uzao ulikuwa unaabudiwa kama miungu mapacha, hii inaonesha chanzo cha uhai/maisha kama Mungu na sio kitendo cha kujamiiana. Katika namna nyingi masimulizi ya uumbaji huu yanadhoofisha na kushusha miungu ya kale ya Mashariki ya Karibu ya kale (maji; nuru/giza; viumbe vya mbinguni; nguvu za asili; na miungu ya uzao) kama tauni ya Kutoka ulipunguzia heshima miungu ya Misri. Mwanzilishi pekee ni ni mmoja na Mungu pekee!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:14-19**
**14 Mungu akasema, Na iwe mianga katika anga la mbingu ili itenge kati ya mchana na usiku; nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka; 15 tena iwe ndiyo mianga katika anga la mbingu itie nuru juu ya nchi; ikawa hivyo. 16 Mungu akafanya mianga miwili mikubwa, ule mkubwa utawale mchana, na ule mdogo utawale usiku; akafanya na nyota pia. 17 Mungu akaiweka katika anga la mbingu, itie nuru juu ya nchi 18 na kuutawala mchana na usiku na kutenga nuru na giza; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. 19 Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya nne.**

**1:14 "kwa ajili ya ishara na kwa majira na siku na miaka"** Mianga ya kimbingu ilikuwa alama ya siku za sherehe (kama vile 18:14; Mambo ya Walawi 23; Kumb. 31:10) na mzunguko wa mapumziko, kazi na kuabudu (kama vile Zaburi 104:19-23). Jua liliumbwa kutenganisha Kalenda na kila siku katika vipengele vya muda ili kuwasaidia binadamu kutimiza majukumu yao yote (yaani ya kiroho nay a kimwili).

**1:16 "mianga miwili mikubwa. . akafanya na nyota pia"** Mungu akafanya na vitu vya angani (kama vile Isa. 40:26). Vyenyewe havina uungu ili kuabudiwa (Kuabudu kwa viumbe vya angani kwa Wa-Mesopotamia, kama vile Kumb. 4:19; Ezek. 8:16) lakini watumishi wa mwilini (kama vile Zaburi. 19:1-6). Hii ni kauli ya Kithiolojia!

**1:17-18** Muundo wa usambamba wa 14 Usambamba wa muundo wa Kiebrania inamaanisha kusudi tatu kwa nyongeza kwa Mstari.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:20-23**

**[20] Mungu akasema, Maji na yajawe kwa wingi na kitu kiendacho chenye uhai, na ndege waruke juu ya nchi katika anga la mbingu. [21] Mungu akaumba nyangumi wakubwa, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho, ambavyo maji yalijawa navyo kwa wingi kwa jinsi zao, na kila ndege arukaye, kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema. [22] Mungu akavibarikia, akisema, Zaeni, mkaongezeke, mkayajaze maji ya baharini, ndege na wazidi katika nchi. [23] Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya tano.**

**1:20-23** Wanyama wasio na uti wa mgongo wanatokea katika kipindi cha Cambrian. Hakuna ushahidi wa mwilini wa ukuaji wa hatua. Vitenzi "kundi/bumba" (BDB 1056, KB 1655) na "wadudu" (BDB 733, KB 800) yaliyotumika katika mstari wa 20 vyote ni KAULI ISIOTIMILIFU vinavyotumika kama kuonesha KAULI AMRISHI.

**1:20 "viumbe hai"** Neno hili hili, *nephesh* (BDB 659), linatumika kibinadamu (kama vile 2:7) na wanyama (kama vile 2:19; Mambo ya Walawi 11:46; 24:18). Inawakilisha nguvu ya maisha (kama vile Ezek. 18:4) inayohusiana na kutegemea juu ya sayari hii.

◙ **"ndege"** Hii kidhahiri inamaanisha "vitu vipaavyo" (BDB 733) kwa sababu ya Kumb. 14:19-20 inaweza pia kumaanisha wadudu.

**1:21 "kuumba"** Hii ni neno *bara* (BDB 135, KB 153, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) kama ilivyo katika Mwanzo. 1:1. Ikimaanisha uumbaji wa kiungu "mwanadamu na wanyama" "wanafanywa" katika 1:24-25 ambayo inamaanisha kutokana na maada iliyokuwepo kabla (yaani uchafu). Hatahivyo *bara* inatumika kwa ajili ya "mwanadamu" katika 1:27 (mara tatu). Hili neno la umaalumu linatumika juu ya (1) ulimwengu (au dunia) katika 1:1; (2) ya viumbe vya baharini 1:21; na (3) na binadamu 1:27.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NRSV, TEV, NJB** | **"wanyama wakubwa wa baharini"** |
| **NKJV, NIV** | **"viumbe wakubwa wa majini"** |
| **LXX, KJV** | **"nyangumi wakubwa"** |
| **JB** | **"nyoka wakubwa wa majini"** |

Hii inamaanisha Walawi (BDB 1072, kama vile Zaburi 104:26; 148:7; Ayubu 41:na kuendelea). Wakati mwingine neno inahusianishwa na maadui wa Israeli: (1) Misri, Isa. 51:9; Ezek. 29:3; 32:2 (wakati mwingine ikimaanisha "Rahabu" kama vile Zaburi 89:10; Isa. 51:9) na (2) Babeli, Yer. 51:34. Mara kwa mara inahusianishwa maadui wa kiulimwengu wa kiroho, Ayubu 7:12; Zaburi. 74:13; Isa. 27:1. Masimulizi ya uumbaji wa wakaanani unafanya mungu huyu kupigana dhidi ya baali lakini katika Biblia ni uumbaji mzuri wa Mungu mmoja wa kweli .

◙**"kila ndege mwenye apaaye"** Hii inajumuisha wote wapaao, ndege na wadudu (kama vile Kumb. 14:19-20). 1:22 Kama mimea ilifanywa ili kuzaa na hivyo pia wanyama. Mungu anataka sayari yake ijae na uhai (mfululizo wa *Qal* KAULI SHURUTISHI [na KAULI AMRISHI moja], kama vile 1:28; 9:1,7). Hii ilikuwa ni moja ya mambo yenye ukaidi na uasi (yaani hali ya kutokuwa na utayari wa kutenganisha na kujaza sayari) ya Mnara wa Babeli (kama vile Mwanzo. 10-11).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, hii ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani sayansi inahusiana na Biblia?

2. Maswali nyeti ni wakina nani na kwanini uumbaji na sio kwa namna gani na lini. Ikiwa hivi ndivyo kweli, je ni kwa namna gani tuifasiri Mwanzo 1-2?
3. Ni kwa namna gani Mungu aliumba ulimwengu wa kimwili unaoonekana? Je tusukume *fiat, ex nihilo* ikiwa hii ndio ushairi?
4. Nini msukumo mkubwa wa Mwanzo. 1?
5. Ni kwa namna gani Biblia inafanana/haifanani na masimulizi ya uumbaji?

## BAADHI YA NYENZO ZA MSAADA

A. Objectives Sustained cha Phillip Johnson
B. Darwinism on Trial cha Phillip Johnson
C. Creation and Time cha Hugh Ross
D. The Creator and the Cosmos cha Hugh Ross
E. The Genesis Question cha Hugh Ross29
F. The Christian View of Science and Scripture cha Bernard Ramm
G. The Scientific Enterprise and Christian Faith cha Malcolm A. Jeeves
H. Coming to Peace with Science cha Darrel R. Falk
I. The Language of God cha Francis S. Collins
J. Who was Adam? cha Fazale Rana na Hugh Ross

## UFAHAMU WA KIMUKTADHA KWA MWANZO 1:24-2:3

## UTANGULIZI

A. Katika karne mbili zilizotangulia, wanataaluma wa Agano la Kale mara kwa mara wameelezea kwamba Mwanzo inaweka kumbukumbu ya uumbaji wa aina mbili, ikitumia majina tofautitofauti kwa Mungu. Hatahivyo:
   1. Hii inaweza kuwa na muundo wa fasihi ya mashariki ya masimulizi ya jumla ikifuatiwa na masimulizi halisi zaidi
   2. Mwanzo 1:1-2:3 inaweza kuwa muhtasari wa uumbaji wa sayari hii na Mwanzo 2:4-25 kwa uumbaji wa maharusi wawili.
   3. Hii inaweza kuaksi vipengele tofauti tofauti za tabia ya Mungu (yaani ki-ualimu)
      a. *Elohim* - muumbaji, mtoaji na mtoshelevu wa maisha yote
      b. *YHWH* - mkombozi, mwokozi na Mungu wa Agano la Israeli
B. Kunaonekana kuwa na utofauti kati ya Mungu kuumba toka kutokuwepo na kitu na kuumba vitu kuvileta katika uhai. Mfano: Katika Mstari wa 21 Mungu aliumba na bado katika mstari wa 20 maji yanazalishwa; katika mstari wa 25 Mungu tayari akavifanya na bado katika mstari wa 24 dunia inazalishwa. Augustine alitambua utofauti huu na kufyatua matendo mawili ya uumbaji: (1) maada na viumbe vya rohoni (2) mpangilio wao na mgawanyiko wake.
C. Habari hii kwa uwazi inafundisha kwamba wanadamu wako kama wanyama wa nchi ya juu: (1) wote wana *nephesh*, 1:24 na 2:7; (2) wote waliumbwa siku ya sita, 1:31; (3) wote waliumbwa kutoka katika ardhi, 2:19; (4) wote wanakula mimea kama chakula, 1:29-30; (5) wote wanazaa na kuzaliana. Hatahivyo wanadamu wako vile vile kama Mungu: (1) uumbaji pekee, 1:26; 2:7; (2) waliofanywa kwa sura ya Mungu, 1:26; na (3) wana mamlaka, 1:26,28.
D. Mwanzo 1:26 "na tufanye . . . " (kama vile 1:26; 3:22; 11:7; 19:24; Isa. 6:8) imekuwa ikijadiliwa sana. Nadharia kadhaa zimeibuka:
   1. Wingi wa mfalme (lakini si mifano ya kwanza katika Biblia au katika fasihi ya kialimu)
   2. Mungu akijizungumza mwenyewe na mahakama ya kimbingu ya malaika, I Wafalme. 22:19
   3. Inaonekana kuelekea wingi katika Mungu, na hivyo kutaja kwanza juu ya Utatu Mtakatifu, 3:22;11:7; Isa. 6:8; 61:14. Ieleweke kwamba (a) Elohim ni WINGI na (b) watu wa kiungu wanatajwa katika Zaburi 2:2; 110:1,4: Zek. 3:8-9,11.
E. Nadharia kama maana ya sura na mfano:
   1. Irenaeus na Tertullian:

        a. sura-vipengele vya kimwili vya kibinadamu
        b. mfano-vipengele vya kiroho vya kibinadamu
    2. Clement wa Alexandria, Origen, Athanasius, Hilary, Ambrose, Augustine, na John of Damascus
        a. sura – tabia zisizo za kimwili za binadamu
        b. mfano - vipengele vya mwanadamu ambavyo vinaweza kukuzwa kama vile utakatifu au maadili, na ikiwa haikukuzwi basi inapotea.
    3. Vya Kitaaluma (Thomas Aquinas)
        a. sura - uwezo wa mwanadamu wa kufikiri na uhuru (asili)
        b. Mfano - haki ya sili na karama za uwezo wa juu ambao ulipotea baada ya anguko.
    4. Wanamageuzi
        a. Wote kimsingi walikataa utofauti kati ya maneno (Mwanzo 5:1; 9:6).
        b. Luther na Calvin wote wanaelezea dhana hii katika maneno tofauti, lakini kimsingi yanaelezea ukweli uleule.
    5. Nafikiri kwamba wanamaanisha (1) utashi binafsi; (2) hali ya kujitambua; (3) stadi za lugha; (4) hiari; na/au (5) maadili.
F. Mada Maalum: Mali asili

## MADA MAALUM: MALI ASILI

I. Utangulizi
    A. Uumbaji wote ni tone au hatua kwa upendo wa Mungu unaomuunga mwanadamu.
    B. Inashirikisha anguko (kama vile Mwanzo. 3:17; 6:1 na kuendelea; Rum. 8:18-20). Pia inashirikisha ukombozi katika matukio ya siku za mwisho (kama vile Isa. 11:6-9; Rum. 8:20-22; Ufu. 21-22).
    C. Asili ya dhambi, anguko la mwanadamu lilichukua mazingira ya asili kwa ajili ya kuyaweka mbali. Ifuatayo ni nukuu kutoka *The Canon of Westminster* by Edward Carpenter. ". . . ulegevu wa mwanadamu katika muktadha wa kidunia, juu ya ulimwengu kumzunguka—yaani uumbaji wa Mungu—kushambuliwa kwa hewa inayochafuliwa; njia za maji zinazoharibiwa; udongo unaotiwa sumu; misitu inayokatwa na kuvunwa, inatengeneza na kusuka athari za muda mrefu za uharibifu. Kushambuliwa huku ni kipande cha chakula kisichoratibiwa. Hali ya kutojali inafanywa bila kuzingatia kujali mazingira na matokeo yake uwajibikaji mdogo kwa kizazi kimoja unapelekea kuaribika kwa kizazi kingine."
    D. Si tu kwamba tunavuna matokeo ya uchafuzi wa hali ya hewa kwenye sayari yetu, lakini vizazi vyetu vinavyofuata wanavuna matokeo mabaya zaidi yasiyoweza kurekebishika.
II. Vitu vya Kibiblia
    A. Agano la Kale
        1. Mwanzo 1-3
            a. Uumbaji ni mahali maalum palipoumbwa na Mungu kwa ajili ya kuwa na ushirika na mwanadamu (kama vile Mwanzo 1:1-25).
            b. Uumbaji ni mzuri (kama vile Mwanzo. 1:4,10,12,18,21,25), ndio, nzuri sana (kama vile Mwanzo. 1:31). Imekusudiwa kuwa ushuhuda kwa Mungu (kama vile Zaburi 19:1-14).
            c. Ubinadamu ni kusudi la kutiwa taji la uumbaji (kama vile Mwanzo 1:26-27).
            d. Ubinadamu umekusudiwa kufanyia kazi mamlaka (Kiebrania, "kuwa juu") kama mawakili wa Mungu (kama vile Mwanzo. 1:28-30; Zab. 8:3-8; Ebr. 2:6-8). Mungu anabaki na anaendelea kuwa Muumbaji/Mtoshelevu/ Mkombozi/Bwana wa uumbaji (kama vile Kut. 19:5; Ayubu 37-41; Zab.24:1-2; 95:3-5; 102:25; 115:15; 121:2; 124:8; 134:3; 146:6; Isa. 37:16).
            e. Uwakili wa kibinadamu wa uumbaji unaweza kuonekana. 2:15, "kuipalilia na kuutunza na kuulinda" (Kama vile Mambo ya Walawi. 25:23; I Nyakati. 29:14).
        2. Mungu anapenda uumbaji, hasa wanyama.
            a. Sheria ya Musa kwa ajili ya kutunza wanyama
            b. YHWH anamuumba Leviathani kucheza ndani ya bahari (kama vile Zab. 104:26)

c. Mungu anajali wanyama (kama vile Yona 4:11)
d. uwepo wa asili ya matukio ya siku ya mwisho (kama vile Isa. 11:6-9; Ufu. 21-22)

3. Asili kwa sehemu fulani inamtukuza Mungu.
   a. Zab.19:1-6
   b. Zab. 29:1-9
   c. Ayubu 37-41
4. Asili ni namna ambayo Mungu anaonesha upendo wake na uthamini wake kwa Agano.
   a. Kumb. 27-28; I Wafalme 17
   b. kipindi chote cha manabii

B. Agano Jipya
1. Mungu anaonekana kama muumbaji. Kuna muumbaji mmoja tu, Utatu Mtakatifu wa Mungu (Elohim, Mwanzo. 1:1; Roho, Mwanzo. 1:2; na Yesu, Agano Jipya). Vingine vyote vinaumbwa
   a. Mdo.17:24
   b. Waebrania 11:3
   c. Ufunuo 4:11
2. Yesu ni wakala wa uumbaji
   a. Yohana 1:3,10
   b. I Kor. 8:6
   c. Kol. 1:16
   d. Ebr. 1:2
3. Yesu anazungumzia ujali wa Mungu kwa asili katika namna ya moja kwa moja katika mahubiri yake
   a. Mt. 6:26,28-30, ndege wa angani na majani ya kondeni
   b. Mt. 10:29, shorewanda
4. Paulo anaelezea kwamba wanadamu ni kuwajibika kwa maarifa ya Mungu katika uumbaji (yaani ufunuo wa asili, kama vile Rum. 1:19-20; Ufu. 21-22).

III. Hitimisho
A. Tunawajibika kwa utaratibu huu wa asili!
B. Asili ya dhambi ubinadamu imeharibu karama ya Mungu ya asili kama wana walivyo na karama zingine zote za Mungu.
C. Huu utaratibu wa kiasili ni wa Muda. Itaenda kupita (II Pet. 3:7). Mungu anatembea katika ulimwengu wetu kwa mfululizo wa kihistoria. Dhambi itaendelea katika utaratibu wake, lakini Mungu ameamua mipaka yake. Uumbaji utakombolewa (kama vile Rum. 8:18-25).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:24-25**
**[24] Mungu akasema, Nchi na izae kiumbe hai kwa jinsi zake, mnyama wa kufugwa, nacho kitambaacho, na wanyama wa mwitu kwa jinsi zake; ikawa hivyo. [25] Mungu akafanya mnyama wa mwitu kwa jinsi zake, na mnyama wa kufugwa kwa jinsi zake, na kila kitu kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake; Mungu akaona ya kuwa ni vyema.**

**1:24 "Mungu akasema,"** *Elohim* (BDB 43) ni jina la kale Mungu lenye wingi ambalo linatawala sura ya 1. Asili yake haijulikani. Walimu wa Kiyahudi wanasema kwamba inaonesha Mungu kama Muumbaji, mtoshelevu na mtoaji wa uhai wote katika sayari dunia. WINGI unaonekana kuwa muhimu kithiolojia wakati ukiunganishwa na 1:26; 3:22; 11:7 na wingi wa neno "mmoja" ambalo linapatikana katika maombi makuu ya kuamini katika Mungu mmoja (Shema), Kumb. 6:4-6. Wakati inapotumika na Mungu wa Israeli KITENZI siku zote inakaribia UMOJA. The Neno *elohim* katika Agano la Kale inaweza kumaanisha (1) malaika (kama vile. 8:5); (2) mahakimu wa kibinadamu (kama

vile Kutoka. 21:6; 22:8,9; Zab. 82:1); au (3) miungu mingine (kama vile Kut. 18:11; 20:3; I Sam. 4:8). Angalia Mada Maalum: Names for Deity at Majina ya Kiungu 2:4.

◙**"Nchi na izae"** Hii (BDB 422, KB 425) ni *Hiphil* KAULI AMRISHI. Huu ni utofauti unaofanywa katika Mwanzo 1 kati ya Mungu kuumba kwa neno litokalo katika kinywa kutoka katika hali ya kutokuwa na kitu na kwamba ambavyo aliviumba, viendelee kuzaana (yaani vizoeane). Linganisha mistari ya 20 na 21 na mistari ya 24 na 25.

◙**"kiumbe hai kwa jinsi zake"** Mistari 24-25 inaelezea wanyama wa nchi kavu wote wakubwa na wadogo, wakufugwa na wa porini. Tazama neno "viumbe hai"(BDB 659 and 311) imejikita katika jina *nephesh* ambalo ni neno linalotumika kwa wanyama katika Mwanzo 2:7. Ni wazi kwamba upekee wa binadamu haupatikani katika neno *nephesh*, mara kwa mara linafasiriwa katika Kiyunani "nafsi."

◙**"nacho kitambaacho"** Kinadharia hii inamaanisha "kuteleza," au "kuteleza" (BDB 943). Hili ni neno lilelile linalotumika katika mst.21, "vinavyotembea." Inaonekana kumaanisha wanyama wote wasiotembea kwa miguu yao mwenyewe au kwamba walikuwa na miguu mifupi kwamba haikutazamwa.

◙ **"ikawa hivyo"** Mungu ana shauku ya kufanyika kwa uhalisia! Angalia dokezo katika 1:7.

**1:25 "Mungu akaona ya kuwa ni vyema"** Uumbaji wa Mungu ulikuwa mzuri (BDB 373) na ukatangazwa kuwa "mzuri sana" katika 1:31. Hii inaweza kuwa nahau ya Kiebrania inayomaanisha kutosheleza kwa kusudi walilopewa. Kithiolojia inaweza pia kuwa kutokuwepo kwa dhambi kutoka katika uumbaji wa asili wa Mungu. Dhambi ni matokeo ya uasi, sio uumbaji.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 1:26-31**
**26 Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. 27**
**Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba, mwanamume na mwanamke aliwaumba. 28 Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi, na kuitiisha; mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi. 29**
**Mungu akasema, Tazama, nimewapa kila mche utoao mbegu, ulio juu ya uso wa nchi yote pia, na kila mti, ambao matunda yake yana mbegu; vitakuwa ndivyo chakula chenu; 30 na chakula cha kila mnyama wa nchi, na cha kila ndege wa angani, na cha kila kitu kitambaacho juu ya nchi, chenye uhai; majani yote ya miche, ndiyo chakula chenu; ikawa hivyo. 31 Mungu akaona kila kitu alichokifanya, na tazama, ni chema sana. Ikawa jioni ikawa asubuhi, siku ya sita.**

**1:26 "Na tumfanye"** Muundo (BDB 793, KB 889) ni *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, lakini inatumika katika namna ya KAULI AMRISHI/YA KUAMURU. Kumekuwa na mjadala mkubwa juu ya WINGI wa neno "sisi." Philo na Eben Ezra wanasema ni "wingi wa ufalme," lakini muundo huu wa kisarufi hautokei mpaka baadaye katika historia ya kiyahudi (toleo la Biblia la NET linasema haitokei pamoja na VITENZI, ukurasa wa 5); Rashi anasema kwamba inamaanisha mahakama ya kimbingu (kama vile Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6-12; 2:1-6; Isa. 6:8), lakini haiwezi kumaanisha kwamba malaika walikuwa na sehemu katika uumbaji wala kwamba wala sura ya kiungu. Wengine wanadhani kwamba ni mfumo pokezi wa dhana ya Utatu Mtakatifu. Kinachofurahisha ni ukweli kwamba masimulizi ya uumbaji wa miungu wa Kimesopotamia (siku zote kuunganishwa kwa mji mmoja mmoja) na siku zote wakishindana wao kwa wao lakini hapa sio tu ni hali ya imani kwa Mungu yenye ushahidi lakini katika vielezo vichache vya WINGI kuna amani na kutoridhika.

◙ **"mtu"** Hili ni neno la kiebrania "Adamu" (BDB 9), ambalo ni utani wa wazi, *adamah* (kama vile Mstari 9). Neno pia linaweza pia kumaanisha "wekundu." Wana taaluma wengi wanaamini kwamba hii inamaanisha wanadamu kutengenezwa kutoka udongo mwekundu au mfinyanzi wa bonde la mto Hedekeli/Frati (kama vile. 2:7). Ni katika sura za Mwanzo za ufunguzi tu ndipo palipo na maneno ya Kiebrania"Adamu" lililotumika kama jina sahihi. Tafsiri ya Agano la Kale la Kiebrania linatumia neno *anthropos* kufasiri neno hili ambalo ni neno la kiujumla

linalomaanisha wanadamu na/au wanawake (kama vile 5:2; 6:1,5-7; 9:56). Neno la kawaida zaidi kwa mwanaume au mme ni *ish* (BDB 35, kama vile 2:23 asili haijulikani) na *ishah* (BDB 61) kwa mwanamke au mke. Kwa hatua hii katika uelewa wangu wa kithiolojia ni ngumu sana kuhusianisha masimulizi ya kibiblia ya uumbaji na jozi za asili pamoja na mabaki ya viumbe ya aina kadhaa ya wakati wa kutembea na miguu miwili *Homo erectus*. Baadhi ya maeneo ya makaburi yanajumuisha vitu ambavyo kidhahiri vimeunganishwa na kuamini katika baada ya maisha haya. Siudhiki na mabadiliko ndani ya viumbe. Ikiwa hivi ndivyo hivyo Adamu ma Hawa ni wanadamu wa kipindi cha wanadamu wa kale na muda wa kihistoria wa Mwanzo 1-11 lazima kimsingi ipanuliwe. Yawezekana Mungu alimuumba Adamu na Hawa katika kipindi cha baadaye cha muda (yaani uumbaji endelevu), making them akiwafanya wanadamu wa "sasa" (*Homo sapiens*). Ikiwa hivyo ndivyo, sasa mahusiano yao na ustaarabu wa Ki-Mesopotamia unadai uumbaji maalum wakati mwingine karibu na utamaduni unapoanzia. Nataka kusisitiza kwamba hii ni madhanio tu kwa wakati huu. Kuna vingi ambavyo wa kisasa hawajui kuhusu kale iliyopita. Tena, kithiolojia "nani" na "kwanini," na sio "kwa namna gani" au "lini" ni muhimu!

◙ **"kwa sura yetu na mfano wetu"** Neno "sura" inaweza pia kupatikana katika 5:1,3; 9:6. Mara kwa mara inatumika katika Agano la Kale kuashiria sanamu (KB 1028 II). Asili yake ya kimsingi ni "kupata sura ya umbo fulani." Kumekuwa na majadala mkubwa katika historia ya utafsiri kubainisha maana halisi ya sura (BDB 853, KB 1028 #5) na mfano (BDB 198). Maneno ya Kiyunani Yanayolinganishwa yanapatikana katika Agano Jipya kuelezea ubinadamu (kama vile I Kor. 11:7; Kol. 3:10; Efe. 4:24; Yak. 3:9. Kwa mawazo yangu mwenyewe ni visawe na yanaelezea sehemu za ubinadamu ambazo kwa upekee zina uwezo wa kuhusianishwa na Mungu. Kuvaa mwili kwa Yesu kunaonesha uwezekano wa nini kile ambacho mwanadamu angeweza kuwa katika Adamu na atakavyokuwa siku moja kupitia Yesu Kristo. Angalia *Who was Adam?* Kilichoandikwa na Fazale Rana na Hugh Ross, ukurasa wa 79.

◙ **"na wakatawale"** Hii kidhahiri ni "kukanyaga chini" (BDB 853, KB 1190, *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU uliotumika katika namna ya KAULI AMRISHI). Hili ni neno la nguvu ambalo linazungumzia utawala wa mwanadamu juu ya asili (kama vile Zab. 8:5-8) Dhana hii hii inapatikana katika mstari wa 28. Maneno mawili, "kutawala" katika mistari ya 26 na 28, na "kutiisha" katika mstari wa 28 kuna asili ya msingi ile ile ambayo inamaanisha "kukanyaga" au "kukanyaga." Ingawa VITENZI hivi vinaonekana vigumu, vinaaksi sura ya utawala wa Mungu. Mwanadamu ana utaala juu ya dunia iliyoumbwa kwa sababu ya uhusiano wake na Mungu. Walitakiwa kutawala/kuwa juu kama wawakilishi wake, katika tabia yake. Nguvu si suala la kithiolojia lakini ni namna llinavyofanyiwa kazi (kwa ajili yake binafsi na kwa ajili ya uzuri wa wengine)! Tazama WINGI, ambao unamaanisha utawala wa pamoja kati ya mwanamke na mwanamume (kama vile 5:23). Pia tazama wingi wa KAULI SHURUTISHI ya mstari wa 28. Unyenyekevu wa mwanamke unakuja tu baada ya kuanguka kwa sura ya 3. Swali halisi ni, "Je unyenyekevu huu unabaki baada ya kizazi kipya katika Kristo"?

**1:27 "Mungu akaumba"** Kuna matumizi ya pande tatu (*Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ikifuatiwa na KAULI TIMILIFU *Qal*) ya neno *bara* (BDB 127) katika mstari huu, ambao unafanya kazi kama kauli ya kimutasari na pia kama msisitizo juu ya uumbaji wa mwanadamu kama mke na mume. Hii imechapishwa kama ushairi katika matoleo ya NRSV, NJB kutambuliwa hivyo katika dokezo la toleo la NIV. Neno *bara* linatumika tu katika Agano la Kale kwa Mungu kuumba.

◙**"kwa Sura yake mwenyewe"** Inashangaza sana kwamba WINGI wa mstari wa 26 sasa upo katika UMOJA. Hii inajumuishwa katika maajabu ya WINGI (BDB 853) ni sawa katika wanaume na wanawake!

◙ **"mwanaume na mwanamke Aliwaumba"** Kipengele chetu cha kujamiiana kinahusianishwa na mahitaji na mazingira ya sayari hii. Mungu anaendelea kutenganisha (angalia dokezo katika 1:4). Tazama u-pamoja hapa, katika 2:18 and 5:2. Sura zetu za kiungu zinaruruhusu kuhusiana na Mungu kipekee.

**1:28 "Mungu akawabarikia . . . Zaeni mkaongezeke"** Sehemu ya Baraka za Mungu (BDB 138, KB 159, *Piel* KAULI ZA WAKATI USIO TIMILIFU) ulikuwa ni uumbaji unaoendelea (kama vile Kumb. 7:13). Baraka hii ilikuwa kwa wote juu ya wanyama (kama vile Mstari wa 22) juu ya mwanadamu (kama vile mstari wa 28;9:1,7). Masimulizi ya

uumbaji wa Kimesopotamia yanatoa taarifa ya kelele ya wanadamu kujaa ni sababu ya uharibifu wa miungu ya kibinadamu. Mwanzo na masimulizi yake inahamasisha kukua kwa idadi ya watu. Inashangaza kwamba kitendo cha kwanza cha uasi (kama vile Mwanzo 10-11) kilikuwa ni hali ya mwanadamu kutotaka kuachana na kuijaza dunia.

◙**"kuitiisha na kuitawala"** Kuna amri mbili katika andiko la Kiebrania ambalo ni sambamba na neno "kuzaa na kuongezeka" (mfululizo wa tatu wa KAULI SHURUTISHI *Qal*). Inafanya vyote kujamiina kwa mwanadamu kuongoza mapenzi ya Mungu.
Vitenzi vyote viwili vya kiebrania, "kutiisha" (BDB 461, KB 460) na "kutawala" (BDB 921, KB 1190), vinaweza kuwa na kidokezo hasi (yaani utawala wa kikatili). Muktadha hasa lazima uamue ikiwa maana ni ya kipole au kichokozi.

**1:29** Jamii ya wanyama imegawanyika katika makundi matatu tofautitofauti. Mnyororo wa utengenezaji wa chakula unaanza na usanidinuru. Maisha ya wanyama wote wa duniani yanategemeana na muujiza wa maisha ya mmea. Katika mstari huu, mwanadamu amepewa nafaka na matunda kwa ajili ya chakula (kama vile 2:16; 6:21), wakati kundi la tatu, majani yanatolewa kwa wanyama. Haikufanyika mpaka baada ya mafuriko kwamba wanadamu walikuwa wanaruhusiwa kula nyama (kama vile Mwanzo 9:3). Hii inaweza kuwa inaunganishwa na ukweli kwamba hakukuwa na mavuno yanayowezekana huo mwaka. Sio sawa kithiolojia kuchukua sheria za kiulimwengu za vyakula kutoka Mwanzo 1. Inawezekana kwamba maelezo haya yanahusiana tu na Bustani ya Edeni. Kifo na wanyama walao nyama wanarudi katika mabaki ya kale kabisa ya viumbe yanayohusiana na tabaka la Cambrian miaka iliyopita 500,000 ambapo kumbukumbu zilizowekwa kama mabaki ya viumbe hai inaanza na utele.

**1:30 "majani yote ya miche, ndiyo chakula chenu"** Msukumo wa kauli hii ni kwamba uhai wote umejikita juu ya mchakato wa usanidinuru (yaani mnyororo wa chakula).

**1:31 "ilikuwa njema sana"** Hii ni hitimisho lenye umuhiu mkubwa sana kwa uumbaji kwasababu katika mawazo ya walimu wa uongo wa Kiyunani, maada ni uovu na roho ni nzuri. Katika mfumo huu wa Kiyunani (na pia katika baadhi ya maandiko ya Mesopotamia) vyote maada na roho vinategemeana na kufanya kazi kwa pamoja yanakuwa kama maelezo yao ya matatizo ya dunia. 35 lakini katika masimulizi ya Kiebrania. Ni Mungu tu ndiye wa milele na maada inaumbwa kwa kusudi lake. Hakukuwa na uovu katika uumbaji wa asili wa Mungu "uhuru"!

◙**"ikawa jioni, ikawa asubuhi, siku ya sita"** Ni muhimu kujua kwamba, kama siku ya tatu, siku ya sita ina matukio mawili ya kiuumbaji, hivyo kuma matukio manane ya uumbaji katika siku ya sita. Walimu wanaanza siku mpya katika utusiutusi, "jioni na asubuhi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2:1-3**
**[1] Basi mbingu na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote. [2] Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya; akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya. [3] Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa kwa sababu katika siku hiyo Mungu alistarehe, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoiumba na kuifanya.**

**2:1 "mbingu"**Hili ni neno (BDB 1029) linamaanisha anga la hewa juu ya dunia. Katika baadhi ya muktadha inamaanisha mbingu ing'aayo juu ya anga la hewa.

◙**"na nchi zikamalizika, na jeshi lake lote"** Uumbaji wa kimwili wa Mungu ulikuwa umefikia kupevuka (BDB 477, KB 476, *Pual* KAULI ISIO TIMILIFU, mstari wa 1 na *Piel* KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU, mstari wa 2). Sasa ilikuwa tayari kwa ajili ya kukaliwa na binadamu. Kila hatua ya uumbaji ina wakazi wake halisi (yaani "majeshi" BDB 838). Hii haimaanishi hasa uumbaji wa malaika (isipokuwa 1:1 inawajumuisha). Andiko hili linahusu uumbaji wa kimwili. Neno la Kiebrania "majeshi," katika baadhi ya muktadha, inamaanisha (1) Kuabudu miungu kwa Ki-Mesopotamia

kulikounganishwa na mianga ya kimbingu (yaani jua, mwezi, nyota, vimondo, sayari (kama vile Kumb. 4:19) au (2) jeshi la Kimalaika la YHWH (kama vile Josh. 5:14), lakini hapa kwa aina mbali mbali za uhai uliotengenezwa.

**2:2 “Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote”** Hii ni namna ya lugha ya kibinadamu kumwelezea Mungu lakini haimaanishi kwamba Mungu alikuwa amechoka au kwamba aliacha moja kwa moja uhusika wake wa kiutendaji wa kuendelea na uumbaji na mwanadamu. Huu ni utaratibu wa msingi uliandaliwa na mwanadamu anayehitaji mapumziko ya mara kwa mara na kuabudu.

◙**“akastarehe”** Huu ni mzizi ule ule wa kiebrania“Sabato” (BDB 991, KB 1407, *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, kama vile Kut. 20:11; 31:12-17). Kumb. 5:15 kinatoa sababu nyingine kwa ajili ya Sabato kwa ajili ya sababu za kijamii, sio sababu za kithiolojia kama katika Kut. 20:8:11. Neno hili linatumika katika namna kadhaa tofauti tofauti na hasa Agano Jipya katika kitabu cha Ebr. 3:7-4:11 na fasiri zake za Zab. 95:7-11. Katika Waebrania neno hili “pumziko” inafanya kazi kwa wote pumziko la sabato, Nchi ya Ahadi, na ushirika pamoja na Mungu (mbingu). Mungu anaandaa mfano kwa uumbaji wake maalumu, mwanadamu. Ushirika wake wa mara kwa mara kati ya Mungu na mwanadamu haujaweka wazi lakini kimuktadha kiini cha kusudi la uumbaji!

◙**“siku ya saba”** Siku ya 1-6 inaanza na jioni na kufungwa na asubuhi (kama vile 1:31), lakini siku ya saba asubuhi haikuwahi kutajwa. Hivyo walimu na pia mwandishi wa Waebrania ya Agano Jipya (3:7-4:11) wanatumia hii kuhitimisha kwamba mapumziko ya Mungu bado yanapatikana (kama vile Zab. 95:7-11).

**2:3“Mungu akaibarikia siku ya saba, akaitakasa”** Neno “kutakaswa” maana “kufanywa takatifu” (BDB 872, KB 1073, *Piel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). Neno hili linatumika katika namna ya kuweka kitu kando kwa ajili ya matumizi ya Mungu. Mapema sana Mungu alianzisha siku maalumu kwa ajili yake na mwanadamu kuwa na ushirika. Hii haimaanishi kwamba siku zingine sio za Mungu lakini moja ni ya kipekee ikitengwa pembeni kwa ajili ya ushirika, ibada, sifa na pumziko linalotia nguvu. Asili ya siku ya saba ya wiki inafunikwa katika nyakati za kale na maajabu. Mtu anaweza kuona namna gani mwezi unahusiana na tungo za mwezi na namna gani mwaka unahusiana na mabadiliko ya kimajira.Hatahivyo kila tamaduni za kale ambazo tunazozijua zinaonekana kujulikana kuihusu wakati historia iliyoandikwa ilianza.

## MADA MAALUMU: KUABUDU

I. Utangulizi

A. Baadhi ya maswali muhimu
   1. kuabudu ni nini?
   2. lini na kwa namna gani kuabudu kulianza?
   3. Nini maudhui yake?
   4. Watu gani walishiriki?
   5. Wapi na lini kuabudu kunafanyika?

B. Maswali haya yatajenga muainisho wa kujifunza kwetu. Lazima ikumbukwe kwamba hakuna majibu hasa ya maswali haya, lakini maana za kimaandiko na makuzi ya kihistoria.

II. Kuabudu ni nini?
   A. Neno la kingereza linatoka katika neno la ki-Saxon, “weorthscipe,” ambalo linamaanisha ambaye anastahili kupewa heshima na adhama.
   B. Maneno makubwa ya Agano la Kale ni:
      1. *‘Abodah*, ambalo linatokea katika mzizi wa Kiebrania “kutumikia” au “kufanya kazi” (BDB 715). Siku zote linafasiriwa “huduma ya Mungu.”
      2. *Hishtahawah*, ambalo inatoka katika mzizi wa kiebrania ambayo inamaanisha “kusujudu” au “mtu kujishusha mwenyewe” (BDB 1005, kama vile Kut. 4:31).
   C. Maneno makubwa ya Agano Jipya yanafuata maneno ya kiebrania.
      1. Kwa *‘abodah* kuna *latreia*, ambayo ni hali ya mfanyakazi aliyeajiliwa au mtumwa.
      2. Kwa *hishtahawah* kuna *proskuneo,* ambayo inamaana“kushuka mwenyewe,” “kutukuza,”

au "kuabudu."(BDB 1005, kama vile Kut. 4:30)

D. Tambua kwamba kuna maeneo mawili ambayo kuabudu kunaleta matokeo.
   1. mtazamo wetu wa heshima
   2. matendo yetu ya mtindo wa maisha

Haya mawili lazima yaende pamoja au kama sivyo matatizo makubwa yatatokea (kama vile Kumb. 11:13).

III. Lini na kwa namna gani ilianza?

A. Agano la Kale halitaji bayana asili ya kuabudu, lakini kuna dondoo kadhaa katika Mwanzo.
   1. Taasisi ya Mungu ya Sabato katika Mwanzo 2:1-3 baadaye inakuzwa katika ibada ya siku ya kila wiki. Katika Mwanzo inataja kwamba Mungu aliandaa kabla pumziko la mwanadamu na kuabudu kwa matendo yake na mtazamo wake kuelekea kipengele cha muda.
   2. Kuuliwa kwa wanyama kunakofanywa na Mungu ili kupata mavazi na kuwafunika wanandoa walianguka ili waweze kustahimili mazingira yao mapya ya anguko katika Mwanzo 3:21 inaonekana kuandaa jukwaa kwa ajili ya kutumia wanyama kwa ajili ya mahitaji ya mwanadamu, ambayo yatakuzwa kama mfumo wa kidhabihu.
   3. Sadaka ya Kaini na Habili ya Mwanzo 4:3ff inaonekana kuwa tukio la mara kwa mara, na sio tukio la mara moja. Hii sio kifungu cha habari cha mparanganyiko juu ya matoleo ya mimea ya majani au pendekezo kwa ajili ya sadaka ya wanyama, lakini mfano halisi kwa mahitaji ya matazamo sahihi kumuelekea Mungu. Haimuoneshi Mungu kwamba kwa namna fulani Mungu alizungumzia kukubaliwa kwake na kukataliwa.
   4. Mpaka wa Umasihi wa kimungu wa Sethi unakuzwa katika Mwanzo. 4:25 na kuendelea. Inataja jina la Agano la Mungu, YHWH, katika Mstari wa 26 katika mazingira ya kuabudu kuliko wazi (kifungu hiki cha habari lazima kipatanishwe na Kut. 6:3).
   5. Nuhu anazungumzia utofauti kati ya wanyama walio safi na wasio safi katika Mwanzo 7:2. Hii inaandaa mazingira kwa ajili ya sadaka zake katika Mwanzo 8:20-21. Hii inamaanisha kwamba sadaka zake zilikuwa zime asisiwa katika kipindi cha mwanzo.
   6. Ibrahimu alifahamu sana habari za Sadaka, jambo lililo wazi kutoka Mwanzo 12:7,8; 13:18; 22:9. Inatengeneza muitikio wake kwa uwepo wa Mungu na ahadi. Kiudhahiri uzao wake uliendeleza tendo hili.
   7. Kitabu cha Ayubu katika mazingira ya utume wa uzao wa kiume (yaani 2000 K.K). Alikuwa anafahamu juu ya sadaka kama inavyoonekana katika Ayubu 1:5.
   8. Vitu vya Kibiblia vinaonekana kuweka wazi kwamba sadaka ilikuzwa nje ya shauku ya mwanadamu na heshima kwa Mungu taratibu zilizofunuliwa na Mungu namna ya kuelezea hili.
      a. sheria kumi na kanuni za utakatifu
      b. desturi za hema takatifu

IV. Je maudhui yake ni nini?

A. Ni dhahiri kwamba mtazamo wa mwanadamu ndio ufunguo katika dhabihu (kama vile Mwanzo 4:3 na kuendelea). Hii elementi ya kibinafsi siku zote imekuwa nguzo katika imani iliyofunuliwa kibiblia (kama vile Kumb. 6:4-9; 11:13; 30:6; Yer. 31:31-34; Ezek. 36:26-27; Rum. 2:28-29; Gal. 6:15).

B. Hata hivyo mtazamo wa wa heshima wa mwanadamu uliwekewa siri katika ibada mapema sana.
   1. ibada za utakazo (inayohusiana na namna ya dhambi)
   2. ibada za huduma (sherehe, dhabihu, zawadi, n.k)
   3. ibada ya kuabudu kwa binafsi (maombi ya jumuiya na binafsi na sifa)

C. Tunapouliza swali la maudhui, ni muhimu kwamba tutambue vyanzo vitatu vya ufunuo (kama vile Yer. 18:18).
   1. Musa na mfumo wa kidini wa kuabudu (makuhani)
   2. Busara za Fasihi za hekima

3. Manabii

Kila moja ya hizi imeongezwa kwa ajili ya uelewa wetu wa kuabudu. Kila moja imeweka shabaha katika vipengele muhimu vya kuendelea kuabudu.

1. muundo (Kutoka - Hesabu)
2. mtindo wa maisha (Zab. 40:1 na kuendelea; Mik. 6:6-8)
3. nia (I Sam. 15:22; Yer. 7:22-26; Hos. 6:6)

D. Yesu anafuata utaratibu wa Agano la Kale wa kuabudu. Hakuridhihaki Agano la Kale (kama vile Mt. 5:17 na kuendelea), lakini alikataa desturi za mdomo kama zilivyokuwa zimekuzwa na karne ya kwanza.

E. Kanisa la kwanza liiliendelea na dini ya Kiyahudi kwa muda (yaani mpaka uamsho wa kiualimu na mabadiliko ya mwaka 90 b.k) na baadaye wakaanza kukuza upekee wao wenyewe, lakini kwa ujumla katika utaratibu wa kisinagogi. Ile dhima ya Yesu, Maisha yake, mafundisho yake, kusulubishwa kwake na kufufuaka kwake kulichukua nafasi ya mfumo wa ibada za kidini wa Agano la Kale. Mahubiri, ubatizo, na Ekaristia ilifanyika kiini cha matendo. Sabato ilichukuliwa na Siku ya Bwana.

V. Nani anayeshiriki?

A. Desturi za ukoo wa kiaskofu za Mashariki ya Karibu ya kale inaweka jukwaa kwa ajili ya nafasi ya uongozi katika maeneo yote ya maisha ikijumuisha dini.

B. Mfumo wa kiaskofu ulifanya kazi kama kuhani kwa familia yake katika vyote kidhabibu na kimaelekezo ya dini (Ayubu 1:5).

C. Kwa Waisraeli kuhani alifanya majukumu katika umma, mazingira ya kuabudu ya watu wote, wakati baba alibaki na nafasi yake katika mazingira binafsi ya kuabudu. Pamoja na Uhamisho wa Babeli (586 K.K.) Sinagogi na walimu wa Kiyahudi walikua katika nafasi muhimu katika mafunzo na kuabudu. Baada ya kuharibiwa kwa Hekalu mwaka 70 B.K, dini ya Kiyahudi ya kiualimu ambayo ilikua kutoka Mafarisayo ilikuwa inatawala.

D. Katika mazingira ya utaratibu wa mfumo wa kiaskofu unatunzwa lakini ukiwa na msisitizo ulioongezwa juu ya karama ya wanawake kama usawa (kama vile I Kor. 11:5; Gal. 3:28; Mdo. 21:9; Rum. 16:1; II Tim. 3:11). Huu usawa katika Mwanzo 1:26-27; 2:18. Huu usawa unaharibiwa na uasi wa Mwanzo 3, lakini unarejeshwa kupitia Kristo. Watoto siku zote wamekuwa wakishirikishwa katika mazingira ya kuabudu kupitia wazazi wao, hatahivyo Biblia ni kitabu ambacho kiko kiutu uzima kimuundo.

VI. Wapi na lini kuabudu kunafanyika?

A. Katika Mwanzo ubinadamu unaheshimu nafasi na mahali walipokutana na Mungu. Maeneo haya huitwa madhabahu. Baada ya kuvuka Yordani maeneo kadhaa yanakuzwa (Gilgali, Betheli, Shekemu), lakini Yerusalemu ni mahali maalum makazi ya Mungu panapounganishwa na Sanduku la Agano (kama vile Kumb.).

B. Nyakati za Kibiblia zimekuwa siku zote kwa ajili ya shukurani kwa Mungu kwa ajili ya utoaji wake. Mahitaji mengine maalum yanayohisiwa kama vile msamaha, yalikuzwa katika siku maalum za kimadhehebu (yaani mambo ya Walawi 16, Siku ya upatanisho). Dini ya Kiyahudi ilianzisha siku za sherehe—Pasaka, Pentekoste, na Hema (kama vile Mambo ya Walawi 23). Lakini pia iliruhusu fursa maalum kwa ajili ya mtu mmoja mmoja (kama vile Ezek. 18).

C. Ukuaji wa Sinagogi ulitoa umbo la dhana ya kuabudu Sabato. Kanisa lilibadili hii kwenda katika Siku ya Bwana (siku ya kwanza ya wiki) inavyoonekana ni juu ya utaratibu unaojirudia wa Yesu wa kuwatokea siku ya Jumapili jioni baada ya Ufufuo.

D. Kwa mara ya Kwanza kanisa la Kwanza lilikutana kila siku (Mdo. 2:46), lakini hii kidhahiri muda mfupi iliachwa kwa ajili ya ibada binafsi wakati wa wiki na kuabudu pamoja siku za Jumapili.

VII. Hitimisho

A. Kuabudu Mungu si jambo ambalo Wanadamu waligundua au kuanzisha. Kuabudu ni hitaji la kujiskia.

B. Kuabudu ni mwitikio kwa namna Mungu alivyo na kile ambacho Mungu alikuwa amefanya kwa

ajili yetu katika Kristo.

C. Kuabudu kunajumuisha mtu kamili. Ni katika muundo wote wa aina mbili na matazamo. Ni katika vyote umma na binafsi. Ni katika vyote vilivyo pangwa na vya papo kwa papo.
D. Ibada ya kweli ni uhusiano binafsi wa ukuaji
E. Kifungu cha kithiolojia chenye msaada zaidi katika agano jipya juu ya kuabudu yumkini ni Yn. 4:19-26

◙**"kufanya"** Hii kidhahiri ni "kufanya." matendo ya Mungu ya Uumbaji yanaendelea (BDB 793 I, KB 889, *Qal* TUNGO ISIYO NA KIKOMO). Mungu aliumba viumbe vyenye miili ili vikue. Tungo inayojirudia "zaeni mkaongezeke na kuijaza dunia" inaaksi muundo wa Mungu na mpango. Mungu aliumba viumbe hai (ikijumuisha wanadamu) ambavyo vinajizalisha vyenyewe kila kimoja kwa

# MWANZO 2:4-25

| MGAWANYO WA AYA WA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Uumbaji wa Mwanaume na Mwanamke | (1:1-2:7) | uumbaji wa mwanaume na Mwanamke | Bustani ya Edeni | Paradiso na jaribu la Utashi |
| 2:4-9 | | 2:4b-9 | 2:4b-6 | 2:4b-7 |
| | Maisha katika Bustani ya Edeni | | 2:7 | |
| | 2:8-9 | | 2:8-9 | 2:8-9 |
| 2:10-14 | 2:10-14 | 2:10-14 | 2:10-14 | 2:10-14 |
| 2:15-17 | 2:15-17 | 2:15-17 | 2:15-17 | 2:15-17 |
| 2:18-25 | 2:18-25 | 2:18-25 | 2:18-20 | 2:18-23 |
| | | | 2:21-24 | (23) |
| (23) | (23) | (23) | (23) | 2:24 |
| | | | 2:25 | 2:25 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa vii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

5. Aya ya kwanza
6. Aya ya pili
7. Aya tatu
8. N.k

## MAZINGIRA YA NYUMA

A. Binafsi nakataa nadharia ya chanzo cha ukosoaji Y(YHWH), E (Elohim), K (Kumbu kumbu la Torati), M (Makuhani) ambayo inaelezea waandishi tofauti kwa vitabu kadhaa Vya Musa vya Agano la Kale (kama vile utangulizi wa Mwanzo, Uanataaluma wa kisasa, D.). Kwa taarifa zaidi juu ya somo hili soma Josh McDowell's More Evidence that Demands a Verdict au H. C. Leupold's Exposition of Genesis, vjuzuu. 1.
B. Mwanzo 2:4-25 ni upanuzi wa ubayana wa kithiolojia wa Mwanzo 1:1-2:3. Hii ni mbinu ya Kiebrania inayotumika sana kifasihi. Kithiolojia Sura ya pili inaweka jukwaa kwa ajili ya sura ya tatu.
C. Mwanzo 1:31 inaweka taji ya mwanzo wa ulimwengu wetu pamoja na kusudio la Mungu "wema"; 2:1-3 inatakiwa iende na Sura ya 1 kwasababu 1:1-2:3 ni kipengele cha kifasihi.
D. Kithiolojia 2:4-25 ina uhusiano zaidi na sura ya 3 kuliko sura ya 1. Inaanzisha jukwaa la kifasihi kwa majaribu ya Hawa na dhambi pamoja na madhara yake ya kutisha kwa sayari nzima (kama vile Rum. 5:12-21; 8:18-23).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 2:4-9**
**[4] Hivyo ndivyo vizazi vya mbingu na nchi zilipoumbwa. Siku ile Bwana Mungu alipoziumba mbingu na nchi [5] hapakuwa na mche wa kondeni bado, wala mboga ya kondeni haijachipuka bado, kwa maana Bwana Mungu hajainyeshea nchi mvua, wala hapana mtu wa kuilima ardhi; [6] ukungu ukapanda katika nchi, ukatia maji juu ya uso wote wa ardhi. [7] Bwana Mungu akamfanya mtu kwa mavumbi ya ardhi, akampulizia puani pumzi ya uhai; mtu akawa nafsi hai. [8] Bwana Mungu akapanda bustani upande wa mashariki wa Edeni, akamweka ndani yake huyo mtu aliyemfanya. [9] Bwana Mungu akachipusha katika ardhi kila mti unaotamanika kwa macho na kufaa kwa kuliwa; na mti wa uzima katikati ya bustani, na mti wa ujuzi wa mema na mabaya.**

**2:4 "Hivyo ndivyo vizazi"** Kiuhalisia hii ni "Hivi ndivyo vizazi" (BDB 41 jumlisha 410). Tungo hii ni njia ya mwandishi ya kuigawa Mwanzo katika sehemu za kifasihi (kama vile 5:1; 6:9; 10:1; 11:10,27; 25:12,19; 36:1,8; 37:2, yaani hii ni njia ya kuainisha kitabu chake). Baadhi ya wanataaluma wanaliona kama sehemu ya utangulizi (yaani Derek Kidner) wakati wengine wanaona kama sehemu ya hitimisho (yaani R. K. Harrison na P. J. Wiseman). Inaonekana kufanya kazi zote mbili. Inawezekana kwamba 1:1-2:3 inshughulikia uumbaji wa ulimwengu mzima 2:4- 15 inaweka shabaha juu ya uumbaji wa mwanadamu jambo ambalo kimuktadha inahusiana na sura za 3 andna 4.

◙**"siku"** Neno la Kiebrania *yom* (BDB 398) siku zote linatumika kwa muda wa masaa 24. Hatahivyo linatumika pia kwa vipindi virefu kama sitiari (kama vile 2:4; 5:2; Ruth 1:1; Isa. 2:11,12,17; 4:2; Zab. 90:4). Yawezekana mstari wa 4a ni kichwa kidogo cha habari na 4b unaanza mjadala. Angalia Mada Maalum katika 1:5.

◙**"BWANA Mungu"** Hii kiuhalisia ni YHWH Elohim ambalo linaunganisha majina mawili yaliyozoeleka kwa Mungu. Hii ni mara ya kwanza yanatumiwa yote kwa pamoja. Wanataaluma wengi wa kisasa wamedhania kuwa na waandishi wawili wa Mwanzo 1 na 2 kwasababu ya matumizi ya majina haya ya ki-Ungu. Hatahivyo walimu wanaelezea kwamba yanamaanisha tabia za ki-Ungu: (1) Elohim ni muumbaji, mtoaji na mtoshelezaji wa maisha yote juu ya sayari hii (kama vile Zaburi 19:1-6) na (2) YHWH ni mwokozi, mkombozi na uungu ufanyao agano (kama vile Zaburi 19:7-14). Kithiolojia inamaanisha Mungu pekee na aishiye milele. Wayahudi walikuwa na hofu kulitamka jina hili takatifu wasije wakavunja amri kuhusu kulitaja bure jina la Mungu. Hivyo, walitafuta jina mbadala la Kiebrania *Adon* (mume, mmiliki, bwana, mkuu, mtawala) mara zote waliposoma maandiko kwa sauti ya juu. Hii ndio maana neno la Kiinereza YHWH inafasiriwa kama BWANA.

## MADA MAALUM: MAJINA YA UUNGU

A. *El* (BDB 42, KB 48)
   1. maana ya asili ya jina la jumla la kale kwa ajili ya Uungu haijulikani, ingawa wanataaluma wengi wanaamini linatoka katika mzizi wao wa lugha ya Akkadia, "kuwa shupavu" au "kuwa mwenye nguvu" (kama vile Mwanzo 17:1; Hesabu 23:19; Kumb 7:21; Zab. 50:1).
   2. Katika hekalu la miungu ya Wakanaani mungu mkuu ni *El* (maandiko ya Ras Shamra),akaitwa "baba wa miungu" na "bwana wa mbinguni"
   3. Kalika Biblia *El* mara nyingi huwa haliambatani na maneno mengine. Miunganiko hii ilifanyika njia ya kuainisha tabia za Mungu.
      a. *El-Elyon* (Mungu aliye Mkuu sana BDB 42 & 751 II ), Mwanzo 14:18-22; Kumb. 32:8; Isa. 14:14
      b. *El-Roi* ("Mungu aonaye" au "Mungu ajifunuaye Mwenyewe" BDB 42 & 909), Mwanzo 16:13
      c. *El-Shaddai* ("Mungu Mkuu" au "Mungu mwenye huruma zote" au "Mungu wa mlima"), BDB 42 & 994)Mwanzo 17:1; 35:11; 43:14; 49:25; Kutoka 6:3
      d. *El-Olam* (Mungu wa milele yote), Mwanzo 21:33. Neno hili linaunganishwa na ahadi ya Mungu kwa Daudi, II Sam. 7:13,16

e. *El-Berit* (Mungu wa Agano"), BDB 42 & 136), Waamuzi 9:46

4. *El* inalinganishwa na
    a. YHWH katika Zaburi. 16:1-2; 85:8; Isa. 42:5, Hes. 23:8
    b. *Elohim* katika Mwanzo 46:3; Ayubu5:8, "Mimi ni *El*, *Elohim* wa baba yako
    c. *Shaddai* katika Mwanzo. 49:25
    d. "wivu" katika Kut. 34:14; Kumb. 4:24; 5:9; 6:15
    e. "rehema" katika Kumb. 4:31; Neh. 9:31
    f. "mkuu na mzuri" katika Kumb. 7:21; 10:17; Neh. 1:5; 9:32; Dan. 9:4
    g. "maarifa" katika I Sam. 2:3
    h. "kimbilio langu" katika II Sam. 22:33
    i. "mlipa kisasi wangu" katika II Sam. 22:48
    j. "mtakatifu" katika Isa. 5:16
    k. "muweza" katika Isa. 10:21
    l. "wokovu wangu" katika Isa. 12:2
    m. "mkuu na mwenye nguvu" katika Yer. 32:18
    n. "anayepatiliza: katika Yer. 51:56
5. Muunganiko wa majina yote makubwa ya Agano la Kale yanapatikana katika Joshua 22:22 (*El, Elohim, YHWH,* kurudiwa)

B. *Elyon* (BDB 751, KB 832)
1. Maana yake ya msingi ni "juu," "aliyetukuzwa," au "kuinuliwa" (kama vile Mwanzo 40:17; I Wafalme. 9:8; II Wafalme.
18:17; Neh. 3:25; Yer. 20:2; 36:10; Zab. 18:13).
2. Inatumika katika namna ya usambamba wa majina mengine/vyeo vya Mungu.
    a. *Elohim* – Zab. 47:1-2; 73:11; 107:11
    b. *YHWH* - Mwanzo 14:22; II am. 22:14
    c. *El-Shaddai* - Zab. 91:1,9
    d. *El* - Hes. 24:16
    e. *Elah* - iliyotumika mara kwa mara katika Danieli 2-6 na Ezra 4-7, inaunganishwa pamoja na *illair* (Kiaramaiki kwa ajili ya "Mungu aliye Juu") katika Dan. 3:26; 4:2; 5:18,21
3. Mara kwa mara inatumika kwa wasio waisraeli.
    a. Melkizedeki, Mwanzo 14:18-22
    b. Balaamu, Hes. 24:15
    c. Musa akizungumzia Mataifa katika Kumb. 32:8
    d. Injili ya Luka katika Agano Jipya, akiandika kwa Mataifa, pia akitumia maneno ya kufanana na Kiyunani *Hupsistos* (kama vile 1:32,35,76; 6:35; 8:28; Mdo 7:48; 16:17)

C. *Elohim* (wingi), *Eloah* (umoja), inatumika kimsingi katika ushairi (BDB 43, KB 52)
1. Neno hili halipatikani nje ya Agano la Kale.
2. Neno hili linaweza kumaanisha Mungu wa Israeli au miungu wa Mataifa (kama vile Kut. 12:12; 20:3). Familia ya Ibrahimu walikuwa Waabudu miungu wengi (kama vile Josh. 24:2).
3. Inaweza kumaanisha waamuzi wa kibinadamu (kama vile Kut. 21:6; Zab. 82:6)
4. Neno *elohim* pia linatumika juu ya viumbe vingine vya kiroho (malaika na mapepo) kama ilivyo katika Kumb. 32:8 (LXX); Zab. 8:5; Ayubu 1:6; 38:7.
5. Katika Biblia cheo cha kwanza, jina kwa ajili ya Uungu (kama vile Mwanzo. 1:1). Linatumika bila mjumuisho mpaka Mwanzo. 2:4, ambapo linaunganishwa na YHWH. Kimsingi (kithiolojia) linamaanisha muumbaji, mtoshelevu na mpaji wa uhai wote juu ya sayari hii (kama vile Zab. 104). Ni sawa na kisawe *El* (kama vile Kumb. 32:15-19). Pia linaweza kuwa likifanana na YHWH kama Zab. 14 (*Elohim* KUR. 1,2,5; YHWH, kur. 2,6; hata *Adoni*, uk. 4) ni sawasawa kabisa na Zab. 53 (YHWH), isipokuwa kwa mabadiliko katika majina ya kiungu.
6. Ingawa wingi unatumika juu ya miungu mingine, neno hili mara kwa mara linamaanisha Mungu wa Israeli lakini siku zote lina kitenzi cha umoja kuelezea matumizi ya imani juu ya Mungu mmoja kama mtawala juu ya dunia nzima.

7. Inashangaza kwamba jina lililozoeleka kwa imani juu ya Mungu mmoja wa Israeli liko katika Wingi! Ingawa hakuna uhakika, hapa zipo nadharia.
    a. Lugha ya Kiebrania ina maneno mengi yenye wingi, mara kwa mara hunatumika kuonesha msisitizo. Kwa ukaribu yanayohusiana na hili ni tabia ya kisarufi cha Kiebrania kinachoitwa "wingi wa ukuu," mahali ambapo wingi unatumika kukuza dhana.
    b. Hii inaweza kumaanisha baraza la kimalaika, ambalo Mungu hukutana nalo mbinguni na ambalo linafanya kazi za utekelezaji (kama vile I Wafalme. 22:19-23; Ayubu 1:6; Zab. 82:1; 89:5,7.
    c. Inawezekana hata inaaksi ufunuo wa Agano Jipya wa Mungu mmoja katika nafsi tatu. Katika Mwanzo. 1:1 Mungu anaumba; Mwanzo 1:2 Roho anachepusha na kutoka katika Agano Jipya Yesu ni wakala wa Baba katika Uumbaji (kama vile Yohana 1:3,10; Rum. 11:36; I Kor. 8:6; Kol. 1:15; Ebr. 1:2; 2:10).

D. YHWH (BDB 217, KB 394)

1. Hili ni jina ambalo linaaksi Uungu kama Mungu afanyaye maagano: Mungu kama mwokozi, mkombozi! Wanadamu wanavunja agano, lakini Mungu ni mwaminifu kwa neno lake, ahadi, agano (kama vile Zab. 103). Jina hili kwanza linatajwa katika munganiko pamoja na *Elohim* katika Mwanzo. 2:4. Hakuna masimulizi mawili ya uumbaji katika Mwanzo. 1-2, lakini msisitizo
    a. Mungu kama muumbaji wa ulimwengu (wa kimwili, Zaburi 104)
    b. Mungu kama muumbaji maalum wa uanadamu (Zaburi 103).
    
    Mwanzo 2:4-3:24 inaanza na ufunuo maalum kuhusu nafasi ya upendeleo na kusudi la mwanadamu, pia tatizo la dhambi na uasi unaohusianishwa na nafasi ya upekee.
2. Katika Mwanzo 4:26 inasema"*wanadamu* wakaanza kuliiitia jina la BWANA" (YHWH). Hatahivyo Kutoka. 6:3 inamaanisha kwamba watu wa kwanza wa agano (wahudumu wa uzao wa kiume na familia zao) walimfahamu Mungu tu kama *El-Shaddai*. Jina YHWH linaelezewa kwa mara moja tu katika Kut. 3:13-16, hasa mstari wa 14. Hatahivyo, maandiko ya Musa mara kwa mara yanafasiri maneno kwa utani maarufu na sio kwa asili na chanzo chake (kama vile Mwanzo. 17:5; 27:36; 29:13-35). Kumekuwa na nadharia kadhaa juu ya maana ya jina hili (likichukuliwa kutoka IDB, vol. 2, kur. 409-11).
    a. kutoka katika mzizi wa kiarabu, "kuonesha upendo wa dhati"
    b. kutoka katika mzizi wa kiarabu "kupuliza" (YHWH kama Mungu wa dhoruba)
    c. kutoka katika mzizi wa lugha ya Ugariti (ya Wakanaani) "kuzungumza"
    d. kufuatia maandiko ya Ki-Foenike, KAULI SABABISHI ENDELEVU ikimaanisha "Yeye anayetosheleza," au "yeye anaye anzisha"
    e. kutoka katika muundo wa Kiebrania *Qal* "Yeye ambaye yupo," au "Yeye aliyepo sasa" (katika namna ya wakati ujao, "Yeye atakayekuwako")
    f. kutoka katika muundo wa kiebrania *Hiphil* "yeye asababishaye kuwa"
    g. kutoka katika mzizi wa Kiebrania "kuishi" (mfano Mwanzo. 3:20), maana "Mungu mmoja tu aishiye milele"
    h. kutoka katika muktadha wa Kut. 3:13-16 mbadilishano juu ya muundo wa KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU iliyotumika katika namna ya KAULI YA WAKATI ULIO TIMILIFU, "nitaendelea kuwa vile nilivyokuwa" au "nitaendelea kuwa vile ambavyo siku zote nimekuwa" (kama vile J. Wash Watts, *A Survey of Syntax in the Old Testament*, ukurasa wa 67 Jina kamili la YHWH mara kwa mara linaelezewa katika vifupisho au yawezekana katika muundo wa asili
        (1) *Yah* (mfano Hallelu – yah, BDB 219, kama vile Kut. 15:2; 17:16; Zab. 89:8; 104:35)
        (2) *Yahu* (majina mfano Isaya)
        (3) *Yo* (majina mfano Joeli)
3. Katika Dini ya Kiyahudi ya baadaye jina la kiagano lilifanyika kuwa takatifu sana (Ni jina la kiebrania la Mungu lililofasiriwa kwa herufi nne) kwamba Wayahudi walikuwa na hofu kusema ili wasije wakavunja amri ya Kut. 20:7; Kum. 5:11; 6:13. Hivyo, alitafta mbadala wa neno la Kiebrania "mmiliki," "Mkuu," "mume," "bwana"—*adon* au *adonai* (bwana wangu). Walipofika kwa YHWH katika kusoma kwao maandiko ya Agano la Kale walitamka "bwana." Hii ndio maana YHWH

inaandikwa BWANA katika fasiri za Kiingereza.

4. Kama ilivyo kwa *El*, mara kwa mara YHWH inaunganishwa na maneno mengine kusisitiza tabia fulani za Mungu wa Agano wa Israeli. Wakati kuna muunganiko mwingi wa maneno, hapa ni baadhi.
    a. *YHWH - Yireh* (YHWH atatoa ), Mwanzo. 22:14
    b. *YHWH - Rophekha* (YHWH ni mponyaji wako), BDB 217 & 950, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Kutoka. 15:26
    c. *YHWH - Nissi* (YHWH ni bendera yangu), BDB 217 & 651,Kutoka. 17:15
    d. *YHWH - Meqaddishkem* (YHWH yeye awatakasaye, BDB 217 & 872, *Piel* HALI YA KUENDELEA),Kut. 31:13
    e. *YHWH - Shalom* (YHWH ni amani BDB 217 & 1022), Waamuzi. 6:24
    f. *YHWH - Sabbaoth* (YHWH wa majeshi ,BDB 217 & 878), I Sam. 1:3,11; 4:4; 15:2; mara kwa mara katika manabii)
    g. *YHWH - Ro'I* (YHWH ni mchungaji wangu ,BDB 217 & 944, *Qal* HALI YA KUENDELEA), Zab. 23:1
    h. *YHWH - Sidqenu* (YHWH ni haki yetu, BDB 217 & 841), Yer. 23:6
    i. *YHWH - Shammah* (YHWH yupo hapa,BDB 217 & 1027), Ezek. 48:35

◙ **"mbingu na nchi"** Mpangilio wa haya maneno inarudishwa nyuma kutoka katika mstari wa 1 lakini kwa nini haina uhakika.

**2:5 "mche wa kondeni"** Hii inamaanisha mimea ya mwituni (kama vile Mwanzo. 21:15; Ayubu 30:4,7).

◙ **"mboga za kondeni"** Hii inamaanisha mimea ya mwituni inayotunzwa nyumbani na kupaliliwa.

**2:6 "ukungu"** Hii (BDB 15, KB 11) ni neno la lugha ya Akkadia kwa maana ya (1) mafuriko au (2) kutiririka kwa maji ya chini. Hii yawezekana kuwa na maana ya kumwagia maji yanayotokana na mafuriko ("yalizoea kupanda," BDB 748, KB 828, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU). Usambamba wa kiarabu ni ukungu ambao ni asili ya tafasiri ya neno "umande." Tungeweza kusema umande mzito.
Hii tena inaweza kuwa iliaksi mazingira katika Bustani ya Edeni pekee. Jiolojia inaonekana kuthibitisha matokeo ya kale ya maji juu ya uso wa nchi zamani kabla ya umaalumu wa Adamu na Hawa.

**2:7 "kutengeneza"** Kiuhalisia hii ni "kutengeneza kwa kutumia mfinyanzi" (BDB 427, KB 428, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU, kama vile Yer. 18:6). Hili ni neno la tatu linalotumika kufunuua au kuelezea matendo ya uumbaji wa Mungu ukihusianisha na mwanadamu ("kufanya," 1:26 (BDB 793, KB 889); "kuumba," 1:27 (BDB 135, KB 153) na "kutengeneza," 2:7). Agano Jipya linafunua kwamba Yesu alikuwa wakala wa Mungu katika uumbaji (kama vile Yohana 1:3; I Kor. 8:6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2).

◙ **"mtu mavumbi kutoka katika ardhi"** Mtu ni neno la Kiebrania, Adam (BDB 9), ambalo lilimaanisha (1) utani wa neno "nyekundu" (kama vile Kut. 25:5; 28:17; Hes. 19:2; Isa. 63:2; Zek. 1:8) au (2) "ardhi" (*adamah*, kama vile mstari wa 6), yawezekana ikielezea "matope ya mfinyanzi ya udongo mwekundu." Hii inaaksi unyonge na udhaifu wa ubinadamu. Kuna mvutano wa kilahaja hapa kati ya nafasi ya mwanadamu inayotukuzwa (kufanywa katika sura na mfano wa Mungu) na hali yake ya unyonge na udhaifu! Wanyama wanaumbwa namna hiyo hiyo katika mstari wa 19. Na pia inawezekana kwamba ilimaanishwa asili ya mwanadamu ni katika ardhi (kama vile Mwanzo. 3:19; Zab. 103; Muh. 12:7). Hii inaeleza mwanadamu kama udongo wa mfinyanzi na Mungu kama Mfinyanzi (kama vile Isa. 29:16; 45:9; 64:8; Yer. 18:6; Rum. 9:20-23).

◙ **"akampulizia. . .pumzi ya uhai"** KITENZI "kumpulizia" (BDB 655, KB 708) ni *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU. NOMINO "pumzi" (BDB 675) inaonesha Mungu alivyokuwa na umakini maalumu alipokuwa akifanya uumbaji wa Mwanadamu. Hatahivyo wanadamu bado wanafanya kazi kimwili kama namna ambavyo wanyama wote wanavyofanya kazi katika sayari (yaani kupumua, kula, kutoa taka na kuzaliana). Wanadamu kipekee wana

uhusiano na Mungu, ila bado kiundani tunashikiliwa katika sayari hii. Kuna vipengele vya asili viwili vya asili yetu (kiroho na kimwili).

◙**"Mtu akawa kiumbe hai"** Wanadamu wanafanyika *nephesh* (BDB 659, KB 711-713), lakini pia hata mifugo (kama vile 1:24; 2:19). Upekee wa mwanadamu ni kuumbwa na Mungu mwenyewe binafsi na kupuliziwa pumzi. Wanadamu hawana nafsi bali wenyewe ni nafsi! Sisi ni umoja wa kimwili na kiroho. Tutakuwa na uelekeo wa kimwili isipokuwa kwa hali ya kimuingiliano kati ya mauti na ufufuo (kama vile I The. 4:13- 15).

Je Adamu alikuwa mtu wa kale au wa kisasa? Ni kwa namna gani anahusianishwa na viumbe vingine vya zama za kale? Watu wa zama za mawe walikuwepo katika ukanda wa Mlima Carmel miaka 200,000 iliyopita. Lini Adamu aliumbwa? Je yeye alikuwa mwisho wa maendeleo haya au alikuwa mwanzo wa uumbaji maalum?

**2:8 "Bustani"** Neno hili (BDB 171) linatumika kwa namna ya uwanja uliowekewa uzio. Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani linafasiri neno hili na neno la Kiashuru, "paradiso."

◙**"Edeni"** Katika Kiebrania *Eden* inamaanisha "kupendezwa" au "ardhi ya furaha" (BDB 727 III, KB 792 II).Tazama bustani haiitwi "Edeni," lakini imewekwa Edeni. Kwa dhahiri ni mahali pa kijiografia, jina la mahali. Neno la Ki-Sumeri linalofanana na hilo ni "uwanda wenye rutuba." Maelezo yapo katika mistari ya 8, 10-14 na inatoa maelezo mengi ambayo yanamaanisha kuwasilisha mahali pake husika lakini sehemu yake ya kijiografia haijulikani. Wafasiri wengi wanaiweka (1) katika kinywa ya mito ya Hidekeli na Frati ya kisasa (2) katika kichwa cha maji ya mito hii. Hatahivyo, majina ya mito yote haishabihiani na jiografia ya leo. Ni kwa kiasi gani cha dunia kilibadilishwa na gharika haijulikani. Habari za Kufanana kwa Biblia na Mesopotamia kimantiki ingaliiweka bustani katika Mesopotamia lakini hili ni mtazamo tu. Angalia *Who was Adam?* By Fazale Rana na Hugh Ross, ukurasa wa 46.

**2:9 "mti wa uzima . .mti wa ujuzi wa mema na mabaya"** Hii ni tungo ya mwisho na yaweza kuwa maelezo ya ziada (kama vile toleo la Biblia ya NET, ukurasa wa 7). Mwanzo 3:3 inamaanisha kwamba kulikuwa na mti mmoja tu wakati 3:22 inamaanisha miti miwili. Mti wa ujuzi wa mema na mabaya haina usambamba katika fasihi ya Mashariki ya Karibu. Mti huu haukuwa wa kimiujiza, lakini ulionekana kuwapatia wanadamu njia ya kuwa huru wenye kujitegemea mbali na Muumba wao Mungu na au angalau kuwaahidi kwamba wangeweza kufikiria na kuwa na maarifa na uwezo wa ndani sawa na au katika kushindana na Mungu. Hii ndio maaana ya kuwepo kwa dhambi. Pia inawezekana kwamba ilimpatia Hawa njia ya kumtawala Adamu, ambayo iliondoa hali ya kutawala kwa pamoja kama wawili..

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2:10-14**

**[10] Ukatoka mto katika Edeni wa kuitilia bustani maji, na kutokea hapo ukagawanyika kuwa vichwa vinne. [11] Jina la wa kwanza ni Pishoni; ndio unaozunguka nchi yote ya Havila, ambako kuna dhahabu; [12] na dhahabu ya nchi ile ni njema; huko kuna bedola, na vito shoham. [13] Na jina la mto wa pili ni Gihoni; ndio unaozunguka nchi yote ya Kushi. [14] Na jina la mto wa tatu ni Hidekeli; ndio unaopita mbele ya Ashuru. Na mto wa nne ni Frati.**

**2:10 "mito"** Hizi zilikuwa "matawi ya mifereji " (BDB 625).

**2:11 "Pishoni"** Kidhahiri hii ni "kutoa" (BDB 810). Hii inaweza kuwa inamaanisha nji ya maji ya kale au mifereji kusini mwa Mesopotamia iitwayo "Pisanu."

◙ **"unaozunguka nchi yote"** Kiuhalisia hili linamaanisha "kuzunguka kupitia " (BDB 685, KB 738, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU).

◙**“Havila”** Hii kiuhalisia inamaanisha “ardhi yenye mchanga”(BDB 296). Hii sio iliyowekwa Misri lakini ikiunganishwa na Kushi katika 10:7. Neno hili linatumika tena katika 10:29 kwa ajili ya ardhi ya mchanga katika Arabia.

**2:12 “bedola”** Hii inawezekana kuwa mti wa mpira wenye gundi (BDB 95). Maana ya neno hili na lile linalofuata haijulikani. Baadhi wamependekeza kwamba hii ifasiriwe “lulu” (kama vile fasiri za Helen Spurrell na James Moffatt).

◙**“vito shoham”** Maneno yote ya kale kwa vito hayajulikani sana (BDB 995). Hili jiwe lilikuwa moja ya mawe kumi na mbili katika kibao cha kifua cha Kuhani Mkuu (kama vile Kut. 28:9). Vito vya Edeni vinatumika kisitiari katika Ezek. 28:13.

**2:13 “Gihoni”** Hii kiuhalisia ni “povu” (BDB 161). Hii inaweza kumaanisha njia za maji za kale au mifereji kusini mwa Mesopotamia iitwayo “Guhana.”

◙ **“Kushi”** Neno hili katika Agano la Kale lilitumiwa katika njia tatu: (1) hapa na 10:6 na kuendelea kumaanisha jamii ya watu walioishi kusini mwa Ziwa Caspian (Kassites) kuelekea mashariki mwa bonde la Hidekeli; (2) Hab. 3:8; II Nyakati 14:9na kuendelea; 16:8; 21:16 kumaanisha Kaskazini mwa Arabia; na (3) ilitumiwa siku zote kumaanisha Ethiopia au Nubia Afrika Kaskazini (BDB 468).

**2:14 “Hidekeli”** Hii kiuhalisia ni “Hiddekel” (BDB 293).

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | |
| **NRSV, TEV** | **“Ashuru”** |
| **NJB** | **“Ashuru”** |
| **JPSOA, NIV** | **“Ashuru”** |

Neno (BDB 78) linaweza kumaanisha (1) watu (mfano Hes. 24:22,24; Hosea 12:2; 14:4) au (2) ardhi (kama vile Mwanzo. 2:14; 10:11; Hosea 5:13; 7:11; 8:9; 9:3; 10:6). Katika Muktadha huu #2 inafaa zaidi.

◙ **“Frati”** Kiuhalisia hii ni “perath.” Mara kwa mara inaitwa“Mto uliojulikana” (kama vile Mwanzo. 15:18; I Wafalme. 4:21,24)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2:15-17**

**15 Bwana Mungu akamtwaa huyo mtu, akamweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. 16 Bwana Mungu akamwagiza huyo mtu, akisema, Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula, 17 walakini matunda ya mti wa ujuzi wa mema na mabaya usile, kwa maana siku utakapokula matunda ya mti huo utakufa hakika.**

**2:15 “ailime na kuitunza”** Kazi ilikuwa jukumu la mwanadamu kabla ya anguko na sio matokeo ya dhambi. Neno “kuipalilia” ikimaanisha “kuhudumia” (BDB 712, KB 773, *Qal* TUNGO ISIYO NA KIKOMO), wakati“kuitunza” ni “kuilinda” (BDB 1036, KV 1581, nyingine *Qal* TUNGO ISIYOKUWA NA KIKOMO). Sehemu hii ni ya majukumu ya utawala wa mwanadamu. Tunatakiwa tuwe mawakili na sio wanyonyaji wa rasilimali za sayari hii.
Katika masimulizi ya hadithi za kishujaa za kufikirika za Ki-Sumeri na ki-Babeli mwanadamu siku zote anafanywa kwa sura na mfano wa Mungu, kuwa na mamlaka juu ya uumbaji. Hii ni kazi pekee walipewa jukumu kufanya na halikuwa na uhusiano na mahitaji ya Mungu!

**2:16 “Matunda ya kila mti wa bustani waweza kula”** Hii ni neno *Qal* lenye kitenzi jina halisi KILICHOUNGANISHWA na *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU ya mzizi huo huo (BDB 37, KB 40), imetumika kwa msisitizo. Amri ya Mungu haikuwa mzigo. Mungu alikuwa anajaribu (kama vile Mwanzo. 22:1; Kut. 15:22-25; 16:4; 20:20; Kumb. 8:2,16; 13:3; Waamuzi. 2:22; II Nyakati. 32:31) Uaminifu na utii wa uumbaji wake mkuu.

**2:17 “mti wa ujuzi wa mema na mabaya”** Huu haukuwa mti wa maajabu. Haikujumuisha siri ya vipengele vya mwili katika matunda yake kusisimua akili ya mwanadamu. Ilikuwa jaribu la utii na uaminifu
Tazama kwamba mti ulishughulikia nguvu na madhaifu. Inashangaza kwangu kile ambacho mwanadamu alikizalisha kutokana na rasilimali za kimwili za sayari hii. Mwanadamu ni uumbaji mzuri sana ikiwa na uwezo wa wema na ubaya.

◙**“uovu”** Hili ni neno la Kiebrania *ra* lililomaanisha “kuvunja” au “kuharibu” (BDB 948). Iliunganisha matendo na matokeo yake (kama vile Robert B. Girdlestone’s *Synonyms of the Old Testament*, ukurasa 80.)

◙**“siku”** Katika ufahamu wa Adamu na Hawa kuendelea kuishi baada ya kula, haya ni matumizi ya “siku” kama kipindi cha muda, na sio saa 24 (BDB 398).

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **“hakika utakufa”** |
| **NKJV** | **“hakika utakufa”** |
| **NRSV** | **“utakufa”** |
| **TEV** | **“utakufa siku hiyo hiyo”** |
| **NJB** | **“utakuwa umeamriwa kufa”** |

Hiki ni KITENZI JINA HALISI na KISHAMIRISHO CHENYE MASHITAKA, “kupotea kwa kufa” (BDB 559, KB 562) ambayo ni sarufi ya kiebrania kama njia ya kuonesha msisitizo. Hii ni sawasawa na mstari wa 16. Muundo huu unabeba fasiri kadhaa zinazowezekana (Fasiri Ishirini na sita za Agano la Kale). Kwa uwazi kifo kinamaanisha kifo cha kiroho hapa (kama vile Efe. 2:1), ambalo ni matokeo ya dhambi ya kimwili (kama vile Mwanzo 5).
Katika Biblia hatua tatu za mauti zinafunuliwa: (1) kifo cha kiroho (kama vile 2:17; 3:1-7; Isa. 59:2; Rum. 5:12- 21; 7:10-11; Efe. 2:1,5; Kol. 2:13a; Yakobo 1:15); (2) kifo cha kimwili (kama vile Mwanzo 5); na (3) kifo cha milele, kiitwacho “kifo cha pili” (kama vile Ufunuo 2:11; 20:6,14; 21:8). Katika namna halisi hii inamaanisha zote tatu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 2:18-25**

**18 Bwana Mungu akasema, Si vema huyo mtu awe peke yake, nitamfanyia msaidizi wa kufanana naye. 19**
**Bwana Mungu akafanyiza kutoka katika ardhi kila mnyama wa msituni, na kila ndege wa angani, akamletea**
**Adamu ili aone atawaitaje; kila kiumbe hai, jina alilokiita Adamu likawa ndilo jina lake. 20 Adamu akawapa**
**majina yao kila mnyama wa kufugwa, na ndege wa angani, na kila mnyama wa mwituni; lakini**
**hakuonekana wa kumsaidia Adamu aliyefanana naye. 21 Bwana Mungu akamletea Adamu usingizi mzito,**
**naye akalala; kisha akatwaa ubavu wake mmoja, akafunika nyama mahali pake, 22 na ule ubavu alioutwaa**
**katika Adamu Bwana Mungu akaufanya mwanamke, akamleta kwa Adamu. 23 Adamu akasema, Sasa huyu**
**ni mfupa katika mifupa yangu, na nyama katika nyama yangu, basi ataitwa mwanamke, kwa maana**
**ametwaliwa katika mwanamume. 24 Kwa hiyo mwanamume atamwacha baba yake na mama yake naye**
**ataambatana na mkewe, nao watakuwa mwili mmoja. 25 Nao walikuwa uchi wote wawili, Adamu na**
**mkewe, wala hawakuona haya.**

**2:18 “Si vema huyo mtu awe peke yake”** Hii ni sehemu pekee katika ufunguzi wa sura ya Agano la Kale ambapo “si vema” inatumika. Mungu ametutengeneza ili tuhitaji mtu, hata nje ya ushirika wake na Yeye! Mwanaume asingeweza kutimiza majukumu yake peke yake ya kutawala juu ya uumbaji bila kuambatana na mwanamke, wala asingeweza kutimiza amri ya kuzaa na kuongezeka na kuijaza dunia.

| | |
|---|---|
| **NASB** | **“msaidizi wa kumfaa”** |
| **NKJV** | **“msaidizi wa kulingana nae”** |

**NRSV** **"msaidizi kama mwenza wake"**
**TEV** **"mwenza mzuri wa kumsaidia"**
**NJB** **"msaidizi"**

Hii ina maana "yeye anayesaidia au kukamilisha" (BDB 740 I, KB 811 I). Toleo la Biblia ya NET ina "u-wenza wa lazima" (ukurasa 8). Neno hili mara kwa mara linatumika kuelezea msaada wa Mungu (kama Kut. 18:4; Kumb. 33:4, 7, 29; Zab. 33:20; 115:9-11; 121:2; 124:8; 146:5). Tazama uwili kati ya mwanaume na mwanamke kama katika 1:26-27 na WINGI SHURUTISHI wa 1:28. Unyenyekevu hauji mpaka baada ya anguko (kama vile 3:16). Haya masimulizi ya kibayana ya uumbaji wa mwanamke ni ya kipekee katika fasihi ya Mashariki ya Karibu ya kale
Kujifunza neno kunakofurahisha kunatoka katika *Hard Sayings of the Bible*, ukurasa 92-94, ambayo Walter Kaiser anaelezea fasiri "nguvu (au uwezo) kuitikia mtu" (au sawa na mtu).

**2:19 "Mungu akafanyiza kila mnyama"** Baadhi wamechukua mstari huu kuelezea kwamba Mungu aliumba wanyama baada ya Adamu katika kile wanachokiita masimulizi ya uumbaji wa pili (kama vile Mwanzo. 2:4-25). KITENZI (BDB 427, KB 428, Qal KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU) ingeweza kufasiriwa "alitengeneza" (kama vile toleo la NIV). Kipengele cha Muda katika VITENZI vya Kiebrania ni cha kimuktadha. Dr. Rich Johnson, Profesa wa dini katika chuo cha East Texas Baptist , alitoa maoni yake kwangu katika mapitio ya fasiri hii:

> "Maana ya KAULI YA WAKATI USIOTIMILIFU ikiwa na kiunganishi cha nyakati (waw) ambacho kitenzi hiki ni njeo ya wakati uliopita wa hali ya kuendelea. Ni njia ambayo kiebrania kinaweka miundo ya matukio. Mfuatano wa aina za kitenzi hiki kinazungumzia matukio katika utaratibu ambao yanatokea. Hapa unaongelea makisio ya wafasiri yanayoathiri fasiri. Hapa ni makisio ya wafasiri wa NIV ambayo yamewapelekea kufasiri vibaya mstari huu na pia 2:8, 'Sasa BWANA alikuwa amepanda bustani...'. Wafasiri wa toleo la NIV wamedhania kwamba sura hii lazima ifanane na sura ya kwanza na wameruka kanuni za kawaida za usomaji wa hadithi za Kiebrania kuendeleza hayo makisio. Swali la dharura ni wapi walipata makisio hayo. Hiki kitendo kilifasiriwa kama kitenzi cha wakati uliopita kwa matoleo ya KJV, ASV, ERV, RSV, NRSV, NASB, ESV, NEB, REB, fasiri ya NET, Fasiri ya Kibayana ya Youngs' Literal, fasiri ya Jewish Publication Society, TANAKH, New American Bible, na New Jerusalem Bible. Toleo la NIV sio la kawaida."

◙**"kuona atakavyowaita"** KITENZI "kuita" (BDB 894, KB 1128) kimetumika mara tatu katika mistari ya 19 na 20. Majina yalikuwa ya muhimu sana kwa Waebrania. Hii inaonesha utawala wa mwanadamu juu ya wanyama. Je hii inarejerea (1) wanyama wote tofauti tofauti katika ulimwengu mzima (2) au aina za wanyama waliokuwa katika kipindi cha Mwanzo (3) wanyama wa Mesopotamia?

**2:21** Mstari huu unahamasisha uhusiano wa kipekee kati ya mwanaume na mwanamke Adamu na hawa (kama vile mstari 23). Inawezekana ikawa nahau ya Kiebrania kwa ukaribu na upendo wa karibu. Neno la Kiebrania kwa "mbavu" inafasiriwa sehemu zingine "kipembeni" (BDB 854, KB 1030 I).
Inafurahisha kwamba katika kitabu hiki, utangulizi kwa Agano la Kale, ukurasa 555-556, R. K. Harrison anaelezea kwamba neno la Kiebrania kwa "mbavu" hapa linamaanisha "kipengele cha unafsi" ambacho kingetengeneza kizazi pamoja na Adamu aliyefanywa katika sura na mfano wa Mungu pia kujumuisha kipengele cha nafsi.
Inafurahisha pia kwamba "mbavu" ni sehemu ya uumbaji wa mwanamke katika masimulizi ya uumbaji ya Ki-Sumeri: kutoka *enki* alikuja *nin-ti* (kama vile D. J. Wiseman's *Illustrations from Biblical Archaeology*). Katika Muktadha huu neno la ki-Sumeri kwa mbavu (yaani *ti*) pia lina maana "kuhuisha." Hawa atakuwa mama wa wenye uhai wote (kama vile 3:20).
Lazima ikumbukwe kwamba Musa anaandika (kurekebisha au kutunga) sura hizi kwa tarehe za baadaye kabisa. Haya ni maneno ya kiutani ya Kiebrania, lakini Kiebrania hakikuwa lugha ya asili iliyotumika.

**2:22 "Akamleta kwa mwanaume"** Walimu wa Kiyahudi wanasema kwamba Mungu alikuwa kama msindikizaji wa ndoa.

**2:23 "Mwanamke. . .Mwanaume"** Mstari huu ni ushairi. Kidhahiri hii ni *Ishah* (BDB 35). . .*ish* (BDB 35), utani wa kimaneno ulio wazi (hasa "jina lake yeye la kike *Ishah*"). Adamu pia anamuita (au angalau anamfunua Hawa

sawasawa na yeye mwenyewe) Hawa. Asili ya neno haijulikani. Siku zote *adam* inamaanisha kwa uanadamu na *ish* kwa mtu mmoja mmoja hasa.

**2:24 "ataacha baba yake na mama yake"** KITENZI hiki (BDB 736, KB 806) ni *Qal* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU, inawezekana inatumika katika namna ya KAULI AMRISHI. Umuhimu wa familia unasababisha maoni kusomeka tena katika masimulizi za kale. Musa inaaksi siku yake mwenyewe na umuhimu wa kipengele cha familia katika mazingira ya kuishi familia iliyopanuka. Ndoa inatanguliwa kwanza juu ya wakwe.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB** | **"ambatana"** |
| **NKJV** | **"..taunganishwa"** |
| **NRSV** | **"fuatana"** |
| **TEV** | **"kuunganishwa na"** |
| **NJB** | **"kuambatana na"** |

Hii ni nahau ya Kiebrania cha uaminifu (BDB 179, KB 209, Qal KAULI YA WAKATI TIMILIFU, kama vile Ruth 1:14; Mt. 19:5-6; Efe. 5:31).

◙ **"Mwili"** Hii inaonesha muunganiko kamili na kipaumbele cha kimahusiano cha wenza waliooana. Muundo wa UMOJA wa "mtu" kuzungumzia kuunganisha watu wawili.

2**:25 "wote walikuwa uchi na wala hawakuona aibu"** Hii inatakiwa iendane na sura ya 3. Maana ya tungo hii ni kwamba Adamu hakuwa na kitu cha kuficha kwake yeye mwenyewe, mwenza wake na Mungu wake (BDB 101, KB 161, *Hithpolel* KAULI YA WAKATI USIO TIMILIFU). Hivyo ni nahau ya kutokuwa na hatia. Mambo haya karibu yatabadilika! Ukweli kwamba Mwanaume na mwanamke walikuwa uchi (BDB 736, KIVUMISHI CHA SIFA) Inamaanisha mazingira yaliyokuwa yaliongozwa vizuri sana. Hii inaweza kuelezea yenyewe maoni kwamba Bustani ya Edeni ilikuwa ikilindwa na baadaye kwa sababu maalumu, uumbwaji maalum, tofauti na sehemu zingine zote za sayari (yaani uumbaji endelevu).

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni <u>mwongozo</u> wa kujisomea wa fasiri, hii ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je kuna utofauti wowote unaotolewa katika Mwanzo 1 kati ya Mungu kuumba na vitu ambavyo alivyoviumba vinazalisha? Ikiwa hivyo ndivyo, hii inamaanisha nini?
2. Ni kwa namna gani mwanadamu ni kama wanyama? Ni kwa namna gani mwanadamu ni kama Mungu?
3. Je wanawake nao waliumbwa kwa mfano wa Mungu ama kwa sura ya Adamu tu?
4. Je inamaanisha nini kwamba mwanadamu atiishe na kutawala utaratibu ulioumbwa?
5. Ni kwa namna gani tungo "zaeni mkaongezeka" inaweza kuhusianishwa na kufumuka kwa idadi ya watu?
6. Je ni mpango wa Mungu kwamba wanadamu wawe wala mboga za majani?
7. Je si sawa kwa mwanadamu kuabudu Jumapili badala ya Jumamosi katika ufahamu wa Mwanzo 2:2,3?
8. Kwanini sura ya 1 na 2 zinafana sana na zinatofautiana sana?
9. Kwanini Adamu inafasiriwa kama Nomino jina na jina la jumla?
10. Kwanini mahali pa Kijiografia pa Edeni panatolewa maelezo ya ndani namna hiyo?
11. Taja miundo mitatu ya vifo vya kibiblia.
12. Mstari wa 18 unasema nini juu ya sisi kuwa viumbe tunaojamiiana?
13. Je "Msaidizi" inamaanisha kufanya kazi kwa kutegemeana wawili?

# MWANZO 3:1-24

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Kaini na Abeli | Jaribu na Kuanguka Kwa Mwanadamu | Simulizi ya hili Jaribu | Kutotii kwa Mwanadamu | Anguko |
| 3:1-7 | 3:1-8 | 3:1-7 | 3:1<br>3:2-2<br>3:4-5<br>3:6-7 | 3:1-7 |
| 3:8-19 | | 3:8-19 | 3:8-9 | 3:8-13 |
| | 3:9-19 | | 3:10<br>3:11<br>3:12<br>3:13a<br>3:13b | |
| (14-16) | (14-16) | (14-16) | Mungu atamka adhabu | |
| ( 17b-19) | (17b-19) | (17-19) | 3:14-15 | 3:14-16<br>(14-16) |
| 3:20-21 | 3:20:-24 | 3:20-21 | 3:20-21 | 3:17-19<br>(17-19)<br>3:20-24 |
| | | | Adamu na Wanatolewa Nje ya Bustani | |
| 3:22-24 | | 3:22-24 | 3:22-24 | |

## USOMAJI MZUNGUKO WA TATU (Angalia ukurasa wa vii")

### *KUFUATIA KUSUDIO ASILIA LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wafasiri, ikiwa na maana kuwa nawajibika kwatafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao.Wewe, Bibilia na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja.Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.
Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Ayaya kwanza
2. Ayayapili
3. Ayatatu
4. N.k

## UTANGULIZI

A. Kitabu cha Mwanzo 3 ni cha msingi sana katika kuielewa asili ya uovu na mateso tuliyonayo katika ulimwengu wetu. Inashangaza kwamba viongozi wengi wa sheria za dini ya Kiyahudi hawalitumii andiko hili katika mijadala yao ihusuyo uovu, dhambi, na uasi mwa mwanadamu.

B. Matokeo ya maamuzi ya uasi wa mwanadamu wa makusudi dhidi ya Mungu wa pendo, mtunzaji, mtoaji, wa ushirika, matokeo haya hayakuathiri maisha ya kidini ya wanadamu tu bali utu wao wenyewe, maisha ya familia zao, na ulimwengu wao.

   Tambua kwamba gharama ya juu ambayo Mungu Mwenyewe aliilipa kwa upekee ili kumfanya mwanadamu atembee katika uhuru. Furaha ya Mungu na makusudi halisi ya /aliyokuwa nayo katika uumbaji yaliharibiwa kwa ujumla (kakini si moja kwa moja) kupitia uasi wa mwanadamu. Ikiwa tuwaza juu ya wema na utoaji wa Mungu, uasi wa mwanadamu (na yamkini malaika) unaonekana katika ukosefu wake wa heshima ya msingi kutojistiri kwake. Pendo la Mungu lililo endelevu na ahadi ya wokovu (kama vile 3:15) pia ni mambo ya msingi zaidi katika sifa ya huruma yake pia!

C. Ingawa sura hii ina vipengele vya kawaida vinavyojirudia mara kwa mara na maandiko mengine ya kale ya Mashariki ya Karibu, uwasilishaji wake ni ule unaomzungumzia Mungu mmoja na si dhana ya miungu wengi.

## ASILI NA KUSUDI LA DHAMBI

A. Nyenzo za ki- Biblia
   1. Hili linaweza kuwa dhahanio la kithiolojia kwamba kusudi la kuumbwa kwa Shetani lilikuwa (1) kumtolea Mungu viumbe wenye uelewa wa uchaguzi ambao ungaliwapeleka kwenye utawala huru na baadaye kwenye mashitaka, Ayubu 1-2; Zek. 3; au (2) Mwanzo 3 inamaanisha uasi wa kimalaika uliokwisha pita katika uumbaji wa Mungu au kumkashifu Mungu kwa wanadamu kupitia matendo ya kimalaika.
   2. Mwanadamu anaathiriwa na ushawishi.
   3. Biblia haitoi maelezo bayana kuhusu asili ama kusudi la "dhambi."
      a. Maandishi mengine ya Kiyahudi yaliyofuatia yalieleza kwamba dhambi ilianzia Mwa. 3 (ndani ya Shetani, kisha ndani ya mwanadamu)
      b. Maandiko mengine ya kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya yanaeleza kwamba dhambi ilianzia Mwa. 6 (ndani ya "wana wa Mungu")
      c. Baada ya kipindi cha Yesu kupita manabii wa uongo waliunganisha dini ya Kiyahudi pamoja na fikra za Kiyahudi na kudai kwamba uovu ulikuwa suala la urithi wa kimwili (yaani, Mafunuo ya Kiyunani ya fikra za uongo, kama vile Kol.; Efe.; I Tim.; II Tim.; na Tito)
   4. Inadhaniwa kwamba kuwepo kwa uovu kulikuwa na kusudi ama usingekuwepo. Bado kuna uchochezi wa kuwepo kwa mwovu Shetani toka Agano la Kale hadi Agano Jipya (kama vile *The Theology of the OT* na A. B. Davidson, ukur. 300-306). Katika Agano la Kale Shetani si adui kwa Mungu (isipokuwa katika sura hii) bali amekuwa adui wa mwanadamu mara kwa mara. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema yule mwovu aliona wivu juu ya pendo la Mungu na namna Mungu alivyomjali wanadamu.
   5. Dhambi ya Adamu iliuathiri uumbaji wote (yaani, neno la Kiebrania la dhana ya ushirika kama vile Mwa. 3:14-24; Rum. 5:12-21; 8:18-23).
   54

B. Ufafanuzi wa Historia ya Kitheolojia (uliochukuliwa kutoka *Systematic Theology* na L. Berkhof).
   1. Viongozi wa dini ya Kiyahudi wanakanusha juu ya asili ya dhambi ya asili na uchaguzi wa malengo mawili (mema dhidi ya mabaya).Agano la Kale halijadili juu ya Mwa. 3 kwa marefu (kama wasivyofanya walimu wa sheria ya Kiyahudi).
   2. Irenaeus (130-202 B.K) ni kanisa la mwanzo kujadili juu ya dhambi ya Adamu na matokeo yake. Mtazamo huu wa anguko la mwanadamu kupitia dhambi ya Adamu ulishamiri sana katika Kanisa la

Magharibi (yaani, Augustine). Mtazamo huu ulitumika kuyashambulia yale mafunuo ya uongo ambayo yalikuwa na maelezo ya utata wa dhambi ndani yake.

3. Origen (182-251 B.K) aliendelea kudai kwamba katika kipindi cha maisha yaliyopita kila mwanadamu alitenda dhambi kwa kukusudia (Platoniki).
4. Makasisi wa Kiyunani (Kanisa la Magharibi) wa karne za tatu na nne walizidi kusistizia kipengele hiki cha Adamu katika utata wa uovu katika ulimwengu wetu. Hili liliboreshwa kwenye mafundisho yasiyo ya kibiblia ya imani ya wafuasi wa Pelagius (mtawa wa kiume) ambayo ilikanusha uhusiano wa aina yo yote ya dhambi za wanadamu kurithiwa toka kwa Adamu.
5. Makasisi wa Kilatini (yaani kanisa la magharibi), wakiufuata mtazamao wa Augustine, walikazia juu ya nafasi ya Adamu katika utata wa uovu, dhambi, na kuteseka kwetu katika ulimwengu tulio nao.
6. Katika kipindi cha Marekebisho ya Waprotestanti warekebishaji wakuu walimuunga mkono Augustine, ambapo Armenius aliboresha sehemu ya mashambulizi ya wafuasi wa Pelagius kwa washikiliaji wa nadharia ya Calvin.
7. Wanafalsafa pamoja na wanathiolojia walieleza nadharia kadhaa zinazohusu dhambi:
    a. Kant—mengine hayajulikani, ni kitu kisichoelezeka katika mazingira thabiti yenye kutambuliwa
    b. Leibnitz—ni kutokana na mipaka ya asili ya mfumo wa ulimwengu
    c. Schleiermacher—ni kutokana na asili ya hisia za mwanadamu
    d. Ritschl—ni kutokana na ujinga
    e. Barth—ilihusishwa ile siri ya wazo la awali
    f. Whitehead—dhambi ni kitu cha kurithi katika mfumo wa ulimwengu huu. Hii inatenda kazi kwa makusudi ya kukuza sehemu zote kati ya Mungu na mwanadamu.
8. Msukumo mkuu wa Biblia ni ukombozi wa mwanadamu kutoka katika dhambi na uovu, aliyeumbwa kwa nafsi, Mungu mwenye pendo kupitia Kristo. Asili ya dhambi haikujadiliwa kamwe.

## MADA MAALUM: ANGUKO (Mwanzo 3; angalia kumbukumbu za fafanuzi za maandiko kwenye mtandao katika fasihi ya Mwanzo) KATIKA AGANO JIPYA

Anguko liliwaathiri wanadamu wote kama inavyoelezwa dhahiri katika mjadala wa Paulo katika Rum. 5:12-21 inaanza na thiolojia ya utendaji dhambi wa mwanadamu katika kitabu cha Warumi. Hoja ya kwanza ya "habari njema"ya injili ndiyo habari mbaya ya hitaji la mwanadamu! Paulo alilianzisha hili toka Rum 1:18-3:18 (hitimisho la muhtasari ni Rum 3:19-31). Warumi kinaelezea juu ya kupotea, halia ya utendaji dhambi, na hitaji la mwanadamu.

1. Wapani wasio wadilifu
2. Wapagani walio wadilifu
3. Wayahudi

Kila mmoja anawajibika kwa Mungu kwa sababu ya

1. Ufunuo wa kiasili, Rum. 1:18-23
2. Ushuhuda adilifu wa ndani, Rum. 2:14-16

Moja ya vifungu vya kuogofya vinavyojirudia katika Warumi 1-3ni kile, "Mungu akawakabidhi kwa"(kama vile Rum. 1:24,26,28; Efe. 4:17-19). Litania ya kushangaza ya maandiko ya Agano la Kale yamenukuliwa katika Warumi 3:9-18! Mwanadamu yuko katika matatizo makubwa, mahitaji, na uasi! Mtu hawezi kuhitaji "mwokozi" mpaka pale atakapotambua hitaji lake!

Warumi 5:12-21 ni mjadala wa Yesu kama Adamu wa pili (kama vile I Kor. 15:21-22, 45-49; Flp. 2:6-8). Hii inatoa msistizo juu ya dhana ya kitheolojia ya dhambi ya watu wote na hatia ya ushirika. Ufafanuzi wa Paulo wa anguko la mwanadamu (na uumbaji) ndani ya Adamu ulikuwa wa kipekee na wa tofauti na ule wa walimu wa sheria za Kiyahudi ambapo mtazamo wake wa ushirika ulikuwa katika mtiririko wa ufundishaji wa walimu wa kisheria.

Ufafanuzi huu ulionyesha uwezo wa Paulo chini ya matumizi ya uvuvio, au maongezeko, kweli alizokuwa

akizifundisha wakati wa mafundisho yake huko Yerusalemu chini ya Gamalieli (kama vile Matendo ya Mitume 22:3).

Mafundisho yaihusuyo asili ya dhambi yanayotokana na Mwa. 3 yaliyofafanuliwa na Augustine na Calvin. Haya yalieleza kwamba wanadamu wamezaliwa wakiwa na dhambi. Mara nyingi Zaburi 51:5; 58:3; na Ayubu 15:14; 25:4 zinatumika kama uthibitisho wa maandiko ya Agano la Kale. Tofauti nyingine ya kitheolojia kwamba wanadamu wanawajibika kimaadili na kiroho katika chaguzi na hatima zao wenyewe zilifafanuliwa kwanza na walimu wa sheria na kisha katika kanisa na Pelagius na Arminius. Kuna baadhi ya ushahidi wa mtazamo wao katika Kumb. 1:39; Isa.7:15; na Yona 4:11; Yohana 9:41; 15:22,24; Matendo ya Mitume 17:30; Rum. 4:15. Msukumo wa hali hii ya kithiolojia ungekuwa kwamba watoto hawakuwa na hatia hadi kufikia umri wa majukumu ya kimaadili (kwa wavulana miaka 13 na kwa wasichana miaka 12).

Kuna hali ya suluhu ambapo mwelekeo wa asili ya uovu na umri wa majukumu ya kimaadili vyote ni sawa! Uovu si ushirika, bali uovu endelevu wa mtu mwenyewe na dhambi (maisha yaliyo tofauti na Mungu). Udharimu wa kibinadamu si tatizo (kama vile Mwa. 6:5,11-12,13; Rum. 3:9-18,23), bali lini, wakati wa kuzaliwa au maisha ya baadaye yanayofuatia?

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 3: 1-7**

**[1]Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya Bwana Mungu. Akamwambia mwanamke, Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?2Mwanamke akamwambia nyoka, Matunda ya miti ya bustanini twaweza kula; 3 lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani Mungu amesema, Msiyale wala msiyaguse, msije mkafa.4 Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa,5 kwa maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho, nanyi mtakuwa kama Mungu, mkijua mema na mabaya.[6]Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa, basi alitwaa katika matunda yake akala, akampa na mumewe, naye akala.[7]Wakafumbuliwa macho wote wawili wakajijua kuwa wa uchi, wakashona majani ya mtini, wakajifanyia nguo.**

**3:1 "Basi"** Hili si la kidunia bali ni mbinu pekee ya kifasihi ya kueleza hatua mpya katika mvuto wa uumbaji. Hatufahamu ni kwa muda gani Adamu na Mungu waliishi pamoja ama Adamu aliiishi muda gani, Eva, na Mungu walikuwa pamoja kabla ya ufafanuzi huu.

◙**"nyoka"** Tazama Mada Maalum ifuatayo. Nyoka pia ni adui kutokana na ushairi wa Gilgamesh (kama vile 11:287-289) ambaye aliiba matunda ya mti wa uzima wa milele.

### MADA MAALUM: NYOKA (MWANZO 3)

A. Hili neno "nyoka" ni *Nachash* (BDB 638, KB 690 I). Neno hili lina asili zifuatazo:
   1. *Kal Stem* - "sauti ya mlio wa nyoka" (kama vile Yer. 46:22)
   2. *Piel Stem* - "kunong'oneza" kama katika usihiri ama uaguzi (kama vile Law. 19:26; Kumb. 18:10; 2 Fal.21:6
   3. Kutokana na 4:22 -"kuangaza" bila shaka neno hili lilihusiana na neno "shaba"(BDB 638, KB 690 II)
   4. Kutokana na mzizi wa Kiarabu -"kutambaa" (BDB 267, KB 2671, kama vile Kumb. 32:24)
B. KIBAINISHI CHA WAZI kipo katika Mwa. 3:1, ambacho kinaonyesha nyoka mmoja wa kipekee ama

mwenye utambulisho binafsi.

C. Uhalisia wa huyu nyoka unashikiliwa kwa:
   1. Kuorodheshwa kama mmoja wa wanyama wa bustani ile iliyoumbwa Mungu.
   2. Ni adhabu inayotolewa kama mnyama halisi.
   3. Huyu anadokezwa kwa upekee katika Agano Jipya, II Kor. 11:3 na I Tim. 2:13-14.

D. Huyu nyoka alitambulishwa kama Shetani (angalia Mada Maalum: Shetani) katika:
   1. Kitabu cha kipindi cha Agano la Kale na Agano Jipya kiitwacho kitabu cha "Hekima," 2:23-24. "Kwa jinsi hiyo Mungu alimuumba mwanadamu ili aishi milele; . . . hata hivyo, kupitia wivu wa Ibilisi kifo kilikuja ulimwenguni."
   2. Irenaeus (yapata 130-202 B.K)
   3. Ufunuo 12:9; 20:2
   4. Ufanano haupatikani katika kitabu cha Agano la Kale lenyewe kwa sababu kitabu hiki hakijadili juu ya Mwa. 3 kwa marefu yo yote. Hili pia halitajwi wala kufasiriwa katika kitabu cho chote cha Agano la Kale.

E. Kwa nini Shetani hatajwi kwa upekee – Msisitizo wa andiko hili juu ya uwajibikaji wa mwanadamu, si jaribu lililoikabili nguvu ya asili. Katika Warumi 1-3 ambapo mwanadamu mwenye dhambi anaonyeshwa na 4-8 ambapo matokeo yake yanaelezwa, Shetani hatajwi kamwe.

F. Kuna uwezekano halisi kuwa nyoka wa Mwanzo 3 anawakilisha mnyama mwenye machafuko wa Kisumeri, hadithi za kubuni za Babeli (angalia Mada Maalum: Leviathan). Sanamu hizi zinatumika kwenye Biblia (kama vile A 2yubu 6:13; 41:1-34; Zab. 74:14; Isa. 27:1; Amos 9:3), lakini pasipo ukweli wenyewe wa hadithi za kubuniwa za kipagani (angalia G. B.Caird, *The Language and Imagery of the Bible,* sura 13, "*The Language of Myth,*" kurasa za 219-242).

◙**"mwerevu"** Kuna uwezekano wa aina mbili wa kucheza na maneno (neno hili lina matamshi yanayokaribiana na neno "kuwa uchi" la 2:25) yanayohusiana na neno hili (BDB 791, KB 886):
(1) "mwerevu" au "mwenye hekima" na
(2) "mwenye mwerevu" (m.f. Mith. 1:4; 8:5,12; 12:16,23; 13:16; 14:8,15,18; 22:3; 27:12). Neno hili halionekani kuwa kinyume kwa namna lilivyotumika kumhusu nyoka bali ni utambuzi wa kipee wa sifa zake (kama vile Mt. 10:16). Huenda ndiyo sababu ya huyu mwovu kuchagua kuuvaa mwili wa mnyama huyu wa kipekee.

◙ **"wanyama wote wa mwitu"** Aya hii inaonyesha kwamba huyu nyoka alikuwa mmoja wa wa muundo wa wanyama wengi walioumbwa.

◙ **"Bwana Mungu"** Neno la kwanza "Bwana" ni jina la Mungu la kimaagano, YHWH, kutoka kitenzi cha Kiebrania "kitenzi" (kama vile Kut. 3:14). Neno la pili "Mungu" ni neno la Kiebrania *Elohim* ambalo lina muundo wa WINGI wa neno la Mungu katika Mashariki ya Karibu ya kale, *El*. Walimu wa sheria walisema kwamba jina YHWH husimama kuwakilisha ya agano la huruma ya Mungu ambapo jina *Elohim* husimama kumwakilisha Mungu muumbaji. Angalia Mada Maalumu: Majina ya Uungu katika 2:4.

◙ **"Akamwambia"** Kumekuwa na madhanio mengi kuhusu maelezo ya nyoka (si kiwakilishi cha nafsi). Hatufahamu uhusiano uliokuwepo kati ya wanadamu na wanyama kabla ya lile anguko japo hawa lazima walikuwa marafiki. Hata hivyo, Nadhani kwamba usemi huu ni sehemu ya sura ya Mungu ndani ya mwanadamu na ndivyo ilivyo, hivyo, si wa kawaida kwa wanyama. Ushirika kama huu unakwenda kurejeshwa katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (kama vile Isa. 11:6-11). Nadhani kwamba Shetani alikaa ndani ya nyoka na hivyo ni sauti yake ambayo ilisikika. Kinachoshangaza kithiolojia ni kwamba Hawa hakushangazwa na hili!

## MADA MAALUM : UOVU BINAFSI

I. SHETANI NI SOMO GUMU KUTOKANA:

1. Agano la Kale halibainishi adui mkubwa wa (Mungu), bali mtumishi wa YHWH ambaye anawapa wanadamu mbadala na kutuhumu huyu mwanadamu kwa kutokuwa na haki (A. B. Davidson, *A Theology of the OT,* kur. 300-306).
2. Dhana ya adui mkubwa wa Mungu ulianza wakati wa fasili kati ya Biblia (zisizo na taratibu za kikanisa) katika kipindi cha dini ya kiislamu iliyoanzishwa na Zoroaster huko Uajemi. Hii kwa namna nyingine, kwa kiwango kikubwa ilisababisha sheria ya dini ya Kiyahudi (yaani, waliokuwa wametengwa na kuishi nje ya Israel yaani Babiloni, na Persia).
3. Agano Jipya linaunda dharura ya Agano la Kale katika ugumu wa ajabu lakini makundi yaliyochaguliwa

kama mtu anaanza kusoma habari za uovu katika mtizamo wa thiolojia ya biblia (kila kitabu au mwandishi au michoro alisoma na kuandika kwa kifupi kwa kutenganisha) basi mawazo mbalimbali kuhusu uovu yangeibuliwa. hata hivyo, mtu ataanza kusoma kuhusu uovu lakini kwa njia isiyo ya kibiblia au nje zaidi ya biblia mfano dini za kiulimwengu au dini za mashariki, basi sehemu kubwa ya mambo mengi ya maendeleo ya agano jipya yalionyeshwa katika pande mbili za uajemi na tabia za uyunani na kiroma.

Kama mtu alidhaniwa kujitoa kwa uwezo wa kiungu neno la Mungu (kama nilivyo!),kwa hiyo mambo ya Agano Jipya lazima yaonekane kama ufunuo endelevu. Wakristo yawapasa wajilinde dhidi ya kuruhusu simulizi za Kiyahudi au fasihi za Kiingereza (yaani, Dante, Milton) kufafanua zaidi dhana hiyo bila shaka miujiza na maana tofauti tofauti katika eneo hili la wokovu. Mungu amechagua kutobainisha mambo yote ya uovu, asili yake,kusudi lake,lakini amebainisha kushindwa kwake!

II. SHETANI KATIKA AGANO LA KALE

Katika Agano la kale neno "Shetani"(BDB 966, KB 1317)au "mshitaki" linaonekana kuhusiana na makundi matatu tofauti.

1. Washtaki wa wanadamu (1 Sam. 29:4; 2 Sam. 19:22; 1 Fal. 5:4, 11:14,23,25; Zab. 109:6,20,29
2. Washtaki wa kimalaika (Hes. 22:22-23; Zak. 3:1)
    1. Malaika wa Bwana –Hes. 22:22-23
    2. Shetani-1 Nya. 21:1; Ayub 1-2; Zak. 3:1
3. Washtaki wa kimapepo (bila shaka shetani) (1 Fal. 22:21; Zak. 13:2)

Baadaye katika kipindi cha kuingia agano jipya ibilisi wa Mwanzo 3 alijulikana ni shetani (kama vile Kitabu cha Hekima 2:23-24; II Enoch 31:3), na hata baadaye ambapo anakuja kuwa chaguo la viongozi wa kidini wa Uyahudi (kama vile. *Sot* 9b na *Sanh*. 29a). "wana wa Mungu" wa Mwanzo 6 wanakuwa malaika wa uovu katika I Enoch 54:6. Wanakuwa waanzilishi wa uovu katika thiolojia ya viongozi wa kidini wa Kiyahudi. Nalitaja hili sio kwa kuonyesha usahihi wake wa kithiolojia, bali kuonyesha maendeleo yake katika Agano Jipya, shuguli hizi za Agano la Kale zinachangia katika uovu wa malaika wa nuru (yaani shetani) katika 2 Kor. 11:3; Ufu. 12:9.

Asili ya uovu wa yule aliyejigeuza kuwa malaika wa nuru ni mgumu au haiwezekani (kutegemea maoni yako) kuupima toka katika Agano la Kale. Sababu moja wapo ni ile imani ya nguvu juu ya uwepo wa Mungu mmoja tu. (kama vile. Kumb. 6:4-6; 1 Fal. 22:20-22; Mhu. 7:14; Isa. 45:7; Amos 3:6). Majeruhi wote walipelekea YHWH kuonyesha kwa vitendo alivyo wa pekee na mkuu (kama vile. Isa. 43:11; 44:6,8,24; 45:5-6,14,18,21,22).

Uwezekano wa vyanzo vya habari ni (1) Ayubu 1-2, ambapo shetani ni mojawapo wa wana wa Mungu "mwana wa Mungu" (yaani, malaika) au (2) Isaya 14; Ezekieli 28, ambapo ujivuni karibu na wafalme wa mashariki (Babeli na Uturuki) wamekuwa wakielezea sifa au ujivuni wa shetani (kama vile 1 Tim. 3:6). Nimechanganya mihemko kuhusu kuliendea suala hili. Ezekieli anatumia bustani ya Edeni kama neno mbadala sio tu kwa mfalme wa Uturuki kama shetani (kama vile. Ezek. 28:12-16), lakini pia

kwa ufalme wa Misri kama mti wa maarifa wa mema na mabaya (Ezekieli 31). Hata hivyo, Isaya 14, hasa kurasa 12-14, anaonekana kuelezea uasi wa malaika kupitia majivuno kama Mungu alivyotaka kubainisha kwetu jinsi alivyo hasa na asili ya shetani hii ni njia isiyo elezea moja kwa moja na mahali pa kuifanya (tazama Mada Mada Maalumu: Lusifa). Lazima tujilinde dhidi ya mwenendo wa Theolojia wa kuchukua sehemu ndogo ndogo, tata toka kwenye maeneo yenye maana mbalimbali ya waandishi, vitabu, na kuviunganisha kama vipande vipande vya fumbo la Kiungu.

III. SHETANI KATIKA AGANO JIPYA

Alfred Edersheim (*The Life and Times of Jesus the Messiah*, juzuu. 2, kiambatisho XIII [kur.. 748-763] na XVI [kur. 770-776]) anasema mafundisho ya sheria za Kiyahudi yameathiriwa wazi kabisa na umiliki wa pande mbili za Uajemi na mtizamo wa kimapepo. viongozi hawa wa kidini sio vyanzo vizuri vya ukweli katika eneo. Yesu kimsingi anakwepa kutoka kwenye mafundisho ya sinagogi. Nafikiri kuwa dhana ya viongozi wa dini ya kiyahudi ya upatanisho wa kimalaika (kama vile Matendo 7:53) na upinzani katika kutoa sheria za Musa kwenye mlima Sinai ilifungua mlango kwa dhana ya adui mkuu wa YHWH kadhalika na mwanadamu. Palikuwa na Mungu wawili wa pande mbili za Iran (ufuasi wa Zoroastra).

1. *Ahura Mazda,* baadaye akaitwa *Ohrmazd*, aliyekuwa mungu muumbaji, mungu mwema
2. *Angra Mainyu,*baadaye aliitwa *Ahriman*,roho aangamizaye, mungu mwovu,

Vita juu ya ukuu na dunia ikawa kama uwanja wa vita. Umiliki wa pande mbili ukajengeka ndani ya pande mbili za Kiyahudi zenye ukomo kati ya YHWH na shetani.

Hakika kuna mafunuo endelevu katika agano Jipya kama ilivyo kwenye uovu, lakini sio kama ilivyoelezewa kama walimu wa dini ya Kiyahudi wanavyodai. mfano mzuri wa utofauti huu ni "vita vya mbinguni." Kuanguka kwa shetani (Mwovu) ni mantiki yenye umuhimu, lakini sehemu husika haikutolewa (Tazama Mada Maalumu: Kuanguka kwa shetani na malaika wake). Hata hivyo kile kilichotolewa kimefichika kwenye mafunuo tanzu (k.v. Ufu. 12:4,7,12-13). Ingawa shetani ameshindwa na kutupwa duniani, bado anatenda kazi kama mtumishi wa YHWH (kama vile. Mt. 4:1; Luka 22:31-32; 1 Kor. 5:5; 1 Tim. 1:20).

Lazima tuthibiti kiu yetu katika eneo hili. Kuna nguvu binafsi ya majaribu na uovu lakini bado kuna Mungu mmoja tu na mwanadamu bado anawajibika kwa uchaguzi wake. kuna vita ya kiroho kabla na baada ya wokovu. Ushindi waweza kuja tu na kubakia ndani na kupitia Mungu wa Utatu. Uovu umekwisha shindwa na utaondolewa (kama vile Ufu.20:10)!

◙ "**mwanamke"** Kumekuwa na madhaanio mengi miongoni mwa watoa maoni kwamba kwa nini Hawa alikwenda mbali na Adamu, hata vitenzi vilivyotumiwa na Shetani ni WINGI. Katika 3:6 hili linamaanisha kuwa Adamu angeonekana kupitia sehemu ya majibizano. Wengine wamedai kuwa hii ni ishara ya kutafuta utambulisho wake binafsi. Wengine wanaamini kuwa Shetani alimshawishi mwanamke kwa sababu mwanamke huyu hakuyasikia maagizo ya Mungu moja kwa moja (kama vile 2:16-17). Yote haya ni madhaanio.

◙ **"Ati! Hivi ndivyo alivyosema Mungu"** Walimu wa sheria wanasema kwamba Shetani angetumia neno YHWH lakini hakulitumia neno hili kwa sababu hakuwa na utambuzi wa huruma ya Mungu. Hata hivyo, neno hili linaonekana kuwa la uchochezi wa udhalimu katika ndani ya mtu anayemilikiwa na shetani aliyeonyeshwa katika Biblia (kama vile *The Theology of the Old Testament na* A. B. Davidson, krp. 300-306).

◙ **"Msile matunda ya miti yote ya bustani"** Hiki kifungu cha Kiebrania ni cha kipekee sana lakini kinaonekana kuwa na uhusiano na uthibitisho, si swali. Nyoka anaanza majibizano na mwanamke katika uhusiano na katazo la Mungu kuhusu mti uliokuwa katikati ya bustani.

**3:2** Hawa alieleza kuhusiana na miti mingine yote iliyoruhusiwa kama chakula (kama vile 2:16). Lakini nyoka alilitupilia mbali hili na kusiatiza juu ya katazo la Mungu kuhusu mti ule wa ujuzi wa mema na mabaya.

**3:3 “lakini matunda ya mti ulio katikati ya bustani”** Kutokana na Mwa. 2:9 tunajifunza kwamba kulikuwa na miti ya aina mbili katikati ya bustani, mti wa mema na mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Ni dhahiri kuwa tunda la miti hii angepewa mwanadamu kwa wakati sahihi, lakini kujitetea kwa mwanadamu katika kulinyakua tunda hili kuliutenga mbali mpango wa Mungu (ndiyo tofauti iliyopo kwa upokaji wa Yesu katika Flp. 2:6-11). Ule mti wa uzima ni wa kawaida kwa maelezo yote ya kale ya Mashariki ya Karibu kuhusu uumbaji, hata hivyo, ule mti wa ujuzi wa mema na mabaya ni wa kipekee katika Biblia. Hakuna mazingaombwe kuhusu tunda. Hii ilikuwa njia ambayo Mungu aliitumia, si kitu cha asili kinachoonekana katika ubora wa tunda lenyewe, ambalo lilifanywa kuwa muhimu.

◙ **“msije mkafa”** Neno hili (BDB 559, KB 502) limetumika mara tatu katika mist. 3 na 4. Haijulikani Hawa alielewa nini kuhusu kifo kwa wanyama ambao walikuwa hawafi. Hata hivyo, kwa kiasi fulani hili linaweza kuwa limemuunganisha mwanamume na mwanamke. Biblia inatambua aina tatu za vifo: (1) kifo cha kiroho ambacho kimeonyeshwa katika Mwa. 3; Isa. 59:2; Rum. 7:10-11; Efe. 2:1; Yakobo 1:15; (2) kifo cha kimwili ambacho ndiyo matokeo, Mwa. 5; na (3) kifo cha milele kama matokeo ya ukaidi wa mwanadamu, moyo wa uasi (kama vile Ufu. 2:11; 20:6,14; 21:8).

**3:4 “Nyoka akamwambia mwanamke, Hakika hamtakufa! ’”** Hiki ni KITENZIJINA HALISI cha neno *Qal* KAULI ISIOTIMILIFU kutokana na mzizi huo huo (BDB 559, KB 562) unaotumika kusistiza. Kwanza Shetani aliishambulia kweli ya Mungu yote; na sasa anaishambulia kweli ya neno la Mungu. Na, katika mst. 5, ataushambulia wema na huruma ya Mungu kwa mwanadamu. Muundo wa Kiebrania wa usemi huu uko katika muundo wa mabishano yaliyozidishwa. Shetani alikanusha usemi wa Mungu.

**3:5 “maana Mungu anajua ya kwamba siku mtakayokula matunda ya mti huo, mtafumbuliwa macho,”**Kulikuwa na kweli iliyowekewa mipaka kwa kile alichokisema Shetani, lakini hii ilikuwa kweli yenye kuhuzunisha (kama vile Tito 1:15). Kwa wafasiri hili linaonekana kuwa na (kistiari) matumizi ya neno “siku,” lenye maana ya “wakati wowote.” Kiuhalisia kifungu hiki cha Kebrania ni “ya kwamba.” Hiki KITENZI “kufumbuliwa” (BDB 824, KB 959, *Niphal* TIMILIFU, kama vile mst. 7) unamaanisha nguvu za asili, bila shaka ni nguvu ya ule mti au yule mwovu.

◙ **“mtakuwa kama Mungu”** Hili neno linalomzungumzia Mungu ni neno *Elohim*. Tazama Mada Maalum katika 2:4. Hili linatumika katika muktadha huu kumaanisha Mungu Mwenyewe na hivi ndivyo tafasiri nyingi zinavyokitafasiri kifungu hiki. Hatahivvo, neno hili pia linaweza kutumika kumaanisha malaika (kama vile Zab. 8:5,6; 82:1,6 [iliyonukuliwa katika Ebr. 2:7]; 97:7); hii inaweza kutumika kumaanisha “kiumbe cha roho” (kama vile I Sam. 28:13) na linaweza kutumika kumaanisha waamuzi wa Israeli (kama vile Kut. 21:6; 22:8-9). Hili linaonekana kuwa la kimantiki zaidi kwamba hii ni ahadi ya kuwa kama malaika, viumbe vya kiroho walio pamoja na Mungu ama huenda baraza la kimbingu (kama vile 3:22). Hili ni la kimzaha kwamba mwanadamu alijaribu kushikiria nafasi kutoka kwa Mungu ambayo tayari ilikuwa yake. Ubinadamu ni mpangilio wa juu wa kiroho kuliko malaika (kama vile EbR. 1:14; 2:14-16; I Kor. 6:3).

**3:6 “Mwanamke alipoona ya kuwa ule mti wafaa kwa chakula, wapendeza macho, nao ni mti wa kutamanika kwa maarifa”** Hapa tunaziona hatua tatu fungamano kuanzia jaribu hadi tendo halisi la dhambi. Walimu wa sheria wanasema kwamba macho na masikio ni madirisha ya nafsi na kile tunachokipokea katika ukuaji ndani ya mioyo yetu hadi kulifikia tendo muhimu lilio la kujitolea.

◙ **“akampa na mumewe, naye akala”** Kumekuwapo na madhanio mengi kuhusu mstari huu. Walimu wa sheria walidai kwamba Adamu alikula tunda ili asitengane na mkewe. Hili pia lilizungumziwa na Milton katika *Paradise Lost*. Hata hivyo, hili linaonekana kutokana na muktadha huu, kwamba Hawa alimtenda Adamu kama nyoka alivyomtenda yeye, mbali na ushahidi wa kiuzoefu kwamba mwanamke huyu alikuwa amekwisha kula na hakufa. Walimu wa sheria nao wakadai kwamba nyoka aliitumia mbinu hii kwa Hawa; kwamba alimlazimisha kuligusa tunda na kusema, “Hakika, hautakufa.” Bila shaka alimwambia Adamu,“Hakika, sitakufa.”

**3:7 "wakajijua kuwa wa uchi"** Hili limekuwa likitumiwa na watoa maoni wengi kuelezea juu ya asili ya zinaa kutokana na jaribu (kama vile Kor. 11:3, "nyoka alimdanganya Hawa"). Hata walimu wa sheria wanasema kwamba nyoka alindanganya Hawa kizinaa, lakini hili linaonekana kuwa kosa la usomaji wa maandiko. Maarifa yao mapya hayakuwa ya baraka yalikuwa ya kuelekea uharibifu (kama vile Tito 1:15).

◙ **"wakashona majani ya mtini"** Mtazamo wa kiutamaduni kwamba Hawa kula tunda ni kisio la hali ya juu. Walimu wa sheria wanasema kwamba mwanamke huyu alikula tini ambapo walichukua majani ya kujitengenezea mavazi. Hata hivyo,"lile tunda" linaweza kuwa tarehe au aina nyingine ya tunda ambalo sisi hatulijui. Aina ya hili tunda ni ya utata.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MWANZO 3:8-13**

**8 Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone. 9 Bwana Mungu akamwita Adamu, akamwambia, Uko wapi? 10 Akasema, Nalisikia sauti yako bustanini, nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi; nikajificha. 11 Akasema, Ni nani aliyekuambia ya kuwa u uchi? Je! Umekula wewe matunda ya mti niliyokuagiza usiyale? 12 Adamu akasema, Huyo mwanamke uliyenipa awe pamoja nami ndiye aliyenipa matunda ya mti huo, nikala. 13 Bwana Mungu akamwambia mwanamke, Nini hili ulilolifanya? Mwanamke akasema, Nyoka alinidanganya, nikala.**

**3:8 "wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini "** Toleo la King James lina kifungu "wakasikia sauti ya Bwana Mungu" lakini neno la Kiebrania linamaanisha sauti yake Yeye aliyekuwa akitembea (BDB 229, KB 246) ni *Hithpael* KAULI ENDELEVU). Muundo wa Kiebrania muktadha unaonekana kumaanisha kwamba hili lilikuwa tendo la kawaida ambapo Mungu na wale wenza wawili wa mwanzo walikutana kwa ushirika. Hasa hasa hiki ni kifungu cha elimu ya kibinadamu kwa Mungu ambaye ni kiumbe cha kiroho na hana mwili. Wengine wamedai kwamba Mungu alijivika Mwenyewe katika mfumo wa mwnadamu kwa ushirika pamoja na wale wenza halisi. Hili linaweza kuwa kweli, lakini sehemu pekee ya Mungu wa Utatu ambaye ana uwepo wa kimwili ni Mwana. Wengine wamedhani kwamba kwa sababu Agano Jipya linaeleza juu ya umuhimu wa uumbaji wa Mwana (kama vile Yohana 1:3,10; I Kor. 8: 6; Kol. 1:16; Ebr. 1:2), na kwamba mara nyingi kumekuwepo na uthihirisho wa Mungu (yaani, Malaika wa Bwana, mf. Mwana.16:7-13; 22:11-15; 31:11, 15; 48:15-16; Kut. 3:2,4; 13:21; 14:19) hili linaweza kurejelea juu ya ule mwili wa awali wa Kristo.

◙ "**wakati wa jua kupunga**" Hiki kifungu cha Kiebrania kinahusiana na neno wingu (BDB 398). Hiki kinazungumzia upepo mwanana wa asubuhi ama jioni.

◙ "**Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone**" KITENZI hiki (BDB 285, KB 284) is *Hithpael* KAULI ISIYO TIMILIFU. Huzuni ya dhambi inaweza kuwa imekwisha kuonekana katika hisia pamoja na utengano wa kimwili kati ya Mungu na uumbaji Wake (kama vile Zab 139; Ufu. 6:16).

**3:9 "Uko wapi"** Kwa uwazi kabisa Mungu hatafuti habari, bali anauliza swali ili waweze kutambua kile walichokifanya (kama vile mst. 11). Hizi aina za maswali ambayo majibu yake Mungu aliyafahamu, katika Agano la Kale yametumika kueleza juu ya kipengele endelevu katika sifa ya Mungu, iitwayo "imani ya wazi ya uwepo wa miungu" (yaani, Clark Pennock, *The Most Moved Mover* ).

**3:10 "nikaogopa kwa kuwa mimi ni uchi"** Ni huzuni ya namna gani! Adamu anamuogopa Mungu wa pendo aliyemuumba na alihitaji kumjua. Nguvu ya uovu inaweza kuonekana wazi hapa namna mwanadamu anavyozidi kujificha mbali na Mungu, yeye mwenyewe, kutoka katika familia yake na kutoka katika mpangilio wa kiasili. Hii dhana ya kwamba alikuwa uchi ilikuwa ni kwa ajili ya kuficha tatizo halisi ambalo lilifungua macho ya uasi wa mapenzi ya Mungu.

**3:12"Adamu akasema"** Hapa tunao msistizo juu ya ile dhana kwamba Adamu anawajibika hata kama anajaribu kumlalamikia Hawa, hata Mungu Mwenyewe. Hata katika woga wa kujitetea, anamlalamikia Hawa au Mungu, mwanadamu anawajibika kwa matendo yake mwenyewe. Theolojia ya Flip Wilson, "*The Devil made me do it*!"si ya msamaha zaidi ya "*Cultural environment made me do it*" au "*Genetic predisposition made me do it*," nk.

**3:13 "Nyoka alinidanganya, nikala"** Hawa kwa haraka alijifunza kutoka kwa Adamu na akaanza kujitetea. Hili neno "kudanganywa" linaonekana kumaanisha "kusababisha kusahau" (BDB 674, KB 728, *Hiphil* KAULI TIMILIFU). Hili inaweza kuwa tanakali- sauti ya mlio wa nyoka yaani,. *hissi'ani*). Kitabu chA Agano Jipya kinayataja matendo ya Hawa katika II Kor. 11:3 nma I Tim. 2:14.

## TAMBUZI ZA NDANI KATIKA MWANZO 3:14-24

## UTANGULIZI

A. Kifungu hiki, kama ilivyo 3:1-12, ni cha muhimu katika kuelewa kwetu juu ya hali ya dhambi ya ulimwengu wa sasa, maradhi, maumivu, kutokuwepo kwa haki, na uovu. Huu si ulimwengu ambao Mungu aliukusudia kuwa. .

B. Kifungu hiki, hasa mst. 15, kinatupa neno letu la kwanza kuhusu namna gani ulimwengu wetu unakwenda kuwa kwa sababu ya Mungu kuingilia kati! Hii ni ahadi kuu ya Mungu ya ukombozi kwa wale walioanguka, ubinadamu wa kuasi ulikuja kupitia "mwanamke."

C. Matokeo ya uasi dhidi ya watu wa Mungu na neno kwa uwazi yanatabiriwa! Katika namna iliyo dhahiri Shetani anaonekana kama mwongo na msababishi wa dhambi katika maisha ya Adamu na Hawa na watoto wao.

D. Uhusiano kati ya mwanamke na mwanamume unaelezwa dhahiri katika mst. 16 (kama vile II Tim. 2:9-15; Efe. 5:22; Kol. 3:18; I Pet. 3:1). Mahusiano ya ulimwengu wetu yaliyotiliwa mkazo ni matokeo ya moja kwa moja ya asili, kutoitikia kwa makusudi. Ikiwa kuna utoaji sababu za matatizo katika Agano la Kale, huu unaweza kuwa mfano. Hata hivyo, hawa pia wameguswa kwa neema ya Mungu katika Kristo (kama vile I Kor. 11:11; Gal. 3:28).

E. Walimu wa sheria wanakanusha juu ya asili ya dhambi na kupendekeza "*yetzers"* mbili (dhamira). Hata hivyo, huu unaonekana kuwa ushahidi wa Agano la Kale juu ya asili ya kutenda dhambi kwa Adamu katika Ayubu; 15:14; 25:4; Zab. 51:5 na vifungu vya sasa vya Agano Jipya katika Rum. 5:12-21.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MWANZO 3:14-19**

***14*** **Bwana Mungu akamwambia nyoka, Kwa sababu umeyafanya hayo, umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote, na kuliko hayawani wote walioko mwituni; kwa tumbo utakwenda, na mavumbi utakula siku zote za maisha yako;** ***15*** **nami nitaweka uadui kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake; huo utakuponda kichwa, na wewe utamponda kisigino.** ***16*** **Akamwambia mwanamke, Hakika nitakuzidishia uchungu wako, na kuzaa kwako; kwa utungu utazaa watoto; na tamaa yako itakuwa kwa mumeo, naye atakutawala.** ***17*** **Akamwambia Adamu, Kwa kuwa umeisikiliza sauti ya mke wako, ukala matunda ya mti ambao nalikuagiza, nikisema, Usiyale; ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako;** ***18*** **michongoma na miiba itakuzalia, nawe utakula mboga za kondeni;** ***19*** **kwa jasho la uso wako utakula chakula, hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa; kwa maana u mavumbi wewe, nawe mavumbini utarudi.**

**3:14 "Bwana Mungu"** Huu ni muungano wa maneno makuu ya Mungu katika Agano la Kale, YHWH na *Elohim*. Tazama maelezo katika 2:4.

◙ **"akamwambia nyoka**" Munga hakumuuliza nyoka maswali kama alivyofanya kwa Adamu na Hawa. Huyu nyoka anahukumiwa kama chombo cha Yule mwovu.

◙ **"umelaaniwa wewe kuliko wanyama wote"** Hiki KITENZI (BDB 76, KB 91) ni *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU. Hili halimaanishi kwamba wanyama wote (ni maana iliyo pana kuliko ile ya myama aina ya ng'ombe, huenda ni wanyama watambaao) walikuwa wamekwisha kulaaniwa. Hiki kifungu "kuliko" kinaweza kumaanisha "kati ya wanyama wote."Walimu wa sheria wanasema kwamba kifungu hiki kinarejelea kipindi cha kuchukua mimba kwa wanyama dhidi ya kipindi kile cha nyoka, ambacho kinaelezewa na buku la sheria za Kiyahudi kuwa ni siku saba.

◙ **"kwa tumbo utakwenda"**Cho chote kilichotambaa kwa tumbo lake kilifikiriwa na Waebrania kuwa si kisafi (kama vile Law. 11:42). Walimu wa sheria wanasema kwamba Mungu aliikata miguu ya nyoka ili kumfanya atambae kwa tumbo, lakini hili linaweza kuwa sawa na ile ishara ya upinde wa mvua wa Mwa. 9:13 ambao huenda ulikuweko mara kwa mara lakini sasa unachukua nafasi ya maana ile iliyomaanishwa na Mungu katika njia ya kipekee.

◙ **"na mavumbi utakula"**Hili linadokezwa katika Isa. 65:25. Hiki kinaonekana kuwa kipengele cha Mungu kumlaani Yule nyoka halisi.Ndani ya Biblia kifungu hiki kinaweza kuwa stiari yenye kurejelea kushindwa na aibu (kama vile Zab. 79:9; Isa. 49:23; Mika 7:17). Hizi kauli zote ZISIZO TIMILIFU za mstari huu zinatumika katika maana ya KITENZI CHA KUAMURU.

**3:15 "nitaweka uadui**" Uadui (BDB 33) ni neno linalotumika kati ya watu wawili. Hili linaonekana kuwa la kimabadiliko ambapo hukumu ya Mungu inatolewa kwa Shetani, si nyoka halisi (kama vile Ufu. 12:9; 20:2). Tazama katika See "*The Presence of God Qualifying our Notions of Grammatical-historical Interpretation*: *Genesis 3:15 as a Test Case*" na Vern S. Poythress, JETS, juzuu. 50.1, kr. 87-103).

◙ **"kati yako na huyo mwanamke, na kati ya uzao wako na uzao wake**" Kumekuwa na mjadala mkubwa miongoni mwa watoa maoni kuhusu mstari huu. Katika muktadha wa kikanuni hili linaonekana kurejelea wana (yaani "Uzao," BDB 282) wa yule mwovu (kama vile Mt. 13:38; Yohana 8:44) na wana wa Masihi (kama vile Irenaeus). Lakini kwa sababu ya mstari unaofuatia muundo wa UMOJA wa neno "yeye" na "wewe" unaonekana kurejelea juu ya mvutano kati ya Mungu na yule mwovu anayeashiriwa katika kazi ya ukombozi Wa Yule Masihi ajaye.

Masihi (kama vile Irenaeus). Ni dhahiri kwamba Adamu na Hawa hawakuelewa matokeo ya hili, ama ndivyo alivyofanya Musa, ingawa Musa alilitambua hili katika Kumb. 18:18 kwamba nabii mkuu kuliko yeye anakuja. Nafikiri kwamba hili huenda lilikuwa dokezo la uzao wa yule bikra, ingwa kwa hakika halikujulikana kwa mwandishi asilia nwa mwanadamu, bali lilijulikana kwa mwandishi wa Uungu (Roho Mtkatifu). Kama mwanadamu alivyoshindwa kupitia msukumo wa ghafla wa mwanamke, mwanamke atakombolewa kupitia utii wa mwanamke katika ngvu ya asili ya kuchukua mimba ya Masihi kupitia Roho Mtakatifu (kama vile Isa. 7:14; Mt. 1:18-25; Luka 1:26-38, tazama *A Guide To Biblical Prophecy*, uk. 78 na 80). Toleo la Biblia ya Kilatini linakibadili kiwakilishi hiki "yeye" katika kifungu kinachofuatia na kuwa "kiwakilishi cha jinsi ya _ke" ambacho kwa ujumla si sahihi, bali kinaweza kushikilia kiini cha umuhumu wa Yule mkamilishaji. Kama unabii ambavyo haukueleweka leweka kwa ukamilifu hadi utimilifu wake wa kihistoria katika uzao wa kibikra wa Yesu, suala hili hili lazima lizungumziwe kuhusu ufasiri wa Mwa. 1 na 2. Historia inafunua ukweli wa kiufunuo kama funzo endelevu la kisayansi la dunia yetu inayoonyesha ugumu na mwingiliano wa mahusiano ya matendo ya Mungu! Hakuna mgogoro, ni utimilifu zaidi wa maarifa ya sehemu ya mwanadamu kama kazi za Mungu!

◙

**NASB "utakuponda kichwa"**
**NKJV "utakuponda kicha chako"**
**NRS "atakugonga kicha chako"**

**TEV “Watato wake watakuseta kichwa chako”**
**NJB “Utakupiga kichwa chako”**

Hili neno “kupiga”linaweza kumaanisha “kuseta,” “twanga / ponda,” “kuondoa kwa kufuta,” “kusaga,” ama “kugonga” (BDB 1003, KB 1446, *Qal* KAULI ISIYOTIMILIFU, limetumika mara mbili, kama vile Yakobo 9:17). Tambua KIWAKILISHI CHA NAFSI cha UMOJA (kama vile Rum. 16:20). Hatimaye mapambano haya yakashuka hadi kwa wanadamu.

◙
**NASB “na wewe utamponda kisigino”**
**NKJV “nawe utampiga kisigino Chake”**
**NRSV “nawe utamgonga kisigino”**
**TEV “utamonda kisigino chake”**
**NJB “nawe utamseta”**

KITENZI hiki hiki (BDB 1003, KB 1446, *Qal* KAULI ISIYOTIMILIFU) kinatumika kwa vyote, lakini ni dhahiri kwamba Shetani alipata mwisho mbaya wa mpango wake. Hili linaonenkana kurejerea juu ya kusulibiwa wakati kipengele hiki kinapoeleweka kutoka katika kilele cha Agano Jipya.

**3:16 Akamwambia mwanamke”** Hapa kunaonekana kuwa na misingi mikuu mitatu:
(1) maumivu ya kuzaa kwa uchungu zaidi (*Hiphil* KITENZI JINA HALISI na *Hiphil* KAULI ISIYO TIMILIFU ya KITENZI hiki hiki, BDB 915, KB 176);
(2) watoto wengi katika viuno;
(3) matatizo yanayohusiana na watoto wa viunoni; na
(4) utawala wa mwanamume. Tunaweza kuona namna haya yanovyohusishwa na uasi wa Hawa:
  (a) huyu alitaka kujitawala, anamtegemea mumewe kwa ujumla (na si Mungu);
  (b) aliitafuta furaha na shangwe ndani ya tunda lililozuiliwa, lakini sasa ana maumivu ya mara kwa mara ndani ya maisha yake. Ni dhahiri kwamba kitabu cha Agano Jipya kinalitambua hili kama umuhimu wa kitheolojia wa uhusiano uliaonguka kati ya mwanamume na mwanamke (kama vile I Tim. 2:9-15). Yatupasa kuweka ulinganifu kati ya wale walio ndani ya Kristo, I Kor. 11:11; Gal. 3:28, kile kinachoendelea kuwa, katika utangulizi mwaingine, ndani ya Adamu, Efe. 5:22; Kol. 3:18; I Pet. 3:1. Kuna mkanganyiko katika andiko la Kiebrania katika kipengele hiki. Neno linalotafsriwa hapa “kama watoto wadogo” kinaandikwa tofauti. Konsonanti za Kiebrania zingeweza kumaanisha “kuweka katika-subiri kwa ajili ya,” kinarejelea juu ya kuwajaribu watoto (kama vile *Hard Sayings of the Bible* , kr. 90-99).

◙ **“na tamaa yako itakuwa kwa mumeo”** Hapa neno la Kiebrania linatafsiriwa “tamaa” au “shauku” (BDB 1003, KB 1801). Walter Kaiser anadai kwamba neno hili linaweza kumaanisha “kugeukia,” bila shaka katika maana ya “kutawala” (kama vile Mwa. 4:7). Hawa alienenda kinyume na YHWH. Adhabu yake ni kuendelea kumgeukia mumewe, ambaye hali hii kwake ni ya kimanufaa (kama vile *Hard Sayings of the Bible, IVP uk*. 97-98).

◙ “**naye atakutawala**” Hiki KITENZI (BDB 605, KB 647) ni *Qa*l KAULI ISIYO TIMILIFU. Yanaonekana kuwa matokeo ya lile anguko na, Mungu atusaidie, kwani asili hii ya dhambi ya mwanaume imetuteka vibaya. Wivu, ubakaji, taraka na utawala usio wa ki-Mungu vimeiongoza shauku ya zinaa ya mwanadamu! Tumekuwa kama wanyama lakini katika tatizo la ubinafsi uliongezeka katika shauku ya kizinaa!

**3:17 “Kwa kuwa umeisikia sauti ya mke wako”**Adamu alitakiwa kuufuata mkono wa kuume wa Mungu, lakini yeye aliufuata mkono wa mkewe na kivunja amri ya Mungu ya kipekee (kama vile 2:15-17).

◙ **“ardhi imelaaniwa kwa ajili yako”** Hiki KITENZI (BDB 76, KB 91, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU) kinamaanisha kinyume cha kubarikiwa. Ardhi haitatoa mazao kwa uhuru na kwa wingi. Dunia ya sasa si ile aliyokusudia Mungu!

Katika neno hili kuna masihara ya neno "Adamu" *Adam*, BDB 9) na neno "ardhi" (*adamah*, BDB 9). Haya yote yana mzizi ule ule. Tunaweza kuona matokeo ya kuanguka kwa mwanadamu na asili katika Rum. 8:18-23. Pia imependekezwa kwamba hili linaaksi hali ya asili nje ya Bustani ya Edeni. Baada ya uasi wao Adamu na Hawa wanatupiliwa mbali na nafasi ya Mungu ya pekee na kwenda katika uwindaji/ ukusanyaji, silaha-na- ulimwengu wenye masumbufu.

◙ **"kwa uchungu utakula mazao yake siku zote za maisha yako"** Adamu alipewa kazi ya kuitunza bustani kabla ya Anguko (kama vile 2:15), ambayo ilikuwa ishara ya utawala, lakini sasa ni kazi ya masumbufu, ya kurudiarudia, ya lazima isiyo na mwisho kamwe (yaani, "uchungu" BDB 781). Na hata kazi ya mwanadamu, ardhi ilizalisha mazao machache (kama vile mst. 18). Tambua idadi ya KITENZI "kula" (BDB 37, KB 46) kilivyotumika katika sura hizi za ufunguzi (kama vile 2:16,17;3:1,2,3,6,11,12,13,14,17 [mara mbili],18,19,22)! Hili linahusiana na vyote utele na laana.

**3:19 "hata utakapoirudia ardhi, ambayo katika hiyo ulitwaliwa**" Haya ni mawasilianao kati ya anguko la Adamu, kifo cha kiroho (sura ya 3) na kifo cha kimwili (sura ya 5). Mungu ni mwaminifu. Yeye alisema kwamba angekizoelea kifo katika matokeo yake yote na kwa hakika walifanya!

◙ **"u mavumbi wewe"** kama vile Mwa. 2:7).

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 3:20-21**

[20] **Adamu akamwita mkewe jina lake Hawa; kwa kuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai.**
[21] **Bwana Mungu akawafanyia Adamu na mkewe mavazi ya ngozi, akawavika.**

**3:20 "Adamu akamwita mkewe jina lake Hawa**, **kwa kuwa yeye ndiye aliye mama yao wote walio hai"** Utawala wa mwanamume kwa mkewe sasa unaashiriwa kwa kumpa jina. Kwa asili ya neno, maneno "Hawa" (*hawwa*) na "walio hai" (*haya*) yanafanana sana na bila shaka huu ni mzaha wa Kiebrania ambao ni maarufu. Hii mizaha inayomhusu Adamu, Hawa, Kaini-Nod inaonyesha asili halisi ya maelezo hayo. Hii kejeli ya kwamba mwanamke huyu aliitwa "Hawa" ikimaanisha "walio hai" na badala ya uhai, yeye alileta kifo 3:21. Si kawaida kwamba wanadamu walihitaji kuvikwa hadi pale hali ya hewa na/au mabadiliko mengine ya mara kwa mara yaliyokuwa yakimgoja mwanadamu nje ya bustani ya Edeni yalipo dhihilika. Hiki kifo cha kwanza, kilianzishwa na Mungu kwa mahitaji ya mwanadamu, kwa uwazi jambo hili linaonyesha mahusiano ya Mungu na utoaji pamoja na ukweli wa hukumu na matokeo!
Tazama Mada Maalum hapa chini

## MADA MAALUM : KWA NINI MUNGU ALIWAVIKA ADAMU NA HAWA KWA NGOZI ZA WANYAMA

A. Kama utoaji wa maisha magumu nje ya Edeni
B. Kuwafunika iabu yao walioihisi ya kuwa uchi
C. Kuonyesha sheria ya kuwatumia wanyama kwa mahitaji ya mwanadamu
D. Kuonyesha tofauti katika utoaji wa mwanadamu (majani) na ule wa Mungu (ngozi)
E. Kuwakumbusha juu ya kifo chao kijacho (kama vile Mwa. 5)
F. Kuwaonyesha sitiari ya kuvika ya haki iliyowekwa ndani ya Kristo vazi iliyotolewa kwetu kama vazi jipya (kama vile Rum. 13:14; Gal. 3:27; Efe. 4:24; Kol. 3:8,10,12,14; Yakobo 1:21 I Pet. 2:1)
G. Kulionyesha pendo la Mungu lisilo na mwisho na utoaji kwa mwanadamu, hata kupitia anguko.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MWANZO 3: 22-24**

**[22]Bwana Mungu akasema, Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu, kwa kujua mema na mabaya; na sasa asije akanyosha mkono wake akatwaa matunda ya mti wa uzima, akala, akaishi milele; *[23]* kwa hiyo Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni, ailime ardhi ambayo katika hiyo alitwaliwa. *[24]* Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima.**

**3:22"Basi, huyu mtu amekuwa kama mmoja wetu"** Kumekuwa na mjadala mkuu kuhusu WINGI huu katika kitabu cha Mwanzo (kama vile 1:26; 3:22; 11:7). Mstari wa 22 unaanza na UMOJA na kufufunuliwa katika WINGI. Ikiwa tunaruhusu Andiko litafsiri Andiko, kwa uwazi kabisa hili hili linamrejelea Mungu wa Utatu, si muundo wa sarufi ya Kiebrania uitwao wingi wa ukuu. Hata hivyo, hili linaweza kurejelea juu ya (1) baraza la kimalaika (kama vile I Fal. 22:19), (2) nafsi mbili za Uungu katika Zab. 110:1, ama hata (3) mfano wa Uungu ujulikanao kama malaika wa BWANA; kwa mfano mmoja kati ya mingi, tazama kichaka kiliochokuwa kikiwaka moto cha Kut. 3:2,4.

◙ **"mti wa uzima"** Tumetambua hapao awali kwamba mti wa uzima ni wa kawaida katika Mashariki ya Karibu ya maandiko uumbaji wa kale. Hapa, mwanadamu anatengwa, si kwa sababu ya miungu, bali ni kwa sababu hii ingekuwa laana kwa mwanadamu kuishi milele katika maisha yake ya sasa ya anguko la hadharani.

◙ **"akaishi milele"** Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM : MILELE (*'olam*)

Asili ya neno la Kiebrania *'olam*, םלוע (BDB 761, KB 798) halijulikani (NIDOTTE, juzuu ya 3, uk. 345). Limetumika kwa maana mbalimbali (mara nyingi hutegemea muktadha mzima). Ifuatayo ni mifano michache iliyochaguliwa.

1. vitu vya kale
   a. watu, Mwa. 6:4; 1 Sam. 27:8; Yer. 5:15; 28:8
   b. sehemu mbali mbali, Isa. 58:12; 61:4
   c. Mungu, Zab. 93:2; Mith. 8:23; Isa. 63:16
   d. Vitu, Mwa. 49:26; Ayub 22:15; Zab. 24:7,9; Isa. 46:9
   e. Muda, Kumb. 32:7; Isa. 51:9; 63:9,11
2. wakati ujao
   a. Maisha ya mtu, Kut. 21:6; Kumb. 15:17; 1 Sam. 1:22; 27:12
   b. ukosoaji sana juu ya kutoa heshima kwa mfalme, 1 Fal. 1:31; Zab. 61:7; Neh. 2:3
   c. Kuendelea kuwepo kwa
      1) Dunia, Zab. 78:69; 104:5; Wimb. 1:4
      2) mbingu, Zab. 148:5
   d. uwepo wa Mungu
      1) Mwa. 21:33
      2) Kut. 15:18
      3) Kumb. 32:40
      4) Zab. 93:2
      5) Isa. 40:28
      6) Yer. 10:10
      7) Dan. 12:7
   e. Agano
      1) Mwa. 9:12,16; 17:7,13,19

2) Kut. 31:16
3) Law. 24:8
4) Hes. 18:19
5) 2 Sam. 23:5
6) Zab. 105:10
7) Isa. 24:5; 55:3; 61:8
8) Yer. 32:40; 50:5

f. Agano maalum na Daudi
   1) 2 Sam. 7:13,16,25,29; 22:51; 23:5
   2) 1 Fal. 2:33,45; 9:5
   3) 2 Nya. 13:5
   4) Zab. 18:50; 89:4,28,36,37
   5) Isa. 9:7; 55:3
g. Masihi wa Mungu
   1) Zab. 45:2; 72:17; 89:35-36; 110:4
   2) Isa. 9:6
h. Sheria za Mungu
   1) Kut. 29:28; 30:21
   2) Law. 6:18,22; 7:34; 10:15; 24:9
   3) Hes. 18:8,11,19
   4) Zab. 119:89,160
i. Ahadi za Mungu
   1) 2 Sam. 7:13,16,25; 22:51
   2) 1 Fal. 9:5
   3) Zab. 18:50
   4) Isa. 40:8
j. Uzao wa Ibrahimu na ahadi ya nchi
   1) Mwa. 13:15; 17:19; 48:4
   2) Kut. 32:13
   3) 1 Nya. 16:17
k. Sherehe za kimaagano
   1) Kut. 12:14,17,24
   2) Law. 23:14,21,41
   3) Hes. 10:8
l. Milele, ya kudumu
   1) 1 Fal. 8:13
   2) Zab. 61:7-8; 77:8; 90:2; 103:17; 145:13
   3) Isa. 26:4; 45:17
   4) Dan. 9:24
m. Nini kile Zaburi inakisema waaamini watakifanya milele
   1) kutoa shukurani, Zab. 30:12; 79:13
   2) kudumu katika uwepo Wake, Zab. 41:12; 61:4,7
   3) Imani katika Rehema Yake, Zab. 52:8
   4) kumsifu Bwana, Zab. 52:9
   5) kuimba sifa, Zab. 61:8; 89:1
   6) kuitangaza haki yake, Zab. 75:7-9
   7) kulitukuza jina lake, Zab. 86:12; 145:2
   8) Kubariki jina lake, Zab. 145:1
n. limetumika katika Isaya kuelezea enzi mpya
   1) agano la kudumu, Isa. 24:5; 55:3; 61:8

2) YHWH ni Mwamba wa kudumu, Isa. 26:4
3) furaha ya kudumu, Isa. 35:10; 51:11; 61:7
4) Mungu wa milele, Isa. 40:28
5) wokovu wa kudumu, Isa. 45:17
6) wema wa kudumu, Isa. 54:8
7) ishara ya kudumu, Isa. 55:13
8) jina la kudumu, Isa. 56:5; 63:12,16
9) nuru ya kudumu, Isa. 60:19,20

matumizi yaliyojikita kinyume yahusianayo na hukumu ya milele juu ya wale waovu yanapatikana katika Isa. 33:14, "moto wa milele." Isaya mara nyingi anatumia "moto" kuielezea ghadhabu ya Mungu (kama vile Isa. 9:18,19; 10:16; 47:14), lakini ni katika Isa. 33:14 tu ndiyo inaelezea kama "ya kudumu."

3. ni nyakati zilizopita na zijazo ("toka milele na milele")
   a. Zab. 41:13 (praise to God)
   b. Zab. 90:2 (Mungu mwenyewe)
   c. Zab. 103:17 (wema wa Bwana)

kumbuka, muktadha ndio unaamua dhima ya maana ya maneno. Maagano ya milele na ahadi ni ya kimashariti (yaani., Yeremia 7, angalia Mada Maalum: Agano). Kuwa mwangalifu juu ya usomaji wa maoni yako ya sasa au mpangilio wa thiolojia ya Agano Jipya katka kila utumiaji wa neno lisilo na maana. Kumbuka, sisi pia, agano jipya linajumuisha ahadi zote za Agao la Kale (angalia Mada Maalum: Unabii wa Agano la Kale ya mambo yajayo dhidi ya Unabii wa Agano Jipya).

**3:23 "Bwana Mungu akamtoa katika bustani ya Edeni"** Huu ni muundo KITENZI chenye nguvu (BDB 1081, KB 1511, *Piel* KAULI ISIYO TIMILIFU) wenye maana hasi. Katika Kumb. 21:14 muundo huu unarejelea kutarakisha, na katika I Fal. 9:7 muundo huu unarejelea hukumu juu ya taifa la Israeli.

**3:24 "akaweka Makerubi"** Hawa ni viumbe wa kimalaika wenye mabawa (BDB 500) ambao waliilinda bustani ya Mungu ili kumwondoa mwanadamu ndani ya bustani. Baadaye hawa walionekana ndani ya hema /hekalu iliyotengenezwa. Ile dhana kwamba Bustani inalindwa inaonyesha kwamba hii ilikuwa sehemu ya kipekee, mazingira yaliyolindwa, ambayo sasa yako nje ya mipaka ya mwanadamu. Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM : MAKERUBI

A. Moja ya aina ya viumbe vya kimalaikavilivyotajwa katika agano la kale (yaani., *Makerubi, Maserafi, Malaika wakuu, Malaika wa kupeleka habari*. Hii aina pekee ililinda maeneo yaliyokuwa yametengwa (kama vile Kut. 25:18-22; I Fal. 8:6-7).

B. Asili ya neno haijulikani:
   1. Kutokana na Akkadia "mwombezi" au "mpatanishi" kati ya Mungu na mwanadamu.
   2. Kutokana na Kiebrania bila shaka hili neno la kimzaha, "magari" na kerubi" (kama vile Eze. 1; 10)
   3. Wengine wanasema hili linamaanisha "mwonekano wa kuwa mwerevu"

C. Muundo wa kimwonekano – Jambo hili limekuwa gumu kulitambua kwa sababu ya maelezo yenye kubadilika yaliyo ndani ya Biblia na tofauti ya muindo ya mnyama - mwanadamu anayepatikana katika Mashariki ya Karibu ya kale. Wengine wanawahusisha hawa na:
   1. Fahari mwenye mabawa wa huko Mesopotamia
   2. Simba Misri wenye mabawa kama tai waitwao " wanyama mabawa"
   3. Viumbe wa Hiram wenye mabawa, kiti cha Mfalme wa Tiro
   4. Sanamu la Misri na muundo wenye kufanana unaopatikana katika kinyago cha ngome ya Mfalme Ahabu huko Samaria

D. Uainishaji wa Kimwonekano
   1. Mfumo wa Mkerubi unahusianishwa na Maserafi wa Isaya 6.
   2. Mifano ya miundo tofauti tofauti
      a. Idadi ya nyuso
         (1) mbili - Eze. 41:18
         (2) nne -Eze. 1:6, 10; 10:14,16,21,22
         (3) mmoja - Ufu. 4:7
      b. Idadi ya mbawa
         (1) mbili - I Fal. 6:24
         (2) nne -Eze. 1:6,11; 2:23; 10:7,8-21
         (3) sita (kama Serafi wa Isa. 6:2) - Ufu. 4:8
   3. Sifa zingine (pia huitwa"viumbe vinavyoishi")
      a. Mikono ya mwanadamu - Eze. 1:8; 10:8,21
      b. Miguu
         (1) Aliyenyooka, asiye na goti - Eze. 1:7
         (2) Miguu kama ya ndama - Eze. 1:7
   4. Flavius Josephus anakiri kwamba hakuna aliyefahamu namna kerubi alivyofanana (kama vile *Antiquities of the Jews,* VIII:3:3).

E. Mahali na makusudi yanayopatika ndani ya Biblia
   1. Mlinzi wa mti wa uzima,Mwa. 3:24 (bila shaka huyu alitumika kistiari kumaanisha Shetani katika Eze.28:14,16)
   2. Mlinzi wa Hema
      a. Juu ya Sanduku la Agano; Kut. 25:18-20; Hes. 7:89; I Sam. 4:4
      b. Aliyetabiri nguo na pazia; Kut. 26:1,31; 36:8,35
   3. Mlinzi wa Hekalu la Suleimani
      a. Kerubi wawili wafunikao katika Patakatifu wa Watakatifu; I Fal. 6:23-28; 8:6-7; II Nya. 3:10-14; 5:7-9
      b. Juu ya kuta za nyumba zilizonakshiwa; I Fal. 6:29,35; II Nya. 3:7-69
      c. Juu ya papi zilizokuwa katikati ya birika; I Fal. 7:27-39
   4. Mlinzi wa Hekalu la Ezekiel-aliye nakishiwa juu ya kuta na milango Ezek. 41:18-20, 25
      a. Aliyechongwa juu ya kuta na milango; Eze. 41:18-20, 25
   5. Anahusianishwa na kuubeba Uungu
      a. huenda hii ni sitiari ya upepo; II Sam.22:11; Zab. 18:10; 104:3-4; Isa. 19:1
      b. mlinzi wa kiti cha enzi cha Mungu; Zab.80:1; 99:1; Isa. 37:16.
      c. mlinzi wa gari lenye kiti cha Mungu kinachohamishika; Eze. 1:4-28; 10:3-22; I Nya. 28:18
   6. Hekalu la Herode-Aliyechorwa katika kuta (yaani, mlinzi kama vile buku la Sheria za Kiyahudi "Yoma" 54a)
   7. Mandhari ya kiti cha enzi cha Ufunuo (yaani, mlinzi wa Ufu. 4-4)

## MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Je! Hili ni ni fumbo, hadithi ya kubuni, au masimulizi ya kihistoria?
2. Je! Kiuhalisia nyoka alizungumza?

3. Nyoka alitiwa nguvu na kumilikiwa na yule mwovu? Ikiwa ni hivyo, ni kwa namna gani nan i kwa nini?
4. Je! Mungu alilitambua lile ambalo Adamu na Hawa wangefanya? Ikiwa ni hivyo, kwa nini Aliliruhusu hili?
5. Toa ufafanuzi katika maneno yako juu ya kiwango cha kukua kwa jaribu la nyoka na mashataka binafsi dhidi ya Mungu.
6. Ni kwa namna gani Mungu, kama kiumbe cha kiroho, anao mwili?
7. Je! Sura ya 3 inaeleza uwepo wa uovu katika ulimwengu wetu na uwepo wa hatia ndani ya moyo wa mwanadamu? Ikiwa ni hivyo, kwa nini sura hii haijadiliwi zaidi na kwa ukamilifu katika Agano la Kale?
8. Je! Nyoka anatumika kama mtumishi wa Mungu ili kumjaribu mwanadamu au tayari amekwisha kuwa chapa ya uasi dhidi ya Mungu (kama vile Yakobo 1-2 na Zek. 3)?
9. Kwa nini Mungu alimhukumu mnyama ambaye kwa upekee alitumiwa na Shetani?
10. Mstari wa 15 ni dokezo la ujio wa Masihi ama woga tu kati ya wanawake na nyoka?
11. Ni dhahiri kwamba jamii yetu ya sasa inasistiza usawa kati ya wanaume na wanawake inakanusha mstari 16 kama kanuni ya kiulimwengu. Kwa nini unaamini kwamba mstari huu ndivyo ulivyo?
12. Mstari wa 20 ni tendo la toba na imani juu ya sehemu ya Adamu au dai la matakwa ambayo yeye na Hawa wanaweza kwa wao wenyewe?
13. Ealeza matumizi ya WINGI ambayo yanatumika kumuhusu Mungu katika mstari wa 22. Je! Hili linamaanisha mafundisho ya Utatu au kitu kingine? Kwa nini au kwa nini si hivyo?

# MWANZO 4:1-26

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Kaini na Abeli | Kaini anamuua Abeli | Kaini, Abeli na Sethi | Kaini na Abeli | Kaini na Abeli |
| 4:1-8 | 4:1-8 | 4:1-7 | 4:1-7 | 4:1-8 |
| | | 4:8-16 | 4:8 | |
| 4:9-15 | 4:9-15 | | 4:9a | 4:9-16 |
| | | | 4:9b | |
| | | | 4:10-12 | |
| | | | 4:13-14 | |
| 4:15-16 | | | | |
| | Familia ya Kaini | | | |
| 4:16 | 4:16-18 | | Vizazi vya Kaini | |
| 4:17-22 | | 4:17-22 | 4:17-22 | 4:17-22 |
| | 4:19-24 | | | |
| 4:23-24 | | 4:23-24 | 4:23-24 | 4:23-24 |
| (23-24) | (23-24) | (23-24) | (23-24) | (23-24) |
| | Mwana | | Sethi na Henoko | Sethi na Uzao Wake |
| 5:25-26 | 4:25-26 | 4:25-26 | 4:25-26 | 4:25-26 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (<u>angalia ukurasa wa vii)</u>

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

9. Aya ya kwanza
10. Aya ya pili
11. Aya tatu
12. N.k

## UTANGULIZI

A. Imekuwa ikielezwa na watoa maoni wengi kwamba 4:1-24 inaainisha mwendelezo wa uasi wa uzao wa Kaini, ambapo 4:25-5:32 inaainisha mwendelezo wa uzao wa ki-Ungu wa Seti. Ingawa hili linasaidia katika kuziangalia sura hizi kwa ujumla linafuta uovu wote wa watu wanaonekana katika 6:5-6, 11-12,13.

B. Wengi wamedai kwamba sura ya 4 si ufafanuzi kamili wa uzao wa magharibi bali uzao wa mashariki wa Kiebrania ambao unadokeza hoja kuu. Ukijumlisha vile vya Mwanzo 4 vinaonekana kupishana na vinakamilisha kipindi cha miaka ipatayo 2,000. Hivyo, Naamini kwamba hii ni sampuli wakilishi au namba za kiishara (kama vile vya Yesu katika Mathayo na Luka), si vizazi kamili.

C. Sura ya 5 imeanishwa kama sura ya kifo, bali mistari ya 21-24 inaendelea kuonyesha tumaini la ukombozi wa mwanadamu katika tafsiri ya Enoshi. Maneno haya haya yanatumika kwa Eliya katika IIFal. 2:3,5,9,10.

D. Mwanzo 3:8-11:9 inafunua matokeo ya dhambi yenye kutisha ambayo yanaendelea kutoka kizazi hadi kizazi.

E. Vizazi vya Kaini havikuchukuliwa katika kumbukumbu kama vizazi vya Sethi (yaani si nyakati au zama zilizotolewa). Mfululizo wa vizazi vya Kaini ulifia katika mafuriko moja kwa moja. Huenda ni kwa sababu ya wale aliowaoa. Viumbe wote wenye miguu miwili, utengenezaji wa zana, viumbe vyenye fuvu la kichwa kubwa hawakuwa katika mfano wa Mungu.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 4:1-8**

**[1] Adamu akamjua Hawa mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Kaini, akasema, Nimepata mtoto mwanamume kwa Bwana. [2] Akaongeza akamzaa ndugu yake, Habili. Habili alikuwa mchunga kondoo, na Kaini alikuwa mkulima ardhi. [3] Ikawa hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana. [4] Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake na sehemu zilizonona za wanyama. Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake; [5] bali Kaini hakumtakabali, wala sadaka yake. Kaini akaghadhibika sana, uso wake ukakunjamana. [6] Bwana akamwambia Kaini, Kwa nini una ghadhabu? Na kwa nini uso wako umekunjamana? [7] Kama ukitenda vyema, hutapata kibali? Usipotenda vyema dhambi iko, inakuotea mlangoni, nayo inakutamani wewe, walakini yapasa uishinde. [8] Kaini akamwambia Habili nduguye, [Twende uwandani]Ikawa walipokuwapo uwandani,Kaini akamwinukia Habili nduguye,akamwua.**

**4:1 "Adamu akamjua Hawa mkewe"** Kiuhalisia, "Adamu alimjua mkewe Hawa." Neno la Kiebrania "kujua" linazungumzia juu ya uhusiano wa karibu sana (BDB 393, KB 390, *Qal* KAULI TIMILIFU, kama vile Yer. 1:5). Haijulikani kama huu ulikuwa muungano wa kwanza wa kujamiina kati ya Adamu na Hawa kwani haijaelezwa. Biblia imenyamaza kuhusu idadi ya watoto waliokuwa nao na lini walikuwa nao. Tunawafahamu wale watatu tu waliotajwa kwa majina. Jambo hili ni la muhimu katika kutafsri maneno ya Agano Jipya la "kujua" ambalo Mungu alilionyesha kwamba si dhana ya starehe tu, bali uhusiano binafsi unaosisitizwa. Kimsingi mwitikio wa mwanadamu kwa Mungu unahusisha (1) kweli inayotakiwa kuaminiwa, (2) mtu wa kukaribisha, na (3) kuishi maisha sahihi! Tazama Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM : AKAMJUA (kama ilivyoelezewa toka Kumbukumbu la Torati)

Neno la Kiebrania "kujua"(BDB 393) lina maana kadhaa (mazingira ya kimaana) katika shina la neno *Qal*.

1. Kuelewa mema na mabaya - Mwa. 3:22; Kumb. 1:39; Isa. 7:14-15; Yohana 4:11
2. Kujua kwa kuelewa - Kumb. 9:2,3,6; 18:21
3. Kujua kupitia mazoea - Kumb. 3:19; 4:35; 8:2,3,5; 11:2; 20:20; 31:13; Yos. 23:14
4. kufikiri - Kumb. 4:39; 11:2; 29:16
5. kujua kibinafsi

a. mtu - Mwa. 29:5; Kut. 1:8; Kumb. 22:2; 33:9, Yer. 1:5
b. mungu -Kumb. 11:28; 13:2,6,13; 28:64; 29:26; 32:17
c. YHWH - Kumb. 4:35,39; 7:9; 29:6; Isa. 1:3; 56:10-11
d. kizinaa - Mwa. 4:1,17,25; 24:16; 38:26
6. ujuzi wa kujifunza - Isa. 29:11,12; Amosi 5:16
7. kuwa mwenye hekima - Kumb. 29:4; Mit. 1:2; 4:1; Isa. 29:24
8. maarifa ya Mungu
a. kwa Musa - Kumb. 34:10
b. kwa Israeli- Kumb. 31:21

kithiolojia #5 ni wa muhimu. Imani ya kibiblia ni ushirika wa ndani, wa kila siku, unaokua pamoja na Mungu(angalia Mada Maalum: *Koinōnia*). Sio sheria pekee au maisha ya kiadilifu pekee. Ni imani binafsi ya kiushirika. Hii ndio sababu Paulo alitumia nyumba ya mshirika katika Efe.5:22-6:9 kuelezea upendo wa Kristo kwa ajili ya kanisa.

◙**"Kaini"** Hili jina "Kaini" (*qayin*, BDB 884 III, KB 1097, na BDB 888-89) ni mzaha wa neno la Kiebrania "kupata zawadi" (*qaniti*). Inaonekana kukubarika kwamba Kaini alikuwa zawadi ya kipekee kwa msaada wa YHWH (huenda ni utimilifu wa 3:15).

◙ **"kwa Bwana "** Hii tafsiri, "mtoto mwanaume," inaonekana kushikilia msistizo huu. Wengine wanadai kwamba hapo awali Hawa alikuwa na mabinti na ya kwamba huyu alikuwa kijana wake wa kwanza, lakini hili ni dhanio tu. Kifungu kinachohitimisha cha mstari wa 1, "kwa Bwana," (BDB 86) kinamanisha kwamba huu ulikuwa usemi wa Hawa wa imani uliojikita katika Mwa. 3:15. Haya ni matumizi ya kwanza ya jina YHWH kwa namna yake. Muda uliofuatia jina hili linaonekana kutumiwa na uzao wa Sethi katika 4:26.

**4:2 "Akaongeza akamzaa ndugu yake, Habili"** Walimu wa sheria wanasema kwamba kwa sababu kifungu "Adamu akamjua Hawa" hakipo katika mst. 2 ambacho kinazungunza kwamba Kaini na Habili walikuwa mapacha, lakini hili linaonekana kutopendeka kabisa.

◙ **"Habili" Neno la Kiebrania linamaanisha** "pumzi," "mvuke," au "majisifu" (BDB 211 II, kama vile Mhu. 1:2). Kuna maana tatu za jina hili: (1) hili linaweza kuakisi (a) Kukata tamaa juu ya hali ya anguko la Hawa au (b) utabiri juu ya ufupi wa maisha yake; (2) ni neno lenye uhusiano na neno la lugha Akkadia "mwana" (*ibil*); na (3) wengine wamedai kwamba jina hili lilihusiana na neno "udhaifu" kwa sababu ya kukata tamaa kwa Hawa juu ya laana la kuwa na watoto wengi (kama vile Mwa. 3:16).

**4:3 "hatimaye Kaini akaleta mazao ya ardhi, sadaka kwa Bwana"** Elewa kwamba Kaini alikuwa wa kwanza kuleta sadaka kwa Bwana (BDB 97, KB 112, *Hiphil* KAULI ISIO TIMILIFU). Hakuna kilicho cha kiurithi katika sadaka ya nafaka dhidi ya sadaka ya mnyama. Umuhimu upo katika imani ya mtoaji, si katika sadaka yenyewe. Huenda waliileta sadaka katika njia ya lango la bustani ya Edeni.

**4:4 "Habili naye akaleta wazao wa kwanza wa wanyama wake"** Kiini kinaonekana kuwa katika neno "wazao" (BDB 114). Kaini alileta sehemu ya mazao yake, lakini Abeli alileta sehemu za wanyama wake walionona, jambo ambalo lilionyesha mtazamo wa imani na heshima. Lakini lazima ikumbukwe kwamba andiko lenyewe ni la kiutata sana na ni fupi sana. Yatupasa kujihadhari katika kusoma maandiko mengi katika maelezo haya ya awali.

◙
**NASB "na sehemu zilizonona"**
**NKJV "na unene wao"**
**NRSV "na sehemu zao zilizo kubwa"**
**TEV "sehemu yake iliyo bora"**
**NJB "na baadhi ya sehemu zao zilizo nene"**
**SEPT "na hata baadhi ya sehemu zao zilizo nene sana"**
**JPSOA "zilizochaguliwa kuwa bora zaidi"**
**NET "hata sehemu zao nene sana"**

Kwa uwazi kabisa hapa na katika dini ya Kiyahudi iliyofuatia, vitu vya nafsi na sehemu nene zilizohusiana na hivyo ndivyo vilivyokuwa vikitolewa sadaka madhabahuni: (1) hivi vilikuwa vikionekana kama vitu vya kugusa moyo (2) unono ni ishara ya utajiri na afya. Toleo la Biblia ya SEPT, JPSOA, na NET inakitambua kifungu hiki kama kifungu kisichorejelea juu ya mazao yaliyotolewa sadaka madhabahuni, bali kama mnyama bora. Hili linaendana na mazingira kwa usahihi.

◙ **"Bwana akamtakabali Habili na sadaka yake"** Kiuhalisia hili linamaanisha "kutazamwa" kwa maana nyingine iliyo njema (BDB 1043, KB 1609, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU, kama vile TEV na NJB). Ni kwa namna gani, hii haijulikani japo kumekuwa na madhahanio mengi. Ni sahihi kwamba Mungu aliionyesha furaha yake mtu na chukizo lake kwa wengine. Imeelezwa na watoa maoni, wa nyakati zote za kale na za sasa, kwamba Mungu alimtakabali Habili na sadaka yake kwanza. Ndivyo ulivyo utaratibu (kama vile Ebr. 11:4). Tatizo la Kaini lilikuwa ni mtazamo wake. Inawezekana kwamba Mungu huonyesha utukufu wake kwa kupenda vitu vipya si vikuu kuu. Jambo hili linaonekana katika kitabu cha Mwanzo kizima.

**4:5 "Kaini akaghadhibika sana**" Haya maneno ya Kiebrania yana nguvu sana ambapo maneno haya yanaeleza hisia za Kaini (BDB 354, KB 351, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU ikiongezea KIELEZI "sana," BDB 547). Elewa kwamba huyu alimgadhabikia Mungu lakini akaibeba ghadhabu yake hadi kwa nduguye. Hapa muktadha ni ghadhabu katikati ya ibada. Huenda alifadhaika kwa sababu ya mazao ya ndugu yake kukubalika machoni pa Mungu, alimtakabali Abeli, naye hakumtakabali.

◙ **"uso wake ukakunjamana"** Kuna neno la kimzaha kati ya "kuanguka" kama mistari ya 5 na 6 (BDB 656, KB 709) na "hutapata kibali" katika mst. wa 7. Hili Neno "kutakabali" linaweza kumaanisha "kukubalika" (BDB 669, KB 724, *Qal* TUNGO ISIYO NA KIKOMO, kama vile NKJV, NRSV, TEV).

**4:6 "Kwa nini una ghadhabu"** Hapa tena Mungu anauliza maswali kadhaa, si kwa ajili ya kupata taarifa, bali ni kwa ajili ya kumsaidia mtu kuzielewa hisia zake mwenyewe na nia yake (kama vile mst. 9 na 3:9,11,13).

**4:7 "dhambi iko, inakuotea mlangoni**" Katika mstari huu dhambi inaelezwa kama mnyama wa kondeni ambaye nia yake ni kuharibu (kama vile I Pet. 5:8). Yawezekana kuna uhusiano wa ki-Akkadia na neno "kukunjamana" ambalo lilitumika kumaanisha mwenye mapepo (BDB 918, KB 1181, *Qal* KAULI ENDELEVU. Hili linaonyesha asili ya kweli ya dhambi katika ulimwengu wetu.

◙ **"nayo inakutamani wewe"** Neno hili hili "kutamani" (BDB 1003, KB 1802) linatumika katika Mwa. 3:16. Hili linaonyesha kwamba kusudi la dhambi ni kutuletea uharibifu kwetu (yaani, "kutawala" na "kumiliki").

◙ **"walakini yapasa uishinde"** Hiki KITENZI (BDB 605, KB 647) ni *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU. Hili linaonyesha kwamba hatukuwa kibaraka mikononi mwa yule mwovu, bali tulikuwa na uwezo, kwa msaada wa Mungu, kumpinga mwovu (kama vile Efe 74 6:13; Yakobo. 4:7; I Pet. 5:9), kutubu na kurejeshwa! Kaini hakuunganishwa na dhambi ya Adamu (kama vile Eze. 18:2-4). Tunaathiriwa na uasi wa Adamu na Hawa, lakini tunawajibika kwa chaguzi zetu.

**4:8 "Kaini akamwambia Habili nduguye"** Kumekuwa na Mjadala mwingi kuhusu kifungu hiki. Wengine wanaeleza kwamba Kaini alimwambia Abeli kuhusu kile ambacho Mungu amekisema katika mistari ya 6 na 7. Wengine wanadai kwamba, pamoja na tafsiri za vitabu vitano vya Musa vya Kisamaria, Agano la Kale la Kiebrania, Siriaki, Toleo la Kilatini, na RSV , aliongozana naye hadi uwandani ili aweze kumuua (yaani, maauaji ya kukusudia).

◙ **"Kaini akamwinukia Habili"** Sura ya 3 ilisisitiza juu ya jaribu la nguvu ya asili; sura ya 4 ailisisitiza juu ya asili ya anguko la ki-Adamu ndani ya mwanadamu. Hapa hakuna mjaribu, ni dhambi kamili na ya pekee iliyochanua yenye matokeo yatokanayo na dhambi ya Adamu na Hawa na ambayo ilienea kwa vizazi vyote (kama vile Rum. 8:9-18,23; I Yohana 3:12). Hivi VITENZI "kumwinukia" (BDB 877, KB 1086, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU) na "kuua" (BDB 246, KB 255, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU) inaonyesha hasira endelevu.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 4:9-15**

**[9] Bwana akamwambia Kaini, Yuko wapi Habili ndugu yako? Akasema, Sijui, mimi ni mlinzi wa ndugu yangu? 1[0] Akasema, Umefanya nini? Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi. [11] Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi, iliyofumbua kinywa chake ipokee damu ya ndugu yako kwa mkono wako; [12] utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake; utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani. [13] Kaini akamwambia Bwana, Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki. [14] Tazama, umenifukuza leo katika uso wa ardhi, nitasitirika mbali na uso wako, nami nitakuwa mtoro na mtu asiye na kikao duniani; hata itakuwa kila anionaye ataniua. [15] Bwana akamwambia, Kwa sababu hiyo ye yote atakayemwua Kaini atalipizwa kisasi mara saba. Bwana akamtia Kaini alama, mtu amwonaye asije akampiga.**

**4:9 "mimi ni mlinzi wa ndugu yangu?"** Tatizo kubwa la Kaini lilikuwa ule moyo wa kutotubu. Hili neno "mlinzi" linaweza kumaanisha "mchungaji" (BDB 1036, KB 1581, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU), ambapo hili mzaha wa umiliki wa Abeli (kama vile mst. 2).

**4:10 "Sauti ya damu ya ndugu yako inanililia kutoka katika ardhi" Hiki kifungu ni cha muhimu sana** ("kulia" BDB 858, KB 1042, *Qal* KAULI TENDAJI ENDELEVU). Kwa Waebrania, uweza wa maisha ulikuwa katika damu (kama vile Law. 17:11; Ufu. 6:9,10). Hili neno "damu" ni WINGI katika Kiebrania. Rashi anasema kwamba WINGI huu unamrejelea Abeli na uzao wake muhimu. Huu WINGI pia unaonyesha mkazo.

**4:11"Basi sasa, umelaaniwa wewe katika ardhi"** Hii ni laana ya kwanza ya moja kwa moja juu ya mwanadamu. Kwa dhambi ya Adamu ardhi ililaaniwa. Ni muhimu kwamba Kaini, kuwa mkulima, hakuweza kuitumia tena kama umiliki wake. Anatupwa nyikani ambapo ni maskani ya mapepo na pamoja na hiyo, sehemu isiyo na shughuli za kilimo.

**4:12 "utakapoilima ardhi haitakupa mazao yake"** Huu ni muundo *Hiphil* muundo wa KAULI AMRISHI (BDB 414, KB 418). Watoa maoni mengi wanaeleza kwamba ndiyo maana mtiriko wa Kaini kuishi mjini dhidi ya maisha ya kijijini (kama vile mst. 16-24).

◙ **"utakuwa mtoro na mtu asiye na kikao "** Haya maneno mawili yenye kushabihiana (BDB 631, KB 681 na BDB 626, KB 678, kama vile mst. 14) yanaeleza juu ya maisha ya Kaini ya ufugaji. Haya ni maneno ya kimzaha yanayozungumza kuhusu nchi ya Nodi (BDB 627 II). Hii mizaha inaonysha uhalisia wa uainishaji wa sura hizi za kale.

**4:13 "Adhabu yangu imenikulia kubwa, haichukuliki!"** Kaini hakulijutia kosa lake bali anajutia matokeo yeke.

**4:14 "umenifukuza leo katika uso wa ardhi"** Haya ni matokeo ya Kaini kumilikiwa na dhambi ambapo kifungu kinachofuatia "nitasitirika mbali na uso wako" ni matokeo ya kiroho (kama vile 3:8) ya dhambi Kaini.

◙ **"hata itakuwa kila anionaye ataniua"** Kaini akihofia juu ya maisha yake mwenyewe. Walimu wa Kiyahudi wanasema kwamba huyu alihofia juu ya wanyama. Hata hivyo, muktadha huu unaonekana kumaanisha jamaa zake mwenyewe, ambao wangekuwa "*go'els*" (mlipa kisasi cha damu) kwa Abeli, ambao wangemuua. Hili lingeweza kumaanisha kwamba Adamu na Hawa walikuwa na watoto wengi wasiokuwa na majina.

Hapa kuna mjadala unaovutia wa uhusiano wa Adamu na Hawa kwa wanadamu wa historia ya awali katika mjadala wa Kidner's *The Tyndale Commentary on Genesis* na Bernard Ramm ulikuwa ni mjadala wa elimu juu ya mwanadamu ya *The Christian's View of Science and Scripture*. Mstari huu unazungumzia viumbe vingine vya kimantiki. Kwa mjadala juu ya mwanadamu wa kale na tarehe zao za mahali walipoishi Mashariki ya Karibu ya kale angalia R. K. Harrison's *Introduction to the Old Testament*, kurasa 147-163 na *Who was Adam?* cha Fazale Rana na Hugh Ross.

Ikiwa Kaini alioa kiumbe kisichofanana naye kisichokuwa na Roho wa Mungu, hiyo Mwanzo 6:1-4 itakuwa inachanganya viumbe maalumu wa Mungu na wanyama watembea kwa miguu miwili badala ya wanadamu pamoja na malaika.

**4:15 "atalipizwa kisasi mara saba"** Neno "mara saba" linaonekana kumaanisha kisasi kikamilifu (BDB 988). Inavyoonekana Mungu alimuacha Kaini hai kama ishara kali ya dhambi yenye kutia uchungu. Walimu wanasema kwamba Mungu atajitwalia kisasa kwa vizazi saba ambaye angekuwa ni Lameki. Kuna hadithi ya kufikirika ya kialimu kwamba mstari wa 23 unamrejerea Lameki na mwanawe wa kiume, Tubali-Kaini, aliyemuua kaini kwa bahati mbaya.

◙ **"akamwekea alama Kaini"** Hii yawezekana ni ishara (BDB 16, "alama") ya (1) rehema za Mungu katikati ya hukumu (2) Utoshelevu wa Mungu katika Hukumu yake kwa muda. Walimu wanasema kwamba Mungu aliweka pembe ya mnyama katikati ya kichwa cha Kaini. Hatahivyo, inavyoonekana zaidi itakuwa kwamba ilikuwa alama katika paji lake la uso (kama vile Ezek. 9:4,6).

| |
|---|
| **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:16** |
| [6] **Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana, akakaa katika nchi ya Nodi, mbele ya Edeni.** |

4:16 "**Kaini akatoka mbele za uso wa Bwana**" Hii inaonekana kuwa matokeo ya kimwili yanayochapisha matokeo ya kiroho ("kwenda nje" BDB 422, KB 425, Qal KAULI ISIYO TIMILIFU). Mistari ya 16-24 kihalisi inaonesha mwanadamu aliyepigwa marufuku akianza mfumo wa kiulimwengu mbali na Mungu. Huu mfumo wa kiiulimwengu umpingao YHWH unaweza kuonekana katika ufalme wa maono ya Danieli. Inafanyika kuchapishwa kwa kahaba mkuu wa Babeli katika kitabu cha Ufunuo na katika matumizi ya Yohana ya neno "ulimwengu."

◙"**nchi ya Nodi**" "Nodi" ni neno la Kiebrania kwa "kutanga tanga" au "nchi ya watangaji/watoro" (BDB 627 II). Huu ni mzawa wa dhahiri juu ya jina la Kaini. Hatujui wapi sehemu hii ipo lakini kiuwazi zaidi mashariki ya Edeni kuliko Adamu na Hawa walipoenda.

| |
|---|
| **ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:17-22** |
| [17] **Kaini akamjua mkewe; naye akapata mimba, akamzaa Henoko; akajenga mji akauita Henoko, kwa jina la mwanawe.** [18] **Henoko akamzaa Iradi, Iradi akamzaa Mehuyaeli; Mehuyaeli akamzaa Methushaeli; Methushaeli akamzaa Lameki.** [19] **Lameki akajitwalia wake wawili, jina la wa kwanza ni Ada, na jina la wa pili ni Sila.** [20] **Ada akamzaa Yabali; huyo ndiye baba yao wakaao katika hema na kufuga wanyama.** [21] **Na jina la nduguye aliitwa Yubali; huyo ndiye baba yao wapigao kinubi na filimbi.** [22] **Sila naye akamzaa Tubal-kaini, mfua kila chombo cha kukatia, cha shaba na cha chuma; na umbu lake Tubal-kaini alikuwa Naama.** |

**4:17"Kaini akamjua mkewe"** Alimuoa nani? Wanataaluma wenye msimamo wanadhania kwamba alioa dada yake lakini haikuwahi kutajwa katika Biblia. Mwanzo 5:4 inasema kwamba Adamu na Hawa walikuwa na watoto wengine wa kike na wa kiume**.** Mtu anaweza kushangaa kuhusu watu waliokuwa nje ya bustani ya Edeni ambao Kaini alikuwa akiwaogopa katika 4:14 (angalia dokezo katika 4:14).

◙ **"naye akapata mimba"** Asili zote za majina haya ni za mashaka. Jina Enoshi lina maanisha "mwanzilishi" au "anayeanzisha" (BDB 335). Kuna mfanano wa wazi kati ya orodha ya watoto wa Kaini na orodha ya watoto wa Sethi katika Sura ya 5 (mfano Enoshi na Lameki). Sababu halisi kwa ajili ya mafanano huu wa kiasili haujulikani, lakini inaonesha (1) kwamba familia mbili hizi zilikuwa na mwingiliano mwingi wa kijamii, au (2) utofauti wa kiroho wa hawa Enoshi wawili.

Pia chunguza uone kwamba umri wa maisha ya Kaini na uzao wake hautolewi. Hii inaweza kumaanisha kwamba vizazi vilivyopanuliwa vya uzao wa Sethi ni vya kiishara vinavyotambulikana au kutukuza (kama ilivyo na orodha ya Wafalme wa ki-Sumeri waliopanua maisha kabla na baada ya mafuriko, umri wa maisha kupungua baada ya mafuriko lakini bado ni muda mrefu kwa viwango vya leo).

◙**"akajenga mji"** Hii inaonekana kuwa kutofautiana moja kwa moja na amri kwamba angekuwa mtoro (kama vile mistari ya 12,14). Wengine wameona hii kama mfano wa hofu ya Kaini kwamba mtu fulani angemuua yeye; hivyo, alijenga ngome kujilinda mwenyewe na familia yake (sawasawa na kusudi la Mnara wa Babeli).

**4:18 "Henoko akamzaa Iradi"** Asili zinazowezekana za neno hili ni: (1) mapambo ya mji; (2) mtu wa mji; au (3) miguu ya mpiganaji (BDB 747).

◙ **"akamzaa Mehuyaeli"** Asili ya neno hili inayowezekana ya neno hili ni (1) "Mungu ni mpaji wa uhai"; (2) "Mungu ni mpaji wa chemichemi ya uzima"; (3) "aliyepondwa pondwa na Mungu"; au (4) "aliyetengenezwa na Mungu" (BDB 562).

◙ **"Methushaeli"** Asili za neno hili zinazowezekana za neno hili ni (1) "Mtu wa Mungu"; (2) "kijana mwenye nguvu"; au (3) "mfalme" (BDB 607).

**4:19 "Lameki akajitwalia wake wawili,"** Haya ni masimulizi ya kwanza ya ndoa za mitaala na kuanza kwa anguko la uzao wa Kaini. Jina la Lameki halijulikani asili yake (BDB 541).

◙ **"Ada. . .Sila"** Haya majina mawili ya wanawake ni utani kwa uzuri wao wa kimwili. Walimu wanasema kwamba mmoja alikuwa mke wake kwa ajili ya kuzaa watoto na mmoja alikuwa mwanamke wake kwa ajili ya starehe. Jina "Ada" linaweza kumaanisha"mapambo" au "asubuhi" (BDB 725) ,wakati jina "Sila" inaonekana kumaanisha "kivuli" au"malazi," "kuwaka waka" au "mcheza mziki" (BDB 853).

**4:20 "Jabali; huyo ndiye baba yao wakaao katika hema na kufuga wanyama"** Neno hili linaonekana kumaanisha "mtangatangaji/mtoro" (BDB 385 II), ambalo linaelezea maisha ya kichungaji ya kuhamahama ambalo kidhahiri alilikuza.

**4:21 "Yubali,……wa wapigao kinubi na filimbi"** Baadhi wanaelezea kwamba jina lake linamaanisha "sauti." Huu ndio mwanzo wa karama fulani za muziki. Muziki umeunganishwa na yule muovu katika Ezekiel 77 18:13. Kama ilivyo kwa karama zote za Mungu, zinaweza kupotoshwa. Hiki kikundi cha kikabila sio tu kwamba kilikuza vyombo vya nyuzi lakini pia vyombo vya upepo.

**4:22 "Tubali-kaini, mfua kila chombo cha kukatia, cha shaba na cha chuma"** Mtu huyu (BDB 1063) alikuwa wa kwanza kutengeneza silaha ya vita. Inawezekana kwamba watu watatu wanaotajwa katika mistari ya 21-22 wanaitwa kulingana na kazi zao.

◙ **"Naama"** Jina hili linamaanisha "ya kupendeza" au "nzuri" (BDB 653 I). Walimu wanasema kwamba aliolewa na Nuhu lakini hii ni kama haina uwezekano kabisa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4: 23-24**

**[23] Lameki akawaambia wake zake, Sikieni sauti yangu, Ada na Sila; Enyi wake za Lameki, sikilizeni usemi wangu; Maana nimemwua mtu kwa kunitia jeraha; Kijana kwa kunichubua; [24] Kama Kaini akilipiwa kisasi mara saba, Hakika Lameki atalipiwa mara sabini na saba.**

*4:23 "***Lameki akawaambia wake zake**" Haya ni matumizi ya kwanza ya kutumia ushairi unaowekwa kumbukumbu katika Biblia (karibu asilimia 40% ya Agano la Kale liko katika muundo wa ushairi). Imeunganika kisarufi na mstari wa 22. Hadithi za kale za walimu wa dini ya Kiyahudi zinasema kwamba wake zake wawili walimuacha yeye kwasababu alikuwa amemuua Kaini kwa bahati mbaya na pia mwanawe wa kiume, Tubali-kaini, wakati alipokuwa akiwinda. Hii inaonesha kutoaminika kabisa. Kile kinachosisitizwa ni kuendelea kwa dhambi kwa kiwango cha Lameki alikuwa anajisifia kiburi cha kisasi chake. Baadhi wameelezea kwamba alimshikia huyu Tubal-Kaini silaha ya kwanza ya vita na kufanya hii kuwa sifa zake za majivuno. Kumekuwa na mjadala mkubwa kati ya wafasiri juu ya kipengele cha muda (uliopita, ujao). Wengi wanadhania kwamba yanarejerea kitu fulani kitatokea, sio kwa kitu kilichotokea.

*4:24* "**mara sabini na saba**" Hii inaonesha hali mbaya ya kisasi cha Lameki (kama vile 4:15). Baadhi ya wafasiri wanaona ulinganifu kati ya hili na maneno ya Yesu kuhusu msamaha katika Mt. 18:21,22.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 4:25-26**

**[25] Adamu akamjua mke wake tena; akazaa mwana mwanamume, akamwita jina lake Sethi; maana alisema, Mungu ameniwekea uzao mwingine mahali pa Habili; kwa sababu Kaini alimwua. [26] Sethi naye akazaa mwana; akamwita jina lake Enoshi. Hapo ndipo watu walipoanza kuliitia Jina la Bwana.**

*4:25-26* Muktadha huu unatakiwa uendane na sura ya 5. Sura na mgawanyo wa mistari haikuwa sehemu ya asili ya andiko ya aidha Agano la Kale la Kiebrania au Agano Jipya la Kiyunani.

*4:25* Huu ni mzaha mwingine kati ya neno la Kiebrania "kuwekwa wakfu" (*shat*, BDB 1011, KB 1483, *Qal* KAULI TIMILIFU) na Sethi (*shet*, BDB 1011 I). Huku kuendeleza (sauti) utani huu wa majina katika Mwanzo 1-11 unaonesha tabia yake ya kifasihi.

*4:26* "**akamwita jina lake Enoshi**" Hili ni moja ya neno la Kiebrania kwa "mtu" (BDB 60), kisawe cha Adamu (kama vile Ayubu 25:6; Zab. 8:4; 96:3; 144:3; Isa. 51:12; 56:2).

◙ **"Hapo ndipo watu walipoanza kuliitia Jina la Bwana"** Hii inaonekana kumaanisha ibada ya umma iliyozoeleka kwasababu ya matumizi ya jina la kiagano la kiungu la YHWH. Wengi wameona utofautiano kati ya mstari huu na Kut. 6:3. Yawezekana watu walikuwa wametumia jina hili la YHWH bila kujua umuhimu wake kamili mpaka kipindi cha Musa. Huu ndio mwanzo wa uzao wa Ki-Masihi (kama vile Luka 3:38).

# MWANZO 5

| MIGAWANYO YA AYA ZA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Uzao wa Adamu | Familia ya Adamu | Kizazi toka Adamu hadi Nuhu | Uzao wa Adamu | Wakuu wa familia kabla ya gharika |
| 5:1-2 | 5:1-5 | 5:1-2 | 5:1-5 | 5:1-2 |
| 5:3-5 | | 5:3-5 | | 5:3-5 |
| 5:6-8 | 5:6-8 | 5:6-8 | 5:6-8 | 5:6-8 |
| 5:9-11 | 5:9-11 | 5:9-11 | 5:9-11 | 5:9-11 |
| 5:12-14 | 5:12-14 | 5:12-14 | 5:12-14 | 5:12-14 |
| 5:15-17 | 5:15-17 | 5:15-17 | 5:15-17 | 5:15-17 |
| 5:18-20 | 5:18-20 | 5:18-20 | 5:18-20 | 5:18-20 |
| 5:21-24 | 5:21-24 | 5:21-24 | 5:21-24 | 5:21-24 |
| 5:25-27 | 5:21-24 | 5:21-24 | 5:21-24 | 5:21-24 |
| 5:28-31 | 5:28-31 | 5:28-31 | 5:28-31 | 5:28-3 |
| 5:32 | 5:32 | 5:32 | 5:32 | 5:32 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa vii)

### KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya ya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:1-2**
**[1]Hiki ndicho kitabu cha vizazi vya Adamu. Siku ile Mungu alipoumba mtu, kwa sura ya Mungu alimfanya; [2]mwanamume na mwanamke aliwaumba, akawabariki akawaita jina lao Adamu, siku ile walipoumbwa.**

**5:1 "Vizazi vya"** Neno hili (BDB 410) limejirudia mara kumi katika kitabu cha Mwanzo (kama vile 2:4; 5:1; 6:9; 10:1; 11:10,27; 25:12,19; 36:1; 37:2). Hii inaonekana kudokeza nyaraka iliyoandikwa (yumkini kwenye vigae vya udongo au gombo la ngozi). Huko Mesopotamia ya kale neno au kifungu cha vikabari vya vigae lilitumika kuunganisha pamoja vigae mbali mbali za vyungu kama fasihi kwa ujumla (yaani wasifu). Ninaamini kuwa Musa

alitumia (1) mapokeo ya kusimuliwa, (2) vyanzo vilivyoandikwa toka kwa wakuu wa kaya, vile vile pia (3) ufunuo wa moja kwa moja kuiandika torati. Kifungu hiki kinajirudia mara nyingi katika kitabu cha Mwanzo. Mara nyingi kinahitimisha muktadha. Kinafanya kazi kama alama ya hitimisho la fasihi.

◙ **"siku ile Mungu alipomuumba mtu"** Hii inaweza kuanzisha kikabari kingine tofauti cha kigae cha jiwe kwa vile kinafupisha Mwanzo 1-2.

**5:2 "akawaita jina"** Tambua kuwa haya ni matumizi ya kizazi cha Adamu, kama ulivyo mstari wa 3 ni utumiaji maalum. Matumizi ya ainasafu ni uthibitisho mwingine wa usawa, kama ilivyo 1:26-27.

◙**"siku ile"** Haya ni matumizi ya neno "siku,"na sio kama muda wa masaa ishirini na manne, bali ni zama au kipindi cha muda. Matumizi haya yenye kufanana yanaonekana katika Mwa. 2:4; Zab. 90:4. Angalia Mada Maalum katika 1:5.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 5:3-5**
**[3]Adamu akaishi miaka mia na thelathini, akazaa mwana kwa sura yake, kwa mfano wake, akamwita jina lake Sethi. [4]Siku za Adamu baada ya kumzaa Sethi zilikuwa miaka mia nane, akazaa wana, waume na wake. [5]Siku zote za Adamu alizoishi ni miaka mia kenda na thelathini, naye akafa.**

**5:3 "Adamu . . . akazaa mwana kwa sura yake, kwa mfano wake"** Kuna uwezekano wa tafsiri mbili kwenye kifungu hiki: (1) kama wanyama wengine walioko duniani, Adamu akazaa wana kwa mfano wake (kama vile 1:11) au (2) hili linaonyesha kuwa sura ya Mungu (kama vile 1:26-27) bado ilikuwepo kwa mwanadamu hata baada ya anguko.

**5:5 "Siku zote za Adamu alizoishi ni miaka mia kenda na thelathini "** Pamekuwepo na mijadala mingi kuhusu umri wa maisha ya mtu kabla na baada ya gharika kubwa kutokea(yaani kipindi kabla ya gharika kutokea). Baadhi wanadai kuwa (1) ni hesabu ya kitamathari; (2)walihesabu miaka kitofauti; (3) dhambi ilikuwa haijaiathiri dunia kama ilivyo sasa; au (4) sehemu kubwa ilitumika kuonyesha heshima kwa viongozi waliopita kama ilivyokuwa kwa orodha ya wafalme kumi wa Kisumeri. Katika orodha hiyo, wafalme kabla ya gharika waliishi miaka mingi kuliko wafalme waliokuwepo baada ya gharika, zaidi kama kwenye unasaba wa Biblia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:6-8**
**[6]Sethi akaishi miaka mia na mitano, akamzaa Enoshi. [7]Sethi akaishi baada ya kumzaa Enoshi miaka mia nane na saba, akazaa wana, waume na wake. [8]Siku zote za Sethi ni miaka mia kenda na kumi na miwili, akafa.**

Hii inarejelea mwanzoni kabisa katika 4:26

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:9-11**
**[9] Enoshi akaishi miaka tisini, akamzaa Kenani. [10] Enoshi akaishi baada ya kumzaa Kenani miaka mia nane na kumi na mitano, akazaa wana, waume na wake. [11] Siku zote za Enoshi ni miaka mia kenda na mitano, akafa.**

**5:10 "Kenani"** Hili linaweza kumaanisha : (1) "mmiliki"; (2) "mwana"; (3) "kitu kilichoumbwa"; (4) "mme"; au (5) "askari mtumia mkuki" (BDB 884). Hili ni dhahiri likiwa na chaguzi nyingi (kama ndivyo mara nyingi inakuwa sababu) kwamba kwa uwazi haijulikani maana yake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:12-14**
**[12]Kenani akaishi miaka sabini, akamzaa Mahalaleli. [13]Kenani akaishi baada ya kumzaa Mahalaleli miaka mia nane na arobaini, akazaa wana, waume na wake. [14]Siku zote za Kenani ni miaka mia kenda na kumi, akafa.**

Ni wazi kuwa haya ni maelezo mfanano ya fasihi

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:15-17**
**[15] Mahalaleli akaishi miaka sitini na mitano, akamzaa Yaredi. [16] Mahalaleli akaishi baada ya kumzaa Yaredi miaka mia nane na thelathini, akazaa wana, waume na wake. [17] Siku zote za Mahalaleli ni miaka mia nane na tisini na mitano, akafa.**

**5:15 "Mahalaleli"** Hili linamaanisha "sifa za Mungu" (BDB 239).

◙ **"Yaredi"** Hili linamaanisha "mteremko" (BDB 434).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5: 18-20**
**[18] Yaredi akaishi miaka mia na sitini na miwili, akamzaa Henoko. [19]Yaredi akaishi baada ya kumzaa Henoko miaka mia nane, akazaa wana, waume na wake. [20] Siku zote za Yaredi ni miaka mia kenda na sitini na miwili, akafa.**

**5:18 "Henoko"** Hili laweza kumaanisha (1) "wa kwanza"; (2) "aliyetolewa kwa"; au (3) "mwanzilishi" (BDB 335). Angalia maelezo katika 4:17b kwa ajili ya kufananisha kwenye majina kati ya uzao wa Kaini (yaani Sura ya 4) na uzao wa Sethi (yaani. Sura ya 5).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:21-24**
**[21] Henoko akaishi miaka sitini na mitano, akamzaa Methusela. [22]Henoko akaenda pamoja na Mungu baada ya kumzaa Methusela miaka mia tatu, akazaa wana, waume na wake. [23]Siku zote za Henoko ni miaka mia tatu na sitini na mitano. [24]Henoko akaenda pamoja na Mungu, naye akatoweka, maana Mungu alimtwaa.**

**5:21 "Methusela"** Hili linamaanisha (1) "mtu wa kurusha mkuki" au (2) "mtu wa silaha" (BDB 607). Anasemekana kuishi miaka mingi kuliko yeyote kwenye Biblia lakini hakuna sababu au msisitizo wowote ulioambatana na ukweli huu. Walimu wa dini ya Kiyahudi wanasema kuwa gharika ilitokea siku ambayo Metusela alifariki.

**5:22 "Henoko akaenda pamoja na Mungu"** Neno la Kiebrania (BDB 229, KB 246) ni shina *Hithpael* lenye kumaanisha ushirika wa ndani kiwastani katika hatua ya "kuishi pamoja na." kama yalivyo majina ya kale ya Kiebrania, hatuna uhakika na maana ya majina haya (BDB 335).Waebrania 11:5 inaelezea kutembea kwa Henoko kwa imani. Mtu mwingine ambaye kifungu hiki kinamwongelea ni Nuhu katika 6:9.

**5:24 "maana Mungu alimtwaa"** Haya maneno yenye kufanana (BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI TIMILIFU) yametumika kumwelezea Eliya kwenye 2 Fal. 2:3,5,9,10. Hili linautafasili uwepo wa Mungu ndani yake pasipo kuyakabili mauti ya mwili. Uhusiano wa Henoko na Mungu ulisababishwa na ushirika binafsi wa ndani. Kwenye sura pamejawa na kifungu "na akafa" ni mfano wa kuchangamsha wenye tumaini (1) la upendo wa Mungu na (2) kwa ajili ya wote wanao amini katika yeye.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:25-27**
**[25]Methusela akaishi miaka mia na themanini na saba, akamzaa Lameki. [26]Methusela akaishi baada ya kumzaa Lameki miaka mia saba na themanini na miwili, akazaa wana, waume na wake. [27]Siku zote za Methusela ni miaka mia kenda na sitini na kenda, akafa.**

**5:26 "Lameki"** Yamkini hili jina linamaanisha" (1) "mwenye nguvu" (2) "kijana"; (3) "mpiganaji"; au (4) "mshindi" (BDB 541). Toleo la KB linataja maana ya mzizi wa Kiarabu "mtu mwenye nguvu." Jina hili pia linapatikana katika uzao wa Kaini (kama vile 4:18na kuendelea). Hili linadokeza (1) jina lilikuwa linajulikana au (2) kuna baadhi ya mahusiano kati ya vizazi viwili.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 5:28-31**
**[28] Lameki akaishi miaka mia na themanini na miwili, akazaa mwana. [29] Akamwita jina lake Nuhu, akinena, Huyu ndiye atakayetufariji kwa kazi yetu na kwa taabu ya mikono yetu katika nchi aliyoilaani Bwana. [30] Lameki akaishi baada ya kumzaa Nuhu miaka mia na tisini na mitano, akazaa wana, waume na wake. [31] Siku zote za Lameki ni miaka mia saba na sabini na saba, akafa.**

**5:28** Ni tofauti gani ya kushangaza iliyopo kati ya hawa Lameki wawili. Mmoja ni mwenye majivuno ya kurudisha visasi (uzao wa Kaini); wa pili ni yule mwenye tumaini la neema ya Mungu (uzao wa Sethi)!

**5:29 "Nuhu. . .atakayetufariji"** Hili ni neno la kawaida, lenye kukua kwa lugha, na asili ya neno "atakayetufariji" (BDB 629). Hii inaonekana kuielezea imani ya Lameki, kuwa kupitia Nuhu, badiliko muhimu la laana ya Mwa. 3:17 ingalichukua nafasi. Haya ni maelezo ya Lameki ya imani.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 5:32**
**[32]Nuhu alikuwa mwenye miaka mia tano, Nuhu akawazaa Shemu, na Hamu, na Yafethi.**

**5:32 "Shemu"** Hili neno lingemaanisha "maarufu" au "jina" (BDB 1028).

◙ **"Hamu"** Hili neno laweza kumaanisha "kuwa mwekundu" au "kuwa mweusi" (BDB 325).

◙ **"Yafethi"** Hili neno laweza kumaanisha "urembo" au "kutawanyika" (BDB 834)

## MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wafasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.
Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni uhusiano upi wa kithiolojia uliopo kati ya Mwanzo 4 na 5?
2. Kwa nini kizazi cha Kaini kiliendelea na baadaye kupotea moja kwa moja toka kwenye maandiko?
3. Kwa nii majina ya watu wa Kaini na Sethi yanafanana?
4. Ni kipi kilichotokea kwa Henoko?

# MWANZO 6:1-22

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Uharibifu wa Mwanadamu | Uovu na hukumu ya mtu | Kuzaliwa kwa Wanefili | Uovu wa Mwanadamu | Wana wa Mungu na binti za wanadamu |
| 6:1-4 | 6:1-4 | 6:1-4 | 6:1-4 | 6:1-4 |
| | | Gharika kubwa | | Uharibifu wa binadamu |
| | | (6:5-8:22) | | |
| 6:5-8 | 6:5-8 | 6:5-8 | 6:5-8 | 6:5-8 |
| | Nuhu amfurahisha Mungu | | Nuhu | |
| 6:9-10 | 6:9-10 | 6:9-10 | 6:9-12 | 6:9-12 |
| | | | | 6:9b-12 |
| 6:11-12 | 6:11-13 | 6:11-22 | | Maandalizi kwa ajili ya Gharika |
| | | | | (6:13-7:16) |
| 6:13-22 | Safina yaandaliwa | | 6:13-22 | 6:13-16 |
| | 6:14-21 | | | |
| | | | | 6:17-22 |
| | 6:22 | | | |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (**Angalia ukurasa wa Vii**)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 6:1-4**

**[1] Ikawa wanadamu walipoanza kuzidi usoni pa nchi na wana wa kike walizaliwa kwao, [2] wana wa Mungu waliwaona hao binti za wanadamu ya kuwa ni wazuri; wakajitwalia wake wo wote waliowachagua. [3] Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu milele, kwa kuwa yeye naye ni nyama; basi siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini. [4] Nao Wanefili walikuwako duniani siku zile;tena ,baada ya hayo ,wana wa Mungu walipoingia kwa binti za binadamu,wakazaa nao wana;hao ndiyo waliokuwa watu hodari zamani ,watu wenye sifa.**

**6:1 "wanadamu"** Huu ni utumiaji wa kawaida wa neno (kama vile 5:2). Kama likitumika kwa maana ya kawaida katika mstari wa 2 ambao unaonekana kuyumkinika hivyo basi nathadhari ya kimalaika imeimalika

◙ **"na wana wa kike walizaliwa kwao"** Hili halidokezi kuwa hawa walikuwa wazaliwa wa kwanza wa kike (kama vile 5:4) bali maelezo ya jumla ya ongezeko la asili ya mwanadamu (BDB 408, KB 411, *Qal* KAULI TENDWA TIMILIFU)

**6:2 "wana wa Mungu"** Angalia Mada Maalum hapo chini

### MADA MAALUM: "wana wa Mungu" katika Mwanzo 6

**A.** Kuna mkanganyiko mkubwa juu ya utambuzi wa kifungu "wana wa Mungu." Pamekuwepo na tafasiri tatu kuu
1. Kifungu kinarejea juu ya uzao wa ki-Mungu wa Sethi (kama vile Mwanzo 5, soma maelezo kwenye 4:14
2. Kifungu kinarejea juu ya kikundi cha viumbe wa kimalaika
3. Kifungu kinarejea juu ya wafalme, wadhalimu au uzao wa Kaini (kama vile Mwanzo 4)

B. Ushahidi kwa ajili ya kifungu hiki unarejea juu ya uzao wa Sethi
1. Muktadha wa haraka wa fasihi wa Mwanzo 4 na 5 unaonyesha maendeleo ya uzao wa uasi wa Kaini na uzao wa Sethi uliochaguliwa. Kwa hiyo, ushahidi wa kimuktadha unaonekana kuupendelea uzao wa ki-Mungu wa Sethi
2. Walimu wa dini ya Kiyahudi wamekuwa wakitofautiana juu ya uelewa wa kifungu hiki. Baadhi wanadai kuwa kinamrejelea Sethi (lakini wengi wanadai malaika)
3. Kifungu cha umoja "wana wa Mungu," ingawa mara nyingi kinatumika kwa viumbe vya kimalaika, mara chache kinarejelea wanadamu.
   a. Kumb. 14:1 – "wana wa YHWH Mungu wako"
   b. Kumb. 32:5 – "Wana wake"
   c. Kut. 22:8-9; 21:6 (yumkini mwamuzi wa Kilawi)
   d. Zaburi 73:15 – "wana wenu"
   e. Hosea 1:10 – "wana wa Mungu aliye hai"

C. Ushahidi wa kifungu unaorejelea viumbe vya kimalaika
1. Huu umekuwa ni uelewa wa kawaida wa kimapokeao wa kifungu hiki. Muktadha mpana wa kitabu cha Mwanzo ungaliunga mkono huu mtizamo kama mfano mwingine wa uovu wa kimiujiza wa kuyazuia mapenzi ya Mungu kwa mwanadamu (walimu wa dini waliyasema haya kwa kinyongo)
2. Wingi wa kifungu(wana wa Mungu) unatumika kwa wingi kabisa katika Agano la Kale kwa ajili ya malaika
   a. Ayubu 1:6
   b. Ayubu 2:1
   c. Ayubu 38:7

   d. Zaburi 29:1
   e. Zaburi 89:6,7
   f. Danieli 89:6
3. Kitabu cha 1 Henoko kipindi kati ya Agano la Kale na Agano Jipya (kama vile I Enoch 6:1-8:4; 12:4-6; 19:1-3; 21:1-10) na Yubileyi (kama vile Ayub 5:1), ambacho kilikuwa kikifahamika kati ya waamini kipindi cha Agano Jipya , kikiwa na *Genesis Apocryphon* toka kwenye magombo ya Bahari ya Chumvi, vinayafasiri haya kama malaika wale walioasi
4. Muktadha wa haraka wa sura ya 6 unaonekana kudokeza kuwa "watu wale wenye nguvu ambao walikuwa ni watu wa kale waliojulikana" walitokana na mchanganyiko huu usio sawa wa utaratibu wa uumbaji.
5. Maandiko ya kale ya Kiyunani yanalitafasiri hili "wana wa Mungu" kama "malaika wa Mungu"
6. 1 Henoko hata anadai kuwa gharika ya Nuhu ilikuwa kuangamiza huu muunganikano wa malaika/mwanadamu ambao haukuwa wa kirafiki dhidi yake na YHWH na mpango wake wa uumbaji (kama vile I Enoch 7:1na kuendelea; 15:1na kuendelea; 86:1na kuendelea)
7. Katika fasihi ya Ugariti "wana wa Mungu" inarejele kwa washirika wa hekalu la miungu wengi (yaani., wale viumbe wa chini wa kiroho)

D. Ushahidi wa kifungu unarejelea kwa wafalme au wadhalimu wa uzao wa Kaini
1. Kuna tafasiri mbali mbali za kale ambazo zinaunga mkono huu mtizamo
   a. Targum wa Onkelo (karne ya pili B.K) inatafasiri "wana wa Mungu" kama "wana wa watu wenye uwezo"
   b. Symmachus (karne ya pili B.K) tafasiri ya Kiyunani, inaritafasiri "wana wa Mungu" kama "wana wa wafalme"
   c. Neno *"elohim"* linatumika kwa viongozi wa Israel (kama vile Kut. 21:6; 22:8; Zab. 82:1,6), kumbuka Biblia ya NIV na NET
   d. *Nephilim* lililounganishwa na *Gibborim* katika Mwa. 6:4, *Gibborim* ni kutoka *Gibbor* likimaanisha "mwanaume mwenye nguvu jasiri; utajiri au nguvu
   e. Ufasiri huu na ushahidi umechukuliwa toka maneno magumu ya Biblia kur. 106-108.

E. Ushahidi wa kihistoria wa watetezi wa matumizi yote
1. Kifungu kinarejelea kwa Sethi
   a. Cyril wa Iskanda
   b. Theodoret
   c. Augustine
   d. Jerome
   e. Calvin
   f. Kyle
   g. Gleason Archer
   h. Watts
2. Kifungu kinarejelea kwa viumbe wa kimalaika
   a. Waandishi wa tafasiri ya maandiko ya kale
   b. b. Philo
   c. Josephus (*Antiquities* 1:3:1)
   d. Justin Martyr
   e. Irenaeus
   f. Clement wa Isakanderia
   g. Tertullian
   h. Origen
   i. Luther
   j. Ewald
   k. Delitzsch
   l. Hengstenberg
   m. Olford
   n. Westermann
   o. Wenham
   p. NET Bible

F. Ni kwa namna gani "Manefili" wa Mwanzo 6:4 wanahusiana na "wana wa Mungu" na "binti za wanadamu" wa Mwanzo 6:1-2? Kumbuka hizi nadharia:
1. Wao ni matokeo ya majitu makubwa (kama vile Hesabu 13:33) ya muunganikano kati ya malaika na binadamu wa kike.
2. Havihusiani kabisa. Vimetajwa tu kama viliwahi kuwepo kwenye uso wa dunia kwenye nyakati za matukio ya Mwanzo 6:1-2 na pia baadaye
3. R. K. Harrison katika *Introduction to the Old Testament*, uk. 557, ana nukuu yenye kutatiza, "kukoswa moja kwa moja thamani ya utambuzi wa ndani juu ya elimu ya binadamu na maendeleo yake kuelekea kwenye mwingiliano wa mahusiano ya *homo sapiens* na viumbe wa mwanzo waliotokana na Adamu ambamo sura nzima imehusika, na ambayo imekubalika kwa wale wasomi ambao wameweza

kuwafatilia." Hili linanijulisha kuwa aliyaona haya makundi mawili kama yenye kuwakilisha makundi tofauti ya tabia za kibinadamu. Hili lingalidokeza uumbaji maalum wa baadae wa Adamu na Hawa, lakini pia maendeleo ya kimabadiliko ya viumbe *Homo erectus*

G. Ni haki kuweka wazi uelewa wangu wa mkanganyiko wa andiko hili. Kwanza, ngoja tukumbushane sisi sote kuwa andiko kwenye Mwanzo ni fupi na ni gumu. Msikiaji wa mwanzo ambaye ni Musa alikuwa amekwisha kuwa na utambuzi wa ndani zaidi wa kihistoria au Musa alitumia utaribu wa simulizi au kuandikwa toka kipindi cha utawala wa kiume kwamba yeye mwenyewe hakuelewa kwa ukamilifu. Hili suala sio mada muhimu ya kithiolojia. Mara nyingi tunakuwa wadadisi kuhusu vitu ambavyo maandiko yanavigusia lakini ni vigumu kueleweka. Itakuwa bahati mbaya kufanya thiolojia kiundani nje ya hili na sehemu zenye kufanana za habari ya kibiblia. Kama tungetaka habari hizi Mungu angaliweza kuzitoa kwa uwazi na ukamilifu. Mimi pekee naamini walikuwa malaika na wanadamu kwa sababu:
   1. Ni mwendelezo, ingawa haikukatazwa, kukitumia kifungu "wana wa Mungu" kwa ajili ya malaika katika Agano la Kale
   2. Mtafasiri wa maandiko ya kale ya Kiebrania (Iskanderia) analitafasiri (karne ya kwanza K.K) "wana wa Mungu" kama "malaika wa Mungu"
   3. Kitabu cha maandiko ya uongo chenye matukio ya mwisho cha 1 Henoko (yumkini yaliandikwa miaka ya 200 K.K) ni halisia kuwa yanarejelea kwa malaika (kama vile sura ya 6-7)
   4. Kithiolojia inaunganisha na 2 Petro 2 na Yuda juu ya malaika waliotenda dhambi na hawakutunza mazingira yao vizuri, ninajua kuwa kwa kiasi Fulani hili linaleta mkanganyiko kwa Mathayo 22:30, lakini hawa malaika maalum hawako mbinguni wala duniani bali wako katika gereza maalum(Tartarus)
   5. Nafikiria kuwa sababu mojawapo ya matukio mengi ya Mwanzo 1-11 yanapatikana katika tamaduni (yaani., habari za uumbaji wenye kufanana , habari za kufanana za gharika, habari mfanano za malaika kuwachukua malaika) ni kwa sababu wanadamu wote walikuwa pamoja na walikuwa na maarifa juu ya YHWH wakati wa kipindi hiki, lakini baada ya kutawanyika kwenye mnara wa Babel maarifa haya yakapotoshwa na kubadilishwa kwenye imani ya miungu wengi.

      Mfano mzuri wa hadithi za kubuniwa zilikuwa ni watu wenye maumbo makubwa nusu wanadamu wenye uwezo mkubwa wa kufikiri yaliyoitwa majitu (titans) yaliyokuwa yamewekwa gerezani kwenye *Tartarus*, hili ni jina lililotumika mara moja kwenye Biblia (kama vile 2 Petro 2) kwa ajili ya sehemu ya kuwaweka malaika wasiotunza vizuri ukazi wao. Katika thiolojia ya sheria za dini ya Kiyahudi kuzimu kuligawanywa katika sehemu mbili kwa ajili ya watakatifu paliitwa Paradiso na kwa ajili ya waovu paliitwa (*Tartarus*).

◙**"binti za wanadamu walikuwa wazuri"** Neno "wazuri" kiuhalisia ni "mwenye sifa njema" au "haki"(BDB 373). Hili limekuwa ni dhana ya jibu la kithiolojia toka sura ya 1 (hasa 1:31). Kile Mungu alichokiona kizuri sasa anakiona kiovu (kama vile mistari ya 5-6).

◙ **"wakajitwalia wake wowote waliowachagua"** Kifungu cha kwanza kinadokeza ndoa ambayo ingalipinga dhidi ya mtazamo kuwa walikuwa malaika (BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU). Hata hivyo, kifungu cha pili kinadokeza kuwa walijitwalia wanawake waliokuwa hawajaolewa, wowote waliojichagulia (BDB 103, 119, *Qal* KAULI TIMILIFU). Hili lingaliweza kudokeza (1) viumbe vya kimalaika au (2) viongozi wenye nguvu wa uzao wa Kaini (yaani wadhalimu) wakitenda ndoa ya wake wengi/mitala.

**6:3 "Roho yangu haitashindana na mwanadmu milele"** Neno"haitashindana" linaweza kutafasiliwa kama "haitaendelea" (BDB 192, KB 220, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU, kama vile toleo la NRSV "kuendelea kuvumuliana"). Hili pia linarejelea (1) uvumilivu wa Mungu (yaani aliahirisha kuwepo na gharika mpaka pale safina ilipokamilika kama vile I Pet. 3:20) au (2) muda wa kuishi mwanadamu ulipopungua. Ni kwa namna gani 6:3 inahusiana na 6:1-2 na 6:4? Ni vigumu kufuatisha kusudio la mwandishi wa awali kupitia muktadha huu. Yumkini ingawa wanadamu wameingiliana na malaika lakini bado wataendelea kufa. Kama Hawa "alivyoona"na kuchukua vivyo hivyo sasa "wana wa Mungu "waliona" na kuchukua, ambavyo kunadokeza aina ile ile ya uasi (yaani yumkini kuuchukua uzima wa milele au uhuru).

◙ **"kwa kuwa yeye naye ni nyama"** Hili linaonekana kuongeza uzito kwenye ufasiri kwamba watu wengine waliozungumzwa juu ya sura hii ni viumbe vya kimalaika wakipingana na wanadamu wa kidunia.Today's English Version inatafasiri "viumbe wa kiulimwengu."

◙ **" siku zake zitakuwa miaka mia na ishirini"** Hili linaonyesha kudokeza kile kipindi cha neema (kama vile II Pet. 2:5) ambapo inadaiwa kuwa Nuhu aliongea kwa ajili ya miaka iliyoingilia kati, kwa hiyo, inarejea kwenye muda mpaka pale mafuliko yalipokuja. Pia ingaliweza kuangalia juu ya kupungua kwa muda wa mwanadamu kuishi baada ya mafuriko kuja.

**6:4 "Manefili"** Hili linadokeza "watu walioanguka" (kutoka kwenye neno la Kiebrania *naphal*, BDB 658, KB 709). Inanionyesha kuwa hawa wanafanana na majitu (kama vile Hesabu 13:33; pia Kumb. 2:10-11; 9:2; na tafasiri ya maandiko ya kale, tafasiri za Vulgate na Peshitta). Hata hivyo, wafasiri wengine kama vile Martin Luther na H.C. Leupold wanadai kuwa neno hili linatakiwa kutafasiliwa kama "wadhalimu" ambalo linamaanisha wafalme wenye nguvu wa uzao wa Kaini waliokuwa wana nyumba kubwa ya harimu. J. Wash Watts in *Old Testament Teaching*, kur. za 28-30, anasema "Manefili wanarejelea kwa Nuhu na familia yake kwa namna wale walivyojitenga wao wenyewe toka kwenye uzao wa Kaini na uzao wa Sethi ambao walikuwa wakioana. Katika kulitafasiri Wanefili ni wana wa "Mungu wa kweli"(kama vile"Mungu" 5:22,24; 6:9). Angalia Mada Maalum hapa chini.

## MADA MAALUM: MANENO YALIYOTUMIKA KWA AJILI YA WAPIGANAJI WENYE NGUVU AU MAKUNDI YA WATU.

Watu hawa wakubwa/warefu/wenye nguvu wanaitwa kwa majina mbali mbali

1. *Wanefili* (BDB 658) - Mwa. 6:4; Hes. 13:33
2. *Warefai* (huenda BDB 952 au BDB 952 II) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:11,20; 3:11,13; Yosh. 12:4; 13:12; II Sam. 21:16,18,20,22; I Nya. 20:4,6,8
3. *Wazamzumi* (BDB 273), *Wazuzi* (BDB 265) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:20
4. *Waemi* (BDB 34) - Mwa. 14:5; Kumb. 2:10-11
5. *Waanaki* (wana wa *Anaki*, BDB 778 I) - Hes. 13:33; Kumb. 1:28; 2:10-11,21; 9:2; Yosh. 11:21-22; 14:12,15

◙ **"walikuweko duniani katika siku zile"** Wale wote wanaoamini malaika kukaa kinyumba na binti za wanadamu wanatumia kipindi cha pili cha mstari wa 4 kama uhakiki wa maandiko kuonyesha kuwa yale majitu yalitokana na uhusiano huu. Hata hivyo, wengine wanatumia kipindi cha kwanza cha mstari wa 4 kudai kuwa haya majitu tayari yalikuweko duniani kwa kipindi hiki. Kitabu cha matukio ya mwisho kati ya agano la kale na agano jipya cha 1 Henoko kinadai kuwa haya majitu yalikuwa matokeo ya muunganikano wa malaika na wanadamu na kuwa muunganikano wa utaratibu wa uumbaji ndio sababu ya Mungu kuleta gharika. Kitabu cha 1 Henoko pia kinadai kuwa haya majitu yaliyopoteza maumbo yao ya mwili kwenye gharika yalikuwa mapepo yakitafuta kuishi ndani ya miili ya binadamu kwa sababu ya ubinafsi wao.

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | **"watu wenye nguvu"** |
| **NRSV, NJB** | **"hodari"** |
| **TEV** | **"watu hodari"** |

Hili ni neno la Kiebrania *gibbor* (BDB 150), ambalo linamaanisha hasa mtu aliyewezeshwa, mnyama, au kitu. Lilitumika kwa (1) Nimrodi wa Mwanzo 10:8-9; (2) wadharimu katika Zab. 52:1; Ezek. 32:27; na (3) malaika katika Zab. 104:20 (pia wimbo wa shukurani 8:11 na 20:34 toka magombo ya bahari ya chumvi)

◙

| | |
|---|---|
| **NASB, NKJV** | |
| **NJB, NIV** | **"watu wenye sifa"** |

**NRSV** **"wapiganaji wenye sifa"**
**TEV** **"watu waliojulikana"**

Uwasilishaji wa kwanza ni tafasiri kuu ya Biblia za Kiingereza vile vile pia na tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania. Hata hivyo, kiuhalisia ni "watu wenye majina"BDB 1027). Hii imesababisha kuwepo kwa nadharia tatu:

1) inarejea kwenye uzao wa ki-Mungu Seth ambaye alimwabudu YHWH (yaani jina la Mungu, kama vile J. Wash Watts)
2) hili linarejelea Manefili kama watoto wenye nguvu wa malaika na mwanadamu (yaani Majitu kama vile toleo la TEV)
3) inarejelea kwa wafalme wa uzao wa miungu ya Kaini ambao walikuwa wadhalimu (kama vile toleo NRSV); waliwachukua wanawake wengi kuwafanya wake (yaani ndoa za kifahari za wake wengi kama vile toleo la NJB) hiki ni kifungu kigumu na kilichoandikwa kwa ufupi. Msukumo wake mkubwa ni mwendelezo na ongezeko la maovu ya uumbaji ambao unaweka hatua muhimu ya hukumu ya Mungu. Hata hivyo, uovu uliendelea hata kwa Nuhu na familia yake.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 6:5-8**
**5 Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu sikuzote. 6 Bwana akaghairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu duniani, akahuzunika moyo. 7 Bwana akasema, Nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemwumba usoni pa nchi; mwanadamu na mnyama, na kitambaacho na ndege wa angani; kwa maana naghairi ya kwamba nimewafanya. 8 Lakini Nuhu akapata neema machoni pa Bwana.**

**6:5 "Bwana akaona ya kuwa maovu ya mwanadamu ni makubwa duniani"** Kipengele hiki cha maandiko kinasisitiza kuendelea kwa uovu moyoni mwa mwanadamu (BDB 906, KB 1157, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU, kama vile Mwa. 6:11- 12,13b; 8:21; Zab. 14:3; 51:5) ambacho ni fumbo la moja kwa moja kwenye wema wa uumbaji katika Mwa.1:31.

◙ **"na kwamba kila kusudi analowaza moyoni mwake ni baya tu siku zote"** Matokeo haya ya anguko la Adamu na Hawa yameisha ufikia ulimwengu mzima. Katika wote ni sita tu hawakuathiriwa na uovu. Waliishi kwa kuufikiria uovu, usiku na mchana! Dhana ya "kusudio la uovu" (*ysr,* BDB 428) ikajakuwa uelewa wa sheria za Kiyahudi za asili ya uadilifu wa mwanadamu. Walimwona mwanadamu kama mwenye kutenda moja kati ya yale makusudio mawili (wema na uovu). Methali hii maarufu, "kwa kila moyo wa mwanadamu kuna mbwa mweusi na mweupe; yule unaye mlisha sana ndiye anaenenepa" (fasili), inamwelezea mwanadamu. Huu mtizamo wa mwanadmu unawezeshwa na 4:7. Mwana thiolojia wa Kiyahudi hasisitizii juu ya Mwanzo 3 bali Mwanzo 6 kama chanzo cha uovu ulimwenguni. Watoto huwa hawana dhambi wakati wakizaliwa kwa sababu wajibu wa kuchagua wema na baya huja na maarifa (*bar mitzvah*, *bat mitzvah*).

**6:6 "Bwana akaghairi. . .akahuzunika moyo"** Hivi ni vifungu venye nadharia ya Mungu kuwa na tabia za kibinadamu. Cha kwanza kinatafasiliwa "Bwana akashikwa na huzuni" (BDB 636, KB 688, *Niphal* KAULI ISIYO TIMILIFU). Ya pili inatafasiliwa "Bwana akahuzunika moyoni" (BDB 780, KB 864, *Hithpael* KAULI ISIYO TIMILIFU). Hivi ni vifungu venye nguvu vya Kiebrania (kama vile 34:7; 45:5; I Sam. 2:33; 20:34; II Sam. 19:2; Zab. 78:40; Isa. 54:6). Mara nyingi Mungu ameongea ndani ya Biblia kama mwenye kuomba msamaha au kutubu (kama vile Mwa. 6:6-7; Kut. 32:14; I Sam. 15:11; II Sam. 24:16; Yer. 18:7,8; 26:13,19; Yona 3:10). Hata hivyo, sura zingine zinadai kuwa kamwe Mungu hajawahi kutubu au kubadili mawazo yake (kama vile Hes. 23:19; I Sam. 15:29; Yer. 4:28; Zab. 132:11). Huu ni mvutano ambao kila mara unatokea pale tunapotumia maneno ya kibinadamu kumwelezea Mungu. Mungu si mwanadamu, lakini maneno pekee tulionayo kumwelezea Yeye na mawazo Yake ni maneno ya kibinadamu. Lazima litetewe kuwa Mungu habadiliki. Amejitoa na kuvumilia kwenye kusudi lake la ukombozi kwa ajili ya mwanadamu, lakini wajibu wa mwanadamu kwenye toba ya dhambi mara zote inategemea matendo ya Mungu kwenye hali Fulani (kama vile Zab. 106:45; Yona). Kithiolojia Mungu ndiye anayebadili, na sio mwanadamu. Lengo lake ni lile lile—kuwa na watu wenye kuaksi tabia zake. Hili litatimilizwa tu kwa kuwa na moyo mpya, agano jipya (kama vile Yer. 31:31-34; Ezek. 36:26-38). Juu ya hukumu Mungu huchagua neema zaidi !

**6:7 "nitamfutilia mbali mwanadamu niliyemuumba"** Neno "kumfutilia mbali" linamaanisha "nitamkatilia mbali" (BDB 562, KB 567, *Qal* KAULI ISIYO TIMILIFU, yaani., gharika). Wanyama nao wanaumia kwa ajili ya dhambi ya mwanadamu (kama vile Rum. 8:19-22). Samaki hawakujumuishwa kwenye hukumu. Hukumu haitegemei kubadilika kwa matendo ya miungu kama habari za huko Mesopotamia bali uchaguzi wa mema na mabaya ya mwanadamu. Uovu huu uliendelea kubaki hata kwenye familia ya mtu mwenye haki Nuhu (kama vile 8:21-22) lakini Mungu alichagua kuendelea kuufunika uovu wa mwanadamu mpaka pale Yesu alipokuja (kama vile Gal. 3).

**6:8 "machoni pa Bwana"** Huu ni mfano mwingine wa kifungu cha nadharia ya Mungu kuwa na tabia ya kibinadamu. Yeye hana macho, Yeye ni Roho. Hii ni sitiari kwa ajili ya ufahamu wa Mungu wa mambo yote (yaani. Mungu kujua mambo yote).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 6:9-10**
**9 Hivi ndivyo vizazi vya Nuhu. Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake; Nuhu alikwenda pamoja na Mungu. 10 Nuhu akazaa wana watatu wa kiume, Shemu, na Hamu, na Yafethi.**

**6:9 "Nuhu alikuwa mtu wa haki, mkamilifu katika vizazi vyake"** Maneno haya mawili yenye kujieleza ni ya muhimu. Lile la kwanza linadokeza kuwa Nuhu alithibitishwa kwenye viwango vya uelewa kuhusu mapenzi ya Mungu. Angalia Mada Maalum: Haki. La pili (BDB 1070) linadokeza kuwa alikuwa na moyo mkamilifu wenye kumwelekea Bwana (mfano. 17:1; Zab. 18:23). Neno la pili ni baaadaye lilitumika kwa ajili ya dhabihu isiokuwa na mawaa. Haya maneno mawili hayamaanishi kuwa Nuhu hakutenda dhambi, kama 9:21 inavyoonyesha.

## MADA MAALUM:HAKI

"Haki"ni mada muhimu ambayo mwannafunzi wa Biblia yampasa kufanya ni upanuzi binafsi wa kusoma juu ya dhana yenyewe.

Katika Agano la Kale sifa za Mungu zinaelezwa kama "halali" au "haki" (KITENZI, BDB 842, KB 1003; NOMINO JINSI YA KIUME, BDB 841, KB 1004; NOMINO JINSI YA KIKE, BDB 842, KB 1006). Neno la Mesopotamia lenyewe linatokana na "mafunjo ya mto" ambayo yalitumika kama chombo cha matengenezo ya utaalamu wa mlalo ulionyooka na uelekeo wa ukuta na ua. Mungu alilichagua neno lililotakiwa kutumika kistiari juu ya asili Yake mwenyewe. Yeye ni ukingo ulionyooka (kiongozi) ambapo vitu vyote vinatathiminiwa toka kwake. Dhana hii inatetea haki ya Mungu pamoja na Haki Yake ya kuhukumu.

Mwanadamu aliumbwa katika mfano wa Mungu (kama vile Mwa. 1:26-27; 5:1,3; 9:6). Mwanadamu aliumbwa kwa ushirika wa Mungu (yaani, Mwa. 3:8). Uumbaji wote ni hatua au mrejesho kwa Mungu na mwingiliano wa wanadamu. Mungu aliutaka uumbaji Wake mkuu, mwanadamu, kumjua Yeye, kumpenda Yeye, kumtumikia Yeye, na kuwa kama Yeye! Uaminifu wa mwanadamu ulipimwa (kama vile Mwanzo 3) na watu hawa wanadoa wa mwanzo walishindwa jaribio. Hii ilileta matokeo ya kuvunjika kwa uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu (kama vile Rum. 5:12-21).

Mungu aliahidi kufanya marekebisho na kurejesha ushirika (kama vile Mwa. 3:15; tazama Mada Maalumu: Mpango wa Wokovu wa Milele wa YHWH). Alifanya hivi kupitia mapenzi Yake mwenyewe na Mwanae . Wanadamu hawawezi kurejesha ahadi iliyovunjwa (kama vile Rum. 1:18-3:20; Ufunuo 5).

Baada ya Anguko,hatua ya kwanza ya Mungu kuuelekea urejesho ilikuwa dhana ya agano lililojikita katika mwaliko Wake na toba ya mwanadamu, imani, mwitikio wa utii (kama vile Yer. 31:31-34; Eze. 36:22-38). Kwa sababu ya Maanguko yote, wanadamu huwakuweza kujitenga na tendo (kama vile Rum. 3:21-31; Wagalatia 3). Mungu Pekee ilimbidi kuanzisha upya agano lililokuwa limevunjwa na wanadamu. Alifanya hivi kwa

A. kutangaza haki ya mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya mahakama)
B. kwa kutoa haki huru kwa mwanadamu kupitia kazi ya Kristo (yaani, haki ya kuzuliwa)

C. kumtoa Roho akaaye ndani ambaye huleta haki (yaani, Ufanano na Kristo, urejeshaji wa mfano wa Mungu) ndani ya mwanadamu

D. kurejesha ushirika wa Bustani ya Edeni (linganisha Mwanzo 1-2 na Ufunuo 21-22)

Hata hivyo, Mungu anahitaji mwitikio wa kimaagano. Mungu hutoa maagizo (yaani, hutoa kwa uhuru, Warumi 5:8; 6:23) lakini yawapasa wanadamu kuitikia na kuendelea kuitika katika

A. Toba

B. Imani

C. Utii kwenye stadi ya maisha

D. Ustahimilivu

Haki, kwa hiyo, ni agano, ni makubaliano kati ya Mungu na uumbaji Wake wa juu, uliyojikita juu ya sifa za Mungu, kazi ya Kristo, na Roho mwezeshaji, ambapo kila mtu kibinafsi anapaswa kuitikia kwa namna ifaavyo.Dhana inaitwa "haki kwa neema kupitia imani" (yaani, Efe. 2:8-9). Dhana inafunuliwa katika Injili, lakini si katika maneno haya. Kimsingi ilielezwa na Paulo, ambaye anatumia neno la Kiyunani "mwenye haki" katika miundo yake mbalimbali zaidi ya mara 100.

Paulo, akiwa mwalimu wa sheria aliyefundishwa, anatumia neno *dikaiosunē* katika maana yake ya Kiebrania ya neno *tsaddiq* lililotumika katika Tafsiri za Maandiko ya Kale ya Kiebrania, na si kutoka katika fasiri ya Kiyunani. Katika maandishi ya Kiyunani neno linamhusu yule ambaye amethibitisha matarajio ya Mungu na jamii (yaani, Nuhu, Ayubu). Katika maana ya Kiebrania mara nyingi limendwa katika maneno ya kimaagano (tazama Mada Maalumu: Agano). YHWH ni haki, maadili, Mungu mwema. Anawataka watu Wake kuwa viumbe vipya ili kwendana na sifa zake. Mwanadamu aliyekombolewa anakuwa kiumbe kipya (kama vile 2 Kor. 5:17; Gal. 6:15). Upya huu unaleta matokeo katika mtindo mpya wa maisha ya Kimungu (kama vile Mathayo 5-7; Gal. 5:22-24; Yakobo; 1 Yohana).Tangu Israeli ilipokuwa katika mfumo wa utawala wa kidini hapakuwepo na maelezo sahihi na ya kinagaubaga kati ya ulimwengu (kanuni za kijamii) na Mungu (mapenzi ya Mungu). Utofauti huu unaelezwa katika maneno ya Kiebrania na Kiyunani kuwa ya kutafsirika katika Kiingereza kama "haki" (yakihusiana na jamii)na "mwenye haki" (ikihusiana na dini).

Injili (habari njema) juu ya Yesu ni kwamba wanadamu walioanguka wamerejesha ushirika na Mungu. Hii limetimizwa kupitia pendo la Baba, huruma, na neema; maisha ya Mwana, kifo, na ufufuo; na kuugua kwa Roho na kielelezo cha injili. Haki ni tendo huru la Mungu, lakini linapaswa kuwa jambo la kimungu (Mtazamo wa Augustine, ambao unaakisi vyote msistizo wa Mabadiliko mapya juu ya uhuru wa injili na msisitizo wa Kanisa Katoriki juu ya maisha yaliyobadilishwa ya upendo na uaminifu). Kwa waleta mabadiliko neno "haki ya Mungu" ni shamilisho milikishi (yaani, tendo la mwanadamu aliyetenda dhambi kukubaliwa na Mungud [ utakaso wa mahali], ambapo kwa Wakathoriki ni kiima milikishi, ambapo ni tendo la kuimarika zaidi kama Mungu [utakaso endelevu na uliozoeleka].

Katika mtazamo wangu, Biblia nzima kutoka Mwanzo 4 – Ufunuo 20 ni maandiko yenye kuonyesha urejesho wa ushirika wa Mungu pale Edeni. Biblia inaanza kati ya Mungu na mwanadamu kuleta ushirika na mpangilio wa dunia (kama vile Mwanzo 1-2) na Biblia inaridhia mpangilio huo huo (kama vile Ufunuo 21-22). Mfano wa Mungu na kusudi lake vitarejeshwa!

Ili kuthibitisha mjadala wa hapo juu andika vifungu vilivyochguliwa vya Agano Jipya vyenye vielelezo vya kundi la neno la Kiyunani.

A. Mungu ni haki (mara kwa mara imeunganishwa kwa Mungu kama Hakimu)

1. Warumi 3:26
2. 2 Wathesalonike 1:5-6
3. 2 Timotheo 4:8
4. Ufunuo 16:5

B. Yesu ni haki
    1. Matendo 3:14; 7:52; 22:14 (jina la Masihi)
    2. Mathayo 27:19
    3. 1 Yohana 2:1,29; 3:7
C. Mapenzi ya Mungu kwa uumbaji Wakeni ya haki.
    1. Mambo ya Walawi 19:2
    2. Mathayo 5:48 (kama vile 5:17-20)
D. Kusudi la Mungu kutoa na kutoa haki
    1. Warumi 3:21-31
    2. Warumi 4
    3. Warumi 5:6-11
    4. Wagalatia 3:6-14
    5. Iliyotolewa na Mungu
        a. Warumi 3:24; 6:23
        b. 1 Wakorintho 1:30
        c. Waefeso 2:8-9
    6. Iliyopokelewa kwa imani
        a. Warumi 1:17; 3:22,26; 4:3,5,13; 9:30; 10:4,6,10
        b. 2 Wakorintho 5:7,21
    7. kupitia matendo ya Mwana
        a. Warumi 5:21
        b. 2 Wakorintho 5:21
        c. Wafilipi 2:6-11
E. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi Wake wawe wenye haki
    1. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
    2. Warumi 2:13; 5:1-5; 6:1-23
    3. Waefeso 1:4; 2:10
    4. 1 Timotheo 6:11
    5. 2 Timotheo 2:22; 3:16
    6. 1 Yohana3:7
    7. 1 Petro 2:24
F. Mungu ataihukumu dunia kwa haki
    1. Matendo 17:31
    2. 2 Timotheo 4:8
G. Kupitia matendo ya Mwana
    a. Warumi 5:21
    b. 2 Wakorintho 5:21
    c. Wafilipi 2:6-11
H. Mapenzi ya Mungu ni kwamba wafuasi wake wawe watakatifu
    a. Mathayo 5:3-48; 7:24-27
    b. Warumi2:13; 5:1-5; 6:1-23
    c. Waefeso 1:4; 2:10
    d. 1 Timotheo 6:11
    e. 2 Timotheo 2:22; 3:16
    f. 1 Yohana 3:7

g. 1 Petro 2:24

I. Mungu atauhukumu ulimwengu kwa haki

a. Matendo 17:31

b. 2 Timotheo 4:8

Haki ni tabia ya Mungu, iliyotolewa huru kwa wanadamu wenye dhambi kupitia Kristo. Hilo ni

A. agizo la Mungu
B. zawadi ya Mungu
C. tendo la Kristo
D. ni maisha yapaswayo kuishi

Lakini pia ni tendo la kuwa mwenye haki ambapo ni lazima kuwa na juhudi, uaminifu na kuishikilia, kwamba siku moja itatimizwa katika Ujio wa Pili. Ushirika na Mungu unarejeshwa katika wokovu lakini unaendelea katika maisha mazima ili kukutana naye ana kwa ana (kama vile 1 Yohana 3:2) katika kifo au ujio wa pili!

Hapa kuna dondoo nzuri ya kuhitimisha mjadala huu. Imechukuliwa kutoka Kamusi ya Paulo na barua zake kutoka IVP "Calvin, zaidi sana kuliko Luther, inasistiza kipengele cha uhusiano wa haki ya Mungu. Mtazamo wa Luther juu ya haki ya Mungu unaonekana kuwa dhana ya kuwa huru. Calvin anasisitiza asili ya ajabu ya mawasiliano au kutuarifu juu ya haki ya Mungu" (uk. 834).

Kwangu mimi uhusiano wa waumini na Mungu una vipengele vitatu.

A. injili ni mtu (msistizo wa Kanisa la Mashariki na Calvin)
B. injili ni ukweli (msisitizo wa Augustine na Luther)
C. injili ni maisha yaliobadilishwa (msistizo wa Katoliki)

Yote ni sawa na yanapaswa kuungamanishwa kwa pamoja kwa ajili ya afya, sauti, Ukristo wa kibiblia. Ikiwa ye yote anasisitizwa sana au anapunguza thamani, matatizo yanatokea.

Yatupasa kumkaribisha Yesu!

Yatupasa kuiamini injili!

Yatupasa kuwa na ushawishi juu ya ufanano wa Kristo!

◙ **"Nuhu alikwenda pamoja na Mungu"** Hiki (BDB 229, KB 246, *Hithpael* KAULI TIMILIFU) ni kifungu mfanano na 5:21-22 (*Hithpael* KAULI ISIO TIMILIFU) ambapo kifungu kimetumika kwa Henoko.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 6: 11-12**
**[11]Dunia ikaharibika mbele za Mungu, dunia ikajaa dhuluma. [12]Mungu akaiona dunia, na tazama, imeharibika; maana kila mwenye mwili amejiharibia njia yake duniani.**

**6:11-12** Mapenzi ya Mungu yalikuwa kwa ajili ya mwanadamu na wanyama kuijaza dunia lakini dhambi ikajaza (BDB 569, KB 583,*Niphal* KAULI ISIO TIMILIFU) dunia kwa vurugu na uovu (kama vile mst. 13; Zab. 14:1-3; Rum. 3:10-18). Hakuna tena "uzuri" wa Mwa. 1:31 aliouona Mungu wenye maelezo mazuri. Huu sio ulimwengu alioukusudia Mungu!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 6:13-22**
**[13] Mungu akamwambia Nuhu, Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia. [14]Ujifanyie safina ya mti wa mvinje; fanya na vyumba ndani ya safina, ukaifunike ndani na nje kwa lami. [15]Hivi ndivyo utakavyoifanya; mikono mia tatu urefu wa safina, mikono hamsini upana wake, na mikono thelathini kwenda juu kwake. [16]Uifanyie safina mwangaza, ukaumalize juu kiasi cha mkono mmoja; ukautie mlango wa safina katika ubavu wake; ukaifanyie dari tatu, ya chini, ya pili, na ya tatu. [17]Na tazama, nitaleta gharika ya maji juu ya nchi, niharibu kila kitu chenye mwili na**

**pumzi ya uhai, kisiwepo chini ya mbingu; kila kilichoko duniani kitakufa. [18]Lakini nitafanya agano langu nawe kuwa thabiti; nawe utaingia katika safina, wewe, na wanao, na mkeo, na wake za wanao, pamoja nawe. [19]Na katika kila kilicho hai chenye mwili, wawili wa kila namna utawaleta ndani ya safina, kuwahifadhi pamoja nawe; wawe mume na mke. [20]Katika vyote virukavyo kwa jinsi yake, na kila namna ya mnyama kwa jinsi yake, kila kitambaacho juu ya nchi kwa jinsi yake, wawili wa kila namna watakuja kwako ili uwahifadhi. [21]Ukajitwalie chakula cha kila namna kinacholika, ukakusanye, nacho kitakuwa ni chakula chenu na chao. [22]Ndivyo alivyofanya Nuhu, sawasawa na vyote alivyomwamuru Mungu, hivyo ndivyo alivyofanya.**

**6:14 "Ujifanyie safina"** KITENZI (BDB 793 I, KB 889) NI *Qal* KAULI SHURUTISHI. Hili linaweza kuwa neno la mkopo la ki-Misri kwa ajili ya "chombo" au "boksi" (BDB 1061). Matumizi mengine ya neno hili ni kwa ajili ya kisafina ambamo Musa aliwekwa (kama vile Kut. 2:3,4).

◙ **"mti wa mvinje"** Hatuna uhakika kuhusu asili ya neno hili (BDB 781 na 172). Baadhi ya tafasiri mbali mbali ni: (1) tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania "mti wa mraba"; (2) toleo la Kilatini (Vulgate) lina "mti mwololo"; (3) wengi wa watoa maoni wanaamini kuwa lilirejelea kwa baadhi ya aina ya miti, wengi walipendelea mti aina ya mvinje (NRSV, REB) kwa sababu nyingi za merikebu Mashariki ya kale zilitengenezwa kutokana na miti hii na kufunikwa juu yake kwa utomvu.

◙ **"fanya na vyumba ndani ya safina"** Hii inavyoonekana ilikuwa na sababu ya kuwagawa wanyama vile vile pia kuweza kusaidia kuwa na umbo la safina (pia kuwa na ngazi tatu).

**6:15 "dhiraa"** Kuna aina mbili ya dhiraa (BDB 52) kwenye Biblia. dhiraa ya kawaida ni kipimo kati ya wastani wa urefu wa kidole na kiwiko chake, mara nyingi yapata inchi 18 (kama vile Kumb. 3:11; II Nya. 2:3). Pia kuna dhiraa ndefu (dhiraa ya kifalme) ambayo hutumika kwenye ujenzi (yaani Hekalu la Sulemani), ambalo lilijulikana huko Misri, Palestina, na kiasi Fulani Babeli. Lilikuwa na urefu yapata inchi 21 (kama vile Ezek. 40:5; 43:13). Vipimo halisi vya safina yumkini vilikuwa yapata futi 450 kwa futi 75 kwa futi 45. Hii yapata kama nusu ya jengo la Malkia Elizabethi II. Imedhaniwa kuwa lilikuwa mraba lakini yawezekana lilikuwa na pande zilizokuwa kimshazari ili kusaidia kuthibiti msukumo wa mawimbi.

Hapo kale sehemu za mwili wa binadamu zilitumika kwa ajili ya kipimo. Watu wa Mashariki ya kale walitumia:

1. Upana kati ya urefu wa mkono ulionyooka
2. Urefu kati ya kiwiko na kidole cha kati (dhiraa)
3. Upana kati ya kidole gumba cha mkono na kidole kidogo cha mkono (upana)
4. Urefu kati ya vidole vinne vya mkono uliokunjwa

Dhiraa (BDB 52, KB 61) kilikuwa sio kipimo kamili, bali palikuwepo na vipimo viwili vya msingi.

a. Toka kiwiko cha mwanaume wa kawaida na kidole cha kati (yapata inchi 18, kama vile Kumb. 3:11)
b. Dhiraa ya kifalme kiwastani ilikuea ndefu (yapata inchi 21, kama vile II Nya. 3:3; Ezek. 40:5; 43:13)

**6:16 "uifanyie safina mwangaza"** Hili sio neno lile lile kwa ajili ya dirisha lililotumika Mwanzo 8:6. Wengi wadhani ya kuwa lilirejelea kwenye mwanga na muundo wa vitundu vya kupitisha hewa sehemu ya juu kuizunguka safina,sehemu ya chini ya paa.

**6:17 "gharika"** Pamekuwepo na baadhi ya mitazamo kuwa neno hili (BDB 550) linahusiana na neno la ki-Ashuru "kuangamiza." Yale mafuriko ya Nuhu yalikuwa ni ya kidunia au ni sehemu ya Mashriki ya kale? Neno "dunia" (*eres*) mara nyingi limetafasiliwa "nchi" kwa maana ya kawaida (kama vile Mwa. 41:57). Kama wanadamu wasingetawanyika sehemu zote za nchi ambacho kwa uhakika kinadokezwa kwenye mnara wa Babeli kwenye kifungu cha 10-11, hivyo gharika la mahala hapo lingalifanya kitu. Kitabu kizuri nilichokwisha soma juu ya ushuhuda wa kawaida kwa ajili ya gharika la mahala ni cha Bernard Ramm's *The Christian View of Science and Scripture.*

◙ **"pumzi ya uhai"** Hili ni neno la Kiebrania *ruach*. Laweza kutumika kwenye upepo, uzima, uhai, au roho. Wote

binadamu na wanyama wanasemekana kuwa na *nephesh* lakini mwanadamu tu ndiye ameumbwa kwa sura ya Mungu (kama vile 1:26-27) na ana uumbaji wa “kipekee”(kama vile 2:7). Katika muktadha huu viumbe vyote venye uhai–hufa (kama vile 7:22, wanyama na binadamu)!

**6:18**
**NASB, NKJV,**
**NRSV “nitaweka”**
**TEV “nitafanya”**
**NET “nitalithibitisha”**

KITENZI (BDB 877, KB 1086, *Hiphil* KAULI TIMILIFU) maana yake ya msingi ni “kuinuka”au “kusimama.” shina la neno *Hiphil* linatumika “kuweka,””thibitisha” (kama vile 6:18; 9:9,11,17; 17:7,19,21; Kut. 6:4; Ezek. 16:62). Haijulikani ni kwa ahadi au agano lipi linalorejelewa. Huenda ni kulitabiria andiko la 9:9,11,17. Jibu ni kuwa Mungu mwenyewe ndiye atathibitisha na kuendeleza ahadi zake kwa mwanadamu aliye anguka, mwenye kuasi. Hata katikati ya uovu wake bado mpango wa Mungu wa milele kuhusu ushirika naye unadumu!

◙ **“Agano langu nawe”** Huu ni utmiaji wa kwanza wa neno hili *berith* (BDB 136). Limeeloezewa na kufanywa vizuri zaidi katika Mwa. 9:8-17. Linaunda kiini cha uelewa wa wazo kati ya Agano la Kale na Agano Jipya cha uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu. Kuna majukumu, uwajibikaji, na ahadi za kirafiki kwa pande zote mbili. Hili linaweka hatua kwa ajili ya uelewa wetu wa mivutano ya kipembuzi kati ya maagano yasiyo na masharti juu ya upande wa Mungu, lakini bado kuna dhana ya masharti juu ya wajibu wa mwanadamu kwa kila moja.

## MADA MAALUM: AGANO

Neno la Agano la Kale *berith* (BDB 136, KB 157), "Agano," sio rahisi kulielezea. Hakuna KITENZI kinachoshabihiana katika Kiebrania. Yote yanajaribu kupata ile asili ya neno au maana inayofanana inayodhihirisha kutoleta ushawishi. Yumkini ubashiri mzuri ni “kukata/kuchinja”(BDB 144) ikimaanisha sadaka ya mnyama inayojumuishwa kwenye agano(kama vile Mwa. 156:10,17). Hata hivyo, kiini dhahiri cha dhana yenyewe kimetizamishwa kwa wasomi kuchunguza matumizi ya kidunia katika jaribio la kupima maana yake ya kiutendaji.

Agano ni namna ambayo Mungu wa kweli (angalia Mada Maalum: Uwepo wa Mungu Mmoja) anavyoshughulika na uumbaji wake wa Mwanadamu. Dhana ya Agano, mkataba, au makubaliano ni ya muhimu katika kuuelewa ufunuo wa Mungu. Mvutano kati ya Ukuu wa Mungu na mapenzi huru ya mwanadamu kwa wazi unaonekana katika dhana ya Agano. Baadhi ya maagano yanaegamia moja kwa moja juu ya tabia ya Mungu na matendo.

1. Uumbaji wenyewe (kama vile Mwanzo 1-2)
2. Utunzaji na ahadi ya Nuhu (kama vile Mwanzo 6-9)
3. Wito wa Abrahamu (kama vile Mwanzo 12)
4. Agano pamoja na Abrahamu (kama vile Mwanzo 15)

Hata hivyo, ile asili ya Agano inahitaji mwitikio.

1. Kwa imani Adamu anapaswa kumtii Mungu na kutokula lile tunda la mti wa katikati ya Edeni
2. Kwa imani Nuhu anapaswa kutengeneza safina mbali na maji na kuwakusanya wanyama wote
3. Kwa imani Abraham anapaswa kuiacha familia yake, na kumfuata Mungu, na kuamini katika kizazi kijacho
4. Kwa imani Musa anawatoa wana wa Israel toka Misri kwenda Mlima Sinai na kupokea maagizo maalum kwa ajili ya maisha ya kidini na kijamii yakiwa na ahadi ya Baraka na laana ( kama vile Walawi 26, Kumbu kumbu la Torati 27-28)

Mvutano ule ule unaohusiana na ushirika wa Mungu kwa mwanadamu unaelezewa katika “agano jipya” (kama vile. Yer. 31:31-34; Ebr. 7:22; 8:6,8,13; 9:15; 12:24). Mvutano kwa wazi unaweza kuonekana katika kulinganisha Ezek. 18:31 na Ezek. 36:27-38 (tendo la YHWH). Je agano linasimamia juu ya matendo ya neema ya Mungu au mamlaka ya mwitikio wa mwanadamu? Hili ni suala mtambuka kati ya Agano la Kale na Agano Jipya. Lengo la yote ni sawa:

1. Urejesho wa ushirika na YHWH uliopotea katika Mwanzo 3 N
2. Uimalishaji wa watu wa haki ambao wanaaksi tabia ya Mungu

Agano jipya la Yer. 31:31-34 linatatua mvutano kwa kuondoa utendaji wa kibinadamu kwa maana ya kupata ukubarifu. Sheria za Mungu zikaja kuwa shauku ya ndani badala ya sheria ya nje. Lengo la ki-Mungu, watu wenye haki linabaki vile vile, lakini njia zinabadilika. Wanadamu waliyoanguka wanathibitisha wao wenyewe pasipo utosherevu kwa kuaksi taswira ya Mungu. Tatizo halikuwa agano la Mungu, bali ni udhaifu na dhambi za mwanadamu (kama vile Mwanzo 3; Warumi 7; Wagalatia 3).

Mvutano wa aina ile ile kati ya maagano ya Agano la Kale yasiyo na masharti na yenye masharti yanabaki katika Agano Jipya. Wokovu ni wa bure katika kazi aliyokwisha kuimaliza Yesu Kristo, lakini unahitaji toba na imani (mwanzoni na kuendelea, angalia Mada Maalum: Kuamini katika Agano Jipya). Yesu anaita ushirika wake mpya na waamini "agano jpya" (kama vile Mt. 26:28; Marko 14:24; Lk 22:20; 1 Kor. 11:25). Yote ni matamko ya kisheria (ya kimahakama) na wito wa kumfanana na Kristo (kama vile Mt. 5:48; Rum. 8:29-30; 2 Kor. 3:18; 7:1; Gal. 4:19; Efe. 1:4; 4:13; 1 The. 3:13; 4:3,7; 5:23; 1 Pet. 1:15), maelezo elekezi ya ukubalifu (Warumi 4) wito wa ushurutishi wa kuwa mtakatifu (kama vile Mt. 5:48)! Waamini hawaokolewi kwa utendaji kazi wao, lakini ni katika utii (kama vile (kama vile Efe. 2:8-10;). Maisha ya ki-Mungu yamekuwa ni ushuhuda wa wokovu, na sio namna ya wokovu (yaani., Yakobo na Yohana. Hata hivyo, maisha ya milele yana tabia zinazochunguzika! Mvutano huu unaonekana kwa wazi kwa katika Agano Jipya (angalia Mada Maalum: Uasi).

◙ **"nawe utaingia katika safina, wewe, na wanao, na mkeo, na wake za wanao, pamoja nawe "** Nuhu pasipo hatia alipanua familia yake (kama vile I Kor. 7:14).

**6:19 "utawaleta"** Hili laweza kudokeza kuwa wanyama (ikiwa ni wa mahali husika au dunia nzima haijulikani) wakaja kwa Nuhu, lakini Nuhu akawaweka ndani ya safina. Yumkini alilifanya hili hata kabla ya wiki ya mwisho. Ni namna gani wanyama waliishi pamoja na kula ndani ya safina ni fumbo, lakini haliondoi uwezekano wa muundo wa kawaida au muundo usio wa kawaida.

**6:21** Palikuwemo na chakula ndani ya safina ya Nuhu na wanyama kwa pamoja (BDB 542, KB 534, *Qal* KAULI SHURUTISHI). Hata hivyo, maelezo hayakuwekewa kumbukumbu. Habari yenyewe ni ya kithiolojia zaidi ya maelezo.

**6:22 "Hivyo Nuhu akafanya"** Dhamira kuu ni kuwa Nuhu alimtii Mungu (kama vile 7:5,9,16), ambapo ndio wajibu uliostahili, hata hivyo, Adamu na Hawa na binadamu waliobaki hawakutii (mf. 6:5,11-12,13).

# MWANZO 7

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Gharika | Gharika Kuu | Gharika Kuu<br>(6:5-8:22) | Gharika | Maandalizi ya Gharika<br>(6:13-7:16) |
| 7:1-5 | 7:1-5 | 7:1-5 | 7:1-5 | 7:1-5 |
| 7:6 -12 | | 7:6-10 | 7:6-10 | 7:6 |
| | | | | 7:7-10 |
| | | 7:11-16 | 7:11-16 | 7:11-12 |
| 7:13-16 | 7:13-16 | | | 7:13-16a |
| | | | | 7:16b |
| 7:17-24 | 7:17-24 | 7:17-24 | 7:17-24 | 7:17-24 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (Angalia ukurasa wa vii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

13. Aya ya kwanza
14. Aya ya pili
15. Aya tatu
16. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7:1-5**
**1 Bwana akamwambia Nuhu, Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina; kwa maana nimekuona wewe u**
**mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki. 2 Katika wanyama wote walio safi ujitwalie saba saba, mume na**
**mke; na katika wanyama wasio safi wawili wawili, mume na mke. 3 Tena katika ndege wa angani saba saba,**
**mume na mke; ili kuhifadhi hai mbegu juu ya uso wa nchi yote. 4 Kwa maana baada ya siku saba nitainyeshea**
**dunia mvua, siku arobaini mchana na usiku; na kila kilicho hai nilichokifanya juu ya uso wa nchi nitakifutilia**
**mbali. 5 Nuhu akafanya kama vile Bwana alivyomwamuru.**

**7:1 "Bwana akamwambia Nuhu"** Jina la Mungu la agano, YHWH, liko hapa lakini katika mstari wa 16 Yeye anaitwa *Elohim*. Uelewa wa walimu wa kisheria kuhusiana na maneno haya yanayomrejelea Mungu kama mwokozi (YHWH) na kama Muumbji (*Elohim*) yanaonekana kukidhi matumizi ya Torati. Tazama Mada Maalum: Majina ya Uungu katika 2:4.

◙**"Ingia wewe na jamaa yako yote katika safina "** Hiki KITENZI (BDB 92, KB 112) ni *Qal* CHENYE MASHARTI.

◙**" kwa maana nimekuona wewe u mwenye haki mbele zangu katika kizazi hiki"** Hili neno "mwenye haki" hapa linatumika katika maana hiyo hiyo kama linavyorejelea katika Ayubu kuhusu neno "isiyo na mawaa" (kama vile 6:9). Hili halimaanishi kutokuwa na dhambi bali mtu aliyetii na kutenda yale yote ambayo anayalewa au yale ambayo kidesturi yanamhusu Mungu. Tambaua kwamba Nuhu kuwa mwenye haki iliiathiri familia yake. Hii ni kweli ya kibiblia. Hili halimaanishi kwamba mtu anaweza kuwa na haki kwa Mungu kwa kujikita katika manufaa ya mtu mwingine, bali hili linamaanisha kwamba baraka za kiroho huwafuata wale waliopashwa habari na wale walio karibu nao (linganisha Kut. 5:9-10; 7:9 na I Kor. 7:14).

**7:2 "wanyama wote walio safi ujitwalie saba saba, mume na mke"** Tambaua tofauti kati ya walio safi na wasio safi katika muktadha huu kwa sababu hili liko katika utaratibu wa utoaji wa dhabihu nyakati za Musa (kama vile Law. 1-7). Hakuna kinachozungumziwa kuhusu kigezo ama sababu ya wanyama walio safi. Nidhahiri kwamba Musa alilifafanua hili baadaye katika Mambo ya Walawi (kama vile sura ya 11) katika uhusiano wa sheria za vyakula na mfumo wa utoaji dhabihu. Kumekuwa na mjadala mwingi kuhusu saba saba (kama vile NRSV, NJB, JPSOA). Je! hili linamaanisha saba kwa kila mnyama au makundi saba saba ya wanyama?

**7:4 "baada ya siku saba nitainyeshea dunia mvua"** Rashi anasema kwamba hiki kilikuwa kipindi cha huzuni kwa mwenye haki Methusela ambaye alikuwa tayari amekwisha kufa. Walimu wa Kiyunani waliamini kwamba Mungu hakutuma mafuriko hadi Methusela alipokufa. Siku ya saba ya juma ni ya kale sana.

Siku ya saba ya juma ni ya kale sana kwamba asili yake haikuelezwa kamwe. Mwezi na mwaka vyote vinaweza kudhahaniwa kutoka katika vifungu vya mwezi na mabadiliko ya majira, lakini si juma. Kwa waamini kitabu cha Mwanzo 1 kinaweka utaratibu.

◙**"siku arobaini mchana na usiku"**Hili neno "arobaini" linatumika mara kadhaa katika Biblia (tazama itifaki). Kwa kipindi fulani hili lilimaanisha kuchukuliwa kwa uhalisia ambapo kwa wakati mwingine lilimaanisha kipindi kirefu kisicho na mwisho (kirefu kuliko mzunguko wa mwezi ambao ni siku ishirini na nane na nusu, lakini kirefu kuliko mabadiliko ya majira). Katika maelezo mbalimbali ya ki-Mesopotamia mpangilio wa wakati wa maji ya gharika ni siku saba.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7: 6-12**

**6 Naye Nuhu alikuwa mtu wa miaka mia sita hapo hiyo gharika ya maji ilipokuwa juu ya nchi. 7 Nuhu akaingia katika safina, yeye, na wanawe, na mkewe, na wake za wanawe pamoja naye; kwa sababu ya maji ya gharika.**
**8 Na katika wanyama walio safi, na wanyama wasio safi, na ndege, navyo vyote vitambaavyo juu ya nchi, 9**
**wakaingia katika safina alimo Nuhu, wawili wawili, mume na mke, kama vile Mungu alivyomwamuru Nuhu. 10**
**Ikawa baada ya siku hizo saba, maji ya gharika yakawa juu ya nchi. 11 Katika mwaka wa mia sita wa maisha ya Nuhu, mwezi wa pili, siku ya kumi na saba ya mwezi, siku ile chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka. 12 Mvua ikanyesha juu ya nchi, siku arobaini mchana na usiku.**

**7:11 "chemchemi zote za vilindi vikuu zilibubujika kwa nguvu, madirisha ya mbinguni yakafunguka"** Upangaji wa tarehe wa mstari wa 11 ni wa kipekee sana katika mstari huu (ambao unamaanisha tukio la kihistoria) pamoja na vitenzi ambavyo vinaeleza juu ya majanga ya asili ambayo yanatokea juu ya nchi ( *Niphal mbili* TIMLIFU, BDB 131, KB 149 na BDB 834, KB 986). Tunaweza kuona kipimo cha uharibifu katika mst. 18 na 19 katika andiko la Kiebrania. Tabia nyingi za mwonekano wa dunia zimekuwa zikibadulika hasa katika mashariki ya karibu. Kuna

vyanzo viwili vya maji: (1) chemichemi zenye kina na (2) kingo za gharika/mafuriko (yaani milango, kama vile Zab. 78:23 na kuendelea; Mal. 3:10) ya mbingu. Huu ni mrejeo halisi wa kile alichokifanya Mungu katika Mwa. 1. kujirudia kwa machafuko ya maji.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7: 13-16**
**[13] Siku ile ile Nuhu akaingia katika safina, yeye, na Shemu na Hamu na Yafethi, wana wa Nuhu, na mkewe Nuhu, na wake watatu wa wanawe pamoja naye; [14] wao na kila mnyama wa mwitu kwa jinsi yake, na kila mnyama wa kufugwa kwa jinsi yake, na kila kitambaacho, chenye kutambaa juu ya nchi, kwa jinsi yake, na kirukacho kwa jinsi yake, kila ndege wa namna yo yote. [15] Waliingia katika safina alimo Nuhu, wawili wawili, wa kila chenye mwili kilicho na pumzi ya uhai ndani yake.[16] Na walioingia, waliingia mume na mke, wa kila kitu chenye mwili, kama vile alivyomwamuru Mungu; Bwana akamfungia.**

**7:14** Hii inahitimisha makundi yote ya wanyama wa nchi kavu waliotajwa katika Mwa. 1 wenye bila kuwemo wale waishio baharini.

**7:16 "Bwana akamfungia "** YHWH (yaani agano, Uungu wa Mwokozi) alifunga milango Mwenyewe. Walimu wa Kiyunani wanasema kwamba Yeye alilifanya hili ili kuwaweka wadharimu mbali na safina. Pia hawa wamekwenda mbali na kudai kwamba Mungu aliizingira safina kwa simba na dubu ili kuwafanya watu wa nje wakae mbali. Kwangu mimi, safina ni huruma ya YHWH kwa mwanadamu ili kuendelea na mtiririko wa ki-Masihi, hata katikati ya hukumu, ambayo hatimaye huleta ukombozi (kama vile Mwa. 3:15).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 7:17-24**
**[17] Ile gharika ilikuwako juu ya nchi siku arobaini; nayo maji yakazidi, yakaieleza safina, ikaelea juu ya nchi. [18] Maji yakapata nguvu, yakazidi sana juu ya nchi; na ile safina ikaelea juu ya uso wa maji. [19] Maji yakapata nguvu sana sana juu ya nchi; na milima mirefu yote iliyokuwako chini ya mbingu ikafunikizwa.[20] Maji yakapata nguvu, hata ikafunikwa milima kiasi cha mikono kumi na mitano. [21] Wakafa wote wenye mwili waendao juu ya nchi, na ndege, na wanyama wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu, na kila kitambaacho chenye kutambaa juu ya nchi, na kila mwanadamu; [22] kila kitu chenye pumzi ya roho ya uhai puani mwake kikafa, kila kilichokuwako katika nchi kavu. [23] Kila kilicho hai juu ya uso wa nchi kikafutiliwa mbali tangu mwanadamu hata mnyama wa kufugwa, na kitambaacho, na ndege wa angani; vilifutiliwa mbali katika nchi, akabaki Nuhu tu, na hao walio pamoja naye katika safina. [24] Maji yakapata nguvu juu ya nchi siku mia na hamsini.**

**7:19** Lugha ya mstari huu kwa hakika inadokeza gharika ya ulimwengu mzima (kama vile 8:21; II Pet. 3:6). Je! Hivi ndivyo? Hili neno "nchi" (*eres*, BDB 75) linaweza kumaanisha "ardhi" (kama vile 41:57).Hii inaweza kuwa nahau sawa sawa na Luka 2:1 na Kol. 1:23 (kama vile *Hard Sayings of the Bible*, IVP kr. 112-114). Kama ilivyo kwa thiolojia ihusuyo gharika, kiwango / kipimo chake hakihusiani**.** Hakuna mkusanyiko wa gharika/mafuriko ya kudumu hata katika Mesopotamia kwa sababu ya kuingia kwa mito miwili mikubwa ambayo inaungana katika mikondo yake. Kwa mjadala ulio mzuri, tazama Bernard Ramm, *The Christian's View of Science and Scripture.*

**7:22 "chenye pumzi ya roho ya uhai"** (kama vile maelezo yaliyo katika 1:30). Wale walioshi majini walitunzwa kwa usalama.

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini uelewa wako kuhusu kifungu "wana wa Mungu" ni kwa nini?

2. Unafikifri ni kwa nini malaika walikuwa na tamaa juu ya mabinti wa wanadanu?
3. Je! Wanefili walikuwa akina nani?
4. Ni kwa namna gani Mungu angeweza kutubu?
5. Je! kutembea na Mungu kunamaanisha nini?
6. Kwa nini samaki hawakuhukumiwa pamoja na wanyama wa mwituni?
7. Katika utaratibu wa Nuhu, ni mnyama gani aliye safi na asiye safi?
8. Je! gharika lilikuwa la mahali au la kiulimwengu? Kwa nini

# MWANZO 8:1-22

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Kupungua kwa Gharika | ukombozi wa Nuhu | Gharika Kuu (6:5-8:22) | Mwisho wa gharika | kupungua kwa gharika |
| 8:1-5 | 8:1-5 | 8:1-5 | 8:1-5 | 8:1-5 |
| 8:6-12 | 8:6-12 | 8:6-12 | 8:6-12 | 8:6-12 |
| 8:13-19 | 8:13-14 | 8:13-19 | 8:13-14 | 8:13 |
| | | | | 8:14 |
| | | | | Wanatoka |
| | 8:15-19 | | 8:15-19 | 8:15-19 |
| | Agano la Mungu Pamoja na uumbaji (8:20-9:17) | | Nuhu anatoa Sadaka | |
| 8:20-22 | 8:20-22 | 8:20-22 | 8:20-22 | 8:20-22 |
| (22) | (22) | (22) | (22) | (22) |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa vii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

17. Aya ya kwanza
18. Aya ya pili
19. Aya tatu
20. N.k

## UTAMBUZI WA KIMUKTADHA

A. Kuna usambamba wa wazi kati ya Mwanzo 1 na Mwanzo 7 katika namna ya kurudi kwa machafuko ya maji.
B. Kuna usambamba wa wazi kati ya Mwanzo 1 na Mwanzo 8 katika Mungu kurejesha kurudisha ardhi inayohimili uhai
   1. linganisha 1:2 pamoja na 8:1

2. Linganisha 1:6-7 pamoja na 8:2
3. Linganisha 1:22, 24 pamoja na 8:17
4. Linganisha 1:28 pamoja na 9:1-2

C. Mwanzo 8:1-19 ni upinduaji wa 7:11-24. Hii hakika ni kutengeneza muundo wa kifasihi.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:1-5**
**[1] Na Mungu akamkumbuka Nuhu, na kila kilicho hai, na wanyama wote waliokuwamo pamoja naye katika safina; Mungu akavumisha upepo juu ya nchi, maji yakapungua; [2] chemchemi za vilindi zikafungwa, pia na madirisha ya mbinguni, mvua kutoka mbinguni ikazuiliwa; [3] maji yakadumu kuondoka katika nchi; na mwisho wa siku mia na hamsini maji yakapunguka. [4] Mwezi wa saba, siku ya kumi na saba ya mwezi, safina ikatua juu ya milima ya Ararati. [5] Maji yakapunguka-punguka hata mwezi wa kumi; mwezi huo wa kumi, siku ya kwanza ya mwezi, vilele vya milima vikaonekana.**

**8:1 "Mungu"** Hili ni neno *Elohim*. Angalia dokezo katika Mwanzo. 1:1 au Mada maalum katika 2:4.

◙**"akamkumbuka"** Neno hili (BDB 269, KB 269, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) linatumika kwa namna ya kuchukua maaamuzi sahihi na ya binafsi juu ya mtu (kama vile 8:1; 9:15; 16; 19:29; 30:22). Agano la Mungu ni kuhusu kufanya kitendo tena kwasababu ya vile alivyo. Nuhu atakuwa chanzo cha ubinadamu mpya.

◙**"Nuhu"** Jina hili (BDB 629) linaweza kumaanisha "pumziko," asili maarufu iliyojikita kwenye sauti na sio muundo na historia ya ukuaji wa lugha.

◙**" Mungu akavumisha upepo"** KITENZI (BDB 716, KB 778) ni *Hiphal* KAULI ISIO TIMILIFU. Mungu alitumia njia ya asili kwa ajili ya maji yaliyojaa kupungua, mstari wa 2, kama alivyofanya katika Kutoka (kama vile Kut. 14:21). Pia inawezekana kuona matendo ya Mungu katika Sura ya 8-9 kama usambamba wa matendo ya Mungu katika sura ya 1. Huu ni mwanzo wa binadamu. Ikiwa hivyo, upepo hapa una usambamba "Roho ilikuwa ikitulia juu" ya 1:2.

◙**" maji yakapungua"** Neno hili hili (BDB 1013, KB 1491, *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU) linatumika kwa hasira ya Mfalme katika Esta 2:1.

**8:4 "juu ya milima ya Ararati"** Hii imeeleaewa katika namna tatu: (1) Mlima katika mipaka ya Uturuki/Urusi; (2) mlima kaskazini karibu na Ziwa Van; na (3) Neno lenyewe linamaanisha uwanja wa mlima mzima (Ashuru *urartu*, BDB 76), sio kusema hasa kilele (chunga wingi "milima").

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA ) 8:6-12**
**[6] Ikawa baada ya siku arobaini, Nuhu akalifungua dirisha la safina, alilolifanya; [7] akatoa kunguru, naye akatoka akaenda huko na huko, hata maji yakakauka juu ya nchi. [8] Kisha akatoa njiwa, aone kwamba maji yamepunguka usoni pa nchi; [9] bali yule njiwa hakuona mahali pa kutua kwa wayo wa mguu wake, akamrudia Nuhu safinani, maana maji yalikuwa juu ya uso wa nchi yote; naye akanyosha mkono, akamtwaa, akamwingiza mle safinani. [10] Akangoja na siku saba tena; kisha akamtoa yule njiwa katika safina mara ya pili, [11] njiwa akamjia jioni, na tazama, alikuwa na jani bichi la mzeituni kinywani mwake, ambalo amelitunda, basi Nuhu akajua ya kwamba maji yamepunguka juu ya nchi. [12] Akangoja na siku saba tena, akamtoa yule njiwa; naye asimrudie tena kamwe.**

**8:6 "siku arobaini "** Tungo hii huwa inamaanisha "kipindi kirefu kisichojulikana kwa urefu wake." Katika muktadha huu, tarehe ziko bayana na yaweza kumaanisha siku arobaini haswa.

◙ **"dirisha"** Hili ni neno tofauti (BDB 319) ukilinganisha na maneno tata ya 6:16 (kidhahiri "paa," BDB 844I). Kipimo chake na mahali lilipokuwa haijulikani lakini yawezekana katika paa lenyewe.

**8:6-12** Kuwa mwangalifu usije kusitiari ndege hawa! Kuna usambamba sawia katika fasihi ya Mesopotamia (yaani Gilgamesh Epic 11:145-55), ambayo inaonekana kibayana sana kuwa utukizi/upatanifu. Hii ni uhusiano wa

kidhahiri kati ya Biblia (yaani Mwanzo 1-11) na fasihi ya Mesopotamia.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:13-19**
**1[3] Ikawa mwaka wa mia sita na moja, mwezi wa kwanza, siku ya kwanza ya mwezi, maji yalikauka juu ya nchi. Nuhu akaondoa kifuniko cha safina, naye akaona, na tazama, uso wa nchi umekauka. [14] Na mwezi wa pili, siku ya ishirini na saba ya mwezi, nchi ilikuwa kavu. [15] Mungu akamwambia Nuhu, akisema, [16] Toka katika safina, wewe, na mkeo, na wanao, na wake za wanao pamoja nawe. [17] Utoe pamoja nawe kila kilicho hai kilichomo pamoja nawe, chenye mwili, ndege, na mnyama, na kila kitambaacho, chenye kutambaa juu ya nchi; wajae katika nchi, wawe na uzazi, wakaongezeke katika nchi. [18] Basi Nuhu akatoka, yeye, na wanawe, na mkewe, na wake za wanawe pamoja naye; [19] kila mnyama, na kila kitambaacho, na kila ndege, kila kinachokwenda juu ya nchi kwa kabila zao, wakatoka katika safina.**

**8: 13 "Nuhu akaondoa kifuniko"** Hii inaonekana kumaanisha kuondoa sehemu ya paa (BDB 492). Ingawa neno hili hili baadaye litamaanisha ngozi ya mnyama inayofunika hema, ni ngumu kukubaliana na hiyo maana.

**8:15 "Mungu akamwambia Nuhu"** Muktadha mzima unafunua uvumulivu na utii wa Nuhu. Sheria na amri za Mungu (yaani 8:15-19) sambamba na 7:1-5.

**8:16 "Nenda nje"** Hii ni amri ya kwanza kati ya mistari kadhaa ya 16-17.

1. "nenda nje," *Qal* KAULI SHURUTISHI (BDB 422, KB 425), mstari wa 16
2. "leta nje," *Hiphil* KAULI SHURUTISHI (BDB 422, KB 425), mstari wa 17
3. "kuzaa kwa wingi," *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU iliyotumika kama namna ya KAULI SHURUTISHI (BDB 1056, KB 1655), mstari wa 17
4. "zaa matunda," *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU limetumika katika namna ya KAULI ULIOTIMILIFU (kama vile 9:1,7 BDB 826, KB 953), mstari wa 17
5. "ongezeka," *Qal* KAULI ISIO TIMILIFU inayotumika katika namna ya KAULI SHURUTISHI (kama vile 9:1,7 BDB 915, KB 1176), v. 17

Amri hizi zina usambamba kwa Mwanzo. 1:22,24. Katika namna ambayo Mungu anaanza upya. Maji ya machafuko yaliharibu ardhi yote isipokuwa kile kilichokuwa katika safina. Mpango na kusudi la asili la Mungu liliendelea (kama vile 6:18).

**8:17** Hizi amri za Mungu (pia 9:1) ni sambamba na Mwanzo 1:22,24. Angalia tambuzi za Kimutadha katika sura hii.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 8:20-22**
**[20] Nuhu akamjengea Bwana madhabahu; akatwaa katika kila mnyama aliye safi, na katika kila ndege aliye safi, akavitoa sadaka za kuteketezwa juu ya madhabahu. [21] Bwana akasikia harufu ya kumridhisha; Bwana akasema moyoni, Sitailaani nchi tena baada ya hayo kwa sababu ya wanadamu, maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake; wala sitapiga tena baada ya hayo kila kilicho hai kama nilivyofanya. [22] Muda nchi idumupo, majira ya kupanda, na mavuno, wakati wa baridi na wakati wa hari, wakati wa kaskazi na wakati wa kusi, mchana na usiku, havitakoma.**

**8:20 "Nuhu akamjengea Bwana madhabahu"** Tendo lake la kwanza lilikuwa ni shukrani ya kuabudu. Dhabihu ni taasisi ya Kale (kama vile 4:3; 12:7,8; 13:18; 22:19). Hili pia ni tendo la kwanza la Gilgamesh katika Masimulizi ya Gilgamesh baada ya gharika (kama vile 11:156-158).

◙**"kila mnyama aliye safi"** Kigezo kilichotumika kung'amua msafi na mchafu hakijulikani (kama vile 7:2), lakini kidhahiri ilikuwa ikihusiana na dhabihu, sio mwongozo wa kichakula (kama vile Lawi. 11; Kumb. 14).

**8:21"Bwana akasikia harufu ya kumridhisha"** Tungo hii inatumika katika Biblia katika namna ya Mungu kukubali sadaka (hasa kitabu cha Walawi na Hesabu.) Haimaanisha kwamba nyama ilikuwa chakula kwa ajili ya Mungu kama ilivyoandikwa katika Masimulizi ya Gilgamesh (kama vile 11:159-161). Biblia haijawahi kuangalia mfumo wa kidhabihu kama chakula cha watu wa kiungu kama mataifa yaliyozunguka yalivyofanya.

◙ **"Sitailaani nchi tena. . wala sitapiga tena baada ya hayo kila kilicho hai"** Hizi kauli za usambamba zinaonesha mvutano katika moyo wa Mungu (kama vile Isa. 54:9) kwa uumbaji wake na haki yake. Mwanadamu ni muovu na mharibifu lakini Mungu amechagua kufanya kazi pamoja na sisi kwa muda na kunyoosha mambo ya matukio ya siku za mwisho (yaani siku za mwisho). Katika hukumu hii mtazamo wa Mungu kuhusu asili ya dhambi ya mwanadamu inabadilishwa. Wanadamu bado ni waovu. Mtazamo wa kimungu utabadilika tena wakati watu wake hawakuwa na uwezo wa kufanyia kazi agano la Musa. Mungu ataweka taasisi ya Agano jipya (kama vile Yer. 31:31-34 na Ezek. 36:27-38). Wanadamu watapatanishwa na Mungu kupitia kufanyika kwa Kimasihi na kifo cha kidhabihu. Ingawa ni kweli kwamba Mungu hajahaidi kutuma gharika lingine, II Pet. 3:10 anaelezea kwamba atasafisha dunia kwa moto. Mungu atafanya kazi na mwanadamu mwenye asili ya dhambi lakini lengo lake likiwa ni haki (kama vile Walawi 19:2; Mt. 5:48).

◙ **"maana mawazo ya moyo wa mwanadamu ni mabaya tangu ujana wake"** Uovu ulikuwa wazi sana kabla ya gharika (kama vile 6:5,11,12,13) na bado upo katika mwanadamu aliyeanguka, kama Nuhu na familia yake itaonesha kwa uwazi!

**8:22** Ni huku kuendelea kwa asili ambako kumetoa kukua kwa sayansi ya Magharibu. Mungu alianzisha hali ya mfumo wa kufanana (yaani shughuli zinazoeleweka na za kufanana za asili). Hata hivyo tazama tungo ya mwanzo "kadiri nchi idumupo." Mstari wa 22 umechapishwa katika fasiri za Kingereza katika kifungu cha ushairi.

# MWANZO 9

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Agano la Upinde wa Mvua | Agano la Mungu juu ya Uumbaji<br><br>(8:20-9:17) | Agano la Mungu juu ya Nuhu | Agano la Mungu juu ya Nuhu | Mpangilio wa Ulimwengu Mpya |
| 9:1-7 | 9:17 | 9:1-7 | 9:16 | 9:1-7 |
| (6-7) | (6-7) | (6) | 9:7 | (6) |
| 9:8-17 | 9:8-17 | 9:8-17 | 9:8-17 | 9:8-11 |
| | | | | 9: 12-16 |
| | | | | 9:17 |
| | Nuhu na Wanae | Laana ya Nuhu Juu ya Kaanani | Nuhu na Wanae | Nuhu na Wanae |
| 9:18-19 | 9:18-19 | 9:18-19 | 9:18-19 | 9:18-19 |
| 9:20-27 | 9:20-23 | 9:20-27 | 9:20-27 | 9:20-27 |
| (25-27) | 9:24-27 | ( 25-27) | (25-27) | (25:27) |
| 9:28-29 | 9:28-29 | 9:28-29 | 9:28-29 | 9:28-29 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa vii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni mwongozo kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

21. Aya ya kwanza
22. Aya ya pili
23. Aya tatu
24. N.k

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 9:1-7**
**[1]Mungu akambariki Nuhu na wanawe, akawaambia, Zaeni, mkaongezeke, mkaijaze nchi. [2] Kila mnyama wa katika nchi atawaogopa ninyi na atawaogopa, na kila ndege wa angani: pamoja na vitu vyote vilivyojaa katika**

**ardhi, na samaki wote wa baharini; vimetiwa mikononi mwenu. [3]Kila kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula chenu, kama nilivyowapa mboga za majani, kadhalika nawapeni hivi vyote. [4]Bali nyama pamoja na uhai, yaani, damu yake, msile. [5]Hakika damu yenu ya uhai wenu nitaitaka; na kwa mkono wa kila mnyama nitaitaka; na kwa mkono wa mwanadamu, kwa mkono wa ndugu ya mtu nitataka uhai wa mwanadamu. [6]Atakayemwaga damu ya mwanadamu, damu yake huyo itamwagwa na mwanadamu, maana kwa mfano wake Mungu alimfanya mwanadamu. [7] Nanyi zaeni, mkaongezeke; zaeni sana katika nchi, mkaongezeke ndani yake.**

**9:1"mkaongezeke, mkaijaze nchi**" Tambaua *Qal* KAULI YENYE MASHARTI: "zaeni" (BDB 826, KB 963), "mkaongezeke" (BDB 915,KB 583). Huu ni uanzilishi wa mara ya pili kwa mwanadamu (kama vile 1: 28), lakini tambua ya kwamba dhambi imesababisha mabadiliko katika amri, amri ya "tiisheni na kutawala" inawekwa kando.

**9:2**"**atawaogopa**. . . **atawaogopa**" Mwanadamu alikuwa na uhusiano na wanyama, si kama ile amani na uhusiano ulivyokuwa ndani ya Edeni katika matukio ya siku ya mwisho (Isaya 11), lakini kuogopa (BDB432) na kuogopa (BDB 369). Agano la Kale la Kiebrania linaongeza neno "kundi la wanyama" katika mstari, lakini wanyama wafugwao hawakukumbwa na maafa haya.

**9:3"Kila kiendacho kilicho hai kitakuwa chakula chenu**" Kiuhalisia mwanadamu alikuwa mwenye kula mboga za kondeni tu (hasa katika bustani ya Edeni) tangu kutokea kwa anguko kwa muda mrefu hakuna mazao yaliyokuwa yakizalishwa, nyama ndiyo iliyokuwa ikipatikana. Pia tambua kwamba hapakuwa na tofauti kati ya wanyama safi na wasio safi kama ulaji ulivyokuwa (hili ni tofauti sana na Law. 11), lakini kulikuwa na tofauti katika utoaji dhabihu (kama vile 7: na kuendelea).

**9:4** "**Bali nyama pamoja na uhai, yaani, damu yake, msile**" Huu ni msingi wa kithiolojia wa mfumo wa utoaji dhabihu (kama vile Lav. 17:10-16; Kumb. 12:16,23; Matendo ya Mitume 15:29) na umuhimu wa kifo cha Kristo. Dhambi ni gharama za kimaisha. Kwa huruma Mungu alimtoa mnyama wa milele.

**9:5-6 "kwa mkono wa ndugu ya mtu nitataka uhai wa mwanadamu.** [6] **Atakayemwaga damu ya mwanadamu, damu yake huyo itamwagwa**" Huu ndiyo usemi wa kwanza wa ufanano wa "jicho kwa jicho". Usemi huu unaonyesha utawala wa Mungu wa kuamuru haki ya kupewa adhabu kuu. Katika Agano la Kale, hili linakamilishwa na neno "go'el" (mkombozi wa karibu). Kwa marajeleo ya Agano Jipya yenye kuvutia tazama Matendo ya Mitume 25:11 na Rum. 13:4.

Mstari wa 5 ni wa kiuandani ambapo mst. 6 umechapishwa katika mtiririko wa ufanano wa kiushairi.

Kuna neno la kimzaha la Kiebrania ambalo pia linaweza kuiathiri asili iliyopo kati neno damu (*dam*) na mwanadamu (*adam*). Katika lugha ya ki-Ashuru neno mwanadamu (*adamu*) linahusiana na takatifuza *(adman*). Hivyo, bila shaka kuna uhusiano kati ya ibada ya mwanadamu wa damu (kama vile Robert B. Girdlestone, *Synonyms of the Old Testament*, uk. 45).

◙ "**maana kwa mfano wake Mungu alimfanya mwanadamu**" Kifungu hiki kinaonyesha upendeleo wa mwanadamu (kama vile 1:26,27; 5:1,3). Ni upendeleo mkuu na uwajibikaji wa namna gani.

**9:7"zaeni sana katika nchi, mkaongezeke ndani yake**" Kifungu hiki kinafanana na 1:22,24,28. Sura za 8-9 zinaunda uanzilishi mpya wa mapenzi na matendo ya Mungu yenye kuelezwa katika Mwa. 1. Mstari huu una *Qal* kauli nne zenye MASHARTI, ambapo mst. 1 una tatu. Walimu wa Kiyunani wanasema kwamba kwa sababu ya muktadha wa mauaji (mst. 5-6) wale waliokaidi kuwa na watoto pia wameivunja amri hii.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): MWANZO 9:8-17**
**[8]Mungu akamwambia Nuhu, na wanawe pamoja naye, akisema, [9]Mimi, tazama, nalithibitisha agano langu nanyi; tena na uzao wenu baada yenu; [10]tena na kila kiumbe hai kilichoko pamoja nanyi, ndege, na mnyama**

**wa kufugwa, na kila mnyama wa mwitu katika nchi pamoja nanyi; wote wanaotoka katika safina, hata kila kilicho hai katika nchi. [11]Na agano langu nitalithibitisha nanyi; wala kila chenye mwili hakitafutwa tena kwa maji ya gharika; wala hakutakuwa tena gharika, baada ya hayo, kuiharibu nchi. [12]Mungu akasema, Hii ndiyo ishara ya agano nifanyalo kati yangu na ninyi, na kila kiumbe hai kilichoko pamoja nanyi, kwa vizazi vyote hata milele; [13]Mimi nauweka upinde wangu winguni, nao utakuwa ni ishara ya agano kati yangu na nchi. [14] Hata itakuwa nikitanda mawingu juu ya nchi, upinde utaonekana winguni, [15]nami nitalikumbuka agano langu, lililoko kati yangu na ninyi, na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili, wala maji hayatakuwa gharika tena kuwaharibu wote wenye mwili. [16]Basi huo upinde utakuwa winguni; nami nitauangalia nipate kulikumbuka agano la milele lililoko kati ya Mungu na kila kiumbe hai katika wote wenye mwili kilichoko katika nchi. [17]Mungu akamwambia Nuhu, Hii ndiyo ishara ya agano nililoliweka kati yangu na wote wenye mwili walioko katika nchi.**

**9:9 "Mimi, tazama, nalithibitisha**" Hili agano si la kimasharti na kwa ujumla linatokana na neema ya Mungu. (kama vile 9,11,12,17). Maagano mengine yakiwemo yale ya ki-Adamu na ya Ki-Abrahamu yalikuwa na masharti. Tazama Mada Maalum: Agano katika 6:18.

**9:12 "kwa vizazi vyote**"“Vyote" (*olam*, kama ilivyo katika mst. 16, inamaanisha "milele." Tazama Mada Maalum katika 3:22. Pia Rashi anataja kwamba neno "vizazi" linatajwa kwa kukosewa katika andiko la Kiebrania. Anafasiri kwamba ndivyo ilivyo maana kwamba agano ni kwa ajili ya vizazi pekee vyenye kosa la imani.

**9:13**"**upinde**. . . **ishara**" Huu upinde wa mvua unaweza kuwa umeonekana hapa kwa mara ya kwanza. Mwanzo 2:5-6 inadokeza kwamba kwa mara ya kwanza maji yaliweza kugawanyika katika namna mbalimbali kutokana na mvua (yaani, mgawanyo mbali mbali wa maji kutoka ardhini). Ni kitu cha kufikiria kwamba upinde (BDB 905) ilikuwa siraha ambayo Mungu aliitumia kutetemesha (yaani, mapenzi yake hayamuathiri mwanadamu katika hukumu). Katika nyakati za kale kuachilia upinde ilikuwa ishara ya amani. Pia inawezekana kwamba Mungu aliiweka maana mpya dhidi ya ile iliyokuwa imezoeleka.

**9:15**"**nitalikumbuka** " Upinde ilikuwa ishara kwa Mungu na kwa mwanadamu. Hili ni neno la kifizikia linaloashiria ile kweli kwamba Mungu hasahau (sawa sawa na dhana ya "kitabu cha uzima" na "kitabu cha hukumu").

◙ "**wala maji hayatakuwa gharika tena kuwaharibu wote wenye mwili** " Hili halimaanishi hapatakuwepo gharika hata kidogo, bali hapatakuwepo gharika ya kiulimwengu yenye kuleta madhara kwa wanadamu wote na wanyama.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 9:18-19**
**[18] Wana wa Nuhu waliotoka katika safina, ni Shemu, na Hamu, na Yafethi; na Hamu ndiye baba wa Kanaani.[19] Hawa watatu walikuwa wana wa Nuhu na kwa hao nchi yote ikaenea watu.**

**9:18 "Shemu "** Asili ya jina hili inaweza kuwa "kujulikana tena" au "ita jina" (BDB 1028 II).

◙ **"Hamu"** jina hili linaweza kumaanisha "yenye joto kali" (KB 325II). Hili pia linaweza kuwa limeakisi jina la kale la Misri (yaani, "ardhi yenye joto kali").

◙ **"Yafethi"** Asili ya neno hili inaweza kuwa "mpanuzi" au "aliyekuzwa (BDB 834, tazama neno la kimzaha la Kiebrania katika mst. 22).

◙ **"Kanaani"** Huyu (BDB 488) huenda anatajwa kwa sababu mbili: (1) ulevi wa Nuhu na matokeo ya laana iliyoikumba Kanaani au (2) Wakanaani waliokuja kuwa chimbuko la tatizo kuu la kithiolojia kwa Israeli katika miaka ya baadaye (yaani, kipindi cha maisha ya Musa).

**9:19** Hii ilikuwa sababu ya Mungu iliyorudiwa (yaani, kuijaza nchi). Mnara wa Babeli ulikuwa wa kiukengeufu juu ya hili.

Inatia shauku kwamba mafunzo ya sasa ya vinasaba vilivyoko ndani ya chembe hai vimehitimisha kwamba wanadamu asilia walitoka Afrika ya Kaskazini ambapo taaluma ya sasa ihusuyo kukua kwa lugha imetoa suruhisho kwamba lugha zote za mwanadamu zilianzia India ya kaskazini. Tambua ni kwa namna gani dhana hii inakaribiana na maelezo ya kibiblia. Kwa udhihirisho kabisa rangi zote za mwanadamu zilizo tofauti moja kwa moja ni vizazi vya hawa ndugu watatu. Utafiti wa Sasa wa vinasaba umeonyesha kwamba wanadamu wa rangi zote ni sawa kwa asili ya uzao wao!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) : MWANZO 9:20-27**
**[20] Nuhu akaanza kuwa mkulima, akapanda mizabibu; [21]akanywa divai, akalewa; akawa uchi katika hema yake.[22] Hamu, baba wa Kanaani, akauona uchi wa baba yake, akawaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje. [23]Shemu na Yafethi wakatwaa vazi, wakalitanda mabegani mwao wote wawili, wakaenda kinyumenyume, wakaufunika uchi wa baba yao; na nyuso zao zilielekea nyuma, wala hawakuuona uchi wa baba yao. [24] Nuhu akalevuka katika ulevi wake, akajua mwana wake mdogo alivyomtendea. [25]Akasema,Na alaaniwe Kaanani; Atakuwa mtumwa kabisa kwa ndugu zake. [26] Akasema,Na atukuzwe Bwana,Mungu wa Shemu;Na kaanani awe mtumwa wake. [27] Mungu akamnafisishe Yafethi, Na akae katika hema za Shemu; Na kaanani awe mtumwa wake.**

**9:20** "**Nuhu akaanza kuwa mkulima**" Tafsri za NASB na RSV zinaonekana kuwa na maneno mengi ya Kiebrania; Nuhu hakuwa mkulima wa kwanza—vipi kuhusu Kaini (4:2) au Lameki (5:29)? Toleo la NRXV lina kifungu "Nuhu, mtu wa kuilima ardhi."

**9:21"akanywa divai"** Ulevi (BDB 1016 I, KB 1500) unashutumiwa tena katika Maandiko (kama vile Mit. 23:29-35). Divai si tatizo, bali matumizi yake mabaya (kama vile Kumb. 14:26; Zab. 104:15; Mit. 31:6-7).

## MADA MAALUM: MTAZAMO WA KIBIBLIA JUU YA KILEO NA ULEVI

I. Maneno ya Kibiblia
 A. Agano la Kale
  1. *Yayin* – Hili ni neno la jumla la divai (BDB 406, KB 409), ambalo limetumika mara 141. Asili ya neno hili si yumkini kwa sababu haitokani na mzizi wa Kiebrania. Hiii mara nyingi inamaanisha juisi ya matunda iliyochacha, mara nyingi tunda aina ya balungi. Baadhi ya vifungu bainishi ni Mwa. 9:21; Kut. 29:40; Hes. 15:5,10.
  2. *Tirosh* – Hiii ni "divai mpya" (BDB 440, KB 1727). Kwa sababu ya tabia ya nchi ya Mashariki ya Karibu, uchachu unaanza ndani ya masaa sita baada ya kutengeneza juisi. Neno hili hurejerea juu ya divai katika hatua ya kuchachusha. Kwa vifungu vibainishi tazama Kut. 12:17; 18:4; Isa. 62:8-9; Hos. 4:11.
  3. *Asis* – Kwa uhalisia hiki ni kinywaji aina ya kileo ("divai mpya" BDB 779, KB 860, m.f. Yoeli 1:5; Isa. 49:26).
  4. *Sekar* – Hili ni neno "kinywaji kikali" (BDB 1016, KB 1500). Mzizi wa Kiebrania unatumika ndani ya neno "kulewa" au "mlevi." Mara nyingi hiki huongezwa ndani yake ili kukifanya kileweshe zaidi. Hiki ni sawa na *yayin* (kama vile Mit. 20:1; 31:6; Isa. 28:7).
 B. Agano Jipya
  1. *Oinos* – neno lililo sawa kimaana na *yayin*
  2. *Neos oinos* (divai mpya) – ni neno linalofanana la Kiyunani sawa na tirosh (kama vile Marko 2:22).
  3. *Gleuchos vinos* (divai mpya, asis) – ni ile divai inayotengenezwa katika hatua za mwanzo kabla ya kuchachushwa (kama vile Matendo ya Mitume 2:13).
II. Matumizi ya Kibiblia

A. Agano la Kale
    1. Mvinyo ni zawadi ya Mungu (Mwa. 27:28; Zab 104:14-15; Mhu. 9:7; Hos. 2:8-9; Yoeli 2:19,24; Amosi 9:13; Zek. 10:7).
    2. Divai ni sehemu ya sadaka ya kuteketeza (Kut. 29:40; Law. 23:13; Hes. 15:7,10; 28:14; Kumb. 14:26; Amu. 9:13).
    3. Mvinyo ilitumika katika sherehe za Israel (kama vile Kumb. 14:26)
    4. Divai inatumika kama tiba (2 Sam. 16:2;Mit. 31:6-7).
    5. Divai inaweza kuwa chanzo cha tatizo (Nuhu –Mwa. 9:21; Lutu – Mwa. 19:33,35; Samsoni – Waamuzi 16; Nabali – 1 Sam. 25:36; Uria– 2 Sam. 11:13; Amnon i– 2 Sam. 13:28; Ela– 1 Fal. 16:9; Ben-hadad i– 1 Fal. 20:12; Watawala – Amosi 6:6; na Wanawake – Amos 4).
    6. Divai inaweza kutumika vibaya (Mit. 20:1; 23:29-35; 31:4-5; Isa. 5:11,22; 19:14; 28:7-8; Hosea 4:11).
    7. Divai ilizuiliwa kwa makundi fulani (makuhani waliokuwa katika zamu, Law. 10:9; Eze. 44:21; Wanazareti, Hesabu 6; na watawala, Mit. 31:4-5; Isa. 56:11-12; Hosea 7:5).
    8. Divai ilitumika katika mpangilio wa matukio ya siku za mwisho (Amosi 9:13; Yoeli 3:18; Zek. 9:17).

B. Kipindi cha utulivu kati ya Agano la Kale na Agano Jipya
    1. Divai katika upatanisho ina msaada (Ecclesiasticus 31:27-33).
    2. Walimu wa Sheria za Kiyahudi wanasema, "Divai ni kuu kuliko tiba zote, mahali palipo na uhaba wa divai, madawa ya kulevya yanahitajika." (BB 58b).

C. Agano Jipya
    1. Yesu alikibadili kiwango kikubwa cha maji kuwa divai (Yohana 2:1-11).
    2. Yesu alikunywa divai (Mt. 11:18-19; Luka 7:33-34; 22:17 na kuendelea)
    3. Petro alidhihakiwa kwa ulevi "mvinyo mpya" siku ya Pentekoste (Mdo. 2:13).
    4. Divai inaweza kutumika kama matibabu (Marko 15:23; Luka 10:34; 1 Tim. 5:23).
    5. Watawala hawatakiwi kuwa watumiaji wabaya. Hii haimaanishi kujinyima moja kwa moja (1 Tim. 3:3,8; Tito 1:7; 2:3; 1 Pet. 4:3).
    6. Divai ilitumika katika kupangili matukio ya siku za mwisho (Mathayo 22:1na kuendelea; Ufu. 19:9).
    7. Ulevi huleta majuto (Mt. 24:49; Luka 12:45; 21:34; 1 Kor. 5:11-13; 6:10; Gal. 5:21; 1 Pet. 4:3; Rum. 13:13-14).

III. Utambuzi wa ndani wa Kithiolojia

A. Mkazo wa Kiupembuzi
    1. Divai ni zawadi kutoka kwa Mungu.
    2. Ulevi ni tatizo kubwa.
    3. Waamini katika baadhi ya tamaduni yawapasa kuweka uhuru wa mipaka yao kwa ajili ya injili (Mt. 15:1-20; Marko 7:1- 23; 1 Wakorintho 8-10; Warumi 14).

B. Mwelekeo wa kwenda nje ya mipaka iliyokusudiwa
    1. Mungu ndiye mwanzilishi wa mambo yote mazuri.
        a. chakula – Marko 7:19; Luka 11:44; 1 Kor. 10:25-26
        b. vitu vyote visivyo najisi – Rum. 14:14,20; 1 Tim. 4:4
        c. Vitu vyote vilivyoko kisheria– 1 Kor. 6:12; 10:23
        d. Vitu vyote vilivyo safi – Titus 1:15
    2. Mwanadamu aliyeanguka amezitumia vibaya karama za Mungu kwa kuzifanyia kazi nje ya mipaka ya Mungu aliyoikusudia.

C. Matumizi mabaya yako ndani yetu, si ndani ya vitu. Hakuna kilicho kiovu ndani ya uumbaji wa vitu vinanyoonekana (kama vile Rum. 14:14,20).

IV. maelezo ya kufungia

A. kuwe na uhakika na uzoefu wako, thiolojia, na utafasiri wa kibilia havimshushi thamani Yesu na tamaduni za Kikristo/ Kiyahudi za karne ya kwanza! Kiuhakika hawakuwa wenye kujizuiya kunywa mvinyo.

B. Mimi sitetei jamiii ya watumia pombe. Hata hivyo, wengi wamekwenda mbali juu ya nafasi ya Biblia kuhusu somo hili na sasa kudai kuwa wenye haki sana wakisimamia juu ya upendeleo wa kimadhehebu/ kitamaduni.
C. Kwangu mimi, Warumi 14 na 1 Wakorintho 8-10 vimetoa mwanga na mwongozo uliosimamia juu ya upendo na heshima kwa wapendwa wengine na uenezaji wa injili katika tamaduni zetu, na sio uhuru binafsi au ukosoaji wa kimaamuzi. Kama Biblia ndio chanzo pekee cha imani na utendaji, kwa hiyo yawezekana wote tulifikirie jambo hili.
D. Tukijizuiya kabisa kunywa mvinyo kama yalivyo mapenzi ya Mungu, tunadokeza nini kuhusu Yesu, pia tamaduni za sasa za wale wanaotumia kileo mara kwa mara (mf., Ulaya, Israel, Argentina)

**9:22 "akauona uchi wa baba yake, akawaeleza ndugu zake wawili waliokuwa nje"** Dhambi ya Hamu ilikuwa (1) kutomuheshimu babaye au (2) ni aina ya tendo la kiasherati (kama vile Law. 18:6,7). Waebrania walikuwa makini sana kuhusu uchi.

Katika maana ya kithiolojia, tendo hili linaonyesha mwendelezo wa msukumo wa anguko. Nuhu alilewa divai! Kwa mkazo Hamu alifurahia vyote ujinga na uchi wa babaye! Uelekeo huu wa ukosefu wa heshima na zinaa haramu unathibitika sana katika vizazi vya Kaanani! Uelekeo huu lazima ulikuwa uthibitisho kwa Nuhu aliyeilaani Kanaani, si Hamu.

Kama ilivyo kwa andiko lililotangulia, sehemu hii haina kitu, hakuna la kufanya juu ya ushushaji thamani wa kibiblia juu ya rangi ya watu weusi. Hakika Waafrika walitokana na Hamu lakini Wakanaani hawakuwa na rangi nyuesi (yaani, picha za ukutani katika Misri)!

**9:24** "**Nuhu** ...**akajua**" bila shaka huyu alijua kwa sababu aliuliza, lakini huenda ni kupitia vazi ambalo Shemu na Yafethi walimfunika .

◙ "**mwana wake mdogo**" Hamu mara nyingi anaorodheshwa wa pili katika orodha ya wana wa Nuhu. Hili neno la Kiebrania linaweza kuwa kichochezi "mdogo sana" au kilinganishi "mdogo zaidi."

**9:25** "**Akasema**" Kumbuka dhana ya Kiebrania ya nguvu ya neno lizungumzwalo, Mwa. 1, pamoja na umuhimu wa baraka za kiuzazi, Mwa. 49.

◙"**Na alaaniwe Kaanani**" Hiki KITENZI (BDB 76, KB 91)ni *Qal* KAULI TENDEWA ENDELEVU. Walimu wa Kiyunani wanasema Kanaani ndiye wa kwanza kuuona uchi wa Nuhu na kumwambia babaye, Hamu, lakini huenda Nuhu aliuona ushahidi uthibitisho kama tabia ya ukosefu wa heshima ndani ya Hamu mwanae mdogo, au Kanaani, mwanae mdogo kabisa, ni njia ya kuvirejelea vizazi vyote vya Hamu. Tambua kwamba hili halikusababishwa na Mungu bali ni kwa sababu ya Nuhu kutumia kileo! Hii Ni wazi kwamba kutokana na historia ya Israeli iliyofuatia kwamba Wakanaani walionekana kama waabudu sanamu za uovu na kwamba iliwapasa kugharikishwa moja kwa moja. Katika nchi zao, wenye nguvu bado waliendelea kuishi. Hii ilikuwa ibada pandikizi ambayo inazuiwa katika kitabu cha Mambo ya Walawi.

## MADA MAALUM : UBAGUZI WA KIMBARI

I. Utangulizi
   A. Tabia hii ya kujikuza ni ya watu wote kwa wanadamu walioanguka ndani ya jamii, huu ni ubinafsi wa mwanadamu ili kujilinda kwa wengine, ubaguzi wa mataifa kwa namna mbalimbali, na kauli ya sasa wakati utaifa (au ukabila) ni mtindo wa kizamani.
   B. Utaifa ulianzia Babeli (Mwanzo 11) na mwanzoni ulihusishwa na wana watatu wa Nuhu ambapo neno hili mataifa lilitokana kwalo (kama vile Mwanzo 1-3; Matendo 17:24-26).
   C. Ubaguzi wa mataifa ni mojawapo ya aina nyingi za uonevu

1. Kutukuza elimu
2. Ujivuni wa kijamii na kiuchumi
3. Uhalalisho wa haki binafsi ya kidini
4. Msimamo usiobadilika wa kuingiza dini katika siasa

II. Matini ya Biblia

A. Agano la Kale

1. Mwa. 1:27 –wanadamu jinsi ya kiume walifanywa kwa taswira na mfano wa Mungu, vitu vinavyomfanya awe wa pekee kuonesha pia uthamani wa mtu na hadhi/ utu (kama vile Yohana 3:18)
2. Mwanzo 1:11-25- inaandika fungu, "… baada ya jinsi yao…" mara kumi. Hii imetumika kusaidia utenganisho wa mataifa. Hata hivyo ni wazi kutokana na mazingira, hii inamaanisha kwa wanyama na mimea na sio kwa watu.
3. Mwa. 9:18-27- Hii imetumika kusaidia utawala wa mataifa. Ikumbukwe kwamba Mungu hakulaani kanani. Nuhu, ambaye ni baba yake, alimlaani kanani baada ya kuzinduka kutoka kwenye ulevi wa pombe. Biblia haioneshi kuwa Mungu alithibitisha kiapo/laana. Hata kama alifanya hivyo haiwaathiri watu weusi. Kaanani alikuwa ni baba wa wote wale waliokuwa wakiishi Palestina na kuta za Misri zilizokuwa zimechorwa zinaonyesha kuwa hawakuwa weusi.
4. Hes. 12:1-Musa alioa mwanamke mweusi
5. Yoshua 9:23- Hii imetumika kuhakiki kuwa taifa moja litatumikia lingine. Hata hivyo katika uhalisia wa Gibeonite ni wa asili moja na Wayahudi.
6. Ezra 9-10 na Nehemia 13- Hivi vimetumika kwa maana ya mataifa, lakini kiuhalisia inaonesha kuwa ndoa zilikuwa zimekatazwa, sio kwa sababu ya mataifa (walitoka kwa kaka mmoja Nuhu Mwanzo 10) lakini kwa misingi ya kidini.

B. Agano Jipya

1. Injili
   a. Yesu alitumia hali hii ya chuki kati ya Wasamaria na Wayahudi katika mifano kadhaa ambayo ilionesha kuwa ubaguzi wa kimataifa haufai.
      1) Fumbo la Msamaria mwema (Luka 10:25-37)
      2) Mwanamke kisimani (Yohana 4)
      3) Mgonjwa wa ukoma aliyeshukuru (Luka 17:11-19)
   b. Injili ni kwa watu wote
      1) Yohana 3:18
      2) Luka 24:46-47
      3) Waebrania 2:9
      4) Ufunuo 14:6
   c. Ufalme utawajumuisha wanadamu wote
      1) Luka 13:29
      2) Ufunuo 5
2. Matendo
   a. Matendo 10 ni habari kamili kuhusu upendo wa Mungu kwa ulimwengu wote na ujumbe wa injili kwa walimwengu wote.
   b. Petro alishambuliwa kwa vitendo vyake katika Matendo 11 na tatizo lake halikutatuliwa hadi baraza la Yerusalemu katika matendo 15 lilipokutana na kupata ufumbuzi. Mvutano kati ya Wayahudi wa Karne ya kwanza na wapagani ulikuwa umezidi.
3. Paulo
   a. Hakuna Vipingamizi/vizuizi katika Kristo.
      1) Gal. 3:26-28
      2) Efe. 2:11- 22

3) Kor. 3:11

b. Mungu haitii watu

1) Rum. 2:11

2) Efe. 6:9

4. Petro na Yakobo

a. Mungu hatii watu (1 Petro 1:17)

b. Kwasababu Mungu haoneshi upendeleo, vivyo hivyo watu wake Yakobo 2:1

5. Yohana

a. Mojawapo ya maelezo marefu kuhusu uwajibikaji wa waamini yanaonekana katika 1 Yohana 4:20.

III. Hitimisho

A. Ubaguzi au kwa maana hiyo, uonevu wa aina yoyote haufai kabisa kwa watoto wa Mungu. Hapa kuna nukuu kutoka kwa Henlee Barnette aliyezungumza katika mkutano/kikao Glorieta New Mexico katika kamisheni ya maisha ya mkristo mwaka 1964. “Ubaguzi ni imani dhidi ya dini kwa sababu si wa kibiblia wala Kikristo wala wa kisayansi”.

B. Suala hili linawapa Wakristo fursa ya kuonesha upendo wao wa Kikristo msamaha na uelewa kuhusu ulimwengu uliopotea kuja kwa Kristo. Ubaguzi kwa Wakristo unaonyesha kutokukomaa na ni fursa kwa uovu kuirudisha nyuma imani ya mwamini, uhakika na makuzi. Pia itatenda kazi kama kizuizi kupoteza watu wli wanaomkimbilia kwa Kristo.

C. “Nifanye nini” (Sehemu hii inatolewa katika kamisheni ya maisha ya Mkristo iitwayo “mahusiano ya mataifa”)

“KATIKA KIWANGO CHA MTU”

- ★ Kubali kuwajibika binafsi katika kutatua matatizo yanayohusiana na taifa.
- ★ Kupitia maombi, kusoma biblia na kushirikiana na mataifa mengine na kupambana na maisha ya uonevu wa mataifa mengine.
- ★ Elezea msimamo wako kuhusu ushindani uliopo, hasa pale waliochochea ushindani wa chuki hawakupingwa

“KATIKA MAISHA YA FAMILIA”

- ★ Tambua umuhimu wa athari ya familia katika kueneza tabia kwa mataifa mengine.
- ★ Jaribu kuendeleza tabia za Kikristo kwa kuzungumza juu ya kile ambacho watoto na wazazi wanasikia kuhusu maswala ya mataifa nje ya nyumbani kwao.
- ★ Wazazi wanapaswa kuwa waangalifu kwa kuonesha mifano ya mienendo ya Kikristo kwa kuhusiana na watu wa mataifa mengine
- ★ Tafuta fursa kufanya urafiki wa kifamilia kwa watu wa mataifa yote.

“NDANI YA KANISA LAKO”

- ★ Kwa mahubiri na mafundisho ya ukweli wa Biblia kuhusiana na mataifa, mkutano unaweza kuhamasisha kuonesha mfano kwa jamii nzima.
- ★ Uwe na uhakika kuwa, ibada, ushirikiano na huduma kupitia kanisani viko wazi kwa wote hata vile ambavyo makanisa ya Agano Jipya yalivyoona kutokuwepo kwa vizuizi vya kimataifa (Efe. 2:11-22 Wagalatia 3:26-29)

KATIKA MAISHA YA KILA SIKU”

- ★ Saidia kuondoa ubaguzi wa kimataifa wa aina zote katika ulimwengu wa kazi.
- ★ Fanya kazi kupitia katika taasisi za kijamii za aina zote ili kupata haki sawa na fursa ukikumbuka kuwa ni tatizo la kimataifa linalotakiwa kushambuliwa, na sio watu, lengo ni kukuza uelewa na sio kuunda machungu.

- ★ Ikionekana inaunda kamati maalumu za wananchi walengwa kwa lengo la kufungua njia za mawasiliano katika jamii kwa ajili ya kuwaelimisha wote katika mambo na vitendo maalumu katika kuboresha mahusiano ya mataifa.
- ★ Saidia vyombo vya sheria na watunga sheria katika kupitisha sheria, kukuza haki za kimataifa na kupinga wale karibu haki kwa faida za kisasa.
- ★ Pendekeza mtumiaji wa maarifa wa sheria kuitumia bila upendeleo.
- ★ Epusha vurugu na hali ya kuheshimu sheria ili kufanya uwezekano wa mambo wa mambo kwenda sana kama raia Mkristo hakkikisha kuwa mfumo wa kisheria haitumiki kama vyombo vya kuwawezesha wanaojenga ubaguzi.

Onesha mfano wa roho na fikra za Kristo kwa mahusiano yote ya wanadamu.

◙ **"mtumwa kabisa"** Hii ni maana chochezi ya Kiebrania "mtumwa wa chini kabisa." Hili lilikamilishwa katika utekaji nyara wa Yoshua juu ya Palestine!

**9:26-27** Hili neno "na" la mistari hii miwili ni KAULI AMRISHI, miundo mitatu ya kipekee na ilimaanishwa kimuktadha.

**9:26 "Bwana"** Jina "YHWH" linaonekana kuwa na matumizi ya kipekee juu ya jina la agano (tazama maelezo katika 2:4) kumtambulisha Shemu kama mtiririko wa Kimasihi (kama vile Luka 3:36).

◙ **"Mungu wa Shemu"** Shemu linamaanisha "jina" na hili linaweza kuwa ombi kwa Mungu kama jina pekee, YHWH (BDB1028 II). Mtiririko wa Shemu ni wa Kimasihi. Hili liko katika upingamizi wa sura ya 11:4!

**9:27"akamnafisishe Yafethi, Na akae katika hema za Shemu**" Baadhi wanaliona hili (1)katika maana ya kisiasa kama ule utamaduni wa Kirumi na ule Ulaya au (2)katika maana ya kiroho ya ujumuisho wa Mataifa pamoja na Baraka za Wayahudi, ambazo pia zilikuwa sehemu ya agano la ki-Ibrahimu (kama vile 12:3; Efe. 2:11-3:13)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) MWANZO 9: 28-29**

[28] **Na Nuhu akaishi baada ya ile gharika miaka mia tatu na hamsini.** [29] **Siku zote za Nuhu zilikuwa miaka mia kenda na hamsini, akafa.**

**9:29** Mauti bado inatawala (kama vile sura ya 5)!

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujifunza wa fasiri, ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Ni kwa namna gani anguko liliathiri agano la Mungu kwa Nuhu?
2. Je! Hii ni adhabu kuu ya kanuni za kibiblia (kama vile mstari wa 6)?
3. Je! Nuhu aliilaani rangi ya watu weusi?
4. Je! Mstari wa 27 unarejerea juu ya nini?

# MWANZO 10:1-32

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Uzao wa Nuhu | Mataifa yanaibuka kutoka Kwa Nuhu | Jedwali la Mataifa | Uzao wa wana wa Nuhu | kuongezeka kwa watu wa duniani |
| 10:1 | 10:1 | 10:1 | 10:1 | 10:1 |
| 10:2-5 | | 10:2-5 | 10:2-5 | 10:2-5a |
| | | | | 10:5b |
| 10:6-14 | 10:6-14 | 10:6-14 | 10:6-12 | 10:6-7 |
| | | | | 10:8-12 |
| | | | 10:13-14 | 10:13-14 |
| 10:15-20 | 10:15-20 | 10:15-20 | 10:15-20 | 10:15-19 |
| | | | | 10:20 |
| 10:21-31 | 10:21-31 | 10:15-20 | 10:21-31 | 10:21-31 |
| | | | | 10:22-23 |
| | | | | 10:24-30 |
| | | | | 10:31 |
| 10:32 | 10:32 | 10:32 | 10:32 | 10:32 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (angalia ukurasa wa vii)

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

1. Aya ya kwanza
2. Aya ya pili
3. Aya tatu
4. N.k

## UTANGULIZI

A. Nini makusudi ya kithiolojia ya asili yenye maelezo mengi ya sura ya 10?
   1. Inaonesha kwamba Mungu anajali mataifa yote. Sura ya 11 kimtiririko wa kimasimulizi ipo nje ya utaratibu. Hii inaonekana kuonesha kwamba sura ya 10 sio tu hukumu (kama vile 11:1-9), lakini kimsingi ni kutimilizwa kwa 1:28 na 9:1,7 (yaani kuzaa na kuijaza dunia).
   2. Mataifa haya haya mara kwa mara yanarejerewa na manabii (kama vile Isa. 7-23; Yer. 46-51; Ezek. 27-30; 38-39) kama makundi ambayo Mungu anayahukumu.
   3. Inaandaa jukwaa kwa ajili ya wito wa Ibrahimu na mbegu yake kama ufalme wa makuhani kuuleta ulimwengu wote kwa YHWH (kama vile 12:3; Kut. 19:5-6).
   4. Inafuata utaratibu wa Mwanzo wa kufupisha shabaha ya uzao wa kimasihi (kama vile 9:26).
   5. Panaonekana kuwepo na makundi yanayotajwa zaidi ya 70. Walimu wa kiyahudi wanasema kwamba kuna lugha 70 ulimwenguni, yawezekana kutoka Kumb. 32:5. Wengi wanaunganisha Luka 10:1 pamoja na hili kuelezea uhamasisho wa kimishionari wa ulimwengu mzima wa Injili.

B. Ni kwa namna gani na kwa nini taarifa hizi zinashindwa kukubaliana/kushabihiana na tafiti za Lugha?

1. Tafiti za kisasa zimejikita katika kanuni za ki-lugha wakati masimulizi ya kibiblia yanalenga taarifa za kijiografia. Taarifa hizi za kijiografia zinaathiriwa na (1) tarehe na (2) kuhama kwa watu kutokana na vyote uhamiaji na vita (kama vile Ezek. 16:3; Hosea 12:7).
2. Mtu lazima azingatie asili ya Kithiolojia ya masimulizi haya
   a. Uchaguzi wa taarifa za kimatukio
   b. umoja wa mwanadamu (Adamu na Nuhu)
   c. Yale mataifa yaliyopo mbali na ukaribiano na Israeli yanapewa nafasi ndogo (au hayapewi kabisa)
3. Sura hii inajumuisha majina ya wingi mwingi. Hii inaonesha kwamba mara kwa mara watu wa kale wanasimama kwa ajili ya kundi. Mara kwa mara makundi yanachukua zaidi ya eneo moja la kijiografia.
4. Haya sio masimulizi ya ndani ya kisayansi ya kimagharibi. Mara kwa mara sisi huwa tunasahau kwamba hili ni jaribio la kwanza katika orodha ya aina hii. Uhakika wake unahakikiwa na kujitoa kwetu kwa madhanio ya kwanza kwa maandiko. Hata hivyo, hii haimaanishai kwamba ilikusudiwa kutupa sisi taarifa ya ndani katika maeneo yote au kututhibitisha katika mfumo wa kiufahamu wa kimagharibi. Kwasababu siku yake kwa hali ya kustaajabisha iko sawa na hakika bila kukosewa!
5. Hii ni orodha kama ilivyo Torati zote zilikuwa zimewekwa chini ya mapitio ya mara kwa mara na uboreshaji wa kiuandishi. Majina kadhaa katika hii orodha (yaani Wasummeri, Wa-Scythia, Wafilisti, na Wamedi) hawapatikani katika fasihi nyingine ya kale ya Mashariki ya Karibu mpaka mwaka 1500-1000 k.k
6. Inawezekana kwasababu watu wa Asia na Polinesia (na kwa Amerika) na wengi wa watu wa Afrika hawashughulikiwi, kwamba orodha hii inaweza kujumuisha sehemu tu za mataifa na rangi za watu wanaoonekana leo. Ikiwa huu ndio ukweli sasa, itakuwa ni kutia chumvi kithiolojia kusema mataifa mengine ya dunia yalitokana na wana watatu Kibiblia.

   Hii haikusudiwi kupunguza ama kuondoa umoja wa wanadamu (ambalo limethibitishwa na Vinasaba) ambao unaelezewa vizuri sana katika jozi ya asili ya wanadamu katika Mwanzo 1 na 2.

C. Muundo wake
1. Yafethi, mistari ya 2-5, inachukua mikoa ya kaskazini mwa Mesopotamia kutoka Uhispania kuelekea bahari ya Caspian.
2. Hamu, mistari ya 6-20, inachukua mikoa ya kusini mwa Mesopotamia kutoka Afrika mpaka India
3. Shemu, mistari ya 21, inashughulikia kazi za wa-Semi wa Mesopotamia kutoka bahari ya Shamu mpaka India.

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:1**

[1] **Hivi ndivyo vizazi vya wana wa Nuhu, Shemu, na Hamu, na Yafethi. Na kwao walizaliwa wana wa kiume baada ya gharika.**

**10:1 "Hivi ndivyo vizazi"** Tungo hii imerudiwa mara tatu katika muktadha wa sura ya 10 na 11 (10:1; 11:10,27). Hii inawezekana ilikuwa njia ya mwandishi kuainisha kitabu au wasifu wa Ki-Babeli ili kuweka alama ya mawe ya udongo wa mfinyanzi chembeo ambavyo vinaenda pamoja

◙ **"Shemu, na Hamu, na Yafethi"** Huu utaratibu wa kuorodhesha majina kimsingi hauhusiani na umri wao lakini mpangilio wa kithiolojia, kuwaorodhesha wale wa uzao wa kikuhani kwanza, na wale wa mbali hatimaye kuwaondoa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:2-5**

[2] **Wana wa Yafethi ni Gomeri, na Magogu, na Madai, na Yavani, na Tubali, na Mesheki, na Tirasi.** [3] **Na wana**

**wa Gomeri ni Ashkenazi, na Rifathi, na Togama. [4] Na wana wa Yavani ni Elisha, Tarshishi, Kitimu, na Warodani. [5] Kwa hao nchi za pwani za mataifa ziligawanyikana kuwa nchi zao, kila moja kwa lugha yake, kwa jamaa zao, kufuata mataifa yao.**

**10:2 "Gomeri"** Hii inaonekana kurejerea Wasummeri (BDB 170), ambao wanatajwa katika Homer's *Iliad*, sura ya 11:13-19. Waliishi kaskazini mwa Asia Ndogo. Yawezekana walihamia kaskazini na ku vikundi vya kikabila vya Ulaya. Hii inaweza kuonekana kupitia neno linalofanana na hilo kwa wao katika Kaskazini mwa Ujerumani, "Simbi" na Wales, "Simri."

◙**"Magogu"** Kumekuwa na mjadala mkubwa kuhusu jina hili kwasababu ya muunganiko wake na Ezek. 38-39 na nyakati za siku za mwisho. Hatahivyo sharti ielezewe kwamba Magogu (BDB 156), sambamba na Mesheki na Tubali, pia wanatajwa katika mstari wa 2, kimsingi ni makabila yenye uhusiano na Asia Ndogo na pwani ya Bahari Nyeusi. Inawezekana kwamba walihama kaskazini na kufanyika makundi ya kikabila ya Urusi ya sasa. Lakini katika nyakati za kale, walikuwa karibu sana na Nchi ya Ahadi. Wengi wanaelezea kwamba Magogu wanauhusiano na Wa-Sithi, kusini mashariki mwa Bahari Nyeusi. Taarifa hii inatoka kwa Josephus.

◙**"Madai"** Wengi wanelezea kwamba hii inarejerea kwa Wamedi (BDB 552), ambao wanaishi kusini magharibi mwa Bahari ya Caspian, ambao wanafanyika muhimu sana kwa Israeli katika kuungana na Uajemi, ufalme wa ki-Babeli wa Neo (Nebukadneza).

◙**"Yavani"** Hii (BDB 402) inaonekana kurejerea Wayunani (wa kusini) Wa-Ioni (kama vile Dan. 8:21; 10:20; 11:2). Kikundi hiki kinatamkwa "Yavana" katika Sanskrit; "Yuna" katika Uajemi ya kale "Jounan" juu ya jiwe la Rosetta. Baadaye walikuwa siyo tu ufalme wa Ugiriki, lakini yawezekana sehemu watu wa bahari katika eneo la Aegean (yaani Wa-Foenike na Wafilisti).

◙**"Tubali"** Wengi wanaelezea kwamba hii (BDB 1063) inarejerea wa-Tibereni wa Asia Ndogo ya kati. Wote Tubali na Mesheki wanatokea katika Ezek. 38-39 kama waishio Asia Ndogo.

◙ **"Mesheki"** Wengi wanaelezea kwamba hiki kikundi cha kikabila (BDB 604) cha ambao wanaishi kusini magharibi mwa Bahari Nyeusi (kama vile Ezek. 27:13; 32:26; 38:2; 39:1). Hii taarifa inatoka kwa Herodotus.

◙ **"Tirasi"** Kumekuwa na utambulisho kadhaa unaowezekana kwa kundi hili (BDB 1066), kama ilivyo kawaida kati ya wafasiri. Wengi wa majina haya na maeneo waishiyo hayana uhakika. Uwezekano unajumuisha (1) wa - Etrusca; (2) mabaharia wa kujitegemea wa Aegean wa taifa liitwalo la wa-Pelasgi; (3) Josephus anasema kwamba wa-Thracia; au (4) Rashi kwamba inarejerea Uajemi.

**10:3 "Ashkenazi"** Hili ni jina (BDB 79) lililofanyika na Wayahudi wa Ulaya waliofuata baadaye (yaani Ujerumani). Nadharia za sasa ni (1) Wa-Scythia katika eneo la Ujerumani; (2) watu walio karibu na Ziwa Urumia; au (3) kikundi cha kikabila cha Bithynia katika Asia Ndogo.

◙**"Rifathi"** Hiki kimekuwa kinakisiwa na kikundi cha kikabila (BDB 937) karibu na mto Rhebas au kikundi cha kikabila karibu na Bosphorus.

◙ **"Togama"** Haya (BDB 1062) ni (1) ni makundi ya kikabila katika eneo la Cappadocia huko Asia Ndogo; (2) karibu na jiji la kale la Kameshi; au (3) kikundi cha kikabila cha Phrygia. Huu uwezekano wa aina tatu upo katika Uturuki ya kisasa.

**10:4 "Elisha"** Wengi wanaelezea kwamba hii inarejerea (BDB 47) idadi ya watu wazawa wa-Cypress. Wanatajwa katika Ezek. 27:7.

◙ **"Tarshishi"** Ingawa Albright aliweka hili eneo la Sardinia, wengi wa watafiti wa kisasa wanaiweka kusini mwa Uhispania (yaani Tartessos). Inatajwa katika II Nyakati 9:21; Zab. 48:7; 72:10; Yona 1:3; 4:2).

◙**"Kitimu"** Kuna maoni ng'ang'anizi kwamba hii inarejerea kwa wakazi wa pwani ya mashariki ya Cypress (BDB 1076 II).

◙ **"Warodani"** Wengi wanaelezea kwamba ufanano kati ya barua za Kiebrania, D ($) na R (&), kumekuwa na kuchanganywa na kwamba hii inarejerea wakazi wa kikabila ya kisiwa cha Rhodes (kama vile fasiri ya NIV). Hatahivyo, wengine wanelezea kwamba ni Kaskazini mwa Ugiriki na bado wengine wanasema kwamba ni kusini mwa Italia. Ni wazi kwamba hii haijulikani (BDB 187).

**10:5 "Kwa hao nchi za pwani za mataifa"** Tungo hii inatumika kisitiari kwa ajili ya watu walioko mbali, lakini hapa panaonekana kumaanisha wakazi pembezoni mwa pwani ya Shamu ambayo inafuata uhamiaji wa watoto wa Yafethi.

◙**"kila ….kwa lugha yake, kwa jamaa zao, kufuata mataifa yao"** Hii inaonekana kuwa mgawanyo wa pande nne wa namna gani sura hii inagawanywa: (1) Kijiografia; (2) ki-lugha; (3) kikabila; na (4) kisiasa.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:6-14**

**6 Na wana wa Hamu ni Kushi, na Misri, na Putu, na Kanaani. 7 Na wana wa Kushi ni Seba, na Havila, na Sabta, na Raama, na Sabteka. Na wana wa Raama ni Sheba, na Dedani. 8 Kushi akamzaa Nimrodi, akaanza kuwa mtu hodari katika nchi. 9 Alikuwa hodari kuwinda wanyama mbele za Bwana. Kwa hiyo watu hunena, Kama Nimrodi, hodari wa kuwinda wanyama mbele za Bwana. 10 Mwanzo wa ufalme wake ulikuwa Babeli na Ereku, na Akadi, na Kalne, katika nchi ya Shinari. 11 Akatoka katika nchi ile akaenda mpaka Ashuru, akajenga Ninawi, na Rehoboth-iri, na Kala; 12 na Reseni, kati ya Ninawi na Kala, nao ni mji mkubwa. 13 Misri akazaa Waludi, na Waanami, na Walehabi, na Wanaftuhi, 14 na Wapathrusi, na Wakasluhi; huko ndiko walikotoka Wafilisti na Wakaftori.**

**10:6 "Kushi, na Misri, na Putu, na Kanaani"** Wana hawa wa Hamu wanajadiliwa zaidi katika mistari inayofuata: Kushi (BDB 468) katika mistari 7-12; Misri (BDB 595) katika mistari ya 13-14; na Kanaani (BDB 488) katika mistari 15-19. Wanaweka (BDB 806), ingawa haijadiliwa inaonekana kurejerea aidha Afrika Mashariki (Somalia), kusini mwa Arabia, Libya au Kirene. Ni wazi kutokana na hii maeneo mengi yanayowezekana kwamba hatuna uhakika nayo.

**10:7 "Seba"** Hili ni eneo la juu la Nile kadiri tunavyoweza kuelezea kutokana na taarifa ambazo zinapatikana (BDB 685). Inatajwa katika Isa. 43:3.

◙**"Havila"** Hii kibayana ni "ardhi yenye mchanga" (BDB 296), yawezekana ikawa eneo la mahali fulani katika Misri.

◙**"Sabta"** Hii (BDB 688) inaweza aidha kuwa eneo la kisasa la Ethiopia, ambalo lingekuwa Afrika Mashariki, au jiji katika Arabia.

◙**"Raama"** Hii inawezekana kuwa Sabateans ya kusini magharibi mwa Arabia (BDB 947).

◙**"Sabteka"** Hii pia inarejerea Ethiopia (BDB 688).

◙**"Sheba"** Hii (BDB 985) inaonekana kuwa eneo maarufu la Malkia Sheba, kusini magharibi mwa Arabia (kama I Wafalme. 10:1-10; Ayubu 1:15; 6:19; Zab. 72:10,15; Isa. 60:6; Yer. 6:20).

◙**“Dedani”** Hii inaonekana kuwa mahali fulani katika Arabia (BDB 186). Ni wazi kwamba wana wa Kushi wako mahali fulani Mashariki mwa Afrika na rasi ya Arabia. Inatajwa katika Isa. 21:13; Yer. 25:23; 49:8; Ezek. 25:13; 27:20.

**10:8 “baba wa Nimrodi”** Nimrodi (BDB 650) Anatajwa kinayana kwasababu alikuwa mwanzilishi wa ustaarabu mkubwa wa kwanza. Hii ingemaanisha kwamba uzao wa Hamu ulikuzwa Babeli. Yeye anaunganishwa na wana wa Kushi kwasababu ya ufanano wa ki-lugha kwa jina Kassites. Kuna makundi mwili kutoka Kushi, moja katika mstari wa 7 katika upande wa Mashariki mwa Bahari nyekundu na hii moja katika mstari wa 8 upande wa magharibi mwa Bahari Nyekundu.

◙**“Nimrodi”** Neno linamaanisha “kupindua” kulingana na Rashi na Leupold. Kwa kutembea na hili kichwani tungo zifuatazo kubwa mbili, “mtu mkubwa” na “mwindaji mkubwa,” zinatafsiriwa hasi kama “dikteta” au “mtawala” au “muuaji wa wanadamu.” Hata hivyo haijulikani ikiwa hiki ni kisawe, lakini inaonekana inashabihiana na muktadha. Mtu huyu anakwenda kujenga baadhi ya miji mikubwa ya Mesopotamia na kidhahiri ataanza nguvu ya ulimwengu wa kwanza. Wengi wameirejerea hii kumaanisha Tukuli-ninurta I, lakini hakuwahi kuishi mpaka karne ya kumi na tatu k.k. Wakati alipotawala Ashuru na Babeli. Aliitwa Ninus, lakini muda wake ulikuwa umechelewa sana kushabihiana na Nimrodi. Wengine wanaelezea kwamba hii inarejerea Sargon I, mtawala wa mji wa Akkad.

**10:9 “hodari kuwinda wanyama mbele za Bwana”** Baadhi ya wafasiri wanaelezea kwamba Mungu anamtambua kama mwindaji ni chini ya Heshima yake, lakini ikiwa tungo inamaanisha mtawala wa kwanza na mkuzaji wa mfumo wa ulimwengu wa kibinadamu (kama vile Mika 5:6), halafu Mungu anavyomtazama ni kwa namna ya kumuelewa.

**10:10 “Babeli”** Wababeli wanasema kwamba neno hili (*bab-ili*) linamaanisha “lango la miungu.” Hatahivyo katika Mwanzo 11, Wayahudi walilitafsiri maana yake kama (*balil*), “alichanganya” (BDB 93).

◙ Majiji yote yanayoorodheshwa katika mstari huu yalikuwa majiji makubwa katika Shina wakati mmoja au mwingine

◙ **“Kalne”** Baadhi wanasema kwamba hii (BDB 484) inarejerea jiji la Nippuri, wakati wengine wanaiweka tena katika kitenzi kumaanisha “wao wote.”

◙ **“katika nchi ya Shinari”** Hii ki-lugha inahusiana na neno “Sumeri” au “Sumeria” (BDB 1042). Inarejerea eneo la kusini mwa Mesopotamia.

**10:11 “akaenda mpaka Ashuru”** Baadhi wanasema kwamba hii inarejerea Nimrodi na kwamba inaonekana kushabihiana na muktadha vizuri zaidi (kama vile Mika 5:6). Hata hivyo kwingine ikijumuisha Tafsiri ya Agano la Kale la Kiyunani, Vulgate, Syriaki, Martin Luther, na John Calvin, wanasema kwamba inamaanisha Ashuru.

◙ **“Ninawi”** Huu (BDB 644) ni mji mkuu wa ufalme wa Ashuru uliopo mto Hedekeli (kama vile II Wafalme 19:36; Isa. 37:37; Yona 1:2; 3:2-7; 4:11; Nah. 1:1; 2:8; 3:7; Sefania 2:13)..

◙ **“Rehoboth-iri”** Hii kidhahiri ni “jiji lenye mtaa mpana” au “sehemu pana za jiji” na yawezekana ni maelezo ya Ninawi (BDB 944 II).

◙ **“Kala”** Hili ni jiji kubwa la mji wa Ashuru (BDB 480 II). Jina lake la kisasa ni Nimrudi ambalo kiuwazi limeunganika na jina la Nimrodi.

**10:13 “Reseni”** Wengi wanaelezea kuwa hii inarejerea Misri ya juu na chini (BDB 595).

◙**“Waludi”** Hii inaweza kumaanisha wa-Lydia katika Asia Ndogo (BDB 530).

◙**“Waanami”** Hiki kinaweza kuwa kikundi cha kikabila kinachokaa eneo la chemichemi za maji za maghabiri mwa Misri (BDB 777).

◙**"Walehabi"** Hii inaonekana kurejerea makabila ya jangwa ya pwani ya Kaskazini mwa Pwani ya Afrika (BDB 529).

◙**"Wanaftuhi"** Hiki kinaonekana kuwa kikundi cha kikabila karibu na jiji la Memphis (BDB 661). Wale wote waliotajwa katika mstari wa 13 ni wazi kuwa wameunganishwa na Misri na eneo linaloizunguka.

**10:14 "Wapathrusi"** Hii inamaanisha ardhi ya kusini na yawezekana inarejerea sehemu ya juu ya Misri (BDB 837).

◙ **"Wakasluhi (ambapo walitokea Wafilisti)"** Kumekuwa na mjadala mkubwa sana kuhusu tungo hii kwasababu kutoka Amosi 9:7 inaonekana kumaanisha kwamba Wafilisti walitokea Krete. Hii ni moja ya maeneo yale ambayo rejea hii inaweza kuwa kijiografia. Huku kuendelea kwa wimbi la uvamizi na uhamiaji wa watu wa bahari wa Aegean wakiathiriwa zaidi na nchi za pwani ya ulimwengu wa Shamu ikijumuisha Misri na Palestina. Kwa Wakasluhi angalia BDB 493.

◙**"Wakaftori"** Hii inaonekana kurejerea wakazi wa kisiwa cha Krete kijulikanacho kama Kaftori (BDB 499)

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:15-20**

**15 Kanaani akamzaa Sidoni, mwanawe wa kwanza, na Hethi, 16 na Myebusi, na Mwamori, na Mgirgashi, 17 na Mhivi, na Mwarki, na Msini, 18 na Mwarvadi, na Msemari, na Mhamathi. Baadaye jamaa za Wakanaani walitawanyikana. 19 Na mpaka wa Wakanaani ulianza kutoka Sidoni kwa njia ya Gerari hata Gaza; tena kwa njia ya Sodoma, na Gomora, na Adma, na Seboimu, hata Lasha. 20 Hao ndio wana wa Hamu, kufuata jamaa zao, kwa lugha zao, katika nchi zao, kufuata mataifa yao.**

**10:15 "Sidoni"** Hii ni bandari bahari maarufu sana ya Foinike na kiasili mji mkuu, kaskazini mwa Palestina (BDB 850).

◙ **"Hethi"** Hili (BDB 366) linaonekana kuwa jina lisilo la kisemitiki. Inawezekana ni mwanzo wa kundi la Wahiti. Katika Biblia maeneo haya yapo sehemu mbili: (1) kuzunguka mji wa Hebroni (2) kaskazini mwa Palestina katika Uturuki kati. Walitawala eneo hili lote kati ya mwaka 1800-1200 k.k. Kundi la Kikabila liitwalo Wahivi linaweza kuwa limeunganishwa na neno Hethi.

**10:16 "Myebusi"** Hawa walikuwa wakazi wa jiji la Salemu au Yebusi, baadaye Yerusalemu (BDB 101).

◙ "**Mwamori"** Neno hili (BDB 57) Mwamwori linaweza kuwa neno la kuwajumuisha wote (kama vile Mwanzo 15:16) kama neno Wakanaani. Tunafikiria ilikuwa na kisawe cha "mkazi wa uwanda wa juu" (Neno bayana lilimaanisha "mtu wa magharibi") wakati Mkanaani ilikuwa na kisawe cha "mkazi wa uwanda wa chini" (neno la kibayana lilikuwa "nchi ya zambarau"). Katika Biblia wakazi wa Kanaani wanaorodheshwa katika maeneo kadhaa: (1) kwa makundi mawili ya kikabila katika Mwanzo 13:7, 34:30; Waamuzi 1:4,5; (2) kwa mataifa saba katika Kumb. 7:1; Josh. 3:10; 24:11; (3) kwa mataifa kumi katika Mwanzo 15:19-20; na (4) matumizi makubwa zaidi yaliyozoeleka ni maelezo ya taifa la sita ambalo linatumiwa mara nyingi zaidi katika vitabu vitano vya Biblia.

◙**"Mgirgashi"** Hili lilikuwa kabila la Wakanaani mara kwa mara likiitwa katika orodha tofauti tofauti ya makabila ya Kanaani (BDB 173, kama vile Mwanzo 10:16; 15:21; Kum. 7:11; Josh. 3:10; 24:11; Neh. 9:8; I Nyakati 1:14), lakini hakuna eneo husika ambalo liliwahi kutambuliwa.

**10:17 "Mhivi"** Wanaonekana kuwa wakazi wa Palestina ya kati (BDB 295). Baadhi wanawatambua pamoja na Wa-Hurri. Hesabu 13:29 ni muhtasari mzuri wa kijiografia wa mgawanyo wa makabila haya katika Palestina.

◙**"Mwarki,"** Hawa wanaonekana kuwa wakazi wa jiji la pwani na kisiwa cha kaskazini mwa Sidoni (BDB 792).

◙ **"Msiniti"** Hawa wanaonekana kuwa wakazi wa jiji karibu na Arki (BDB 696).

**10:18 "Mwarvadi"** Hawa wanaonekana kurejerea wakazi wa kisiwa nje ya pwani mwa Palestina (BDB 71). Kama yale mawili yaliyotangulia ni kaskazini mwa Tripoli.

◙**"Mhamathi"** Hawa wanarejerea wakazi wa jiji katika mto Orontes (BDB 333).

**10:19 "Sodoma, na Gomora, na Adma, na Seboimu"** Hii ni miji ya uwanda ambayo Mungu baadaye aliiharibu. Miji ipo maeneo ya kusini mwishoni mwa Bahari ya Chumvi.

◙ **"Lasha"** Jerome anasema kwamba huu ulikuwa mashariki mwa Bahari ya Chumvi (BDB 546).

**10:20** Muhtasari huu wa mgawanyiko ni kama wa mstari wa 5.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10: 21-31**

**[21] Naye Shemu ambaye ni baba wa wana wote wa Eberi, na ndugu mkubwa wa Yafethi, akazaliwa wana. [22] Wana wa Shemu ni Elamu, na Ashuru, na Arfaksadi, na Ludi, na Aramu. [23] Na wana wa Aramu ni Usi, na Huli, na Getheri, na Mashi. [24] Arfaksadi akamzaa Sela, Sela akamzaa Eberi. [25] Eberi akazaliwa wana wawili wa kiume; jina la wa kwanza ni Pelegi maana katika siku zake nchi iligawanyika; na jina la nduguye ni Yoktani. [26] Yoktani akamzaa Almodadi, na Shelefu, na Hasarmawethi, na Yera, [27] na Hadoramu, na Uzali, na Dikla, [28] na Obali, na Abimaeli, na Seba, [29] na Ofiri, na Havila, na Yobabi. Hao wote ndio wana wa Yoktani. [30] Makao yao yalikuwa kutoka Mesha kwa njia ya Sefari, mlima wa mashariki. 31 Hao ndio wana wa Shemu, kufuata jamaa zao, na lugha zao, katika nchi zao, kufuata mataifa yao.**

**10:21 "Shemu"** Hili ni neno la Kiebrania "jina" (BDB 1028 II). Umuhimu wake unaonekana kwasababu anatajwa kote hapa na katika 11:10-26. Watu waasi wa Sura za 10-11 anataka kujenga "jina" kwa ajili yao wenyewe. Jina lake linaunganishwa na 4:26 (yaani jina la YHWH linatukuzwa). Atawakilisha uzao mteule wa Baraka (kama vile 12:2).

◙ **"Eberi"** Asili ya jina hili ni sawa kabisa na jina "Mwebrania" (BDB 720 II), ambalo linamaanisha kikundi kipoana zaidi kuliko kuwa Wayahudi tu. Kumekuwa na makisio mengi kuhusu muunganiko kati ya Ebri na tungo inayopatikana katika nyaraka nyingi na Stele (s) katika Misri iitwayo "Habirv" (kama vile Mwanzo 14:13). Asili inayowezekana ya jina Eberi ni "kupita juu na kupenya," ambalo linaonekana kuwa kundi la ufugaji la kuhamahama.

◙**"ndugu mkubwa wa Yafethi"** Rashi anaelezea kwamba Ebrania ni tata kama kama vile swali la ni nani aliye kaka mkubwa.

**10:22 "Elamu"** Huu ulikuwa ni ufalme mkubwa mashariki mwa mto Hedekeli ambayo mji wake Mkubwa ulikuwa ni Shushani. Hii inawezekana makundi ya mashariki zaidi yanayotajwa katika sura hii (BDB 743).

◙ **"Ashuru"** Hii (BDB 78) inaweza kumaanisha (1) mtu; (2) jiji; au (3) taifa (yaani Ashuru).

◙ **"Arfaksadi"** Hii (BDB 75) inaonekana kuwa kikundi cha kikabila kaskazini mwa Ninawi (Mji Mkuu mwingine wa Ninawi). TheFasiri ya NIV ina Arfaksadi.

◙**"Ludi"** Hii inawezekana kurejerea taifa la Lydia la Asia Ndogo (BDB 530). Heroditus anaelezea kwamba walidai kuwa ni asili ya Ninawi, jiji la kisemiti.

◙**"Aramu"** Hii inarejerea eneo la Siria ya sasa (BDB 74).

**10:25 "Pelegi"** Huu ni uzao wa kibayana ambao Ibrahimu atatokea na imejadiliwa kikamilifu ki-vizazi/ki-uzao katika 11:18-27. Inaweza kumaanisha "kugawanywa" (BDB 811 II).

◙**“maana katika siku zake nchi iligawanyika”** Neno la Kiebrania kibayana linamaanisha “mifereji ya umwagiliaji” ambayo ingeshabihiana na kusini mwa Mesopotamia, lakini asili maarufu zaidi “migawanyiko” (BDB 811, KB 928, *Niphal* KAULI YA WAKATI TIMILIFU). Kuna mzaha wa sauti Pelegi na kugawanyika (*niplega*). Hii inaweza kurejerea kugawanyika kwa lugha zinazotajwa katika sura ya 11. Hivyo, mtawanyiko wa sura ya 10 uko nje ya utaratibu wa mfuatano ukilinganishwa na sura 11.

**10:26-29** Huu ni ufafanuzi wa kinagaubaga wa makabila ya Arabia.

**10:28 “Seba. . .Havila”** Hii sambamba na Ashuru mstari wa 22, inaonekana kujumuisha wote orodha yaw a-Hami na orodha ya Wa-Semiti. Hii ni kwasababu ya (1) uhamiaji wa kijiografia; (2) ushindi wa kivita; au (3) kuungana kwa familia mbili kupitia ndoa. Orodha hii si bayana kwa njia nyingi.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA) 10:32**

[32] **Hizo ndizo jamaa za wana wa Nuhu, kufuata vizazi vyao, katika mataifa yao; na kwa hao mataifa yaligawanyika katika nchi baada ya gharika.**

## MASWALI YA MJADALA

Huu nimwongozo wa kujifunza wa fasiri, inamaanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazimaa tembee katika mwanga tulionao.Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu ya natolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini kusudio la Mwanzo 10?
2. Kwanini Nimrodi anawekewa upekee kuwa anahitaji kusaidiwa kimaalumu?
3. Kwanini Israeli, Moabu na Edomu hawatajwi katika orodha hii ya mataifa

# SURA YA 11:1-32

| MIGAWANYO YA AYA YA TAFSIRI ZA KISASA | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **NASB** | **NKJV** | **NRSV** | **TEV** | **NJB** |
| Lugha ya kiulimwengu Babeli, machafuko | Mnara wa Babeli | Mnara wa Babeli | Mnara wa Babeli | Mnara wa Babel |
| 11:1-9 | 11:1-9 | 11:1-9 | 11:1-9 | 11:1-4<br>11:5-9 |
| Kizazi cha Shemu | Ukoo uliotokana na Shemu | Uzao wa Abraham | Kizazi cha Shemu | Wazee wa kaya baada ya gharika |
| 11:10-11 | 11:10-11 | 11:10-11 | 11:10-11 | 11:10 |
| | | | | 11:10b-11 |
| 11:12-13 | 11:12-13 | 11:12-13 | 11:12-13 | 11:12-13 |
| 11:14-15 | 11:14-15 | 11:14-15 | 11:14-15 | 11:14-15 |
| 11:16-17 | 11:16-17 | 11:16-17 | 11:16-17 | 11:16-17 |
| 11:18-19 | 11:18-19 | 11:18-19 | 11:18-19 | 11:18-19 |
| 11:20-21 | 11:20-21 | 11:20-21 | 11:20-21 | 11:20-21 |
| 11:22-23 | 11:22-23 | 11:22-23 | 11:22-23 | 11:22-23 |
| 11:24-25 | 11:24-25 | 11:24-25 | 11:24-25 | 11:24-25 |
| 11:26 | 11:26 | 11:26 | 11:26 | 11:26 |
| | Kizazi cha Tera | | kizazi kilichotokana na Tera | kizazi kilichotokana na Tera |
| | 11:27-30 | 11:27-30 | 11:27-30 | 11:27 |
| 11:27-30 | | | | 11:27b-30 |
| 11:31-32 | 11:31-32 | 11:31-32 | 11:31-32 | 11:31 |
| | | | | 11:32 |

## MZUNGUKO WA TATU WA USOMAJI (<u>angalia ukurasa wa vii)</u>

### *KUFUATILIA KUSUDIO LA ASILI LA MWANDISHI KATIKA NGAZI YA AYA*

Huu ni <u>mwongozo</u> kwa kujisomea wa fasiri, ikiwa na maana kuwa unawajibika kwa tafsiri yako mwenyewe ya Bibila. Kila mmoja wetu sharti atembee katika mwanga tulionao. Wewe, Bibila na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Usimwachie kazi hii mfasiri.

Soma sura katika mkao mmoja. Tambua masomo linganisha mgawanyo wako na tafsiri tano hapo juu.

Kuandika ki-aya sio kazi iliyovuviwa, lakini ni mwongozo wa kufuata kusudio la mwandishi wa kwanza ambacho ndicho kiini cha tafsiri. Kila aya ina somo moja tu.

3. Aya ya kwanza
4. Aya ya pili
5. Aya tatu
6. N.k

## TAMBUZI ZA KIMUKTADHA

A. Sura za 10-11 zimebadilishwa katika utaratibu wa kupanga matukio
B. Ingawa mkanganyiko wa lugha pamoja na matokeo yake ya kutawanyika kwa watu unaonekana kuwa kitendo cha hukumu, kumbuka kuwa ni maendeleo ya utaifa ndio uliopo, mpaka kufikia hapa, umeathiri mwenendo wa kisiasa kuelekea kwenye serikali moja ya kidunia. Kwa hiyo, hii ilikuwa ni maana nyingine ya Baraka ya Mungu.
   Kwa Wakristo, Pentekoste ilikuwa ni kinyume cha thiolojia cha mnara wa Bbabeli

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:1-9**
**1Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja. 2Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki waliona nchi
tambarare katika nchi ya Shinari; wakakaa huko. 3Wakaambiana, Haya, na tufanye matofali tukayachome
moto. Walikuwa na matofali badala ya mawe, na lami badala ya chokaa. 4Wakasema, Haya, na tujijengee
mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, tujifanyie jina; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi
yote. 5Bwana akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu. 6Bwana akasema,
Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa
hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya. 7Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili
wasisikilizane maneno wao kwa wao. 8Basi Bwana akawatawanya kutoka huko waende usoni pa nchi yote;
wakaacha kuujenga ule mji. 9Kwa sababu hiyo jina lake likaitwa Babeli; maana hapo ndipo Bwana
alipoichafua lugha ya dunia yote; na kutoka huko Bwana akawatawanya waende usoni pa nchi yote.**

**11:1 "Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja"** Ni dhahiri kuwa sura ya 11 inaelezea kutawanyika kulikoelezewa katika sura ya 10. Hii lugha moja, ambayo inavyoonekana ilikumbushia nyuma hadi Edeni, ilikuwa sio Kiebrania. Lugha ya kale inayofahamika kwa watu wa leo ni kikabari cha Summeri, ikiandikwa mwaka 3,000 K.K. (ABD, juzuu 1, uk. 1213), na uatamaduni yapata toka mwaka 10,000-8,000 K.K.

**11:2 "walisafiri pande za Mashariki"** Hii inaonekana kudokeza mwelekeo mbali na mahali palipokuwepo na safina, Mlima Ararat. Kifungu halisi "wakasafiri" kinamaanisha "waling'oa vigingi" (BDB 652, KB 704), *Qal* TUNGO ISIO NA KIKOMO). Mesopotamia iko Kusini Mashariki mwa Mlima Ararati (ambao umeenea toka Uturuki ya sasa mpaka Irani).

◙**" katika nchi ya Shina"** Hii inamaanisha Mesopotamia ya chini au Babeli, ambayo pia iliitwa Kaldea (BDB 11042).

**11:3** Mstari huu una neno moja *Qal* KAULI SHURUTISHI na miundo miwili inayohusiana VITENZI AMRISHI. Hili linaelezea mbinu za kimuundo ambazo ni usahihi wa kihistoria mahali palipo Mesopotamia. Hapakuwepo na mawe katika eneo hili, kwa hiyo matofari ndiyo yalikuwa yakichomwa. Toleo la King James lina neno "tope la mfinyanzi," lakini kiuhalisia linarejelea kwenye kitu cheusi, kigumu kinachochemka katika eneo hili. Tunaweza kukiita nta, au lami (BDB 330, kama vile 6:14).

**11:4** Mstari huu una neno moja *Qal* KAULI SHURUTISHI na KAULI ZISIZO TIMILIFU zinazohusiana zilizotumika kama VITENZI AMRISHI. Kunaonekana kuwepo na vipengere vinne vilivyohusishwa katika habari hii: (1) kujengwa kwa Mji na Mnara; (2) kipimo ambacho kingalishindana na majengo mengine ya siku hizo; (3) wao walitaka kutengeneza jina; na (4) hawakutaka kutawanyika nje ya nchi (yaani Dunia nzima). Kidokezo halisi cha hili hakijulikani. Wengi wamedai kuwa linahusiana na Wababeli ziggurats, lakini neno la Kiebrania ni *migdal* ambalo linatafasiriwa "ngome imara" (BDB 153, kama vile Amu. 8:9-17). Kiuhalisia ni jaribio la mwanadamu kujiongoza wao wenyewe tofauti na Mungu, na kwa hali hiyo kuathiri mapenzi ya Mungu. Filo hata anasema kuwa waliandika majina yao kwenye kila tofali ili kwamba wasije wakatawanyika. Huu ndio mfano wa kwanza wa majivuno ya mwanadamu, kusanyiko na utendaji mbali na Mungu (kama vile Danieli na Ufunuo 18 na 19).

◙ **"na kilele chake kifike mbinguni"** Watu wa Mesopotamia walikuwa waabudu nyota (yaani Nyota za angani zilikuwa miungu yao). Minara hii ilikuwa ni ngazi zilizoinuliwa kuchunguza anga la usiku. Palikuwa ni mahali pa kukutana ambapo miungu iliabudiwa.

**11:5** Hii ni namna ya Mungu kuelezewa kwa lugha ya kibinadamu (kama vile 18:21; Kut. 3:8).

**11:7 "Na tushuke chini"** Mstari huu pia una neno *Qal* KAULI SHURUTISHI ukiwa na VITENZI AMRISHI vinavyohusiana. Huu ni muundo wa UWINGI, zaidi kama 1:26; 3:22. Ingawa sura hii inaonekana kuwa namna ya mwanadamu kumwelezea Mungu katika Kiingereza, hairejelei udhaifu juu ya sehemu ya Mungu bali ni kitendo cha neema ambapo alizuia utendaji dhambi wa mwanadamu wa kujaribu kuendesha maisha yake kwa namna ya njia ya anguko (kama vile Rum. 1-3). Na "tushuke"ya utendaji wa ki-Ungu ukaathiri ile "tushuke" ya uasi wa mwanadamu (kama vile mistari ya 3,4,7).

**11:9 "Babeli"** inafurahisha kutambua kuwa Mwanaakiolojia alifukua nyaraka za kifasihi za utamaduni wa Kisummeri huko Mesopotamia ambao unadai kuwa kwa muda huu watu wote walikuwa wakiongea lugha moja (yaani. Samuel Noah Kramer katika makala yake "The Babel of Tongues: A Sumerian Version" in *Journal of the American Oriental Society*, 88:108-111). Asili ya neno la Kiebrania lililojulikana ni "machafuko" (yaani. *balal*, BDB 93), linaloonekana kuelezea namna Mungu alivyochafua lugha zao. Kiuhalisia Babeli inamaanisha "lango la Mungu" (Akkadian *bab-ilani*), ambalo linafanana na baadhi ya majina ya Ziggurats, ambayo yalikuwa ni majengo makubwa yenye hekalu juu yake kwa ajili ya kuabudu miungu nyota. Babeli ikaja kuwa ni alama ya ulimwengu yenye nguvu iliyoanguka, ikionyeshwa katika Nimrodi, na baadaye Nebukadneza, na mwishowe katika mnyama wa baharini wa kile kitabu cha Ufunuo.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:10-11**
**[10] Hivi ndivyo vizazi vya Shemu; Shemu alikuwa mtu wa miaka mia akamzaa Arfaksadi miaka miwili baada ya gharika. [11] Shemu akaishi baada ya kumzaa Arfaksadi miaka mia tano, akazaa wana, waume na wake.**

Kizazi cha Shemu kiliendeleza uzao wa Kimasihi toka kwa Sethi Mwa. 5:3-32 na 10:21-31. Uzao utaendelea mpaka kwa Tera/Ibrahimu katika 11:10-25 (kama vile Luka 3:23-38).

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:12-13**
**[12]Arfaksadi akaishi miaka thelathini na mitano, akamzaa Sela. [13]Arfaksadi akaishi baada ya kumzaa Sela miaka mia nne na mitatu, akazaa wana, waume na wake.**

Andiko la ki-Masoretiki linaliondoa neno *Kainan* katika mst. 13 lakini tafasiri ya maandiko ya kale ya Kiebrania yanalijumuisha kama anavyofanya Luka 3:36.

◙ **"Sela"** Angalia BDB 1019 II.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:14-15**
**[14]Sela akaishi miaka thelathini, akamzaa Eberi. [15] Sela akaishi baada ya kumzaa Eberi miaka mia nne na mitatu, akazaa wana, waume na wake.**

◙ **"Eberi"** Angalia BDB 720.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:16-17**
**[16] Eberi akaishi miaka thelathini na minne, akamzaa Pelegi. [17] Eberi akaishi baada ya kumzaa Pelegi miaka mia nne na thelathini, akazaa wana, waume na wake.**

◙**"Pelegi"** Angalia BDB 811 II.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:18-19**
**18 Pelegi akaishi miaka thelathini, akamzaa Reu. 19 Pelegi akaishi baada ya kumzaa Reu miaka mia mbili na kenda, akazaa wana, waume na wake.**

◙**"Reu"** Angalia BDB 946.

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 11: 20-21**
**20 Reu akaishi miaka thelathini na miwili, akamzaa Serugi. 21 Reu akaishi baada ya kumzaa Serugi miaka mia mbili na saba, akazaa wana, waume na wake.**

◙ **"Serugi"** Angalia BDB 974.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11: 22-23**
**22 Serugi akaishi miaka thelathini, akamzaa Nahori. 23 Serugi akaishi baada ya kumzaa Nahori miaka mia mbili, akazaa wana, waume na wake.**

◙ **"Nahori"** Angalia BDB 637

## MASWALI YA MJADALA

Huu ni mwongozo wa kujisomea wa fasiri, hii ina maanisha kwamba unawajibika kwa tafsiri zako mwenyewe za Biblia. Kila mmoja wetu lazima atembee katika mwanga tulio nao. Wewe, Biblia, na Roho Mtakatifu ni vipaumbele katika tafsiri. Hutakiwi uvitelekeze vitu hivi kwa mfasiri.

Maswali ya mjadala huu yanatolewa kukusaidia kufikiri juu ya mambo makubwa ya sehemu za kitabu hiki. Yanalenga kukuamsha kimawazo na sio kutoa maana.

1. Nini maana ya mnara wa Babeli?
2. Ni kipi mwanadamu alichokuwa akikifanya kinyume na matakwa ya Mungu katika Mwanzo 11

## UTANGULIZI WA MWANZO 11:24-13:18

A. Hii sehemu ya kitabu cha Mwanzo inaanza na maelezo kamili ya uzao wa Kimasihi kupitia Abraham.
B. Sura ya Hamsini ya kitabu cha Mwanzo inahusiana na ukombozi wa watu wa Mungu wa agano, na sio uumbaji. Kumwita mtu mmoja kwa ajili ya kuwaita wote ndio mtazamo wa kitabu .
C. Abram anaonekana katika udhaifu huu vile vile pia katika uaminifu wake. Mungu wa uchaguzi na rehema akamwita toka kwenye kusudio lake la ukombozi.
D. Mungu akamchagua Ibrahimu kuuchagua ulimwengu (kama vile 12:3c; Kut. 19:4-6; II Pet. 2:5,9; Ufu. 1:6). Mungu anahitaji watu wote aliowaumba kwa sura yake waweze kukombolewa (kama vile Mwa. 3:15; Ezek. 18:23,32; I Tim. 2:4; II Pet. 3:9)
E. Buku la sheria za Kiyahudi linaelezea juu ya Baraka saba za wito:
    1. Abram angalikuwa baba wa mataifa yote.
    2. Angelibarikiwa katika maisha yake yote.
    3. Jina lake lingalijulikana vizazi hadi vizazi.
    4. Angalikuwa ni Baraka kwa wengine.
    5. Wangalibarikiwa wengine wanaomheshimu.
    6. Wengine wangelilaaniwa wanao mkataa.
    7. Mamlaka yake yangelikuwa ya kiulimwengu

## USOMAJI WA NENO NA KIFUNGU CHA NENO

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 11:24-25**
**[24]Nahori akaishi miaka ishirini na kenda, akamzaa Tera. [25]Nahori akaishi baada ya kumzaa Tera miaka mia na kumi na kenda, akazaa wana, waume na wake.**

**11:24 "Tera"** "Tera" yumkini linamaanisha "lami," "kuchelewa," au "kuhamahama" (BDB 1076). Kutokana na Yosh. 24:2 ni dhahiri kuwa Yeye na familia yake walikuwa ni watu wa kuabudu miungu wengi. Jina la familia yake kimsingi linapendekeza kuwa waliabudu mungu wa mwezi aitwae *Zir*. Huyu mungu aliabudiwa huko Uru, Tema na Harani. Ingawa, Mwanzo 31:53 inadokeza kuwa alimfahamu YHWH.

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:26**
**[26] Tera akaishi miaka sabini, akamzaa Abramu, na Nahori, na Harani.**

**11:26 "Abramu, Nahori and Harani"** Huu waweza kuwa ni utaratibu uliowekwa na sio umri. Jina la Abram laweza kumaanisha (1) "baba aliyeinuliwa"; (2) "yeye amwinuaye baba"; au (3) "pekee aliyeinuliwa ni baba yangu" (BDB 4). Jina la Nahori linamaanisha "kupweta" au jina mojawapo la sehemu huko Ashuru (BDB 637), wakati Harani linamaanisha "mpanda milima" (BDB 248).

**ANDIKO LA NASB(LILILOBORESHWA): 11:27-30**
**[27]Na hivi ndivyo vizazi vya Tera. Tera akamzaa Abramu, na Nahori, na Harani. Harani akamzaa Lutu. [28]Harani akafa kabla ya baba yake Tera katika nchi aliyozaliwa, yaani, katika Uru wa Wakaldayo. [29] Abramu na Nahori wakajitwalia wake. Jina la mkewe Abramu aliitwa Sarai, na jina la mkewe Nahori aliitwa Milka, binti Harani, ambaye alikuwa baba wa Milka na wa Iska. [30]Na Sarai alikuwa tasa, hakuwa na mtoto.**

**11:27 "Lutu"** Angalia BDB 532 II.

**11:28 "Harani akafa kabla ya baba yake"** Hii ni nahau ya Kiebrania kwa ajili ya Harani akifa kabla ya baba yake.

◙ **"Uru wa Wakaldayo"** Utamaduni wa Wakaldayo ulistawi (yaani. Ulijengwa juu ya nguvu za tamaduni za Kisummeri)na kustawi baada ya siku za Abram (BDB 505).

**11:29 "Sarai"** Angalia BDB 979.

◙ **"Milka"** Angalia BDB 574.

◙ **"na Iska"** Mtu huyu (BDB 414) na sababu za uwepo wake katika mstari huu haijulikani. Walimu wa dini ya Kiyahudi (Yosefati, Jerome, na Augustine) wanasema ni Sarai, lakini andiko linadai kuwa walikuwa na baba tofauti.

**11:30 "Sara alikuwa tasa"** Kutokuweza kwa Sarai, Raheli, na Rebeka kupata watoto (BDB 785) ilikuwa ni njia mojawapo ya Mungu kuonyesha uwezo na udhibiti wa historia ya mwanadamu na uzao wake. Kizazi cha mwanadamu sio dhana muhimu kwenye uzao wa Kimasihi. Huu mtindo wa aina moja wa dhana ya thiolojia kwa historia ya Israeli pia inaonekana katika ukweli kwamba mzaliwa wa kwanza hayuko katika uzao wa Kimasihi. Kitamaduni mzaliwa wa kwanza alipaswa kuwa mkuu wa ukoo, lakini sivyo kati ya watu wa YHWH. Ilikuwa ni uchaguzi wake!

**ANDIKO LA NASB (LILILOBORESHWA): 11:31-32**
**[31]Tera akamtwaa Abramu mwanawe, na Lutu mwana wa Harani, mwana wa mwanawe, na Sarai mkwewe, mke wa Abramu mwanawe, wakatoka wote katika Uru wa Wakaldayo, waende nchi ya Kanaani, wakafika mpaka**

**Harani wakakaa huko. [32]Siku za Tera zilikuwa miaka mia mbili na mitano; Tera akafa katika Harani.**

**11:31 "wakatoka wote"** Kuna majadiliano mengi ikiwa Tera alichukua familia yake au ikiwa Abram aliwachukua. Baadhi wanabashiri ni wito wa kwanza wa Mungu kwa Tera lakini alijikwaa na kurudi kwenye ibada ya sanamu. Inaonekana kwangu kuwa Abraham ndio kitovu cha kipengele chote, na sio Tera. Kwa kuondoka kwake Uru Abramu alikuwa haachi tu familia yake, lakini pia miungu ya taifa lake. Aliacha maisha ya raha, yaliyo imarika kumfuata Mungu mpya ambaye aliongea naye kwa mtindo wa ajabu..

**11:32 "siku za Tera zilikuwa miaka 205"** Mtu akiongeza miaka ile ya Mwanzo 11:26 na ya Mwanzo 12:4 ambayo ni sawa na miaka 145 na kutoa hii kwenye miaka 205, inakuwa dhahiri kuwa Tera aliishi miaka 60 baada ya Abraham kuondoka Harani. Hili linaonekana kutofautiana na hotuba Stefano katika Mdo.7:4. Mitazamo mbali mbali ya uchunguzi wa kihistoria wa Stefano unatofautiana na uelewa wetu wa leo wa historia ya agano la kale. Yumkini alikuwa akitumia njia ya utafasiri wa sheria za Kiyahudi. Wasomi wengine wanadai kuwa Abramu, ingawa ametajwa katika 11:26, alizaliwa muda kitambo na Stefano alikuwa sahihi. Inafurahisha kuwa torati ya Kisamaria ina "144" hapa.
lapse

# MAELEZO YA KIMAFUNDISHO YA BOB

Mimi siangalii hasa habari za imani au kanuni za imani. Napendelea kuthibitisha Biblia yenyewe. Ingawa, natambua kuwa habari ya imani itawaleta wale tusiojuana ili kupima mtizamo wa mafundisho yangu. Katika siku zetu za leo zenye makosa mengi ya kithiolojia na upotofu, natoa muhtsari mfupi wa thiolojia yangu kama ufuatavyo.

1. Biblia, yote katika Agano la Kale na Agano Jipya, ni neno la Mungu lililovuviwa, lenye uhakika, lenye uzima na lenye mamlaka. Ni ufunuo pekee wa Mungu ulioandikwa na watu chini ya uongozi wa nguvu za ajabu. Ni kiini pekee cha ukweli sahihi kuhusu Mungu na Kusudi Lake. Pia ni kiini pekee cha imani na utendaji wa kanisa lake.
2. Kuna Mungu mmoja tu wa uzima, uumbaji na ukombozi. Yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote, vionekanavyo na visivyo onekana. Amejidhihilisha mwenyewe kama Mungu wa upendo na anayejali ingawa pia ni Mungu asiye na upendelea. Amejidhihilisha mwenyewe katika nafsi tatu tofauti: Baba, Mwana na Roho; haswa wanatengana lakini wanafanya kazi moja.
3. Muda wote Mungu yuko hai kuangalia ulimwengu huu. Kuna mpango wa ndani wa uumbaji wake usiobadilika na mtazamo wa kipekee unaomfanya binadamu kutenda mapenzi huru. Hakuna kinachoweza kutokea pasipo ruhusa na maarifa ya Mungu, bado anaruhusu uchaguzi kwa wote malaika na wanadamu. Yesu ni chaguo la Baba na wote kimanufaa wamechaguliwa katika Yeye. Ufahamu wa mbele wa Mungu kuhusu matukio hayampunguzii binadamu kubainisha maandiko yaliyoandikwa kabla. Wote tunahusika kwa mawazo yetu na matendo
4. Binadamu, japo aliumbwa kwa sura ya Mungu na mbali na dhambi, aliamua kumwasi Mungu. Ingawa alijaribiwa na kitu chenye nguvu ya ziada. Adamu na Hawa waliwajibika kwa utashi wao wenyewe kuamua. Uasi wao umeathiri utu wa uumbaji. Watu wote tunahitaji rehema na huruma ya Mungu yote kwa hali ya ushirika katika Adamu na uasi binafsi wa hiari.
5. Mungu anatoa aina ya msamaha na urejesho kwa binadamu aliyeanguka. Yesu Kristo, Mwana pekee wa Mungu Baba, akawa mwanadamu, akaishi maisha yasio na dhambi, na kwa kifo chake mbadala, akalipa malipo ya dhambi ya mwanadamu. Ndiyo njia pekee ya kurejesha ushirika wetu na Mungu. Hakuna njia nyingine ya wokovu isipokuwa kupitia imani ya kazi yake aliyoimaliza.
6. Kila mmoja wetu binafsi yampasa kupokea ahadi ya msamaha na urejesho katika Kristo. Hilo linatimizwa kwa njia ya imani ya hiari katika ahadi za Mungu kupitia Kristo Yesu na kugeuka kwa mapenzi huru kwa dhambi inayojulikana.
7. Sisi sote tumesamehewa jumla na urejesho umelenga juu ya kuamini katika Kristo na toba toka dhambini. Ingawa, ushahidi wa mahusiano mapya unaonekana katika mabadiliko na badiliko endelevu. Dhumuni la Mungu kwa wanadamu sio tu kwenda mbinguni siku moja, lakini kufanana na Kristo kwa sasa. Wale wote ambao wanakombolewa kweli ingawa wakati mwingine wanatenda dhambi, wataendelea katika imani na toba siku zao zote za maisha.
8. Roho Mtakatifu ni “Yesu mwingine.” Yuko duniani kuwaongoza wale wote waliopotea katika Kristo na kujenga ufanano wa Kristo katika kuokolewa. Karama za rohoni zinapewa toka kwenye wokovu. Ni maisha na huduma ya Yesu yaliyogawiwa katika mwili wake, yaani kanisa. Vipawa 358 ambavyo kimsingi ndio mwelekeo na msukumo wa hitaji la Yesu likihamasishwa na tunda la Roho. Roho yu hai katika siku zetu kama alivyokuwa katika enzi za Biblia.
9. Baba amemfanya Yesu Kristo aliyefufuka kama mwamuzi w vitu vyote. Atarudi duniani kuhukumu wanadamu wote. Wale wote walioamini Yesu na majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima cha mwanakondoo watapata mwili na utukufu ataporudi. Wataishi nae milele. Ingawa, wale wote walioikataa kweli ya Mungu watatengwa milele toka katika furaha ya ushirika wa Mungu wa Utatu. Watahukumiwa

pamoja na shetani na malaika zake. Hii hakika haijaisha au kukamilika lakini natarajia itakupa ladha ya kithiolojia ya moyo wangu, nafurahia maelezo:

“Katika mambo ya msingi-umoja, mambo yaliyo ukingoni-uhuru, katika mambo yote-upendo.